JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

HALI YA UCHUMI WA TAIFA KATIKA MWAKA 2011

Kimetolewa na:
Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango
DAR ES SALAAM – TANZANIA
Juni, 2012

HALI YA UCHUMI WA TAIFA

KATIKA MWAKA 2011

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ..... **IX**

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO ..... **XIV**

MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2011 ..... **XVIII**

SURA YA I **1**

HALI YA UCHUMI WA TAIFA **1**

UKUAJI WA UCHUMI 1
MWENENDO WA BEI 6
UKUZAJI RASILIMALI 11

SURA YA 2 ..... **41**

HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA **41**

UKUAJI WA UCHUMI DUNIANI 41
MWENENDO WA BIASHARA DUNIANI 42
HALI YA UCHUMI WA NCHI ZA AFRIKA 43
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI 45
UMOJA WA AFRIKA NA TUME YA UCHUMI YA BARA LA AFRIKA 46
JUMUIYA YA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA 47
SHIRIKISHO LA BIASHARA ULIMWENGUNI 48

SURA YA 3 ..... **49**

SEKTA YA NJE **49**

UTANGULIZI 49
BIDHAA ZILIZOUZWA NJE 49
Bidhaa Asilia *49*
Bidhaa Zisizo Asilia *51*
MAPATO YA HUDUMA 54
BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE 54
Bidhaa za Kukuza Mitaji *54*
Bidhaa za Kati *55*
Bidhaa za Matumizi ya Kawaida *55*
MALIPO YA HUDUMA 55
MWENENDO WA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI MBALIMBALI 56
MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE 61
AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI 62
THAMANI YA FEDHA YA TANZANIA 63

SURA YA 4 ..... **77**

FEDHA ZA SERIKALI **77**

UTANGULIZI 77
MWENENDO WA MAPATO 78
Mapato ya Ndani *78*
Misaada na mikopo *79*
Mikopo ya ndani *79*
Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara *80*
MATUMIZI 80
Malipo ya Deni *81*
Mgawanyo wa Matumizi kwa Baadhi ya Sekta *82*
DENI LA TAIFA 82
Deni la Ndani *82*
Deni la Nje *84*
Deni la Nje kwa Wakopeshaji *84*

SURA YA 5 ..... **90**

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA **90**

UJAZI WA FEDHA NA KARADHA 90
MWENENDO WA MIKOPO KWA SEKTA BINAFSI 91
AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA 91
MWENENDO WA VIWANGO VYA RIBA 92
MABORESHO YA SEKTA YA FEDHA 92
MFUKO WA PENSHENI WA MASHIRIKA YA UMMA 93
MFUKO WA PENSHENI KWA WATUMISHI WA UMMA 94
MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII 95
MFUKO WA AKIBA YA WAFANYAKAZI WA SERIKALI 96
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA 97
MFUKO WA PENSHENI WA SERIKALI ZA MITAA 98
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA BIMA TANZANIA 99
SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM 100
BENKI YA POSTA 102

SURA YA 6 ..... **109**

RASILIMALI WATU **109**

IDADI YA WATU NA MAENDELEO 109
NGUVUKAZI NA AJIRA 111

SURA YA 7 ..... **115**

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI **115**

UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI NCHINI 115
MCHANGANUO WA MIRADI KIMKOA 116
UWEKEZAJI MITAJI YA KIGENI YA MOJA KWA MOJA 116
UBORESHAJI WA MAZINGIRA WEZESHI KWA SEKTA BINAFSI 117
UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI 118
Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi *118*
Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira *119*
Utoaji na Upatikanaji wa Mikopo Kupitia Mifuko Mbalimbali *119*

SURA YA 8 ..... **122**

MASUALA MTAMBUKA **122**

UKIMWI 122
MAZINGIRA 122
UTAWALA BORA 124
JINSIA 125
USALAMA WA RAIA 125

SURA YA 9 ..... **127**

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI TANZANIA **127**

UTANGULIZI 127
UKUAJI WA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI WA KIPATO 127
KUBORESHA MAISHA NA USTAWI WA JAMII 128
UTAWALA BORA NA UWAJIBIKAJI 129

SURA YA 10 ..... **132**

MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO **132**

UTANGULIZI 132
MAANA YA MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO 132
HISTORIA YA MIPANGO YA MAENDELEO TANZANIA 133
DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025 134
MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO -2011/12-2015/16 135
Mchakato wa Utayarishaji wa Mpango *135*
Malengo ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12- 2015/16) 136
Sifa Mahsusi za Mpango *136*
Hatua za Kimkakati za Utekelezaji wa Mpango *137*
Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano *139*
Gharama za Utekelezaji za Mpango *141*
Mfumo wa Utekelezaji *143*

Utekelezaji na Uratibu wa Mpango wa Mwaka *144*
HITIMISHO 145

SURA YA 11 147

KILIMO NA USHIRIKA 147

KIWANGO CHA UKUAJI 147
UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA 147
UZALISHAJI WA MAZAO YA BIASHARA 148
UZALISHAJI WA MAZAO YA MAFUTA 149
UWEKEZAJI KATIKA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA KILIMO 150
KILIMO CHA UMWAGILIAJI 150
HUDUMA ZA UGANI NA MAFUNZO 151
SHUGHULI ZA UTAFITI 151
MFUKO WA PEMBEJEO 152
UTOAJI WA RUZUKU ZA PEMBEJEO 152
UZALISHAJI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE 153
BIASHARA YA MIFUGO NA MAZAO YAKE 155
MAENDELEO YA USHIRIKA 158
MWENENDO WA BEI ZA MAZAO YA BIASHARA 159

SURA YA 12 169

MALIASILI NA UTALII 169

KIWANGO CHA UKUAJI 169
MISITU NA NYUKI 169
WANYAMAPORI 171
UVUVI 173
UTALII 176
MALIKALE 177

SURA YA 13 190

MADINI 190

KIWANGO CHA UKUAJI 190
UTAFUTAJI MADINI 190
UCHIMBAJI NA UUZAJI MADINI 190
THAMANI YA MAUZO YA MADINI 192

SURA YA 14 195

VIWANDA NA BIASHARA 195

KIWANGO CHA UKUAJI 195
VIWANDA VIDOGO 195
GHARAMA ZA UZALISHAJI 195

UZALISHAJI KATIKA BAADHI YA VIWANDA NCHINI 195
BIASHARA YA NDANI 196
MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA 197

SURA YA 15 205

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI....205

UJENZI....205
Kiwango cha Ukuaji 205
Mtandao wa Barabara 205
Matengenezo ya Barabara na Madaraja 206
Bodi ya Mfuko wa Barabara 206
Bodi ya Usajili wa Makandarasi 207
Bodi ya Usajili ya Wahandisi....207
Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi 208
Baraza la Taifa la Ujenzi 209
Wakala wa Majengo Tanzania....209
Wakala wa Ufundi na Umeme 210
MAENDELEO YA ARDHI 210
Upimaji wa Mipaka ya Vijiji 210
Ukaguzi na Uhakiki wa Miliki 211
Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki za Kimila....211
Utoaji wa Hati Miliki 212
Upimaji wa Ardhi ya Baharini....213
Upimaji wa Mashamba na Viwanja....213
Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 214
Mipango ya Matumizi ya Ardhi 216
Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo 216
Hazina ya Ardhi 216
Maendeleo ya Nyumba....216

SURA YA 16 218

MAWASILIANO NA UCHUKUZI 218

KIWANGO CHA UKUAJI....218
USAFIRI WA BARABARA 218
USAFIRI WA ABIRIA MIJINI 218
USAFIRI KWA NJIA YA RELI....220
Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) 220
Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)....220
USAFIRI WA ANGA....221
Mamlaka ya Usafiri wa Anga 221
USAFIRI WA MAJINI....223
UCHUKUZI BAHARINI 223

SHEHENA YA NCHI JIRANI 224
UCHUKUZI KWENYE MAZIWA 225
Kampuni ya Huduma za Meli *225*
Kampuni ya Meli ya China na Tanzania *225*
HUDUMA ZA MAWASILIANO 226
Shirika la Posta Tanzania *226*
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) *228*
TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO 228
Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano *228*
Maendeleo ya Teknolojia ya Habari *229*
SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU 229
Masijala ya Utafiti Tanzania *229*
Uendelezaji wa Rasilimali Watu *230*
Udhibiti wa Mionzi *230*

SURA YA 17 238

NISHATI 238

KIWANGO CHA UKUAJI 238
UMEME 238
UTAFUTAJI MAFUTA NA GESI 242
UAGIZAJI NA MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA 242
NISHATI MBADALA 243
Maporomoko Madogo ya Maji *243*
Umeme wa Jua *243*
Jotoardhi na Biofueli *243*
MATUMIZI BORA YA NISHATI 243

SURA YA 18 244

MAJI 244

UTANGULIZI 244
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI 244
HUDUMA YA MAJI VIJIJINI 245
HUDUMA ZA MAJI MIJINI 245

SURA YA 19 248

ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI 248

ELIMU YA AWALI 248
ELIMU YA MSINGI 248
ELIMU YA SEKONDARI 249
ELIMU YA UALIMU 250
ELIMU YA WATU WAZIMA 251
UKAGUZI WA SHULE NA VYUO 251

ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO 252
ELIMU YA UFUNDI STADI 252
ELIMU YA JUU 253

SURA YA 20 264

AFYA 264

UTANGULIZI 264
VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA YA AFYA 264
UKAGUZI WA VITUO VYA AFYA 266
MATIBABU NJE YA NCHI 266
ELIMU YA AFYA KWA WANANCHI 266
AFYA YA UZAZI NA MTOTO 266
MUDA WA KUISHI 267
MPANGO WA TAIFA WA KUDHIBITI MALARIA 267
CHAKULA NA LISHE 268
HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII 269

SURA YA 21 273

MAENDELEO YA JAMII 273

VYUO VYA MAENDELEO YA WANANCHI 273
JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE 273
MAENDELEO YA WATOTO 274
URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI 275

Ukurasa

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali A: Takwimu Muhimu Katika Uchumi – Tanzania Bara xix

Jedwali B: Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi, 2002 – 2011…....xx

Jedwali 1: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) 13

Jedwali 1A Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko – Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za miaka inayohusika)..... 14

Jedwali 2: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa kwa Bei za Soko (bei za miaka inayohusika) 15

Jedwali 2A: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko- Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za miaka inayohusika)..... 16

Jedwali 2B: Pato la Taifa (PLT) na Matumizi yake, kwa bei za soko (bei za miaka inayohusika)..... 17

Jedwali 3: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001)..... 18

Jedwali 3A: Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) 19

Jedwali 4: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) 20

Jedwali 4A: Ukuaji wa Pato la Taifa (PLT) kwa shughuli za kiuchumi, kwa Bei za Soko - Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) 21

Jedwali 4B: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko (bei za mwaka 2001) 23

Jedwali 4C: Mchango wa shughuli za kiuchumi kwa Pato la Taifa (PLT), kwa Bei za Soko -Sehemu inayouzika na isiyouzika (bei za mwaka 2001) 26

Jedwali 4D: Pato la Taifa (PLT) na matumizi yake, kwa bei za soko (bei za mwaka 2001) 27

Jedwali 5: Ukuzaji Rasilimali (bei za miaka inayohusika)..... 28

Jedwali 6: Ukuzaji Rasilimali (bei za mwaka 2001) 29

Jedwali 7: Ukuzaji Rasilimali (sekta za umma na binafsi)..... 30

Jedwali 8: Fahirisi ya bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2001=100) 31

Jedwali 9: Fahirisi ya bei za rejereja ya bidhaa zitumiwazo na watu wa kipato cha chini Dar es Salaam (2001=100) 32

Jedwali 10: Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (2001=100)..... 33

Jedwali 11: Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa kima cha kati Dar es Salaam (2001=100)..... 34

Jedwali 12: Fahirisi ya gharama ya maisha ya wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2001=100) 35

Jedwali 13: Fahirisi ya gharama ya maisha wenye kipato cha juu Dar es Salaam (2001=100)..... 36

Jedwali 14: Fahirisi ya bei ya bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2001=100) 37

Jedwali 15: Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini - Tanzania Bara (2001=100) 38

Jedwali 16: Fahirisi mbali mbali za bidhaa na huduma zitumiwazo na wakazi wa mijini – Tanzania Bara (2001=100) 40

Jedwali 17: Thamani ya Bidhaa za biashara baina ya Tanzania na nchi za nje..... 64

Jedwali 18: Kiasi na thamani ya bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje 65

Jedwali 19: Kiasi na thamani ya bidhaa za asilia na zisizo asilia zilizouzwa nchi za nje..... 66

Jedwali 20: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (Sh.)..... 71

Jedwali 21: Wastani wa bei za bidhaa muhimu zilizouzwa nchi za nje (US $)..... 72

Jedwali 23: Aina na thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za nje 74

Jedwali 24: Mizania ya malipo na nchi za nje..... 75

Jedwali 25: Mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali 86

Jedwali 26: Mgawanyo wa Matumizi ya Serikali kwa huduma mbalimbali .. 88

Jedwali 27: Mwenendo wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania bara..... 104

Jedwali 28: Viwango vya ukuaji wa karadha na ujazi wa fedha - Tanzania bara 105

Jedwali 29: Mwenendo wa Viwango vya ubadilishaji kati ya Shilingi na Dola ya Marekani 106

Jedwali 30: Mikopo ya benki za biashara kwa sekta mbalimbali..... 107

Jedwali 31: Mwenendo wa amana katika benki za biashara 108

Jedwali 32: Viwango vya wastani vya riba 109

Jedwali 33: Idadi ya watu nchini Tanzania kimkoa 113

Jedwali 34: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC): Miradi iliyopitishwa 121

Jedwali 35: Uzalishaji wa miwa na sukari 160

Jedwali 36: Pamba iliyonunuliwa na mauzo nchini 161

Jedwali 37: Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana 162

Jedwali 38: Kahawa iliyonunuliwa na mauzo nchini 163

Jedwali 39: Eneo lililopandwa mkonge na katani iliyopatikana 164

Jedwali 40: Tumbaku iliyonunuliwa na mauzo nchini 165

Jedwali 41: Maua ya pareto yaliyonunuliwa na mauzo ya bidhaa za pareto 166

Jedwali 42: Korosho zilizonunuliwa na mauzo nchini. 167

Jedwali 43: Muhtasari wa mazao muhimu ya biashara yaliyonunuliwa 168

Jedwali 45: Idadi ya miti iliyopandwa (Miche iliyooteshwa) Kimkoa 180

Jedwali 47: Mauzo ya bidhaa za misitu nchi za nje 181

Jedwali 48: Mwenendo wa biashara ya ndege, wanyamapori na vipusa nchi za nje 182

Jedwali 48A: Mwenendo wa biashara ya wanyama hai na uwindaji wa kitalii 183

Jedwali 48B: Idadi ya Wawindaji wa Kitalii..... 183

Jedwali 50: Uzalishaji katika sekta ya uvuvi 184

Jedwali 51: Mauzo ya mazao ya uvuvi nchi za nje 185

Jedwali 51A: Muhtasari wa Mauzo ya Mazao ya Uvuvi Nchi za Nje 186

Jedwali 51B: Mwelekeo wa Mauzo ya Sangara Nje ya Nchi 186

Jedwali 52: Mwenendo wa Biashara ya Utalii 187

Jedwali 53: Idadi ya Watalii walioingia nchini na kiasi cha fedha zilizopatikana 188

Jedwali 55: Watalii Waliotembelea Hifadhi za Taifa..... 189

Jedwali 56: Uchimbaji wa madini: Kiasi kilichopatikana 193

Jedwali 57: Madini yaliyouzwa nchi za nje..... 194

Jedwali 58: Matumizi ya saruji nchini..... 198

Jedwali 59: Uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwanda..... 199

Jedwali 60: Viwanda - Idadi ya Watu walioajiriwa 200

Jedwali 61: Viwanda - Gharama za kazi 201

Jedwali 62: Viwanda - Muhtasari wa matokeo 202

Jedwali 63: Viwanda - Muhtasari wa matokeo kimkoa..... 203

Jedwali 65: Vigezo vya Ufanisi katika Sekta ya Viwanda..... 204

Jedwali 67: Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)..... 231

Jedwali 68: Reli ya Uhuru (TAZARA) 232

Jedwali 69: Usafirishaji kwa Meli..... 233

Jedwali 70: Huduma za Posta..... 236

Jedwali 73: Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) 237

Jedwali 74: Uwezo wa mitambo ya umeme na kiasi cha umeme uliotengenezwa kwa vituo…….239

Jedwali 75: Mauzo ya umeme kwa watumiaji mbali mbali 240

Jedwali 76: Mauzo ya umeme kwa mikoa..... 241

Jedwali 77: Uzalishaji wa maji na mapato yatokanayo na maji 247

Jedwali 80: Shule za sekondari za Serikali - Idadi ya wanafunzi kwa kidato 255

Jedwali 81: Shule za sekondari za binafsi - Idadi ya wanafunzi kwa kidato 263

Jedwali 84: Vyombo vya afya nchini 270

Jedwali 85: Huduma za Afya: waliofaulu mafunzo ya Afya..... 271

Jedwali 87: Idadi ya wahitimu wauguzi 272

Jedwali 87A: Idadi ya Vitanda katika hospitali zote nchini 272

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

ASDP	-	Agricultural Sector Development Programme (Program ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo)
ARVs	-	Anti-retrovirals (Dawa za Kupunguza Makali ya UKIMWI)
TAA	-	Tanzania Airpots Authority (Mamlaka ya Viwanja vya Ndege)
AU	-	African Union (Umoja wa Afrika)
BoT	-	Bank of Tanzania (Benki Kuu ya Tanzania)
Cif	-	Cost, insurance and freight (Thamani ya bidhaa ikijumuisha gharama za usafiri na Bima)
CPI	-	Consumer Price Index (Fahirisi ya Bei za Walaji)
CRDB	-	Benki ya CRDB
COICOP	-	Classification of Individual Consumption by Purpose
COMESA	-	Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika)
CUM	-	City Urgent Mail (Kampuni ya usambazaji barua za haraka ndani ya Mji
CHMT	-	Council Health Management Team (Kamati za Afya za Halmashauri)
DSM	-	Dar es Salaam
DSE	-	Dar es salaam Stock Exchange (Soko la Hisa la Dar Es Salaam)
DADPs	-	District Agricultural Development Plan (Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya)
ECA	-	Economic Commission for Africa (Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika)
EAC	-	East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki)
EPZ	-	Export Processing Zones (Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje)
EWURA	-	Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati)
EFD	-	Electronic Fiscal Divices Machines (Mashine za Kielektroniki)
f.o.b	-	free on board (Thamani ya Bidhaa bila Kujumuisha Gharama za Usafiri na Bima
FDI	-	Foreign Direct Investment (Uwekezaji wa Mitaji ya Kigeni)
GEPF	-	Government Employees Provident Fund (Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali)
GBS	-	General Budget Support (Misaada na Mikopo ya Bajeti)
GDP	-	Gross Domestic Product (Pato la Taifa)

HBS	-	Household Budget Survey (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya)
IFS	-	International Financial System
IFMS	-	Integrated Financial Management System (Mfumo Tungamanishi wa Usimamizi wa Fedha)
LSRP	-	Local Sector Reform Programme (Programu ya Maboresho katika Serikali za Mitaa)
LAPF	-	Local Authorities Pensions Fund (Mfuko wa Pension wa Serikali za Mitaa)
LGRP	-	Legal Governments Reform Program (Programu ya Maboresho katika Sekta ya Sheria)
MTEF	-	Medium Term Expenditure Framework (Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Serikali)
M_2	-	Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana)
M_3	-	Extended Broad Money Supply (Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi)
IMF	-	International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa)
MDGs	-	Millenium Development Goals (Malengo ya Maendeleo ya Milenia)
MKUKUTA	-	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania
MPAMITA	-	Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania
MKURABITA	-	Mpango wa Kurasimisha Biashara na Mali za Wanyonge Tanzania
MMEM	-	Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi
MMES	-	Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari
MTN	-	Kampuni ya kutoa huduma za simu za mkononi
MMS	-	MKUKUTA Monitoring System (Mfumo wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA)
MSCL	-	Marine Service Company Ltd (Kampuni ya Huduma za Meli)
MSMEs	-	Medium, Small and Micro Enterprises (Viwanda vya Kati, Vidogo na Vidogo sana)
MUKEJA	-	Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii
MEMKWA	-	Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Waliyoikosa
MMAM	-	Mpango Maalum wa Afya ya Msingi
MW	-	Mega Watts
NDC	-	National Development Corporation (Shirika la Maendeleo la Taifa)
NSSF	-	National Social Security Funds (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii)
NASCAP	-	Anti-Corruption Strategy and Action Plan (Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa)
NGO's	-	Non-Governmental Organisations (Asasi Zisizo ya Kiserikali)
NHIF	-	National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya)

NIC	-	National Insurance Corporation (Shirika la Bima la Taifa)
NMB	-	National Microfinance Bank (Benki ya Taifa ya Mikopo Midogo)
OSBP	-	One Stop Border Posts (Vituo vya Pamoja Mipakani)
PSRP	-	Public Service Reform Program (Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma)
PRS	-	Poverty Reduction Strategy (Mkakati wa Kupunguza Umaskini)
PAP	-	Priority Action Plan (Vipaumbele vya Utekelezaji).
PSPF	-	Public Service Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma)
PPF	-	Parastatal Pensions Fund (Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma)
PFMRP	-	Public Financial Management Reform Program (Program ya Maboresho ya Fedha za Umma)
RAHCO	-	Railway Holding Company (Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli)
TMRC	-	Tanzania Mortgage Refinancing Company (Kampuni ya Utoaji Mikopo ya Nyumba)
RITA	-	Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini)
TAM	-	Tathmini ya Athari kwa Mazingira
TANAPA	-	Tanzania National Parks (Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania)
SAGCOT	-	Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania)
SACCOS	-	Savings and Credit Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo)
SADC	-	Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika)
SMEs	-	Small and Medium Enterprises (Viwanda Vidogo na vya Kati)
SELF	-	Small Enterpreneurs Loan Facility (Mradi wa Kuhudumia Biashara Ndogondogo)
SUMATRA	-	Surface and Marine Transport Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini)
TAKUKURU	-	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TaESA	-	Tanzania Employment Service Agency (Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania)
TANESCO	-	Tanzania Electricity Supply Company (Shirika la Umeme Tanzania)

TANROADS	-	Tanzania Roads Agency (Mamlaka ya Barabara Tanzania)
TAZARA	-	Tanzania Zambia Railway Authority (Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia)
TEUS	-	Twenty Equivalent Units
TDHS	-	Tanzania Demographic and Health Survey (Utafiti wa Afya na Demografia Tanzania)
TIRA	-	Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania)
TCAA	-	Tanzania Civil Aviation Authority (Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania)
TMA	-	Tanzania Meteorology Agency (Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania)
TCRA	-	Tanzania Communications Regulatory Authority (Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania).
TEHAMA	-	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TICTS	-	Tanzania International Container Terminal Services (Kampuni ya Kupakua Makontena katika Bandari ya Dar es Salaam)
TRA	-	Tanzania Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Tanzania)
TRC	-	Tanzania Railways Corporation (Shirika la Reli Tanzania)
TRL	-	Tanzania Railways Company Limited (Kampuni ya Reli Tanzania)
TTCL	-	Tanzania Telecomunications Company Limited (Kampuni ya Simu Tanzania)
UPU	-	Universal Postal Union
UAE	-	United Arab Emirates (Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu)
UFI	-	Global Association of the Exhibition Industry – Fomerly known, Union Des Foires Internationales (Shirika la Maonesho ya Dunia)
UDA	-	Shirika la Usafiri Dar es Salaam
UKIMWI	-	Ukosefu wa Kinga Mwilini
VAT	-	Value Added Tax (Kodi ya Ongezeko la Thamani)
VVU	-	Virusi Vya Ukimwi
WEF	-	World Economic Forum (Mdahalo wa Uchumi Duniani)

MATUKIO MUHIMU YA KIUCHUMI KWA MWAKA 2011

TAREHE	MWEZI	MATUKIO
	Januari	Serikali kupitia kampuni ya kutoa mikopo ya nyumba ya muda mrefu (TMRC) yaanza utekelezaji wa mradi wa kutoa mikopo ya makazi.
08	Juni	Siku ya Bajeti kwa Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki.
07	Juni	Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania azindua kongamano la Kujadili Rasimu ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16).
1-7	Julai	Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yafanyika Dar es Salaam.
09	Julai	Sudani ya Kusini yatangazwa kuwa nchi huru.
02	Oktoba	Sensa ya majaribio yafanyika katika maeneo 44 ya kuhesabia watu.
10	Novemba	Kampuni ya utoaji mikopo ya nyumba ya muda mrefu (TMRC) yaanza rasmi kazi zake.
12	Desemba	Tanzania yaadhimisha miaka 50 ya uhuru.
21	Desemba	Mafuriko makubwa yaikumba jiji la Dar es Salaam ambayo yalisababisha vifo na uharibifu wa mali, Mvua ambazo zilinyesha siku mbili mfululizo. Mvua kubwa kama hiyo mara ya mwisho ilinyesha mwaka 1954.

TAKWIMU MUHIMU KATIKA UCHUMI - TANZANIA BARA

Jedwali Na. A

Maelezo	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011p	2010-11 Badiliko (%)
Idadi ya Watu (milioni)	36.2	37.5	38.3	39.5	40.7	41.9	43.2	3.0
Pato la Taifa kwa Bei za miaka inayohusika (Sh. milioni)	15965294	17941268	20948403	24754457	28212646	32293479	37532962	16.2
Pato la Taifa kwa Bei za mwaka 2001 (Sh. milioni)	12068090	12881163	13801920.84	14828344.81	15721301	16828563	17913803	6.4
Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za miaka inayohusika (Sh.)	441030	478434	547081.1	627097.2	693470.1	770464.3	869436.3	12.8
Wastani Pato kwa Kila Mtu kwa bei za 2001 (Sh.)**	333373	343498	360446	375642	386431	401499	414966	3.4
Kasi ya Upandaji Bei (asilimia)	4.3	7.3	7.0	10.3	12.3	5.5	12.7	130.9
Urari wa Biashara ya Bidhaa (US$ milioni)	-1321.8	-1946.5	-2634.0	-3433.5	-2539.5	-2842.4	-4728.8	66.4
Urari wa Bidhaa,Huduma na Uhamisho wa Mali (US$ milioni)	-867.6	-1143.2	-1580.1	-2595.4	-1727.6	-1863.8	-3967.4	112.9
Saruji Iliyotumika (Tani '000)	1375.2	1421.5	1629.9	1755.8	1940.8	2312.0	2408.8	4.2
Umeme Uliouzwa (KWH milioni)	3623.0	2464.0	3057.0	3369.0	4802.1	5138.0	5153.0	0.3
Utalii (Mapato US$ milioni)	823.0	862.0	1198.0	1354.0	1159.8	1254.5	1324.8	5.6
Reli: Uchukuzi Mizigo (Tani '000)	1639	1330	1283	954	570	805	386	-52.0
Elimu: Wanafunzi katika Shule za Msingi ('000) *	72035.0	79598.8	83169.3	84372.4	84415.5	84193.0	83633.9	-0.7
Elimu: Wanafunzi katika Shule za Sekondari ('000) *	524.3	675.7	1020.5	1222.4	1466.4	1638.7	1711.1	4.4
Hospitali: Idadi ya Vitanda	37048	37228	37228	37228	40118	45241	48480	7.2
Madaktari	-	862	1198	1354	1159.8	578	-	-
Mauzo Nje ya Mazao Muhimu ya Biashara (mil. US$)								
Bidhaa Asilia								
Kahawa	74.30	61.40	98.10	103.32	111.66	117.31	142.60	21.6
Pamba	111.50	55.80	66.40	80.87	111.15	97.79	61.60	-37.0
Katani	7.30	6.10	6.80	0.00	0.00	0.00	0.00	
Chai	25.60	31.00	28.70	41.96	34.50	47.32	47.20	-0.3
Tumbaku	80.80	65.20	72.90	175.92	127.29	129.19	281.20	117.7
Korosho	46.60	39.40	13.20	69.37	71.51	125.34	107.00	-14.6
Karafuu	8.50	8.20	4.20	13.52	14.73	8.14	29.00	256.2
Bidhaa zisizo Asilia								
Madini	711.30	836.80	886.50	42.52	1114.80	1560.10	2284.12	46.4
Bidhaa za Viwanda	156.10	155.90	309.20	94.19	98.70	93.40	861.52	822.4
Bidhaa nyinginezo	454.40	436.30	520.70	2163.84	2163.17	2072.40	347.08	-83.3
	2005/06	**2006/07**	**2007/08**	**2008/09**	**2009/10**	**2010/11**	**2011/12p**	**10/11-11/12 Badiliko (%)**
Ujazi wa Fedha								
Ujazi wa Fedha-M3 (Sh. bilioni) [2]	3266.5	5317.2	6527.8	7834.1	9801.8	11957.9		
Karadha (Sh. bilioni)	1504.2	2169.5	2477.7	4771.7	6124.1	8470.5		
Fedha za serikali								
Mapato ya Kawaida ya Serikali (Sh. bilioni)	2066.8	2739.0	3502.6	4293.1	4661.5	5578.0	6776.0	19.7
Matumizi ya Kawaida ya Serikali (Sh. bilioni)	2649.9	3137.5	3796.9	4681.5	5562.4	6690.3	7714.3	20.3
Matumizi ya Maendeleo ya Serikali (Sh. bilioni)	1385.2	1337.2	2201.1	2130.4	2611.3	2749.0	4925.6	5.3

Chanzo: Wizara ya Fedha

* Kwa shule za serikali na binafsi

** Kuanzia 1998 ni kwa bei za mwaka 2001

[1] Kwa mwaka wa masomo unaoishia mwaka unaohusika

[2] Kwa tafsiri pana (M3)

- Takwimu hazikupatikana

- [P] Takwimu za Awali

Jedwali Na. B: Mwenendo wa Viashiria vya Ukuaji wa Uchumi, 2005 - 2011

	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
PATO LA TAIFA							
Ukuaji halisi wa Pato la Taifa	7.4%	6.7%	7.1%	7.4%	6.0%	7.0%	6.4%
Kilimo, Uwindaji na Misitu	4.3%	3.8%	4.0%	4.6%	3.2%	4.2%	3.6%
Uvuvi	6.0%	5.0%	4.5%	5.0%	2.7%	1.5%	1.2%
Viwanda na Ujenzi	10.4%	8.5%	9.5%	8.6%	7.0%	8.2%	6.9%
Viwanda	9.6%	8.5%	8.7%	9.9%	8.0%	7.9%	7.8%
Ujenzi	10.1%	9.5%	9.7%	10.5%	7.5%	10.2%	9.0%
Huduma	8.0%	7.8%	8.1%	8.5%	7.2%	8.2%	7.9%
Biashara na Matengenezo	6.7%	9.5%	9.8%	10.0%	7.5%	8.2%	8.1%
Mawasiliano	18.8%	19.2%	20.1%	20.5%	21.9%	22.1%	19.0
Fedha	10.8%	11.4%	10.2%	11.9%	9.0%	10.1%	10.7%
Ukuaji wa Pato la taifa katika bei za miaka husika	14.3%	12.4%	16.8%	18.3%	13.8%	14.5%	16.2%
MWENENDO WA BEI							
Kasi ya Upandaji Bei (Wastani wa Mwaka)	5.0%	7.3%	7.0%	10.3%	12.1%	5.5%	12.7%
GDP deflator inflation (market price)	6.4%	5.3%	9.0%	10.1%	7.4%	7.1%	9.5%
Riba za Mikopo ya muda mfupi	15.7%	15.7%	15.0%	13.6%	14.0%	14.4%	13.7%
Riba za Mikopo ya muda mrefu	14.1%	14.9%	16.7%	16.5%	14.5%	146%	14.3%
Riba za Amana (miezi 12)	7.7%	8.8%	10.1%	8.3%	9.0%	7.1%	9.1%
Riba za Akiba	2.6%	2.6%	2.7%	2.7%	2.8%	2.4%	2.9%
FEDHA							
Kiwango cha ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	34.8%	21.5%	20.5%	19.8%	17.7%	25.4%	18.2%
Kiwango cha ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)	33.9%	16.7%	27.2%	24.4%	20.8%	21.8%	15%
Kiwango cha ukuaji wa Mikopo kwa sekta binafsi	29.3%	40.1%	43.1%	44.6%	9.6%	20.0%	27.2%
UWIANO WA MIZANIA YA MALIPO YA NJE NA PATO LA TAIFA							
Bidhaa zilizouzwa nje	11.9%	12.2%	12.0%	15.0%	15.7%	18.8%	21.1%
Bidhaa na huduma zilizouzwa nje	20.9%	22.9%	23.1%	24.7%	24.4%	27.7%	30.9%
Bidhaa zilizonunuliwa toka nje	21.2%	27.1%	28.8%	33.8%	27.3%	31.0%	40.8%
Bidhaa na huduma zilizonunuliwa toka nje	29.8%	35.8%	37.1%	41.8%	35.3%	39.0%	50.0%
Akiba (miezi ya ununuzi toka nje)	6.0	5.0	4.8	4.3	5.6	5.8	4.0
UWIANO WA BAJETI YA SERIKALI NA PATO LA TAIFA							
	2004/05	**2005/06**	**2006/07**	**2007/08**	**2008/09**	**2009/10**	**2010/11**
Mapato	11.9%	12.4%	14.1%	15.9%	16.2%	15.4%	16.6%
Matumizi	29.4%	31.9%	31.7%	22.8%	25.7%	27.0%	26.6%
Matumizi ya kawaida	22.2%	24.2%	24.8%	14.9%	17.7%	18.3%	19.0%
Matumizi ya Maendeleo	7.2%	7.7%	6.9%	7.9%	8.0%	8.6%	7.6%
Nakisi(kabla ya Misaada)	-9.7%	-11.4%	-9.9%	-8.6%	-9.3%	-11.0%	-11.6%
Nakisi (baada ya Misaada)	-4.9%	-5.5%	-4.9%	-1.7%	-4.5%	-6.4%	-6.9%
Mikopo ya Nje	3.9%	3.3%	3.7%	3.2%	3.6%	4.6%	3.4%

Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu

SEHEMU YA KWANZA

MAENDELEO YA UCHUMI JUMLA

SURA YA I

HALI YA UCHUMI WA TAIFA

Ukuaji wa Uchumi

1. Katika mwaka 2011, Pato halisi la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 6.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2010. Kiwango kidogo cha ukuaji kilitokana na hali mbaya ya ukame iliyojitokeza katika sehemu mbalimbali nchini ambapo imeathiri sekta ya kilimo, pamoja na ukosefu wa nishati ya umeme ya uhakika, ambayo ilisababisha kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na shughuli nyingine zinazohitaji nishati.

2. Mwaka 2011, Pato la Taifa lilikuwa shilingi 37,532,962 milioni kwa bei za mwaka husika. Kutokana na idadi ya watu Tanzania Bara kukadiriwa kuwa 43,169,305 pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 869,436.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 770,464.3 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.8.

3. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo kilikuwa asilimia 3.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na kuchelewa kwa mvua za msimu kwa mwaka 2009/10 ambazo ziliathiri uzalishaji wa mazao. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za uzalishaji mazao kilishuka hadi kufikia asilimia 3.5 mwaka 2011 kutoka asilimia 4.4 mwaka 2010 kutokana na kupungua kwa uzalishaji kufuatia kuwepo kwa hali mbaya ya hewa katika msimu wa 2009/10. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za mifugo kilikuwa asilimia 3.9 mwaka 2011 kikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2010. Ufanisi katika utekelezaji wa programu za kuboresha maeneo ya malisho na uimarishaji ubora wa mazao ya mifugo ni miongoni mwa sababu zilizochangia kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji katika sekta hii. Shughuli ndogo za kiuchumi katika misitu na uwindaji zilikua kwa kiwango cha asilimia 3.5 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2010. Hii ilitokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii na hatua ya Serikali kudhibiti uvunaji holela wa mazao ya misitu na hivyo kupunguza uvunaji na uuzaji wa mazao ya misitu.

4. Pato lililotokana na shughuli za kilimo sehemu ya kuuza lilikua kwa kiwango cha asilimia 4.1 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2010, kutokana na kushuka kwa uzalishaji wa mazao kufuatia kuwepo kwa hali mbaya ya hewa. Kwa upande wa kilimo sehemu isiyo ya kuuza, kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 2.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 2.0 mwaka 2010. Katika mwaka 2011, shughuli za kilimo zilichangia asilimia 23.7 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.1 mwaka 2010.

5. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za uvuvi kilishuka kufikia asilimia 1.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2010. Hii ilitokana na kuendelea kutumika kwa vifaa duni vya uvuvi, uharibifu wa mazalia ya samaki na uzalishaji mdogo usiokidhi mahitaji ya soko la dunia sambamba na kuongezeka kwa ushindani katika soko la dunia. Kwa miaka mitatu mfululizo, mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa umeendelea kubaki asilimia 1.4.

6. Shughuli za kiuchumi katika viwanda na ujenzi zilikua kwa asilimia 6.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2010. Kushuka kwa ukuaji huo kulisababishwa na kiwango kidogo cha ukuaji katika shughuli ndogo zote kulikotokana na ukosefu wa nishati ya umeme ya uhakika. Mchango wa shughuli za kiuchumi za viwanda na ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 22.7 mwaka 2011 kutoka asilimia 22.4 mwaka 2010.

7. Kiwango cha ukuaji wa uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 7.8 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2010. Kiwango kidogo cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kutokana na athari za mgawo wa umeme ulioanza katika robo ya nne ya mwaka 2010 ambao kwa kiasi uliathiri shughuli za uzalishaji viwandani; na kuongezeka kwa gharama za uagizaji wa malighafi za viwandani, hususan mafuta. Hata hivyo, uzalishaji kwa baadhi ya bidhaa kama vile chakula na maziwa, saruji, vinywaji na vyakula vya mifugo uliongezeka. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 9.0 mwaka 2010 hadi asilimia 9.3 mwaka 2011.

8. Kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe kilishuka kutoka asilimia 2.7 mwaka 2010 hadi asilimia 2.2 mwaka 2011. Upungufu huo ulitokana na kushuka kwa uzalishaji wa madini katika migodi mikubwa. Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa uliendelea kuwa asilimia 3.3 mwaka 2011 kama ilivyokuwa kwa miaka miwili iliyotangulia.

9. Katika mwaka 2011, shughuli za kiuchumi katika ujenzi zilikua kwa asilimia 9.0 ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2010. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa: barabara na madaraja; majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi; na upanuzi wa miundombinu ya maji na barabara. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.0 mwaka 2011 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

10. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kilipungua kwa kiasi kikubwa kufikia asilimia 1.5 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 10.2 mwaka 2010. Hali hii ilitokana na upungufu wa mvua kwenye vyanzo vya maji ya mabwawa ya Mtera na Kihansi; kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi ambazo zinachangia uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji ya mabwawa ya kufua umeme; uchakavu wa mitambo ya umeme; na kufungwa kwa muda kwa mitambo ya uzalishaji wa umeme wa gesi kupisha ukarabati. Shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi zilichangia asilimia 1.8 katika Pato la Taifa mwaka 2011 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

11. Shughuli za kiuchumi za usambazaji maji zilikua kwa kiwango cha asilimia 4.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2010. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini; uchakavu wa mitambo na ongezeko kubwa la idadi ya watu lililozidi kasi ya ujenzi wa miradi ya maji. Mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa ulipungua kidogo kufikia asilimia 0.3 mwaka 2011 kutoka asilimia 0.4 mwaka 2010.

12. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikuwa asilimia 7.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2010. Hii ilitokana na kupungua kwa viwango vya ukuaji katika shughuli ndogo za huduma isipokuwa shughuli ndogo za huduma za fedha, utawala, na elimu. Sambamba na kushuka kwa kiwango cha ukuaji katika sekta ndogo ya umeme na gesi mwaka 2011, viwango vya ukuaji vilipungua katika sekta ndogo za biashara na matengenezo, hoteli na migahawa na maeneo mengine yanayotegemea nishati ya umeme. Hata hivyo, shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma ndizo zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ukilinganisha na sekta nyingine, ikiwemo sekta ndogo ya mawasiliano iliyokuwa na kiwango cha juu zaidi cha ukuaji cha asilimia 19.0. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 44.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 43.9 mwaka 2010.

13. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo zilikua kwa kiwango cha asilimia 8.1 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2010. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na kuimarika kwa biashara ya kikanda na kuboreka kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini. Hata hivyo, changamoto za umeme ziliathiri shughuli za kibiashara na matengenezo na hivyo kupungza kasi ya ukuaji wake. Shughuli ndogo za biashara na matengenezo zilichangia asilimia 12.2 ya Pato la Taifa mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2010.

14. Shughuli ndogo za mahoteli na migahawa ambazo zinajumuisha utalii zilikua kwa asilimia 4.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2010. Ukuaji huo mdogo ulitokana na kupungua kwa idadi na kiwango cha matumizi ya watalii wa ndani. Mchango wa shughuli ndogo za huduma za mahoteli na migahawa katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.3 mwaka 2011 kama ilivyokuwa miaka miwili iliyotangulia.

15. Shughuli za kiuchumi katika huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Hii ilitokana na kupungua kwa shughuli za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara, reli na anga hususani kwa makampuni ya TRL na ATCL. Hata hivyo,

mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa umeongezeka na kuwa asilimia 5.3 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 5.1 mwaka 2010.

16. Shughuli ndogo za kiuchumi za huduma za mawasiliano zimeendelea kukua kwa kiwango kikubwa zaidi ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi japokuwa kasi ya ukuaji ilipungua mwaka 2011. Kiwango cha ukuaji cha shughuli hizi kilikuwa asilimia 19.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 22.1 mwaka 2010. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa wateja wa huduma za mawasiliano ya simu za mkononi na mauzo ya vocha za simu. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2010.

17. Shughuli ndogo za kiuchumi za huduma za fedha zilikua kwa asilimia 10.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 10.1 mwaka 2010. Ukuaji huu ulitokana na utekelezaji madhubuti wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Fedha uliopelekea kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa na mabenki kwenda sekta binafsi na kuongezeka kwa mahitaji ya kifedha kwa ajili ya uwekezaji, huduma za bima, na za kibiashara na shughuli nyingine za kiuchumi. Mchango wa shughuli za huduma za fedha katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.8 mwaka 2011 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

18. Kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika huduma za upangishaji majengo na biashara ilipungua na kufikia asilimia 6.5 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba za kuishi na zisizo za kuishi katika maeneo mbalimbali nchini. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za kiuchumi za upangishaji wa majengo na huduma za kibiashara sehemu ya kuuza kilikuwa asilimia 6.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2010. Hii ilitokana na kupungua kwa ukuaji wa shughuli za biashara nchini na upangishaji wa majengo. Aidha, upangishaji wa majengo na huduma za kibiashara sehemu isiyo ya kuuza ulikua kwa asilimia 7.1 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2010. Mchango wa shughuli za upangishaji majengo na huduma za biashara katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2010.

19. Katika mwaka 2011, shughuli za utawala zilikua kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2010. Ukuaji huu ulitokana na jitihada za Serikali za kuendelea kugharamia utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma pamoja na kuongezeka kwa ajira mpya serikalini na huduma nyingine za umma. Mchango wa shughuli za utawala katika Pato la Taifa mwaka 2011 umeendelea kuwa asilimia 8.0 kwama ilivyokuwa mwaka 2010.

20. Viwango vya ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu na afya vilikuwa asilimia 7.4 na 5.4 mwaka 2011, ikilinganishwa na asilimia 7.3 na 6.9 mwaka 2010 kwa mtiririko huo. Ukuaji katika shughuli za utoaji huduma za elimu ulitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES); na kuongezeka kwa ajira mpya za walimu. Kwa upande wa shughuli za huduma za afya, ukuaji ulichangiwa na utekelezaji wa programu za chanjo, malaria, kifua kikuu na VVU/UKIMWI. Mchango wa shughuli za huduma za afya katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2010. Aidha, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo, sekta ndogo ya elimu ilikuwa ikichangia asilimia 1.4 katika Pato la Taifa kila mwaka.

Mwenendo wa Bei

21. Katika mwaka 2011, wastani wa kasi ya upandaji bei za bidhaa na huduma ulikuwa asilimia 12.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2010. Kasi hiyo ya ongezeko la bei ilichangiwa hasa na kuendelea kupanda kwa wastani wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia; upungufu wa mvua za vuli katika robo ya nne ya mwaka 2010 ambao ulipunguza mavuno; kupanda kwa bei ya umeme, gesi, mafuta ya kupikia na sukari; upungufu wa nishati ya umeme; kuporomoka kwa thamani ya shilingi; na upungufu wa chakula katika kanda ya Afrika Mashariki kutokana na hali ya ukame. Bei za bidhaa na huduma mbalimbali zimekuwa zikipanda kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji kulikotokana na sababu zilizotajwa hapo juu. Wastani wa ongezeko la fahirisi ya bei ya chakula na vinywaji baridi katika mwaka 2011 ulikuwa asilimia 16.0. Fahirisi ya bei katika makundi mengine makuu ya bidhaa na huduma ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 1 hapo chini. Uchambuzi

umefanyika kwa mwaka 2011 peke yake kwa vile takwimu zilirekebishwa wakati wa zoezi la marejeo ya fahirisi za bei za Taifa yaliyofanyika mwishoni mwa mwaka 2010. Changamoto katika uchambuzi inatokana na ukweli kwamba takwimu mpya za fahirisi za bei zilianza kutumika rasmi mwezi Oktoba, 2010, na hivyo zinakosekana takwimu za mwaka mzima wa 2010 zenye mtiririko na namna sawa ya ukokotoaji za kulinganisha mwenendo wa kasi ya upandaji bei.

Jedwali 1.1: Mwenendo wa Kasi ya Upandaji Bei kwa Makundi Mbalimbali (Jan – Des, 2011)

S/N	MAKUNDI MAKUU	Mizania	Jan/111	Feb/11	Mac/11	Apr/11	Mei/11	Jun/11	Jul/11	Aug/11	Sep/11	Okt/11	Nov/11	Des/11	Wastani
1	Vyakula na Vinywaji baridi	47.8	7.1	9.2	8.6	9.7	10.4	12.3	15.9	18.6	22.5	24.0	26.1	27.1	**16.0**
2	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	3.3	1.8	3.0	2.7	5.6	6.8	5.8	5.0	5.2	5.7	5.6	5.1	5.8	**4.8**
3	Mavazi ya nguo na viatu	6.7	5.8	8.6	9.5	9.4	9.8	9.8	9.4	9.4	9.6	10.7	11.2	10.6	**9.5**
4	Nishati, maji na makazi	9.2	17.7	11.1	13.6	13.4	15.7	18.8	21.3	19.7	21.7	22.0	23.5	24.8	**18.6**
5	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	6.7	7.2	13.9	14.5	13.6	14.1	14.4	14.5	13.9	14.2	15.4	15.3	14.6	**13.8**
6	Gharama za Afya	0.9	0.6	2.1	1.4	1.4	2.1	1.5	1.6	1.9	2.3	4.1	3.5	3.0	**2.1**
7	Usafirishaji	9.5	0.3	0.3	3.3	3.9	8.0	8.4	9.9	8.8	10.8	11.8	12.0	11.2	**7.4**
8	Mawasiliano	2.1	-0.2	-1.3	-1.8	-2.0	-2.2	-2.0	-1.4	-1.3	-1.8	-1.6	-1.7	-1.2	**-1.5**
9	Utamaduni na Burudani	1.3	3.5	3.5	3.8	3.1	2.4	3.6	3.1	2.7	1.1	2.3	3.3	3.2	**3.0**
10	Elimu	1.7	2.2	3.2	2.8	2.2	3.1	3.5	4.2	4.8	5.8	5.6	5.7	5.9	**4.1**
11	Hoteli na migahawa	6.4	2.9	3.9	5.7	5.2	7.4	6.7	6.8	8.0	11.5	12.8	13.2	13.6	**8.1**
12	Bidhaa na huduma nyingine	4.5	4.0	1.1	4.0	3.4	3.8	2.8	3.5	3.5	6.5	7.0	7.8	8.6	**4.7**
	Mfumuko wa Bei		**6.4**	**7.5**	**8.0**	**8.6**	**9.7**	**10.9**	**13.0**	**14.1**	**16.8**	**17.9**	**19.2**	**19.8**	**12.7**
	MAKUNDI MENGINE MAALUM	**Mizania**	**Jan/111**	**Feb/11**	**Mac/11**	**Apr/11**	**Mei/11**	**Jun/11**	**Jul/11**	**Aug/11**	**Sep/11**	**Okt/11**	**Nov/11**	**Des/11**	
1	Chakula	51.0	6.7	8.6	8.3	9.2	10.1	11.7	14.8	17.4	21.3	22.8	24.7	25.6	**15.1**
2	Nishati na Mafuta	5.7	19.1	13.0	17.2	22.1	24.5	29.0	34.2	30.1	33.1	37.4	39.2	41.0	**28.3**
3	Bidhaa zote isipokuwa chakula	49.0	6.1	6.1	7.7	7.8	9.3	10.0	10.8	10.2	11.4	12.2	12.6	12.7	**9.7**
4	Bidhaa zote isipokuwa chakula, nishati na mafuta	43.3	4.4	5.2	6.3	5.7	7.1	7.2	7.4	7.3	8.2	8.5	8.8	8.7	**7.1**

Chanzo: Wizara ya Fedha

22. Kwa ujumla, mfumuko wa bei katika makundi mengine maalum ulikuwa na mwelekeo wa kupanda kila mwezi katika kipindi cha mwaka 2011 kutokana na sababu zilizoelezwa hapo juu. Mfumuko wa bei ya chakula uliongezeka kwa wastani wa asilimia 15.1 mwaka 2011. Kasi ya ongezeko la bei kwa bidhaa zisizo za vyakula imeongezeka hadi asilimia 12.7 kwa mwezi Desemba 2011 kutoka asilimia 4.7 mwezi Desemba 2010. Mfumuko wa bei ya nishati na mafuta umeongezeka kwa asilimia 41.0 kwa mwezi Desemba 2011 ikilinganishwa na asilimia 12.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2010. Kundi hili ndilo lililokuwa na mfumuko wa bei wa juu zaidi kuliko makundi mengine lakini lina uzito kidogo wa asilimia 5.7 kwenye kapu la walaji. Wastani wa mfumuko wa bei wa kundi hili kwa mwaka 2011 ulikuwa asilimia 28.3. Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi Desemba 2011 ulikuwa asilimia 8.7 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwezi Desemba 2010 na wastani wa mfumuko wa bei wa kundi hili kwa mwaka 2011 ulikuwa asilimia 7.1 .

Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Makundi Maalum (Jan – Des, 2011)



23. Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma kwa makundi ya watu kulingana na kipato inaonesha kupungua kwa ongezeko la kasi ya upandaji bei katika makundi ya watu wa tabaka la kipato cha chini na kati. Hii ilitokana na kushuka kwa fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zinazotumiwa kwa wingi na makundi hayo zikiwemo bidhaa na huduma za elimu na hoteli na migahawa. Wastani wa fahirisi ya bei kwa makundi ya kipato cha chini na kati ulikuwa asilimia 7.4 na 7.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 13.2 na 10.0 mwaka 2010[1] kwa mtiririko huo. Katika kundi la watu wa kipato cha juu, wastani wa fahirisi ya bei ulipanda kwa asilimia 10.6 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 2010 kutokana na kuongezeka kwa wastani wa bei za bidhaa na huduma zinazotumiwa zaidi na kundi hili hususani chakula; vinywaji vyenye kilevi na tumbaku; nguo na viatu; nishati, maji na makazi; na hoteli na migahawa.

24. Mwaka 2011, bidhaa na huduma zilikuwa na mwenendo tofauti wa ongezeko la wastani wa fahirisi ya bei kulingana na kundi la watu kimapato kwa wakazi wa Dar es Salaam. Wakati ambapo wastani wa fahirisi ya bei ilikuwa kubwa zaidi katika bidhaa na huduma za mavazi ya nguo (asilimia 17.3) na usafirishaji (asilimia 15.0) kwa wakazi wa Dar es Salaam wa kipato cha chini, wastani huo ulikuwa mkubwa zaidi katika huduma na bidhaa za nishati (asilimia 12.6) na chakula (asilimia 9.1) kwa wakazi wa Dar es salaam wa kipato cha kati, na usafirishaji (asilimia 14.2) na chakula (asilimia 13.5) kwa wakazi wa Dar es Salaam wa kipato cha juu. Hata hivyo, kwa wastani, chakula na nishati ndizo bidhaa zilizoleta athari kubwa zaidi kwa wakazi wa Dar es salaam wa tabaka zote kimapato. Wastani wa fahirisi ya bei katika makundi hayo ya bidhaa na huduma kwa wakazi wa Dar es Salaam wa kipato cha juu, kati na chini kwa mtiririko huo ulikuwa kama ifuatavyo: chakula asilimia 13.5, 9.1, na 7.1; na nishati asilimia 10.9, 12.6 na 7.3. Fahirisi ya bei za bidhaa na huduma zilizobaki zilikuwa na mwenendo unaotofautiana kulingana na tabaka la watu kimapato. Majedwali Na. 8 – 16 yanaonyesha mwenendo wa fahirisi ya bei kwa makundi na sehemu mbalimbali.

[1] Takwimu za mwaka 2010 zimerekebishwa

Ukuzaji Rasilimali

25. Mwaka 2011, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 33.1 kufikia shilingi 13,762,066 milioni kutoka shilingi 10,342,536 milioni mwaka 2010. Aidha, ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2001 uliongezeka kutoka shilingi 4,385,837 milioni mwaka 2010 hadi kufikia shilingi 5,762,294 milioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 31.4. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 36.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 32.0 mwaka 2010.

26. Ukuzaji rasilimali za kudumu unaojumuisha majengo, shughuli nyingine za ujenzi na vifaa kwa bei za mwaka 2001 uliongezeka kwa asilimia 31.4 mwaka 2011 kufikia shilingi 5,694,294 milioni mwaka 2011 kutoka shilingi 4,332,960 milioni mwaka 2010. Ukuzaji rasilimali katika shughuli za ujenzi wa majengo kwa bei za mwaka 2001 uliongezeka hadi kufikia shilingi 1,363,255 milioni mwaka 2011 kutoka shilingi 1,284,866 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Katika mwaka 2011, viwango vya ukuaji wa majengo yasiyo ya kuishi; majengo ya kuishi; na ujenzi vijijini vilikuwa asilimia 6.3; asilimia 6.6; na asilimia 5.4 kwa mtiririko huo, sawa na ilivyokuwa mwaka 2010. Ukuaji huu ulitokana na juhudi za Serikali za kuboresha mazingira ya biashara na kuhamasisha ujenzi wa nyumba bora za kuishi na za biashara.

27. Shughuli nyingine za ukuzaji rasilimali katika ujenzi ikijumuisha uendelezaji ardhi, barabara na madaraja na usambazaji maji ziliongezeka kutoka shilingi 1,004,548 milioni mwaka 2010 hadi shilingi 1,060,483 milioni mwaka 2011 kwa bei za mwaka 2001, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Viwango vya ukuaji katika shughuli za uendelezaji ardhi na usambazaji maji vilikuwa asilimia 5.3 na 6.3 mwaka 2011 sawa na ilivyokuwa miaka miwili iliyotangulia. Hata hivyo, shughuli za ukuzaji rasilimali katika ujenzi wa barabara na madaraja zilikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 9.5 mwaka 2011, ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 10.2 mwaka 2010. Hali hii ilitokana na hatua ya serikali kupunguza matumizi katika ujenzi wa barabara na madaraja ili kugharamia mahitaji ya dharura yaliyojitokeza mwaka 2011 kama vile chakula cha njaa na umeme.

28. Uagizaji vifaa nchini kwa bei za mwaka 2001 uliongezeka kutoka shilingi 2,043,546 milioni mwaka 2010 hadi shilingi 3,270,556 milioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 60.0. Ukuaji huu kwa kiasi kikubwa ulitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa mitambo ya kufulia umeme, majenereta na mitambo mingine katika kukabiliana na tatizo la umeme lililojitokeza mwaka 2011. Ununuzi wa mitambo na vifaa vinginevyo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 98.8 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 8.5 mwaka 2010. Aidha, thamani ya ununuzi wa vifaa vya usafiri iliongezeka kwa kiwango kidogo cha asilimia 6.2 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 27.5 mwaka 2010. Kwa upande mwingine, uagizaji vifaa kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 57.6 kutoka shilingi 3,624,582 milioni mwaka 2010 hadi shilingi 5,711,068 milioni mwaka 2011.

29. Thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za mwaka 2001 ilikuwa shilingi 68,000 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 52,877 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Thamani ya limbikizo la rasilimali kwa bei za miaka husika iliongezeka kwa asilimia 38.3 kutoka shilingi 164,843 milioni mwaka 2010 hadi shilingi 228,000 milioni mwaka 2011.

Robo ya tatu	116.9	103.3	111.9	147.1	106.5	104.2	109.7	101.3	105.1	107.7	102.8	123.2	115.1
Robo ya nne	120.3	103.3	111.9	147.7	107.8	102.3	108.5	101.1	102.3	110.2	102.3	120.6	117.3
2005 Robo ya kwanza	123.3	104.1	111.9	152.3	104.3	107.8	103.4	105.5	109.4	113.1	105.6	120.6	119.7
Robo ya pili	124.3	106.0	111.9	162.9	104.9	109.9	105.0	106.4	110.5	113.2	107.5	121.0	121.3
Robo ya tatu	130.5	109.1	126.7	165.7	105.4	112.1	107.2	107.9	119.2	115.7	109.1	122.7	126.0
Robo ya nne	133.2	109.6	126.5	170.6	105.4	112.9	107.7	106.6	116.7	115.2	110.0	127.3	127.9
2006 Robo ya kwanza	134.5	114.0	129.9	178.7	109.1	126.9	108.4	110.9	118.7	127.6	115.3	123.8	131.5
Robo ya pili	136.7	119.1	132.8	195.1	110.8	131.2	109.0	115.2	114.2	132.7	117.3	119.3	135.2
Robo ya tatu	134.3	126.8	134.3	204.8	110.2	135.3	110.5	118.0	113.4	137.1	116.7	108.5	135.6
Robo ya nne	136.8	130.9	134.3	207.6	113.8	139.1	111.7	118.6	110.9	137.1	119.1	109.8	137.9
2007 Robo ya kwanza	142.5	133.3	146.1	215.7	118.8	144.2	113.6	117.3	114.4	140.0	143.4	106.4	143.2
Robo ya pili	148.7	142.8	146.1	215.1	128.9	148.8	112.6	117.8	118.1	142.0	151.7	106.3	148.7
Robo ya tatu	149.4	144.2	146.1	227.2	134.0	148.6	120.2	114.7	119.3	157.4	157.8	106.1	152.3
Robo ya nne	157.3	150.1	146.1	221.2	135.4	148.1	133.8	117.9	119.5	164.0	156.4	105.3	157.9
2008 Robo ya kwanza	166.4	160.2	195.1	259.4	122.7	163.5	130.5	125.9	124.2	161.4	168.4	103.9	166.5
Robo ya pili	173.8	160.8	195.1	266.9	119.1	167.7	140.7	128.2	129.0	162.1	168.4	104.0	171.4
Robo ya tatu	174.0	165.5	197.9	286.6	120.3	172.9	157.8	132.2	129.5	176.7	182.7	106.9	175.7
Robo ya nne	180.1	171.2	203.5	287.1	121.7	175.6	165.8	137.5	130.6	183.9	179.4	107.8	180.8
2009 Robo ya kwanza	194.7	183.2	206.6	275.9	125.7	178.4	168.5	155.5	132.1	192.1	183.1	109.4	191.1
Robo ya pili	202.1	189.1	206.6	276.2	128.3	179.9	169.9	156.2	135.1	196.5	184.9	109.3	196.7
Robo ya tatu	214.8	195.8	227.8	295.3	134.3	179.6	172.9	170.3	131.5	195.1	203.3	114.4	206.9
Robo ya nne	224.0	196.2	270.1	306.8	136.8	178.6	157.2	187.4	129.7	193.8	217.2	118.9	213.8
Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2010* Robo ya kwanza	98.0	97.4	98.3	95.4	98.3	100.0	99.3	99.6	97.2	100.0	98.7	100.5	97.9
Robo ya pili	99.6	96.3	99.1	96.6	97.7	100.0	99.3	99.5	96.9	100.0	98.8	100.2	99.0
Robo ya tatu	100.0	97.9	99.7	99.0	98.9	100.0	99.6	100.0	100.1	100.0	99.7	100.3	99.8
Robo ya nne	100.8	100.2	100.1	100.6	99.6	100.0	100.1	100.0	99.8	100.0	100.0	99.8	100.5
2011 Robo ya kwanza	105.4	101.1	102.7	105.5	103.3	102.5	102.2	100.0	100.6	99.6	99.0	102.3	104.1
Robo ya pili	107.0	101.9	105.3	110.0	106.7	104.5	103.3	100.0	101.9	99.4	100.2	106.0	106.1
Robo ya tatu	108.9	103.7	105.4	112.3	107.5	104.7	103.5	100.1	102.2	99.8	100.9	108.4	107.7
Robo ya nne	113.3	104.7	105.9	113.2	108.3	104.7	104.3	100.3	103.1	99.9	101.0	109.6	110.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Sept. 2010 kwa kufuata makundi yanayokubalika kimataifa yanayoitwa Mchanganuo wa matumizi Binafsi (COICOP)

FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (2001=100)

Jedwali Na.12

Mwaka	Chakula	Vinyaji na Sigara	Kodi ya Nyumba	Umeme, Mafuta ya Taa, Maji	Nguo na Viatu	Fenicha , Vyombo Vya Ny-	Huduma Mahitaji ya Nyu-mbani	Huduma za Afya	Michezo na Starehe	Usafiri	Elimu	Vinginevyo	Fahirisi Bidhaa Zote
2004 Machi	111.3	112.0	118.0	127.6	112.4	104.2	111.3	101.6	107.2	107.2	107.5	103.4	110.7
Juni	114.2	112.0	118.0	134.6	110.2	109.9	108.7	106.2	107.1	111.4	107.3	105.4	113.5
Septemba	114.6	112.0	118.0	149.2	108.4	113.7	106.9	111.6	107.1	114.7	107.7	104.4	115.4
Desemba	117.7	112.0	118.0	149.6	109.6	115.3	109.2	112.9	112.3	118.7	108.3	101.0	118.0
2005 Machi	120.4	111.9	120.0	153.5	112.0	116.4	101.4	113.3	115.3	119.8	114.1	104.6	120.1
Juni	119.3	111.9	120.0	161.9	113.4	116.7	102.4	114.0	116.8	122.6	114.0	106.3	121.1
Septemba	120.9	116.5	120.0	170.0	113.9	117.3	114.9	117.8	112.3	127.5	117.4	109.6	124.2
Desemba	131.1	116.6	120.0	176.7	114.7	115.5	116.4	126.8	114.8	136.5	117.4	108.0	131.5
2006 Machi	141.1	118.2	120.0	182.7	120.2	119.4	112.8	122.8	106.1	135.2	114.3	112.3	135.4
Juni	144.1	124.0	123.3	188.8	119.8	122.6	113.8	122.4	105.3	136.2	115.1	108.3	137.6
Septemba	141.5	137.2	125.0	200.5	123.9	125.7	115.8	122.7	108.0	140.0	115.4	93.5	139.0
Desemba	145.2	142.3	125.0	204.7	127.7	127.0	121.9	122.5	107.0	147.0	119.2	93.0	143.4
2007 Machi	153.3	144.3	140.0	215.6	131.1	131.2	127.1	120.3	110.0	150.4	152.3	90.9	150.7
Juni	158.3	152.0	140.0	217.0	136.4	131.6	127.3	119.1	110.9	155.7	155.6	92.7	155.3
Septemba	157.8	153.1	140.0	225.2	139.6	130.1	128.7	116.3	111.6	170.8	159.4	88.0	159.7
Desemba	164.9	161.5	140.0	216.8	144.1	129.1	140.1	119.5	112.9	175.6	156.7	81.1	164.2
2008 Machi	177.3	172.0	160.0	253.9	135.2	130.2	142.4	125.8	124.5	178.7	185.1	79.3	174.6
Juni	184.2	171.4	173.3	260.0	135.3	133.8	146.7	128.2	129.5	181.5	185.1	86.1	179.1
Septemba	191.6	182.0	180.0	270.7	128.8	140.5	155.8	131.3	131.8	217.1	188.9	91.1	192.6
Desemba	198.3	192.3	186.7	301.4	130.9	149.4	164.2	135.8	135.4	214.2	190.9	91.8	198.0
2009 Machi	219.8	198.3	200.0	275.0	130.0	157.4	169.0	149.3	191.2	212.7	193.0	92.0	206.3
Juni	225.3	199.3	200.0	275.2	134.5	163.9	170.7	155.0	193.1	210.2	193.3	93.0	208.7
Septemba	237.8	237.8	200.0	293.0	139.7	176.4	180.1	172.5	190.8	225.0	193.5	94.9	220.2
Desemba	247.4	207.4	200.0	305.1	147.2	137.0	163.7	185.5	189.4	228.1	195.9	94.7	225.9
Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirisha ji	Mawasili ano	Utamadu ni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahaw a	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2010* Robo ya kwanza	95.6	95.5	93.9	95.2	96.5	100.0	98.8	99.4	94.4	100.0	99.4	96.1	96.3
Robo ya pili	99.4	100.2	93.3	97.1	97.1	100.0	99.4	99.7	97.1	100.0	99.9	98.7	98.6
Robo ya tatu	99.2	100.4	98.1	101.6	100.3	100.0	100.4	100.0	99.7	100.0	100.7	100.4	100.0
Robo ya nne	100.7	100.7	101.2	100.9	99.2	100.0	101.4	100.0	100.9	100.0	100.1	100.8	100.7
2011 Robo ya kwanza	106.7	102.3	100.8	105.7	101.6	100.9	103.8	100.0	102.1	100.0	102.6	97.2	104.4
Robo ya pili	108.9	103.7	104.7	107.3	104.9	103.8	113.2	100.0	104.4	100.1	109.7	99.1	107.5
Robo ya tatu	112.6	106.3	105.2	110.9	104.2	103.8	118.1	100.2	105.0	100.5	116.0	100.7	110.6
Robo ya nne	120.1	107.2	107.0	113.8	105.9	106.0	121.6	100.5	105.3	100.7	117.3	102.4	114.9

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Sept. 2010 kwa kufuata makundi yanayokubalika kimataifa yanayoitwa Mchanganuo wa matumizi Binafsi (COICOP)

FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR-ES-SALAAM (2001=100)

Jedwali Na 13

Mwaka	M I E Z I				Wastani	Badiliko Asilimia
	Machi	Juni	Sept.	Desemba		
1980		0.5		0.6	0.5	16.7
1981		0.6		0.7	0.6	26.9
1982		0.8		0.9	0.8	27.5
1983		1.0		1.1	1.0	24.2
1984		1.1		1.4	1.2	18.4
1985		1.4		1.7	1.5	23.6
1986		1.9		2.5	2.1	41.2
1987		2.7		3.9	3.1	49.3
1988		4.1		5.2	4.5	41.8
1989		5.6		7.7	6.4	43.8
1990		8.1		9.5	8.5	32.2
1991		10.8		12.3	11.1	31.0
1992		13.6		15.5	14.0	26.0
1993		15.8		19.9	17.1	22.4
1994		21.7		26.0	22.9	34.1
1995	26.2	25.1	26.6	28.6	26.6	16.1
1996	31.8	30.9	31.1	30.9	31.2	17.1
1997	32.9	32.2	32.8	33.5	32.8	5.2
1998	32.9	33.5	33.5	33.8	33.4	1.9
1999	35.2	34.9	36.1	39.2	35.5	6.3
2000	36.7	36.7	38.4	39.2	37.8	6.2
2001	46.9	42.8	41.1	39.2	42.5	12.5
2002	44.0	43.9	43.9	43.9	43.9	6.6
2003	45.4	45.9	45.9	45.9	45.8	4.2
2004	47.1	48.3	49.1	50.2	48.6	6.2
2005	51.1	51.5	52.8	55.9	52.8	8.6
2006	57.5	58.5	59.1	60.9	59.0	11.8
2007	64.1	66.0	67.9	69.5	66.9	13.3
2008	74.2	76.1	81.9	84.2	79.1	18.3
2009	87.7	88.7	93.6	96.0	91.5	15.7
2010*	96.3	98.6	100.0	100.7	98.9	8.1
2011	104.4	107.5	110.6	114.9	109.4	10.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Sept. 2010 kwa kufuata makundi yanayokubalika kimataifa yanayoitwa Mchanganuo wa matumizi Binafsi (COICOP)

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (2001=100)

Jedwali Na.14

Mwaka	Chakula	Vinywaji na Sigara	Kodi ya Nyumba	Umeme, Mafuta ya Taa, Maji	Nguo na Viatu	Fenicha , Vyombo Vya Ny-umbani	Huduma Mahitaji ya Nyu-mbani	Huduma za Afya	Michezo na Starehe	Usafiri	Elimu	Vinginevyo	Fahirisi Bidhaa Zote
2004 Robo ya kwanza	122.8	111.7	107.7	113.2	89.1	95.5	101.6	95.7	91.4	99.7	108.6	92.0	113.9
Robo ya pili	122.8	112.6	108.8	114.1	92.9	94.2	98.6	97.2	85.3	98.4	105.3	93.3	114.0
Robo ya tatu	121.3	111.1	113.7	122.0	91.3	94.7	100.7	94.2	87.0	103.6	106.1	93.8	114.2
Robo ya nne	127.4	110.6	113.8	127.7	89.2	95.2	100.1	92.0	91.8	106.5	101.5	93.4	118.1
2005 Robo ya kwanza	127.9	113.3	118.7	128.8	90.9	96.3	102.1	92.1	93.4	107.2	90.0	93.3	118.7
Robo ya pili	129.5	114.5	122.1	132.9	91.5	96.3	102.4	93.4	92.4	108.2	89.7	93.8	120.2
Robo ya tatu	128.8	116.3	129.5	135.5	93.3	96.2	102.4	97.2	91.9	110.4	89.9	93.5	120.7
Robo ya nne	131.5	120.0	131.5	140.3	95.6	98.1	102.7	105.2	98.2	114.8	94.5	95.1	123.9
2006 Robo ya kwanza	138.6	119.7	128.8	138.2	98.1	100.8	101.0	107.6	98.0	115.3	90.2	102.0	127.9
Robo ya pili	142.4	121.4	131.5	145.5	98.2	102.9	102.7	106.2	97.5	119.1	91.5	101.0	131.3
Robo ya tatu	133.3	127.7	134.5	151.7	99.7	105.9	105.0	107.3	98.3	122.7	94.4	101.6	127.8
Robo ya nne	139.7	131.1	134.5	147.9	101.2	107.6	108.9	110.3	100.8	123.8	96.9	101.3	131.7
2007 Robo ya kwanza	147.3	133.6	136.0	149.1	104.5	111.4	111.6	109.9	105.3	125.9	100.6	101.8	137.0
Robo ya pili	148.2	137.6	136.6	154.7	105.3	112.3	114.0	110.6	106.9	127.8	101.4	103.1	138.7
Robo ya tatu	147.0	138.0	137.5	158.3	105.2	112.4	114.3	110.9	108.5	129.9	102.8	102.0	138.5
Robo ya nne	150.2	143.0	138.3	157.0	105.6	113.8	113.8	112.3	108.9	130.9	104.1	102.2	140.8
2008 Robo ya kwanza	163.4	146.8	138.9	161.6	105.3	116.6	115.1	113.6	110.0	132.9	106.2	103.4	149.2
Robo ya pili	165.1	148.5	139.5	172.0	106.4	118.1	117.1	114.7	111.4	136.5	107.8	103.9	151.7
Robo ya tatu	164.5	149.7	141.6	179.2	106.4	120.1	116.8	117.4	114.5	141.0	110.8	104.2	152.8
Robo ya nne	175.0	152.1	141.6	172.5	108.6	122.1	119.1	120.3	117.6	139.6	112.7	105.2	158.4
2009 Robo ya kwanza	193.5	154.8	156.4	164.5	109.7	124.8	120.7	122.3	121.4	137.7	116.9	106.9	168.7
Robo ya pili	194.0	158.2	156.5	158.7	112.5	126.1	122.7	125.9	121.4	135.3	122.4	108.6	168.9
Robo ya tatu	193.6	165.7	159.4	168.9	115.7	128.0	123.0	126.1	124.6	140.3	122.4	108.3	170.6
Robo ya nne	203.8	170.9	159.6	181.7	115.6	127.1	126.0	126.1	127.6	140.3	122.7	106.3	178.2

Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2010* Robo ya kwanza	100.4	99.7	95.9	92.4	96.5	99.7	101.0	98.8	95.7	102.6	100.7	97.1	98.9
Robo ya pili	101.9	97.7	96.3	97.2	97.7	100.0	100.8	99.4	96.8	102.7	100.7	97.8	100.2
Robo ya tatu	99.9	99.8	98.8	98.9	99.3	100.1	100.4	99.7	98.6	100.8	101.2	100.0	99.8
Robo ya nne	101.3	100.5	100.9	98.9	100.3	99.7	100.5	99.7	98.2	100.1	99.9	99.9	100.6
2011 Robo ya kwanza	108.8	102.1	103.6	105.3	107.9	101.1	102.4	97.7	99.2	105.4	104.9	100.0	106.1
Robo ya pili	112.9	103.6	105.5	112.7	111.4	101.6	107.6	97.4	99.8	105.8	107.1	101.1	109.9
Robo ya tatu	118.9	105.0	108.1	119.5	113.4	102.0	110.3	98.2	100.9	105.8	110.1	104.5	114.5
Robo ya nne	127.3	106.0	111.8	122.1	115.4	103.2	112.2	98.2	101.1	105.8	113.1	107.7	119.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Sept. 2010 kwa kufuata makundi yanayokubalika kimataifa yanayoitwa Mchanganuo wa matumizi Binafsi (COICOP)

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (2001=100)

Jedwali Na.15

Mwaka	Robo ya Mwaka				Wastani wa Fahirisi	Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne		
1980	0.5	0.5	0.6	0.6	0.6	-
1981	0.7	0.7	0.7	0.8	0.7	25.7
1982	0.8	0.9	1.0	1.1	0.9	28.9
1983	1.1	1.2	1.2	1.3	1.2	27.1
1984	1.4	1.5	1.7	1.9	1.6	36.1
1985	2.0	2.1	2.1	2.4	2.2	33.3
1986	2.6	2.6	2.9	3.2	2.9	32.4
1987	3.5	3.5	3.7	4.2	3.7	29.9
1988	4.6	4.6	5.0	5.4	4.9	31.2
1989	5.8	6.2	6.5	6.9	6.4	30.4
1990	8.0	8.2	8.8	9.5	8.6	35.9
1991	10.4	10.9	11.3	12.0	11.1	28.8
1992	13.0	13.1	13.7	14.5	13.6	21.9
1993	15.7	16.6	16.7	18.3	16.8	24.0
1994	20.8	22.4	22.8	25.0	22.8	35.3
1995	28.0	28.4	29.0	30.5	29.0	27.4
1996	35.1	35.3	34.3	35.6	35.1	21.0
1997	40.4	41.2	40.2	41.1	40.7	16.1
1998	46.3	46.4	45.1	46.0	45.9	12.9
1999	50.4	50.2	48.5	49.2	49.6	7.8
2000	53.6	53.2	51.3	52.0	52.5	6.0
2001	56.4	56.0	53.9	54.6	55.2	5.1
2002	57.1	57.5	57.3	58.5	57.6	4.3
2003	59.9	60.6	60.2	61.8	60.6	5.3
2004	62.9	62.9	63.0	65.2	63.5	4.7
2005	65.5	66.4	66.6	68.4	66.7	5.0
2006	70.6	72.4	70.5	72.7	71.5	7.3
2007	75.6	76.5	76.4	77.7	76.6	7.0
2008	82.3	83.7	84.3	87.4	84.4	10.3
2009	93.1	93.2	94.2	98.3	94.7	12.1
2010*	98.9	100.2	99.8	100.6	99.9	5.5
2011	106.1	109.9	114.5	119.7	112.5	12.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Tkwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Sept. 2010 kwa kufuata makundi yanayokubalika kimataifa yanayoitwa Mchanganuo wa matumizi Binafsi (COICOP)


MWENENDO WA KASI YA UPANDAJI BEI - Tanzania Bara
Asilimia
14.0
12.0
10.0
8.0
6.0
4.0
2.0
0.0
4.3
5.3
4.7
5.0
7.3
7.0
10.3
12.1
5.5
12.7
2002
2003
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
2011

FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA (2001=100)

Jedwali Na.16

Mwaka	FAHIRISI			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA	BADILIKO %			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA
	KIPATO CHA				KIPATO CHA			
	CHINI	KATI	JUU		CHINI	KATI	JUU	
1982	1.1	1.0	0.8	0.9	21.8	25.9	25.9	28.9
1983	1.4	1.2	1.0	1.2	23.6	25.1	24.2	27.1
1984	1.6	1.5	1.2	1.6	17.5	25.2	18.4	36.1
1985	2.3	2.2	1.5	2.2	45.1	44.2	23.6	33.3
1986	3.3	3.0	2.1	2.9	42.2	37.3	41.2	32.4
1987	4.2	3.9	3.1	3.7	26.6	30.9	49.3	29.9
1988	5.4	5.2	4.5	4.9	29.5	33.2	41.8	31.2
1989	7.0	6.8	6.4	6.4	30.7	30.1	43.8	30.4
1990	9.3	8.5	8.5	8.6	31.8	25.8	32.2	35.9
1991	12.6	12.0	11.1	11.1	36.0	41.1	31.0	28.8
1992	13.5	14.4	14.0	13.6	7.0	20.2	26.0	21.9
1993	16.6	18.6	17.1	16.8	22.9	29.0	22.4	24.0
1994	24.9	24.9	22.9	22.8	50.5	34.1	34.1	35.3
1995	27.1	31.9	26.6	29.0	8.5	27.9	16.1	27.4
1996	32.4	37.1	31.2	35.1	19.9	16.3	17.1	21.0
1997	34.6	39.4	32.8	40.7	6.8	6.3	5.2	16.1
1998	37.0	41.4	33.4	45.9	6.8	5.0	1.9	12.9
1999	37.3	41.7	35.5	49.6	0.9	0.8	6.3	7.8
2000	38.0	42.7	37.8	52.5	1.7	2.5	6.2	6.0
2001	41.2	44.7	42.5	55.2	8.5	4.5	12.5	5.1
2002	42.8	46.2	43.9	57.6	3.8	3.5	3.3	4.3
2003	45.2	47.3	45.8	60.6	5.8	2.3	4.3	5.3
2004	48.1	51.2	48.6	63.5	6.4	8.2	6.2	4.7
2005	52.1	55.2	52.8	66.7	8.3	7.9	8.6	5.0
2006	58.1	60.3	59.0	71.5	11.5	9.2	11.8	7.3
2007	63.5	67.2	66.9	76.6	9.3	11.5	13.3	7.0
2008	74.5	77.5	79.1	84.4	17.3	15.3	18.3	10.3
2009	87.0	90.3	91.5	94.7	16.8	16.4	15.7	12.1
2010*	98.6	99.3	98.9	99.9	13.2	10.0	8.1	5.5
2011	105.9	107.1	109.4	112.5	7.4	7.9	10.6	12.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Sept. 2010 kwa kufuata makundi yanayokubalika kimataifa yanayoitwa Mchanganuo wa matumizi Binafsi (COICOP)

SURA YA 2

HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

HALI YA UCHUMI DUNIANI

Ukuaji wa Uchumi Duniani

31. Matumaini ya kuendelea kutengemaa kwa uchumi wa dunia baada ya mtikisiko wa uchumi duniani yalianza kufifia mwaka 2011. Katika kipindi hicho, kasi ya ukuaji wa Pato la dunia ilipungua hadi kufikia asilimia 3.9 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 5.3 mwaka 2010. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa Pato la Dunia kulitokana na kudorora kwa uchumi wa Marekani na nchi za bara la Ulaya sanjari na tishio la msukosuko wa madeni unaoikumba baadhi ya nchi za Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Aidha, tetemeko kubwa la ardhi lililosababisha tsunami Mashariki ya Japani, kusambaa kwa vurugu za kisiasa Kaskazini mwa Afrika na Mashariki ya Kati na ongezeko la muda kwa bei ya mafuta katika robo ya pili ya mwaka 2011 kuliongeza changamoto kwa ukuaji wa Pato la Dunia.

32. Kasi ya ukuaji Pato la Nchi Zilizoendelea ilipungua hadi kufikia asilimia 1.6 mwaka 2011, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.2 mwaka 2010. Kwa upande wa Nchi Zinazoendelea, kasi ya ukuaji ilipungua na kuwa asilimia 6.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.5 mwaka 2010. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na utekelezaji wa mikakati iliyochukuliwa na nchi hizo ya kupunguza nakisi ya bajeti na kudhibiti ujazi wa fedha ikiambatana na vyazo hafifu vya kukuza uchumi. Aidha, kasi ya ukuaji wa Pato la Nchi za Asia Zinazoendelea za China na India ilipungua kufikia asilimia 7.8 mwaka 2011 kutoka asilimia 9.7 mwaka 2010. Hali hii kwa kiasi fulani ilitokana na kukwama kwa mlolongo wa ugavi wa bidhaa duniani ikiambatana na kutokuwepo kwa soko la uhakika la bidhaa kutoka Nchi Zilizoendelea.

Jedwali Na 2.1: Pato la Dunia 2004 – 2011

	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Ukuaji kwa asilimia								
Pato la Dunia	5.1	4.6	5.2	5.4	2.8	-0.6	5.3	3.9
Nchi Zilizoendelea	3.1	2.6	3.0	2.8	0.0	-3.6	3.2	1.6
Nchi Zinazoendelea	7.5	7.3	8.2	8.7	6.0	2.8	7.5	6.2
Nchi za Asia Zinazoendelea	8.5	9.5	10.3	11.4	7.8	7.1	9.7	7.8
Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara	7.1	6.2	6.4	7.1	5.6	2.8	5.3	5.1

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Aprili 2012

Mwenendo wa Biashara Duniani

33. Mwaka 2011, mwenendo wa ukuaji wa biashara duniani ulipungua hadi kufikia asilimia 5.0 kutoka ukuaji wa asilimia 13.8 mwaka 2010. Kupungua kwa ukuaji wa biashara duniani kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo vurugu za kisiasa kwa baadhi ya nchi za Kiarabu kama vile Libya na Misri ambazo zilisababisha ukuaji wa mauzo nje ya Afrika kupungua. Aidha, matetemeko ya ardhi yaliyoambatana na tsunami huko Japani yalikwamisha mlolongo wa ugavi kwa biashara katika Nchi Zinazoendelea kama vile China na hatimaye kupunguza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo nje ya nchi.

34. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje duniani ilikuwa dola za Kimarekani 18.0 trilioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 15.1 trilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 19.0. Ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa nje lilitokana na kupanda kwa bei za bidhaa hizo kwenye soko la dunia. Aidha, kwa nchi za Afrika, thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 17.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 30.0 mwaka 2010. Thamani ya uagizaji kwa nchi za Afrika iliongezeka kwa asilimia 18.0 mwaka 2011 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.0 mwaka 2010. Kutokana na mwenendo huu wa biashara, nchi za Afrika zilipata ziada katika urari wa biashara ya bidhaa nje yenye thamani ya dola za Kimarekani 42.0 bilioni mwaka 2011 ikilinganishwa na urari wa biashara wa ziada ya dola za Kimarekani 37.0 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 13.5.

Jedwali Na.2.2: Mwenendo wa Biashara Duniani (Thamani - USD bilioni na Asilimia)

	Mauzo ya Nje					Manunuzi kutoka Nje				
	Thamani	*Badiliko kwa mwaka (Asilimia)*				*Thamani*	*Badiliko kwa mwaka (Asilimia)*			
	2011	**2005-11**	**2009**	**2010**	**2011**	**2011**	**2005-11**	**2009**	**2010**	**2011**
Dunia	**17,779**	**10.0**	**-23.0**	**22.0**	**20.0**	**18,000**	**9.0**	**-23.0**	**21.0**	**19.0**
Amerika ya Kaskazini	**2,283**	**8.0**	**-21.0**	**23.0**	**16.0**	**3,090**	**5.0**	**-25.0**	**23.0**	**15.0**
Marekani	1,481	9.0	-18.0	21.0	16.0	2,265	5.0	-26.0	23.0	15.0
Canada	452	4.0	-31.0	23.0	17.0	462	6.0	-21.0	22.0	15.0
Mexico	350	9.0	-21.0	30.0	17.0	361	8.0	-24.0	28.0	16.0
Amerika ya Kusini na Kati	**749**	**13.0**	**-23.0**	**26.0**	**27.0**	**727**	**16.0**	**-25.0**	**30.0**	**24.0**
Brazil	256	14.0	-23.0	32.0	27.0	237	20.0	-27.0	43.0	24.0
Nchi nyingine za Amerika ya Kusini na Kati	493	12.0	-24.0	22.0	27.0	490	14.0	-25.0	24.0	25.0
Ulaya	**6,601**	**7.0**	**-22.0**	**12.0**	**17.0**	**6,854**	**7.0**	**-25.0**	**13.0**	**17.0**
Umoja wa Nchi za Ulaya	6,029	7.0	-22.0	12.0	17.0	6,241	7.0	-25.0	13.0	16.0
Ujerumani	1,474	7.0	-23.0	12.0	17.0	1,254	8.0	-22.0	14.0	19.0
Ufaransa	597	4.0	-21.0	8.0	14.0	715	6.0	-22.0	9.0	17.0
Uholanzi	660	8.0	-22.0	15.0	15.0	597	9.0	-24.0	17.0	16.0
Uingereza	473	4.0	-23.0	15.0	17.0	636	4.0	-24.0	16.0	13.0
Italia	523	6.0	-25.0	10.0	17.0	557	6.0	-26.0	17.0	14.0
Jumuiya ya Madola ya Nchi huru (CIS)	**788**	**15.0**	**-36.0**	**31.0**	**34.0**	**540**	**17.0**	**-33.0**	**24.0**	**30.0**
Shirikisho la Urusi	522	14.0	-36.0	32.0	30.0	323	17.0	-34.0	30.0	30.0
Afrika	**597**	**11.0**	**-30.0**	**29.0**	**17.0**	**555**	**14.0**	**-15.0**	**15.0**	**18.0**
Afrika ya Kusini	97	11.0	-24.0	31.0	20.0	122	12.0	-27.0	27.0	29.0
Afrika bila Afrika ya Kusini	500	12.0	-31.0	29.0	17.0	433	14.0	-12.0	12.0	15.0
Wauza mafuta Nje	331	11.0	-38.0	34.0	15.0	160	15.0	-9.0	8.0	11.0
Wasiouza Mafuta Nje	169	13.0	-14.0	21.0	20.0	274	14.0	-14.0	15.0	18.0
Mashariki ya Kati	**1,228**	**15.0**	**-31.0**	**27.0**	**37.0**	**665**	**12.0**	**-15.0**	**13.0**	**16.0**
Asia	**5,534**	**12.0**	**-18.0**	**31.0**	**18.0**	**5,568**	**13.0**	**-20.0**	**33.0**	**23.0**
China	1,899	16.0	-16.0	31.0	20.0	1,743	18.0	-11.0	39.0	25.0
Japan	823	6.0	-26.0	33.0	7.0	854	9.0	-28.0	26.0	23.0
India	297	20.0	-15.0	33.0	35.0	451	21.0	-20.0	36.0	29.0
Nchi zinazochipukia kiviwanda	1,290	10.0	-17.0	30.0	16.0	1,302	10.0	-24.0	32.0	18.0
Nchi Masikini Duniani	**203**	**16.0**	**-25.0**	**28.0**	**25.0**	**202**	**15.0**	**-5.0**	**11.0**	**19.0**

Chanzo: Shirika la Biashara Duniani (WTO) Aprili 2012

Hali ya Uchumi wa Nchi za Afrika

35. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika ilipungua mwaka 2011 kutokana na vurugu za kisiasa katika nchi za Kaskazini mwa Afrika na kuendelea kudorora kwa uchumi wa Nchi Zilizoendelea. Vurugu za kijamii na kisiasa Kaskazini mwa Afrika ziliwavunja moyo wawekezaji na hivyo kupunguza mitaji kutoka nje na uwekezaji binafsi. Aidha, uzalishaji na uuzaji nje wa mafuta ambayo ndio nguzo ya uchumi wa nchi za Kaskazini mwa Afrika ulivurugika vibaya na utalii kuanguka. Kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka mitano, kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi zinazouza mafuta nje kwa bara la Afrika ilikuwa ya chini ikilinganishwa na ukuaji kwa nchi zinazoagiza mafuta. Kasi ya ukuaji kwa kundi linalouza mafuta nje ilipungua kutoka asilimia 5.1 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 1.5 mwaka 2011, licha ya kuwepo kwa ongezeko la mapato ya mafuta kutokana na kupanda kwa bei.

36. Mwaka 2011, kasi ya ukuaji wa Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ilipungua hadi kufikia asilimia 5.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka 2010. Kasi ndogo ya ukuaji ilitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji kwa nchi zinazouza mafuta nje ambapo kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 6.3 mwaka 2011, kutoka ukuaji wa asilimia 6.5 mwaka 2010.

37. Kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi za kipato cha kati Kusini mwa Jangwa la Sahara nacho kilipungua kidogo kutoka asilimia 3.1 mwaka 2010 hadi asilimia 3.0 mwaka 2011. Vile vile, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za kipato cha chini Kusini mwa Jangwa la Sahara kiliongezeka kutoka asilimia 5.3 mwaka 2010 hadi asilimia 5.8 mwaka 2011. Kwa wastani, ukuaji wa Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulionesha mwelekeo mzuri wa kuendelea kuimarika baada ya msukosuko wa fedha na uchumi duniani wa mwaka 2009.

38. Mwaka 2011, kasi ya ukuaji wa bei za mlaji kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara iliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 8.2 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2010. Kasi hiyo ya ukuaji wa bei za mlaji ilijionesha pia kwa nchi za kipato cha kati na zile za kipato cha chini kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Ongezeko hilo la wastani wa bei lilitokana hasa na kupanda kwa bei za chakula na mafuta katika soko la dunia. Hata hivyo, nchi zinazouza mafuta nje zilionesha mwenendo tofauti ambapo kasi ya ukuaji wa bei za mlaji ilipungua na kuwa asilimia 10.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 12.4 mwaka 2010.

Jedwali Na.2.3: Mwenendo wa Baadhi ya Viashiria vya Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara: 2009 – 2011

	Pato halisi la Taifa			Bei za Mlaji			Urari wa Biashara ya Nje		
	Ukuaji kwa mwaka			*Ukuaji kwa mwaka*			*Sehemu ya pato la taifa*		
	2009	2010	2011	2009	2010	2011	2009	2010	2011
Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara	**2.8**	**5.3**	**5.1**	**10.6**	**7.4**	**8.2**	**-3.1**	**-2.4**	**-1.8**
Nchi zinazouza mafuta	**4.8**	**6.5**	**6.2**	**11.0**	**12.4**	**10.2**	**5.3**	**2.6**	**5.6**
Nigeria	7.0	8.0	7.2	12.5	13.7	10.8	7.9	1.3	6.2
Angola	2.4	3.4	3.4	13.7	14.5	13.5	-8.9	10.4	8.1
Equatorial Guinea	5.7	-0.8	7.1	7.2	7.5	7.3	-17.1	-24.1	-9.7
Gabon	-1.4	6.6	5.8	1.9	1.4	1.3	6.3	9.1	12.0
Jamhuri ya Kongo	7.5	8.8	4.5	4.3	5.0	1.9	-7.4	5.1	6.2
Chad	-1.2	13.0	1.6	10.1	-2.1	1.9	-4.0	-3.5	-17.7
Nchi za Kipato cha Kati	**-1.7**	**3.1**	**3.0**	**7.1**	**4.4**	**5.4**	**-4.1**	**-3.1**	**-3.8**
Afrika ya Kusini	-1.5	2.9	3.1	7.1	4.3	5.0	-4.0	-2.8	-3.3
Botswana	-4.9	7.2	4.6	8.1	6.9	8.5	-5.8	-5.2	-6.8
Ghana	4.0	7.7	13.6	19.3	10.7	8.7	-3.2	-7.3	-10.0
Cameroon	2.0	2.9	4.1	3.0	1.3	2.9	-3.7	-2.8	-3.5
Cote d'Ivoire	3.7	2.4	-4.7	1.0	1.4	4.9	7.0	1.1	6.7
Senegal	2.1	4.1	2.6	-1.7	1.2	3.4	-6.7	-6.1	-8.3
Nchi za Kipato cha Chini	**4.7**	**5.3**	**5.8**	**13.5**	**6.2**	**10.6**	**-6.8**	**-7.0**	**-9.7**
Ethiopia	10.0	8.0	7.5	36.4	2.8	18.1	-5.0	-4.4	-0.2
Kenya	2.6	5.6	5.0	10.6	4.1	14.0	-5.7	-6.5	-11.8
Tanzania	6.7	6.5	6.7	11.8	10.5	7.0	-10.7	-9.3	-9.7
Uganda	7.2	5.9	6.7	14.2	9.4	6.5	-8.7	-9.6	-11.1
Jamhuri ya Kongo	2.8	7.0	6.9	46.2	23.5	15.5	-10.5	-6.9	-8.7
Mozambique	6.3	6.8	7.1	3.3	12.7	10.4	-12.2	-11.7	-13.0

Chanzo:-Shirika la Fedha Duniani (IMF) Aprili 2012.

USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA

Jumuiya ya Afrika Mashariki

39. Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walikutana mwezi Aprili 2011 katika Mkutano ambao waliagiza kufanyika kwa utafiti juu ya namna ya kuanzisha Himaya Moja ya Forodha (Single Customs Territory). Utekelezaji wa agizo hilo ulianza mwezi Oktoba 2011 na ulitarajiwa kukamilika mwezi Aprili 2012. Aidha, katika kupunguza vikwazo vya biashara visivyo vya kiforodha, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikamilisha mfumo wa kisheria wa uanzishaji Vituo vya Pamoja Mipakani (One-Stop-Border Posts – OSBPs). Mshauri elekezi aliyepewa kazi ya kufanya Utafiti wa Kuwiainisha Uzito wa Magari aliwasilisha Ripoti ya Awali mwezi Februari 2011. Nchi wanachama wa Jumuiya wanaendelea kuichambua ripoti hiyo kuhusu kuwiainisha uzito wa magari yanayotumika ndani ya Jumuiya.

40. Katika utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya, Nchi Wanachama hazitakiwi miongoni mwao kujiwekea vikwazo vya kibiashara vya forodha na visivyo vya forodha. Kufuatia hali ya uhaba wa chakula na sukari iliyojitokeza mwaka 2011 miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya, Tanzania iliimarisha ulinzi katika maeneo ya mipakani ili kudhibiti uuzaji nje wa bidhaa hizo kwa njia zisizo halali. Hata hivyo, hatua hii ilitafsiriwa na Nchi Wanachama kuwa ni vikwazo vya biashara (Non Trade Barriers - NTB). Sambamba na hilo, Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Kilimo na Usalama wa Chakula lilikutana miezi ya Agosti na Novemba, 2011 mjini Arusha kujadili hali

ya chakula katika Jumuiya na pia uondoaji vikwazo katika biashara ya chakula na mbegu. Katika mikutano hiyo, Nchi Wanachama zilikubaliana kuwa kila nchi ifanye uhakiki wa hali ya chakula na kuwasilisha taarifa zao katika Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Sekretarieti iliagizwa kuandaa mapendekezo ya kutafuta fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Jumuiya wa Usalama wa Chakula.

41. Mkutano Mkuu wa 13 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanyika mwezi Novemba 2011 huko Bujumbura, ambapo Rais wa Burundi Mheshimiwa Pierre Nkurunziza alimkabidhi Uenyekiti wa Jumuiya Rais wa Kenya Mheshimiwa Mwai Kibaki. Mkutano huo ulipokea na kuidhinisha Ripoti ya Timu ya Wataalam kuhusu kero, hofu na changamoto za kisiasa na kuiagiza Sekretarieti ya Jumuia kutekeleza maandalizi ya Mpango Kazi wa kuanzisha na kuimarisha Taasisi zilizopendekezwa na Timu ya Wataalam. Miongoni mwa Taasisi zilizopendekezwa ni Mamlaka ya Mapato ya Jumuiya; Mamlaka ya Soko la Pamoja la Jumuiya; Tume ya Muungano wa Kiuchumi kwa Nchi za Jumuiya; Mamlaka ya Muungano wa Fedha kwa Nchi za Jumuiya; Hazina ya Pamoja kwa Nchi za Jumuiya, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Bunge la Afrika Mashariki.

42. Katika azma ya kuwa na miundombinu imara na ambayo itarahisisha uchukuzi na usafirishaji wa bidhaa na watu ndani ya Jumuiya, miradi na programu za miundombinu ya uchumi zimeendelea kutekelezwa. Kwa upande wa Tanzania, miradi iliyotekelezwa mwaka 2011 ni ile ya ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – Athi River yenye urefu wa kilometa 104.4 ambayo imekamilika kwa kuwekewa lami na madaraja yote 39 kujengwa. Ujenzi wa barabara ya Malindi – Lunga Lunga na Tanga – Bagamoyo yenye jumla ya kilometa 400 ambapo kwa upande wa Tanzania ina urefu wa kilometa 240 ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Mradi mwingine ni wa ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro wenye urefu wa kilometa 65 unaoendelea na kufikia asilimia 67.5 hadi mwishoni mwa mwaka 2011.

Umoja wa Afrika na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika

43. Migogoro ya kijamii na kisiasa iliyotokea katika nchi za Kaskazini mwa Bara la Afrika pamoja na kudorora kwa uchumi wa dunia kulichangia kupunguza fursa za ajira barani Afrika. Aidha, uchumi wa Afrika ulikua kwa kiwango kidogo cha asilimia 2.7 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2010, ukuaji ambao haujaweza kutoa fursa za ajira na usawa wa mgawanyo wa rasilimali. Kwa kuzingatia hali hiyo, Umoja wa Afrika (AU) na Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika (ECA) katika kikao chake cha nne cha

pamoja kilichofanyika Addis Ababa, Machi 2011, kilijadili namna ya kuongoza maendeleo ndani ya Afrika kwa kuzingatia wajibu wa Serikali katika mageuzi ya kiuchumi. Katika mjadala huo, kulikuwa na mambo makuu matatu ya kuzingatia ambayo ni kuwa na uchumi wa kijani ambao unalenga kuinua hali za maisha bila kuharibu rasilimali kwa ajili ya kizazi kijacho; kugharamia afya na kuongeza fursa za ajira; na kuchochea ukuaji wa uchumi.

44. Katika kikao hicho, nchi za Afrika zilikubaliana vipaumbele muhimu katika kipindi cha miaka kumi ijayo. Vipaumbele hivyo ni: kuhamasisha ukusanyaji wa rasilimali; kukabiliana na changamoto za miundombinu; kuwajengea wananchi uwezo wa kielimu; kuimarisha Jumuiya za Mtengamano (RECs) na biashara ndani ya Afrika; na kuimarisha ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma. Aidha, masuala yaliyojitokeza katika mjadala huo ni kwamba mfumo wa soko peke yake hautoshi kufanya mageuzi ya kiuchumi bali Serikali ina wajibu wa kuongoza mageuzi hayo. Vile vile, Serikali ni muhimu ziwe na utashi na uwezo wa kisiasa katika kuelekeza na kutekeleza sera za mabadiliko na ukuaji. Mwisho, nchi za Afrika ziwe na ushirikiano imara wa kikanda na kibara kwa kuwa na taasisi na utaratibu katika kuratibu, kutekeleza na kusimamia sera za ushirikiano.

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika

45. Mwaka 2011, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ilishiriki katika mkutano wa pamoja wa eneo huru la biashara kwa Jumuiya Tatu za Afrika Mashariki (EAC), Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Soko la Pamoja la Nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) jijini Johannesburg. Mkutano huo wa pamoja ulijadili uunganishwaji wa masoko kwa nchi 26 ambazo zinakadiriwa kuwa na jumla ya wakazi wapatao milioni 600. Uanzishaji wa eneo huru la biashara kwa Jumuiya Tatu (Tripartite) utaimarisha biashara miongoni mwa nchi za Jumuiya hizo kwa kupanua wigo wa soko, kuongeza uwekezaji, kuzidisha ushindani na kuendeleza miundombinu ndani ya Jumuiya hizo. Ujenzi wa miundombinu utaboresha muunganiko na kupunguza gharama za kufanya biashara na vile vile utarahisisha ujenzi wa viwanda ili kukabiliana na tatizo la uzalishaji.

46. Katika hatua nyingine, SADC ilishiriki katika mkutano wa kwanza kuhusu baraza la kujadili biashara kwa Jumuiya Tatu uliofanyika Nairobi, Kenya mwezi Desemba 2011. Dhumuni la mkutano huo lilikuwa kuanzisha rasmi baraza la majadiliano ya kibiashara kwa Jumuiya tatu za COMESA, EAC na SADC. Aidha, mkutano huo ulijadili mipangilio ya kiutawala ambayo itasaidia majadiliano katika Eneo Huru la Biashara kwa Jumuiya hizo.

Shirikisho la Biashara Ulimwenguni

47. Mwaka 2011, Urusi ilipatiwa idhini ya kuwa mwanachama wa Shirikisho la Biashara Ulimwenguni (WTO) baada ya jitihada zake za kujiunga na Shirikisho kwa kipindi cha takribani karne mbili. Kabla ya hapo, Urusi ilikuwa miongoni mwa nchi sita zenye uchumi mkubwa duniani na mwanachama pekee wa kundi la nchi 20 zinazoongoza kiuchumi duniani iliyokuwa nje ya nchi 153 wanachama wa WTO. Uanachama wa Urusi utachochea ukuaji wa biashara duniani, hususan mauzo ya bidhaa nje (gesi na mafuta) kwa Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU) na uagizaji wa bidhaa za Ulaya kwa bei nafuu.

48. Mwezi Julai 2011, Shirikisho la Biashara Ulimwenguni lilifanya kikao cha tatu mjini Geneva kufanya mapitio ya msaada wa kibiashara duniani ikishirikisha wanachama wake na taasisi za misaada na maendeleo za kimataifa. Msaada huo wa kibiashara unalenga kuzisaidia nchi zinazoendelea na ambazo ziko nyuma kimaendeleo kuongeza uuzaji wa bidhaa na huduma nje, kuziunganisha na miundo ya biashara za kimataifa, kuzinufaisha na biashara huria na kuongeza fursa za kupata masoko. Aidha, msaada huo ulilenga kuzisaidia nchi hizi kukabiliana na changamoto zinazokwamisha uzalishaji, kujenga miundombinu ya kiuchumi na kuongeza ushindani.

SURA YA 3

SEKTA YA NJE

Utangulizi

49. Mwaka 2011, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje ulikuwa wa kuridhisha, japokuwa ulikabiliwa na changamoto za kupungua kwa uzalishaji viwandani na kupungua kwa bei na mahitaji ya bidhaa nje kutokana na matatizo ya madeni katika nchi za Jumuiya ya Ulaya. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 17.1 ambazothamani ya mapato ya bidhaa zilizouzwa nje yaliongezeka kwa asilimia 17.9. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa mwaka 2011 iliongezeka kwa asilimia 33.0, sehemu kubwa ikiwa ni ongezeko la uagizaji wa mafuta.

Bidhaa Zilizouzwa Nje

50. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 5,098.8 milioni ikilinganishwa na dola 4,323.1 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 17.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia. Aidha, mauzo hayo yanajumuisha bidhaa zisizorekodiwa zilizokuwa na thamani ya dola za Kimarekani 664.9 milioni mwaka 2011. Mchango wa mauzo ya bidhaa asilia katika mauzo yote ya bidhaa nje kwa mwaka 2011 ulikuwa asilimia 13.1, bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 73.8 na bidhaa zisizorekodiwa zilikuwa asilimia 13.0.

Bidhaa Asilia

51. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka kwa asilimia 16.8 hadi dola za Kimarekani 668.7 milioni kutoka dola 572.3 milioni mwaka 2010 . Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha bidhaa zilizouzwa nje hasa mazao ya tumbaku na kahawa, sambamba na kupanda kwa bei ya kahawa, karafuu na korosho katika soko la dunia. Bei ya karafuu katika soko la dunia ilipanda na kufikia wastani wa dola za Kimarekani 13,087.3 kwa tani kutoka dola 3,449.6 kwa tani mwaka 2010. Ongezeko hili kubwa lilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa zao la karafuu katika nchi ya Indonesia, ambayo ni moja ya nchi zinazozalisha zao la karafuu kwa wingi duniani. Mauzo ya bidhaa asilia yalichangia asilimia 13.1 ya mauzo yote ya bidhaa nje ikilinganishwa na asilimia 13.2 mwaka 2010.

Kahawa

52. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya kahawa nje iliongezeka kwa asilimia 40.3 hadi dola za Kimarekani 142.6 milioni kutoka dola za Kimarekani 101.6 milioni mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha kahawa iliyouzwa nje na kuongezeka kwa wastani wa bei ya kahawa katika soko la dunia. Wastani wa bei ya kahawa ulikuwa dola za Kimarekani 3,654.9 kwa tani mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 2,853.1 kwa tani mwaka 2010. Vilevile, kiasi cha kahawa iliyouzwa nje kiliongezeka kutoka tani 35,600 mwaka 2010 hadi tani 39,000 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 9.5.

Pamba

53. Mwaka 2011, thamani ya mauzo pamba nje iliendelea kupungua hadi dola za Kimarekani 61.6 milioni kutoka dola 84.0 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 26.6. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa kiasi cha pamba kilichouzwa nje licha ya kwamba wastani wa bei ya pamba uliongezeka katika soko la dunia. Kiasi cha pamba kilichouzwa nje kilipungua kutoka tani 67,600 mwaka 2010 hadi tani 40,300 mwaka 2011, sawa na upungufu wa asilimia 40.4. Hata hivyo, wastani wa bei ya pamba katika soko la dunia uliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,529.0 kwa tani mwaka 2011 kutoka dola za Kimarekani 1,241.9 kwa tani mwaka 2010.

Chai

54. Thamani ya mauzo ya chai nje ilipungua hadi dola za Kimarekani 47.2 milioni mwaka 2011 kutoka dola za Kimarekani 49.8 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 5.3. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa wastani wa bei ya chai katika soko la dunia. Wastani wa bei ya chai katika soko la dunia ulipungua kutoka dola za Kimarekani 1,840.2 kwa tani mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 1,739.7 kwa tani mwaka 2011. Kiasi cha mauzo ya chai nje mwaka 2011 kilikuwa tani 27,100, sawa na ilivyokuwa mwaka 2010.

Tumbaku

55. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya tumbaku iliyouzwa nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 281.2 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 232.4 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 21.0. Ongezeko hili lilitokana hasa na kuongezeka kwa kiasi cha tumbaku kilichouzwa nje kutoka tani 53,600 mwaka 2010 hadi tani 73,300 mwaka 2011. Hata hivyo, wastani wa bei ya tumbaku katika soko la dunia ulipungua hadi dola za Kimarekani 3,839.4 kwa tani mwaka 2011 kutoka dola 4,337.0 kwa tani mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 11.5.

Korosho

56. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya korosho nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 107.0 milioni kutoka dola za Kimarekani 96.9 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Ongezeko hili lilichangiwa na kupanda kwa wastani wa bei ya korosho katika soko la dunia japokuwa kiasi cha mauzo nje kilipungua. Wastani wa bei ya korosho katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 15.2, kutoka dola 963.2 kwa tani mwaka 2010 hadi dola 1,110.0 kwa tani mwaka 2011. Hata hivyo, kiasi cha korosho kilichouzwa nje kilipungua hadi tani 96,400 mwaka 2011 kutoka tani 100,600 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 4.2.

Karafuu

57. Thamani ya mauzo ya karafuu nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 29.0 milioni kutoka dola za Kimarekani 7.6 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 280.8. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa wastani wa bei ya karafuu katika soko la dunia na kiasi cha karafuu kilichouzwa nje. Wastani wa bei ya karafuu katika soko la dunia uliongezeka kwa asilimia 279.4 kutoka dola za Kimarekani 3449.6 kwa tani mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 13087.3 kwa tani mwaka 2011. Hali hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa karafuu katika nchi ya Indonesia ambayo ni moja ya nchi zinazozalisha zao la karafuu kwa wingi duniani kufuatia mlipuko wa ugonjwa uliathiri zao hilo. Aidha, kiasi cha mauzo ya karafuu nje kiliongezeka kwa asilimia 0.4 kutoka tani 2206 mwaka 2010 hadi tani 2,214 mwaka 2011.

Bidhaa Zisizo Asilia

58. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka hadi dola za Kimarekani 3,765.1 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 3,186.9 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 18.1. Ongezeko hili lilitokana na kuendelea kukua kwa mauzo ya bidhaa za madini hasa dhahabu na pia kukua kwa biashara ya maua nje. Mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 86.9 ya mauzo yote ya bidhaa nje ikilinganishwa na asilimia 86.8 mwaka 2010, ikijumuisha bidhaa zisizorekodiwa.

Madini

59. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya madini iliongezeka hadi dola za Kimarekani 2,284.1 milioni kutoka dola za Kimarekani 1,560.2 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 46.4. Dhahabu iliendelea kutoa mchango mkubwa katika mauzo nje, ambapo kwa mwaka 2011 ilichangia asilimia 97.4 ya thamani ya mauzo yote ya madini nje na asilimia 59.1 ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia. Thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kutoka dola za Kimarekani

1,516.6 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 2,224.1 milioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 46.7. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa kiasi cha mauzo ya dhahabu nje na wastani wa bei ya dhahabu katika soko la dunia. Kiasi cha mauzo ya dhahabu nje kiliongezeka kutoka tani 35.6 mwaka 2010 hadi tani 40.4 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Aidha, katika kipindi hicho, bei ya dhahabu katika soko la dunia iliongezeka kwa asilimia 28.0, hadi dola za Kimarekani 1,568.0 kwa aunzi moja.

Bidhaa za Viwandani

60. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani nje ilipungua kutoka dola za Kimarekani 964.0 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 861.5 milioni mwaka 2011, sawa na upungufu wa asilimia 10.6. Upungufu huu ulitokana na athari za mgao wa umeme ambao ulisababisha kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani hususan bidhaa za karatasi, plastiki, na nyuzi za pamba. Aidha, mchango wa bidhaa za viwandani katika mauzo ya bidhaa zisizo asilia nje ulikuwa asilimia 22.9 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 30.3 mwaka 2010.

Samaki na Mazao ya Samaki

61. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya samaki na mazao ya samaki ilipungua kwa asilimia 8.4 hadi dola za Kimarekani 137.7 milioni kutoka dola za Kimarekani 150.0 milioni mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa kiasi cha mauzo ya samaki na mazao ya samaki nje.

Mazao ya Mboga na Maua

62. Mwaka 2011,thamani ya mauzo ya mazao ya mboga na maua nje ilikuwa dola za Kimarekani 36.4 milioni ililinganishwa na dola za Kimarekani 30.8 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 18.3. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za maua kufuatia kuimarika kwa uwekezaji katika shughuli za uzalishaji wa maua kwa miaka ya hivi karibuni.

Bidhaa Nyinginezo Zilizouzwa Nje

63. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa nyinginezo nje (zikiwemo bidhaa za mbegu za mafuta, ngozi, nafaka, kakao na bidhaa za mazao ya miti) ilikuwa dola za Kimarekani 347.1 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 349.1 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 0.6. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa zilizouzwa tena ilikuwa dola za Kimarekani 98.3 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 132.5 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 25.8. Vile vile, mauzo ya bidhaa ambazo hazikurekodiwa yalikuwa na thamani ya dola za Kimarekani 664.9 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 563.9 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 17.9.

Jedwali Na.3.1: Thamani, Kiasi na Bei ya Bidhaa Zilizouzwa Nje (2007-2011)						
Bidhaa	**2007**	**2008**	**2009**	**2010r**	**2011p**	**2010/11 (Badiliko)**
Bidhaa Asilia						
Kahawa						
Thamani (US$ milioni)	98.1	99.1	111.2	101.6	142.6	40.3
Kiasi (‘000 ttani)	45.0	45.4	56.0	35.6	39.0	9.5
Bei (US$ kwa tani)	2177.6	2185.7	1984.6	2853.1	3654.9	28.1
Pamba						
Thamani (US$ milioni)	66.4	115.8	111.0	84.0	61.6	-26.6
Kiasi (‘000 ttani)	59.1	87.9	99.4	67.6	40.3	-40.4
Bei (US$ kwa tani)	1123.8	1317.6	1116.7	1241.9	1529.0	23.1
Katani						
Thamani (US$ milioni)	8.8	15.7	-	-	-	-
Kiasi (‘000 ttani)	9.5	13.8	-	-	-	-
Bei (US$ kwa tani)	928.4	1137.7	-	-	-	-
Chai						
Thamani (US$ milioni)	28.7	42.5	47.2	49.8	47.2	-5.3
Kiasi (‘000 ttani)	21.5	28.1	30.6	27.1	27.1	0.2
Bei (US$ kwa tani)	1334.8	1511.2	1538.7	1840.2	1739.7	-5.5
Tumbaku						
Thamani (US$ milioni)	87.8	176.4	127.4	232.4	281.2	21.0
Kiasi (‘000 ttani)	37.9	53.6	33.8	53.6	73.3	36.7
Bei (US$ kwa tani)	2318.1	3293.3	3764.0	4337.0	3839.4	-11.5
Korosho						
Thamani (US$ milioni)	25.6	44.3	68.6	96.9	107.0	10.4
Kiasi (‘000 ttani)	41.3	52.7	95.5	100.6	96.4	-4.2
Bei (US$ kwa tani)	621.1	839.6	718.2	963.2	1110.0	15.2
Karafuu						
Thamani (US$ milioni)	4.2	13.5	14.4	7.6	29.0	280.8
Kiasi (‘000 ttani)	1.4	3.7	4.8	2.2	2.2	0.4
Bei (US$ kwa tani)	2968.3	3605.5	2977.9	3449.6	13087.3	279.4
Jumla (Bidhaa Asilia)	**319.7**	**507.3**	**479.6**	**572.3**	**668.7**	16.8
Bidhaa Zisizo Asilia						
Madini	848.7	1186.7	1271.4	1560.1	2284.1	46.4
Dhahabu	788.2	1108.3	1229.5	1516.6	2224.1	46.7
Almasi	26.0	20.3	15.5	10.1	10.9	7.4
Madini mengine	34.4	58.1	26.4	33.5	49.2	46.9
Bidhaa za Viwandani	309.8	741.8	506.5	964.0	861.5	-10.6
Samaki na Mazao ya Samaki	163.6	184.7	155.0	150.4	137.7	-8.4
Mazao ya mboga na Maua	19.1	45.7	33.3	30.8	36.4	18.3
Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports)	149.7	160.3	120.4	132.5	98.3	-25.8
Bidhaa nyinginezo	213.7	285.5	289.6	349.1	347.1	-0.6
Jumla (Bidhaa zisizo Asilia)	**1704.5**	**2604.7**	**2376.1**	**3186.9**	**3765.1**	18.1
Bidhaa zisizorekodiwa	202.4	466.8	438.9	563.9	664.9	17.9
JUMLA KUU (BIDHAA ZOTE)	**2226.6**	**3578.8**	**3294.6**	**4323.1**	**5098.7**	17.9

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

- Takwimu Hazikupatikana

Mapato ya Huduma

64. Mwaka 2011, mapato yatokanayo na huduma nje yalikuwa dola za Kimarekani 2,362.5 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 2,045.7 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 15.5. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na huduma za utalii na huduma ya usafirishaji, ambazo kwa pamoja zilichangia zaidi ya asilimia 80 ya mapato ya biashara ya huduma nje. Mapato yatokanayo na huduma za utalii yaliongezeka kwa asilimia 16.1 na kufikia dola za Kimarekani 1,456.9 milioni mwaka 2011 kutoka dola za Kimarekani 1,254.5 milioni mwaka 2010 kufuatia kuongezeka kwa idadi ya watalii na juhudi za Serikali za kuitangaza Tanzania kama kivutio cha utalii. Vile vile, mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji yaliongezeka kwa asilimia 33.2 na kufikia dola za Kimarekani 507.0 milioni kutoka dola za Kimarekani 445.5 milioni mwaka 2010. Hii ilitokana na kuongezeka kwa bidhaa zilizosafirishwa kwenda na kutoka nchi jirani.

Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje

65. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje (f.o.b) kwa mwaka 2011 ilikuwa dola za Kimarekani 9,827.5 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 7,165.5 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 37.2. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa mafuta na mitambo kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la umeme lilijitokeza mwaka 2011 sambamba na kupanda kwa wastani wa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Bidhaa za Kukuza Mitaji

66. Mwaka 2011, thamani ya bidhaa za kukuza mitaji zilizoagizwa toka nje iliongezeka hadi dola za Kimarekani 3,560.5 milioni kutoka dola za Kimarekani 2,715.2 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 31.1. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa mitambo kutokana na kukua kwa shughuli za uwekezaji katika sekta ya gesi asilia na mafuta ya petroli. Uagizaji wa mitambo uliongezeka kwa asilimia 49.1 hadi dola za Kimarekani 1,794.3 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 1,203.4 milioni mwaka 2010. Aidha, thamani ya uagizaji wa vifaa vya usafirishaji iliongezeka kwa asilimia 11.9 kufikia dola za Kimarekani 1,008.5 milioni mwaka 2011 kutoka dola za Kimarekani 901.1 milioni mwaka 2010. Vile vile, uagizaji wa vifaa vya ujenzi uliongezeka kwa asilimia 24.1 kufikia dola za Kimarekani 757.7 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 610.6 milioni mwaka 2010.

Bidhaa za Kati

67. Mwaka 2011, thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati iliongezeka hadi dola za Kimarekani 4,139.0 milioni kutoka dola za Kimarekani 2,741.2 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 51.0. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia na kuongezeka kwa uagizaji wa mafuta nchini kwa ajili ya uzalishaji wa umeme. Uagizaji wa mafuta peke yake uligharimu asilimia 32.9 ya thamani ya uagizaji wa bidhaa zote toka nje. Thamani ya uagizaji wa bidhaa za mafuta ilikuwa dola za Kimarekani 3,228.7 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 2,024.2 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 59.5. Uagizaji wa mbolea uliongezeka kutoka dola za Kimarekani 115 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 176.6 milioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 53.6. Hii ilitokana na kupungua kwa uzalishaji wa mbolea katika viwanda vya ndani. Vile vile, thamani ya uagizaji wa malighafi za viwanda iliongezeka kwa asilimia 21.9 kutoka dola za Kimarekani 602 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 733.7 milioni mwaka 2011.

Bidhaa za Matumizi ya Kawaida

68. Mwaka 2011, uagizaji wa bidhaa za matumizi ya kawaida uliongezeka hadi dola za Kimarekani 2,128.0 milioni kutoka dola za Kimarekani 1,709.2 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 24.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za chakula na bidhaa nyinginezo za matumizi ya kawaida. Uagizaji wa bidhaa za chakula uliongezeka kwa asilimia 30.6 kutoka dola za Kimarekani 461.6 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 603.1 milioni mwaka 2011 kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za nafaka hasa ngano na wastani wa bei za nafaka katika soko la dunia. Thamani ya uagizaji wa ngano iliongezeka hadi dola za Kimarekani 391.3 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 287.2 milioni mwaka 2010, wakati ambapo wastani wa bei ya ngano katika soko la dunia uliongezeka kutoka dola za Kimarekani 229.7 milioni kwa tani mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 285.9 milioni kwa tani mwaka 2011. Aidha, uagizaji wa bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida uliongezeka kwa asilimia 22.3 kufikia dola za Kimarekani 1,522.7 milioni 2011 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 1,245.3 mwaka 2010.

Malipo ya Huduma

69. Mwaka 2011, malipo ya huduma yalikuwa dola za Kimarekani 2,165.3 milioni ikilinganishwa na dola 1,849.6 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 17.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa gharama za malipo ya huduma za usafirishaji wa mizigo sambamba na kukua kwa kiasi cha bidhaa zilizoagizwa

kutoka nje. Malipo ya huduma za usafirishaji yaliongezeka kutoka dola za Kimarekani 722.8 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 973.3 milioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 34.7. Aidha, malipo ya huduma za utalii yaliongezeka kwa asilimia 8.2 kutoka dola za Kimarekani 830.4 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 898.6 milioni mwaka 2011. Hata hivyo, malipo ya huduma nyingine yalipungua kutoka dola za Kimarekani 299.1 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 293.4 milioni mwaka 2011, sawa na upungufu wa asilimia 1.9.

Mwenendo wa Biashara Baina ya Tanzania na Nchi Mbalimbali

70. Mwaka 2011, Tanzania iliendelea kuwa na uhusiano mzuri wa kibiashara na nchi nyingi duniani zikiwemo nchi za Bara la Ulaya, Amerika, Asia na Afrika. Katika kipindi hicho, Tanzania iliuza bidhaa zake kwa wingi katika nchi ya Afrika Kusini ambayo ilichangia asilimia 16.3 ya mauzo yote nje ikifuatiwa na Uswisi asilimia 16.1; China asilimia 12.9; Japan asilimia 6.8; Ujerumani asilimia 4.4; Kenya asilimia 4.1 na India asilimia 4.0. Baadhi ya bidhaa zilizouzwa nje kwa wingi ni pamoja na madini, maua, kahawa na tumbaku. Aidha, Tanzania ilinunua bidhaa kwa wingi kutoka China ambayo ilichangia asilimia 8.1 ya bidhaa zote zilizoagizwa kutoka nje ikifuatiwa na India asilimia 8.0; Afrika Kusini asilimia 6.9; Umoja wa Falme za Kiarabu asilimia 6.0; Japan asilimia 5.1; Uswisi asilimia 5.0; Singapore asilimia 4.0 na Kenya asilimia 2.5. Baadhi ya bidhaa zilizoagizwa ni pamoja na magurudumu ya magari, vifaa vya mawasiliano vikiwemo simu za mkononi, pikipiki, magari, bidhaa za mafuta ya petroli na dawa za binadamu.

71. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Bara la Ulaya iliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,382.0 milioni kutoka dola 1,151.1 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 20.1. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi ya Uswisi kwa asilimia 19.3. Thamani ya mauzo kwa nchi ya Uswisi iliongezeka hadi dola za Kimarekani 818.4 milioni kutoka dola za Kimarekani 685.9 milioni mwaka 2010. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Bara hilo iliongezeka kutoka dola za Kimarekani 1,669.8 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 1,721.5 milioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Bara la Ulaya uliimarika zaidi na kuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 339.5 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani 518.7 milioni mwaka 2010.

72. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ilipungua kwa asilimia 21.7 hadi dola za Kimarekani 352.4 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 450.0 milioni mwaka 2010. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa mauzo kwenda nchi za Jumuiya hiyo isipokuwa Rwanda. Mauzo kwenda nchi ya Rwanda yaliongezeka kwa asilimia19.6 kutoka dola za Kimarekani 55.0 mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 65.8 mwaka 2011. Mauzo kwenda nchi ya Burundi yalipungua kwa asilimia 39.6, Kenya asilimia 28.9 na Uganda kwa asilimia 4.7. Mauzo ya bidhaa kwa nchi ya Kenya yalichangia asilimia 59.9 ya mauzo yote kwa Jumuiya, Rwanda asilimia 18.7, Uganda ilichangia asilimia 12.7 na Burundi asilimia 8.7. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Afrika ya Mashariki ilipungua hadi dola za Kimarekani 263.8 milioni mwaka 2011 kutoka dola dola za Kimarekani 285.2 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 7.5. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa na ziada ya dola dola za Kimarekani 88.6 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola dola za Kimarekani 164.8 milioni mwaka 2010.

73. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) iliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,158.9 milioni kutoka dola za Kimarekani 625.1 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 85.4. Hii ilitokana hasa na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi ya Afrika Kusini. Thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda Afrika Kusini iliongezeka kwa asilimia 99.4 na ilichangia asilimia 71.7 ya mauzo yote kwenda nchi za SADC kwa mwaka 2011. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za SADC ilipungua kwa asilimia 5.6 hadi dola 781.3 milioni mwaka 2011 kutoka dola 827.7 milioni mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nchi zote za Jumuiya hiyo. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za SADC ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 377.6 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na nakisi ya dola 202.6 milioni mwaka 2010.

74. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania kwa nchi zote za Afrika iliongezeka hadi dola za Kimarekani 1,579.2 milioni kutoka dola za Kimarekani 1,080.9 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 46.1. Hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi za SADC hasa Afrika Kusini. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Afrika ilipungua kwa asilimia 1.3 kutoka dola za Kimarekani 1,112.9 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 1,098.1 milioni mwaka 2011. Hii ilitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Afrika Kusini na Kenya. Urari

wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi zote za Afrika ulikuwa na ziada ya dola dola za Kimarekani 481.1 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na nakisi ya dola dola za Kimarekani 32.0 milioni mwaka 2010.

75. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia zikiwemo China, Japan, India, Hong Kong, Singapore na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 17.9 hadi dola za Kimarekani 1,414.6 milioni kutoka dola za Kimarekani 1,200.2 milioni mwaka 2010. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo kwenda nchi za Japan na China. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi za Bara hilo ilipungua kidogo kutoka dola za Kimarekani 4,083.4 milioni mwaka 2010 hadi dola za Kimarekani 4,037.3 milioni mwaka 2011, sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Bara la Asia uliimarika kidogo na kuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 2,622.7 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani 2,957.9 milioni mwaka 2010.

76. Mwaka 2011, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda Bara la Amerika iliongezeka hadi dola za Kimarekani 59.9 milioni kutoka dola za Kimarekani 51.0 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 17.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Marekani na Canada. Thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka Bara hilo ilipungua kwa asilimia 7.3 hadi dola za Kimarekani 240.2 milioni mwaka 2011 kutoka dola za Kimarekani 259.0 milioni mwaka 2010. Aidha, urari wa biashara ya bidhaa kati ya Tanzania na nchi za Bara la Amerika uliimarika pia na kuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 180.3 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani 208.0 milioni mwaka 2010.

Jedwali Na. 3.2: Urari wa Biashara ya Bidhaa Kati ya Tanzania na Jumuiya Mbalimbali za Ushirikiano Kikanda (Dola milioni)

Jumuiya/ Mwaka	**2005**	**2006**	**2007**	**2008**	**2009**	**2010r**	**2011p**
Bara la Ulaya	3.9	(77.8)	(515.2)	(567.0)	(313.1)	(518.7)	(339.5)
Jumuiya ya nchi za SADC	(103.2)	(284.8)	(355.4)	(510.2)	(417.8)	(202.6)	377.6
Jumuiya ya Afrika Mashariki	(64.0)	(56.7)	66.5	110.7	(46.7)	164.8	88.6
Bara la Asia	-	-	(1,582.0)	(2,212.8)	(2,352.2)	(2,957.9)	(2,622.7)
Bara la Amerika	-	(174)	(291.5)	(313.7)	(217.1)	(208.0)	(180.3)

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha,
r = iliyorekebishwa
p = ya muda

Jedwali Na. 3.3: Thamani ya Bidhaa Zilizouzwa Nje							(Dola milioni)	
JUMUIYA/ NCHI	**2005**	**2006**	**2007**	**2008**	**2009**	**2010r**	**2011p**	**2010/11 (Badiliko, %)**
JUMUIYA YA ULAYA	359.7	334.1	346.7	461.9	440.0	464.0	553.5	**19.3%**
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	259.9	421.6	454.2	533.3	469.0	687.1	828.5	**20.6%**
JUMLA - BARA LA ULAYA	**619.6**	**755.7**	**800.9**	**995.2**	**909.0**	**1151.1**	**1382.0**	**20.1%**
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)								
Afrika ya kusini	275.4	268.9	176.1	232.5	170.9	416.8	831.1	**99.4%**
Zambia	8.7	18.5	22.4	36.6	44.3	53.5	47.1	**-12.0%**
Swaziland	0.6	1.9	0.2	0.6	20.8	0	12.5	**-**
Zimbabwe	1.6	1.2	0.7	1.2	5.7	0	4.1	**-**
Msumbiji	6.5	10.6	19.1	31.4	20.3	17.7	61.9	**249.7%**
Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo	12.6	18.3	58.9	124	79.9	137.1	119.5	**-12.8%**
Nchi nyingine za SADC	**16.9**	**21.7**	**23.7**	**17.1**	**32.3**	**0**	**82.6**	**-**
JUMLA- SADC	**322.3**	**341.1**	**301.1**	**443.4**	**374.2**	**625.1**	**1158.8**	**85.4%**
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)								
Burundi	0	0	41.5	19.5	23.6	51.0	30.8	**-39.6%**
Kenya	76.3	97.2	101.1	235	177.4	297.3	211.2	**-29.0%**
Rwanda	0	0	11.2	20.6	15.1	55.0	65.8	**19.6%**
Uganda	20.1	20.5	19.3	40.5	47.7	46.8	44.6	**-4.7%**
JUMLA – EAC	**96.4**	**117.7**	**173.1**	**315.6**	**263.8**	**450.1**	**352.4**	**-21.7%**
Nchi nyingine za Afrika	**34.7**	**29.9**	**72.8**	**96.1**	**0.6**	**5.8**	**67.9**	**1070.7%**
JUMLA –AFRIKA	**453.4**	**488.7**	**547.0**	**855.1**	**638.6**	**1081.0**	**1579.1**	**46.1%**
BARA LA AMERIKA								
Marekani	16.5	20.7	34.2	55.1	39.5	46.5	47.5	**2.2%**
Canada	39.2	6	2.3	3.8	6.1	4.6	5.0	**8.7%**
Nchi nyingine za Bara la Amerika	3.7	1.1	6	5.4	0	0	7.4	**-**
JUMLA- BARA LA AMERIKA	**59.4**	**27.8**	**42.5**	**64.3**	**45.6**	**51.1**	**59.9**	**17.2%**
ASIA								
China	0	0	141.3	223.5	363.9	634.2	659.2	**3.9%**
India	63.2	63.8	77.3	171.8	183.8	218.5	202.7	**-7.2%**
Japan	68.7	82	57.1	136.9	164.7	209.7	346.8	**65.4%**
Umoja wa Falme za Kiarabu	33.7	47.3	88.4	65.4	66.8	55.3	74.9	**35.4%**
Hong Kong	9.6	7.6	14.1	13.4	85.6	12.6	11.1	**-11.9%**
Singapore	18.7	4.4	4.0	11.0	6.4	13.5	10.9	**-19.3%**
Nchi nyingine za Asia	133.8	123.1	65.1	52.4	59.1	56.4	109.1	**93.4%**
JUMLA- ASIA	**327.7**	**328.2**	**447.3**	**674.4**	**930.3**	**1200.2**	**1414.7**	**17.9%**
NCHI NYINGINEZO	**242.4**	**317.2**	**388.9**	**989.9**	**771.1**	**839.8**	**663.0**	**-21.1%**
JUMLA KUU	**1,702.50**	**1,917.60**	**2,226.60**	**3,578.90**	**3,294.60**	**4,323.20**	**5,098.70**	**17.9%**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

r = iliyorekebishwaa

p = ya muda

Jedwali Na. 3.4: Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa Nje (Dola milioni)

JUMUIYA/ NCHI	2006	2007	2008	2009	2010r	2011p	2010/11 (Badiliko, %)
JUMUIYA YA ULAYA NA USWISI	744.4	1061.6	1280.8	1076.6	1111.4	1074.4	-3.3
NCHI NYINGINE ZA ULAYA	74.7	181.7	153.8	145.5	558.4	647.1	15.9
JUMLA - BARA LA ULAYA	**819.1**	**1243.3**	**1434.6**	**1222.1**	**1669.8**	**1721.5**	3.1
AFRIKA							
JUMUIYA YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA (SADC)							
Afrika ya Kusini	569.6	585.8	791.0	672.8	745.5	676.5	-9.3
Zimbabwe	1.3	1.8	27.6	0.6	1.1	1.0	-9.1
Zambia	11.6	18.5	27.6	23.3	29.8	27.0	-9.4
Msumbiji	17.2	16.9	18.2	9.0	18.5	16.9	-8.6
Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo	0.2	0.6	19.6	1.2	1.1	1.0	-9.1
Swaziland	16.8	20.1	76.5	26.3	31.7	29.0	-8.5
Nchi nyingine za SADC	**9.2**	**12.4**	**19.2**	**-**	**-**	**29.9**	
JUMLA –SADC	**625.9**	**656.1**	**979.7**	**733.2**	**827.7**	**781.3**	-5.6
JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (EAC)							
Burundi	0.0	0.0	0.4	0.3	0.6	0.6	0.0
Kenya	169.1	100.1	197.9	298.3	265.9	246.1	-7.4
Rwanda	0.0	0.0	0.1	0.0	1.4	1.2	-14.3
Uganda	5.3	6.4	6.4	11.9	17.3	15.9	-8.1
JUMLA –EAC	**174.4**	**106.5**	**204.8**	**310.5**	**285.2**	**263.8**	-7.5
Nchi nyingine za Afrika	**62.9**	**60.2**	**71.9**	**0.3**	**0.0**	**53.2**	177233.3
JUMLA NCHI ZOTE ZA AFRIKA	**863.2**	**822.8**	**1256.4**	**1044.0**	**1112.9**	**1098.3**	-1.3
BARA LA AMERIKA							
Marekani	123.1	187.1	200.4	136.0	150.6	138.5	-8.0
Canada	37.5	35.6	57.1	35.2	36.4	33.1	-9.2
Nchi nyingine za Bara la Amerika	**41.2**	**111.2**	**120.4**	**91.5**	**72.0**	**68.6**	-4.7
JUMLA - BARA LA AMERIKA	**201.8**	**333.9**	**377.9**	**262.7**	**259.0**	**240.2**	-7.3
ASIA							
China	309.4	406.0	711.8	678.1	846.8	787.6	-7.0
India	241.3	507.0	891.2	757.3	864.6	784.5	-9.3
Japan	257.5	261.8	711.8	413.6	548.8	502.9	-8.4
Hong Kong	0.0	11.8	18.1	30.7	23.3	21.1	-9.4
Singapore	13.2	25.3	433.0	188.2	429.3	390.4	-9.1
Umoja wa Falme za Kiarabu	500.6	773.6	859.7	618.8	649.3	590.9	-9.0
Nchi nyingine za Asia	677.7	741.5	386.0	438.3	796.0	959.9	20.6
JUMLA - ASIA	**1975.3**	**2460.6**	**4024.0**	**3282.5**	**4083.4**	**4037.3**	-1.1
NCHI NYINGINEZO	**4.7**	**0.0**	**-80.6**	**22.7**	**40.4**	**2730.2**	6657.9
JUMLA KUU	**3864.1**	**4860.6**	**7012.3**	**5834.0**	**7165.5**	**9827.5**	37.1

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha

p = ya muda

r = iliyorekebishwa

Mizania ya Malipo na Nchi za Nje

Urari wa Biashara ya Bidhaa

77. Mwaka 2011, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 4728.8 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani 2842.4 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 66.4. Kuongezeka kwa nakisi kulitokana na kuongezeka kwa kasi ya uagizaji wa bidhaa hasa mitambo na mafuta kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika sekta ya nishati ikilinganishwa na kasi ndogo ya ongezeko la mauzo ya bidhaa nje.

Urari wa Biashara ya Huduma

78. Mwaka 2011, urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 197.2 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola 193.4 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 2.0. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na biashara ya huduma za utalii na huduma ya usafirishaji.

Urari wa biashara ya Bidhaa na Huduma

79. Mwaka 2011, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 4531.6 milioni kutoka nakisi ya dola 2649.0 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 71.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa malipo ya bidhaa na huduma toka nje.

Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi

80. Mwaka 2011, urari wa mapato ya vitega uchumi yanayojumuisha fidia kwa wafanyakazi, mapato ya uwekezaji na malipo ya riba ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 55.7 milioni kutoka nakisi ya dola za Kimarekani 40.8 milioni mwaka 2010 sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 36.5. Hii ilitokana na ongezeko kubwa la malipo ya fidia kwa wafanyakazi kutoka malipo ya dola 44.0 milioni mwaka 2010 hadi dola 82.9 milioni mwaka 2011.

Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida

81. Urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha, misaada na unafuu wa kulipa deni ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 619.9 milioni mwaka 2011 ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani 826.0 milioni mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 25.0. Upungufu huu ulitokana na kupungua kwa misaada ya nchi wahisani kwa Serikali kutokana na nchi nyingi wahisani kukabiliwa na matatizo ya kiuchumi na kisiasa. Mwaka 2011, Serikali ilipokea misaada kutoka kwa wahisani yenye thamani ya dola za Kimarekani 609.7 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 798.1 milioni zilizopokelewa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 23.6.

Urari wa Malipo ya Kawaida

82. Mwaka 2011, urari wa malipo ya kawaida, unaojumuisha urari wa biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi, na uhamisho mali wa kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 3967.4 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola dola za Kimarekani 1863.8 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 112.9. Hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa na huduma kulikotokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa toka nje na malipo ya huduma.

Urari wa Uhamisho wa Mitaji

83. Mwaka 2011, urari wa uhamisho wa mitaji, unaojumuisha misaada ya vitega uchumi na misamaha ya madeni ya nje kutoka kwa mashirika ya fedha ya kimataifa na nchi wahisani, uliongezeka kwa asilimia 39.9 hadi ziada ya dola za Kimarekani 750.5 milioni kutoka ziada ya dola dola za Kimarekani 536.5 mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa misaada ya vitega uchumi.

Urari wa Malipo ya Fedha katika Uwekezaji

84. Mwaka 2011, urari wa malipo ya fedha unaojumuisha uwekezaji wa moja kwa moja na mikopo ya fedha kutoka nje ulikuwa na ziada ya dola za Kimarekani 2,582.2 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola 1,732.5 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 49.0. Ongezeko hili lilitokana na kupungua kwa rasilimali za kigeni zinazomilikiwa na benki za biashara nchini kutoka rasilimali zenye thamani ya dola za Kimarekani 75.2 milioni mwaka 2010 hadi rasilimali zenye thamani ya dola 22.2 milioni mwaka 2011.

Urari wa Malipo Yote

85. Mwaka 2011, urari wa malipo yote ulikuwa na nakisi ya dola za Kimarekani 158.7 milioni ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani 343.1 milioni mwaka 2010. Nakisi katika mwaka 2011 ilitokana hasa na kuongezeka kwa nakisi katika urari wa malipo ya kawaida.

Akiba ya Fedha za Kigeni

86. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Decemba 2011, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani 3,761.2 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 3,948.0 milioni katika kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 4.7. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kwa mwaka 2011 kilikuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi 3.8 ikilinganishwa na miezi 5.3 iliyofikiwa mwaka 2010.

Thamani ya Fedha ya Tanzania

87. Mwaka 2011, thamani ya Shilingi ya Tanzania ilishuka kwa asilimia 10.3 kufikia wastani wa shilingi 1,579.5 kwa dola moja ya Kimarekani ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,432.3 kwa dola moja ya Kimarekani mwaka 2010.Thamani ya shilingi ya Tanzania ilishuka kutokana na sababu mbalimbali hususan kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje ikilinganishwa na mauzo nje; tofauti ya mfumuko wa bei kati Tanzania na nchi tunazofanyanazo biashara; ulanguzi au kuotea katika fedha za kigeni (Market Speculation); na kuimarika kwa dola ya Kimarekani dhidi ya sarafu za mataifa mengine. Hadi mwishoni mwa Desemba 2011 bei ya dola moja ya Kimarekani ilikuwa na thamani ya shilingi 1,566.7 ikilinganishwa na shilingi 1,453.5 mwishoni mwa Desemba 2010.

THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na.17 Sh. Milioni

Aina ya Bidhaa	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Zilizouzwa Nje	926,892	1,267,322	1,582,111	1,874,265	2,156,732	2,628,866	3,194,929	3,671,935	4,050,561	7,331,020
Bidhaa Halisi	853,158	1,178,027	1,437,423	1,726,241	1,967,358	2,413,809	2,992,530	3,568,071	3,921,648	7,175,377
Zilizouzwa Tena	73,734	89,295	144,688	148,024	189,374	215,057	202,399	103,864	128,913	155,643
Zilizoagizwa	1,615,037	2,277,176	2,758,953	3,659,962	5,534,418	7,296,763	8,839,274	8,446,721	11,086,891	17,217,173
Jumla	2,541,929	3,544,498	4,341,064	5,534,227	7,691,150	9,925,629	12,034,203	12,118,656	15,137,452	24,548,193
Urari	(688,145)	(1,009,854)	(1,176,842)	(1,785,697)	(3,377,686)	(4,667,897)	(5,644,345)	(4,774,785)	(7,036,330)	(9,886,153)
Thamani ya Fedha (Shs/US$)	966.7	1038.4	1,089.4	1,122.7	1,251.9	1,232.8	1,196.31	1,320.3	1,409.3	1,557.4

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 18

	Kiasi(Tani)						Thamani(sh. Milioni)					
Bidhaa	2007	2008	2009	2010	2011	Badiliko(%) 2010/11	2007	2008	2009	2010	2011	Badiliko (%) 2010/11
Kahawa	53685	46229	56079	35359	40456	14%	143,255	122,162	147,427	162,310	225,748	39%
Pamba	40743	54089	100361	74859	43042	-43%	49,807	95,613	146,752	133,087	103,855	-22%
Katani	7101	13786	8198	-	-		7,438	13,046	28,490	-	-	
Chai	30506	26654	19191	44254	27114	-39%	48,258	49,615	45,552	65,479	73,509	12%
Tumbaku	40743	45284	33839	69095	74022	7%	116,893	208,004	168,057	327,521	437,941	34%
Korosho	14841	60468	99313	132675	116583	-12%	33,816	82,025	94,413	173,572	189,592	9%
Karafuu	3200	3805	4853	2566	2306	-10%	10,628	15,991	19,453	11,265	48,362	329%
Almasi (Carat)	149592	132477	158838	367849	4170000	1034%	23,381	20,891	24,988	14,234	16,976	19%
Dhahabu(gms)	67334000	32319880	34600000	35600000	40400000	13%	672,111	1,115,163	1,420,756	2,137,344	3,463,813	62%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mapato Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 19

	Kiasi (Tani)								Thamani (Mill.US$)							
Bidhaa	2005	2006	2007	2008	2009	2010r	2011p	Badiliko(%) 2010/11	2005	2006	2007	2008	2009	2010r	2011p	Badiliko (%) 2010/11
Bidhaa Asilia:																
Kahawa	46,100	38,822	53,685	44,248	56,079	35,359	40,455	14	74.3	61.4	98.1	99.1	111.2	101.6	142.6	40.3
Pamba	112,900	46,467	40,743	86,995	100,361	74,859	43,042	(43)	111.5	55.8	66.4	115.8	111.0	84.0	61.6	-26.6
Katani	9,300	9,984	7,101	2,659	8,198	9,041	-	(100)	7.3	6.1	8.8	15.7	-	-	-	
Chai	21,800	24,803	30,506	25,898	19,191	44,254	27,113	(39)	25.6	31.0	28.7	42.5	47.2	49.8	47.2	-5.3
Tumbaku	31,100	37,525	40,743	35,557	33,839	69,095	74,022	7	80.8	65.2	87.8	176.4	127.4	232.4	281.2	21.0
Korosho	62,000	59,180	14,841	55,011	99,313	132,675	117,041	(12)	46.6	39.4	25.6	44.3	68.6	96.9	107.0	10.4
Karafuu	3,000	3,033	3,200	3,774	4,853	2,566	2,306	(10)	8.5	8.2	4.2	13.5	14.4	7.6	29.0	280.8
Jumla									354.6	267.1	319.7	507.3	479.6	572.3	668.7	16.8
Bidhaa zisizo asilia:																
Madini									711.3	836.8	848.7	1186.7	1271.4	1560.1	2284.1	46.4
Bidhaa za Viwanda									156.1	195.8	309.8	741.8	506.5	964.0	861.5	-10.6
Samaki na Mazao ya Samaki									147.5	145.9	163.6	184.7	155.0	150.4	137.7	-8.4
Mazao ya Mboga na Maua									18.3	15.4	19.1	45.7	33.3	30.8	36.4	18.3
Bidhaa zilizouzwa tena									127.1	128.3	149.7	160.3	120.4	132.5	98.3	-25.8
Bidhaa nyinginezo									454.4	154.0	213.7	285.5	289.6	349.1	347.1	-0.6
Jumla									1614.7	1476.2	1704.5	2604.7	2376.1	3186.9	3765.1	18.1
Bidhaa Zisizorekodiwa										174.3	202.4	466.8	438.9	563.9	665.1	17.9
JUMLA KUBWA									1969.3	1917.6	2226.6	3578.8	3294.7	4323.1	5098.9	17.9

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Takwimu

- Takwimu Hazikupatikana

r - Iliyorekebishwa

p -Takwimu za Awali

I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE
(US$ Milioni)



II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
(Kiasi kwa Tani '000)




IIIA: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2010
Bidhaa Zisizorekodiwa 13.0%
Kahawa 2.4%
Pamba 1.9%
Tumbaku 5.4%
Bidhaa zilizouzwa tena 3.1%
Bidhaa nyinginezo 8.1%
Chai 1.2%
Korosho 2.2%
Mboga na Maua 0.7%
Karafuu 0.2%
Samaki na Mazao ya Samaki 3.5%
Madini 36.1%


IIIB: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2011
Bidhaa zilizouzwa tena 1.9%
Bidhaa Zisizorekodiw 13.0%
Bidhaa nyinginezo 6.8%
Kahawa 2.8%
Pamba 1.2%
Mboga na Maua 0.7%
Samaki na Mazao ya Samaki 2.7%
Chai 0.9%
Tumbaku 5.5%
Korosho 2.1%
Karafuu 0.6%
Madini 44.8%

WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 20 Sh./Tani*

Bidhaa	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011p	Badiliko(%) 2010/11
Kahawa	1,107,030	1,380,191	1,812,959	2,390,243	2,668,414	2,642,540	2,628,934	4,069,399	5,580,087	37.1%
Pamba	1,051,900	1,147,061	1,126,467	1,221,942	1,222,475	1,767,694	1,462,236	1,775,008	2,412,876	35.9%
Katani	533,190	624,068	879,366	931,090	1,047,444	946,323	3,475,213	-	-	
Chai	1,233,010	1,495,671	1,322,780	1,680,523	1,581,921	1,861,435	2,373,683	2,501,897	2,711,109	8.4%
Tumbaku	2,101,200	2,109,220	2,938,727	3,440,586	2,869,021	4,593,309	4,966,396	2,586,996	5,916,361	128.7%
Korosho	618,290	890,338	874,903	1,058,854	2,278,459	1,356,504	950,656	1,284,308	1,626,241	26.6%
Karafuu	1,901,360	2,524,410	3,210,533	3,285,196	3,321,160	4,202,786	4,008,131	4,390,290	20,972,246	377.7%
Almasi (kwa carat)	29,421	128,582	129,576	138,878	156,300	157,692	15,732	38,695	4,071	-89.5%
Dhahabu (kwa gramu)	8,679	11,316	24,223	21,778	9,982	34,504	41,062	60,038	85,738	42.8%

Chanzo:Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

p - Takwimu za Awali

WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 21

US$/Tani*

Bidhaa	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011p	Badiliko(%) 2010/11
Kahawa	1,080	1,285	1,612	1,932	2,165	2,203	1,991	3,318	3,609	8.8%
Pamba	1,020	1,063	988	988	992	1,321	1,108	1,306	1,431	9.6%
Katani	520	578	785	751	850	1,251	2,632	-	-	
Chai	1,200	1,386	1,174	1,359	1,283	1,575	1,798	1,125	1,741	54.7%
Tumbaku	2,050	2,079	2,598	2,779	2,327	3,041	3,762	3,363	3,799	12.9%
Korosho	600	831	752	855	1,848	730	720	730	914	25.2%
Karafuu	1,850	2,338	2,833	2,638	2,694	3,578	3,036	3,173	13,443	323.7%
Almasi (kwa carat)	29	119	115	111	127	133	1,192	3,028	2,395	-20.9%
Dhahabu (kwa gramu)	8.45	10.47	12.30	17.40	8.10	1.78	6.22	42.58	55.01	29.2%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Mapato Tanzania

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

p - Takwimu za Awali


MWENENDO WA BEI YA PAMBA NA KAHAWA
ILIYOUZWA NCHI ZA NJE (US$/Tani)
US$
4000
3500
3000
2500
2000
1500
1000
500
0
2002
2003
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
2011
Kahawa
Pamba

AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA TOKA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 23 Sh. Milioni

Mwaka	Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	Bidhaa za Kati	Bidhaa za Viwanda	Jumla
1987	13180	23819	41948	78947
1988	29841	55284	43950	129075
1989	34779	60176	96804	191759
1990*	18783	116277	96223	231283
1991	62000	69710	139668	271378
1992	101641	94233	196791	392665
1993	194604	107481	229657	531742
1994	247076	128544	290638	666258
1995	201347	294224	275207	770778
1996	182340	267600	252501	702441
1997	301018	203418	198670	703106
1998	441025	155225	311244	907495
1999	503868	197271	360225	1061363
2000	401612	222399	444427	1068438
2001	468173	386317	648361	1502851
2002	499346	408872	697209	1605426
2003	654630	705729	846251	2206610
2004	917953	1024705	1029389	2972046
2005	934526	1447183	1337876	3719585
2006	1068323	1977275	1799472	4845070
2007	1399488	2479491	2195837	6074816
2008	1689789	3191039	3508181	8389009
2009	1854493	2495763	3352506	7702762
2010	2447801	3926221	3888981	10263002
2011	3361176	6537551	5623810	15522536

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.

MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 24 US $ milioni

	2002 Halisi	2003 Halisi	2004 Halisi	2005 Halisi	2006 Halisi	2007 Halisi	2008 Halisi	2009 Halisi	2010 Halisi	2011 Matarajio
Urari wa Biashara	**-531.7**	**-717.4**	**-1009.7**	**-1321.8**	**-1946.5**	**-2634.1**	**-3433.5**	**-2539.5**	**-2842.4**	**-4728.8**
Zilizouzwa nje (fob)	979.6	1216.1	1473.1	1675.8	1917.6	2226.6	3578.8	3294.6	4323.1	5098.7
Zilizonunuliwa toka nje (fob)*	1511.3	1933.5	2482.8	2997.6	3864.1	4860.6	7012.3	5834.1	7165.5	9827.5
Urari wa Huduma	287.6	222.1	158.9	61.8	278.8	462.1	349.9	145.6	193.4	197.2
Mapato	920.1	947.8	1133.6	1269.2	1528.1	1875.7	1998.8	1854.6	2045.7	2362.5
Malipo	632.5	725.7	974.7	1207.3	1249.3	1413.7	1648.9	1709.1	1852.4	2165.3
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-88.9	-149.1	-119.1	-104.1	-94.8	-105.7	-95.1	-30.5	-40.8	-55.7
Yaliyoingia	67.9	87.1	81.8	80.9	80.3	107.3	122.7	161.1	160.1	184.2
Yaliyotoka	156.8	236.2	200.9	185.0	175.1	213.0	217.8	191.6	200.8	239.9
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	431.3	556.9	586.7	496.4	588.7	651.5	609.5	696.9	826.0	619.9
Iliyoingia	494.3	619.9	651.7	563.9	654.6	724.0	689.0	765.4	905.0	712.6
Serikalini	427.7	553.3	582.0	478.5	559.7	626.9	588.5	658.4	798.1	609.7
Sekta nyingine	66.6	66.6	69.7	85.4	94.9	97.1	100.5	106.9	106.9	102.9
Iliyotoka	63.0	63.0	65.0	67.5	65.9	72.5	79.6	68.4	79.0	92.7
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	**98.3**	**-87.5**	**-383.2**	**-867.6**	**-1173.8**	**-1626.2**	**-2569.3**	**-1727.5**	**-1863.8**	**-3967.4**
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	785.7	692.8	460.0	393.2	5183.5	911.7	537.0	446.6	536.5	750.5
Iliyoingia	785.7	692.8	460	393.2	5183.5	911.7	537.0	446.6	536.5	750.5
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Urari katika uwekezaji	255.4	61.2	275.6	807.6	-4081.6	924.6	1661.9	1252.1	1732.5	2582.2
Uwekezaji katika miradi	387.6	308.2	330.6	494.1	403.0	581.5	400.0	414.5	433.9	854.2
Uwekezaji katika hisa	2.2	2.7	2.4	2.5	2.6	2.8	2.9	3.0	3.2	3.4
Uwekezaji aina nyingine	-134.4	-249.7	-57.4	311.0	-4487.3	340.4	1258.9	834.5	1295.4	1724.6
Makosa na Masahihisho	-806.8	-277.4	-146.3	-555.4	532.6	194.5	518.4	395.0	-62.1	476.0
Urari wa Malipo yote	**332.6**	**389.1**	**206.1**	**-222.2**	**460.8**	**404.6**	**148.0**	**366.2**	**343.1**	**-158.7**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)


MWENENDO WA URARI KATIKA MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE
1000.0
0.0
-1000.0
-2000.0
-3000.0
-4000.0
-5000.0
US $ milioni
2002
2003
2004
2005
2006
2007
2008
2009
2010
2011
Urari wa Biashara
Huduma na Uhamisho Mali
Urari wa Malipo yote

SURA YA 4

FEDHA ZA SERIKALI

Utangulizi

88. Mfumo wa Bajeti ya mwaka 2011/12 ulizingatia maeneo muhimu ya utekelezaji ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12- 2015/16); Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II- 2011/12- 2015/16); Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Madeni.

89. Misingi na shabaha ya Bajeti ya Serikali ya 2011/12 ilikuwa ni: kukabiliana na changamoto za kupunguza makali ya maisha kwa wananchi; kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani; kuboresha mazingira ya uwekezaji wa ndani na nje na uendelezaji wa sekta binafsi; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Vitambulisho vya Taifa; uanzishwaji wa anuani za makazi na utekelezaji wa MKURABITA; kuhakikisha kwamba maduhuli ya Serikali yanakusanywa ipasavyo na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali; kutenga rasilimali katika maeneo ya kuongeza kasi ya ukuaji uchumi; na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji. Misingi mingine ilikuwa ni: kutekeleza mipango na mikakati maalum ya kuharakisha ukuaji wa uchumi; kuimarisha urari wa malipo kwa kusindika bidhaa kabla ya kusafirishwa nje; kutafuta mikopo ya masharti nafuu na ya kibiashara kutoka benki mbalimbali; kuharakisha utekelezaji wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na ya Binafsi ili kupanua fursa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na kulinda na kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za huduma za jamii (Elimu, Maji na Afya).

90. Kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za Bajeti katika mwaka 2011/12, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya shilingi 13,525.9 bilioni kutoka katika vyanzo mbalimbali na kutumia kiasi hicho kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Vyanzo vya mapato ni kama ifuatavyo: mapato ya ndani ya shilingi 6,775.9 bilioni; mapato kutoka Serikali za mitaa kiasi cha

shilingi 350.5 bilioni; misaada na mikopo ya kibajeti shilingi 869.4 bilioni; misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na ya kisekta kiasi cha shilingi 3,054.1 bilioni; mikopo ya ndani na nje shilingi 1,664.9 bilioni; na mikopo ya kulipia dhamana na hatifungani zilizoiva (rollover) shilingi 810.9 bilioni. Kwa upande wa matumizi, mgawanyo ulikuwa shilingi 8,600.3 bilioni kwa matumizi ya kawaida na shilingi 4,925.6 bilioni kwa matumizi ya maendeleo.

Mwenendo wa Mapato

Mapato ya Ndani

91. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia kiasi cha shilingi 5,157.6 bilioni, sawa na asilimia 99 ya makisio ya kukusanya shilingi 5,217.2 bilioni katika kipindi hicho. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yalikuwa shilingi 4,765.5 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya kukusanya shilingi 4,505.9 bilioni na mapato yasiyotokana na kodi yalikuwa shilingi 272.1 bilioni ikiwa ni asilimia 57 ya lengo la kukusanya shilingi 473.5 bilioni na kiasi cha shilingi 120 bilioni ni mapato ya Halmashauri, sawa na asilimia 50 ya lengo kwa kipindi hicho.

92. Mwenendo huu wa makusanyo ya kodi ulitokana na uimarishaji wa hatua za kiutawala zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania zilizowezesha kuongezeka kwa mapato. Hatua hizo zinajumuisha: kuhakikisha mashine za kielectroniki (EFD) zinatumika ipasavyo, hatua ambayo ilianza kutumika rasmi kuanzia Julai 2010; kuimarisha mfumo wa kusimamia vitalu vya kodi; kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwa wateja za kukusanyia mapato katika maeneo oevu kama vile Kariakoo, Kimara, Temeke; na kuboresha mfumo wa uthamanishaji kwa kuimarisha ukaguzi wa hesabu za walipa kodi na biashara.

93. Mapato yasiyotokana na kodi yalikuwa si ya kuridhisha kutokana na sababu kadhaa ikiwemo kushindwa kwa Mashirika na Taasisi kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyoamuliwa kutokana na sheria iliyoanzisha taasisi/mashirika hayo kuelekeza matumizi ya faida wanazopata. Kwa upande wa maduhuli yanayokusanywa na idara za Serikali, hakuna mifumo madhubuti inayoingiliana ya kukusanya mapato ambayo ingeboresha makusanyo na

kudhibiti uvujaji wa mapato. Vile vile kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa kulitokana na, pamoja na mambo mengine, kuchelewa kuanza kutekeleza utozaji wa ada za leseni.

Misaada na mikopo

94. Misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje iliendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato kwa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/12. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, Serikali ilipokea misaada na mikopo ya kibajeti ya jumla ya shilingi bilioni 759 ambazo ni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya shilingi bilioni 713.6 katika kipindi hicho. Ongezeko hilo lilitokana na nchi za Norway na Canada kutoa zaidi ya makadirio ya awali. Licha ya mafanikio hayo, kumejitokeza changamoto mbalimbali chini ya utaratibu wa Misaada ya Kibajeti (GBS) ikiwa ni pamoja na kujiondoa kwa baadhi ya wahisani katika utaratibu huo kama vile Uswisi na Uholanzi. Changamoto nyingine ni kwa Washirika wa Maendeleo kutokutekeleza makubaliano ya GBS ya kutoa fedha mwanzoni mwa mwaka (front loading). Katika kukabiliana na ucheleweshaji unaofanywa na wahisani, Serikali imeendelea kufanya mazungumzo na wahisani ili kutimiza ahadi zao kulingana na makubaliano ya MPAMITA.

95. Kwa upande mwingine, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha mifuko ya kisekta ilifikia shilingi bilioni 1,262.9 ambayo ni asilimia 53 ya bajeti ya shilingi bilioni 2,327.2. Upungufu wa misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo unatokana na kutotolewa kwa wakati kwa misaada na mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kulikotokana na kuyumba kwa uchumi wa nchi za Ulaya (Euro zone) ambayo imefanya uwezo wa nchi hizo kutoa misaada na mikopo kupungua.

Mikopo ya ndani

96. Kwa upande mwingine, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha mifuko ya kisekta ilifikia shilingi bilioni 1,262.9 ambayo ni asilimia 53 ya bajeti ya shilingi bilioni 2,327.2. Upungufu wa misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo unatokana na kutotolewa kwa wakati kwa misaada na mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kulikotokana

na kuyumba kwa uchumi wa nchi za Ulaya (Euro zone) ambayo imefanya uwezo wa nchi hizo kutoa misaada na mikopo kupungua.

Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara

97. Mwaka 2011/12, Serikali ilipanga kukopa kiasi cha Dola za Kimarekani 822 milioni, sawa na shilingi 1,271.6 bilioni kama mikopo ya kibiashara. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, Serikali ilisaini Mkataba wa mkopo wa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 310 kutoka Benki ya Standard na Mkataba wa mkopo wa Euro 61 milioni kutoka Benki ya HSBC. Hadi kufikia Machi 2012, jumla ya Dola 229 milioni kutoka Benki ya standard zilikuwa zimeshatolewa, na sehemu ya fedha hizo zilitumika kulipia madeni ya barabara ambayo Serikali ilivuka nayo mwaka 2010/11 na Euro 61 milioni ni kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 60 Nyakato mwanza kwa utaratibu wa "Export Credit Agency". Aidha, Serikali imesaini barua ya kuidhinisha mkopo (mandate letter) wa Dola za Kimarekani milioni 350 kutoka Benki ya Credit Suisse na sasa Mkataba wa mkopo huo unaandaliwa kwa ajili ya kusainiwa ambapo Dola milioni 200 zinatarajiwa kupatikana kabla ya Juni 2012. Majadiliano na Benki ya Barclays Capital ya Uingereza yamefikia hatua za mwisho ili kupata kiasi kilichobaki kukopwa kutoka chanzo hiki.

Matumizi

98. Mwaka 2011/12, Serikali iliendelea kutekeleza sera za matumizi kulingana na mapato ya ndani, misaada ya nje pamoja na mikopo ya ndani na nje. Aidha, Serikali ililenga kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, yakijumuisha udhibiti wa ulipaji wa mishahara, matumizi katika miradi ya maendeleo, ruzuku ya pembejeo, ununuzi wa umma na kuendelea kudhibiti malimbikizo ya madeni. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, matumizi yalikuwa yakiwianishwa na upatikanaji wa mapato. Matumizi halisi katika kipindi hicho yalikuwa shilingi 7,084.6 bilioni, sawa na asilimia 80 ya makadirio ya shilingi 8,895.8 bilioni. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,703.3 bilioni zilikuwa ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 66.4 ya matumizi kwa kipindi hicho, na shilingi 2,381.2 bilioni ni matumizi ya maendeleo.

99. Malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai 2011 hadi Machi, 2012 yalikuwa shilingi 2,026.2 bilioni, sawa na asilimia 96 ya lengo la shilingi 2,102 bilioni kwa kipindi hicho. Kati ya malipo hayo, kiasi cha shilingi 663.9 bilioni zililipwa kwa watumishi wa Serikali kuu, shilingi 60.98 bilioni zilitolewa kwa ajili ya watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi 1,301.3 bilioni kwa ajili ya mishahara ya Halmashauri, Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma jumla ya shilingi 453.7 bilioni kwa kipindi hicho.

100. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, matumizi mengineyo katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi 1,366.3 bilioni, ikiwa ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya shilingi 1,832.9 bilioni kwa kipindi hicho. Matumizi katika miradi ya maendeleo yalifikia shilingi 2,381.2 bilioni, ambapo fedha za ndani zilikuwa shilingi 1,118.4 bilioni, sawa na asilimia 105 ya makadirio ya shilingi 1,060.7 bilioni kwa kipindi hicho. Matumizi ya maendeleo yaliyogharamiwa na fedha za nje yalifikia shilingi 1,263.9 bilioni, ikiwa ni sawa na asilimia 53 ya makadirio ya shilingi 2,372.9 bilioni.

Malipo ya Deni

101. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, malipo ya deni la Serikali yalikuwa shilingi 759 bilioni, sawa na asilimia 68.7 ya makadirio ya shilingi 1,104.5 bilioni kwa kipindi hicho. Malipo ya deni la nje kwa kipindi hicho yalikuwa shilingi 121.3 bilioni. Kati ya hizo, shilingi 59.9 bilioni zilikuwa ni malipo ya mtaji na shilingi 61.5 bilioni zilikuwa ni malipo ya riba. Kiasi kikubwa cha malipo ya deni la nje ni riba kwa sababu mikopo mingi ni mipya na ni ya muda mrefu hivyo muda wa kuanza kulipa mtaji bado haujafika. Malipo ya deni la ndani kwa kipindi hicho yalikuwa shilingi 637.7 bilioni. Kati ya hizo, shilingi 433.7 bilioni zilitumika kulipia dhamana za Serikali zilizoiva kwa utaratibu wa kukopa na kulipia dhamana zilizoiva (rollover) na shilingi 203.9 bilioni zilikuwa ni malipo ya riba. Matumizi kwa madeni mengine (CFS Others) yalikuwa shilingi 448.3 bilioni ikiwa ni asilimia 73 ya makadirio ya shilingi 610.3 bilioni.

Mgawanyo wa Matumizi kwa Baadhi ya Sekta

102. Mwaka 2011/12, Serikali iliendelea kutenga fedha katika bajeti za sekta mbalimbali kulingana na vipaumbele vya bajeti. Katika mwaka 2011/12, kiasi cha shilingi 2,781.4 bilioni zilitengwa kwa ajili ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na mkongo wa Taifa ikilinganishwa na shilingi 1,505.1 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 85. Vile vile, sekta ya nishati na madini ilitengewa shilingi 539.3 bilioni ikilinganishwa na shilingi 327.2 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 65.

103. Katika mwaka wa fedha 2011/12, sekta ya kilimo na umwagiliaji ilitengewa kiasi cha shilingi 926.2 bilioni ikilinganishwa na shilingi 903.8 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 2.5. Vile vile, sekta ya elimu ilitengewa shilingi 2,283 bilioni ikilinganishwa na shilingi 2,045.4 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 12. Sekta ya maji ilitengewa shilingi 621.6 bilioni ikilinganishwa na shilingi 397.6 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 56 wakati sekta ya afya ilitengewa shilingi 1,209.1 bilioni ikilinganishwa na shilingi 1,205.9 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 0.3.

Deni la Taifa

104. Hadi kufikia mwishoni mwa Desemba 2011, deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na sekta binafsi lilifikia shilingi 18,819.4 bilioni, sawa na ongezeko la asilimia 12.6 ikilinganishwa na shilingi 16,708.2 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2010. Kati ya kiasi hicho, shilingi 15,928.8 bilioni zilikuwa ni deni la Serikali na shilingi 2,890.6 bilioni ni deni la sekta binafsi. Kuongezeka kwa deni kulitokana na mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, malimbikizo ya riba kwa mikopo ya nje kwa nchi zinazotakiwa kutoa msamaha wa madeni lakini bado hazijatoa na kushuka kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na dola ya Kimarekani.

Deni la Ndani

105. Hadi kufikia Disemba 2011, deni la ndani la Serikali lilifikia shilingi 4,641 bilioni ikilinganishwa na shilingi 4,385.4 bilioni mwezi Disemba, 2010, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Hii inatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya

Serikali kugharamia miradi ya miundombinu na utumiaji wa dhamana za muda mfupi za Serikali kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei katika uchumi.

106. Uchambuzi wa deni la ndani la Serikali kwa makundi yanayohodhi ulibainisha kuwa benki za biashara zinahodhi sehemu kubwa ya deni hilo. Hadi kufikia Desemba 2011, benki za biashara zilikuwa zinahodhi asilimia 48.5 ya deni la ndani ikilinganishwa na asilimi 48.8 ya kipindi kama hicho mwaka 2010. Hii ilichangiwa na kukua kwa sekta ya benki nchini pamoja na hofu ndogo ya kuikopesha Serikali ikilinganishwa na sekta binafsi. Benki kuu ya Tanzania ni ya pili ikihodhi asilimia 26.9, mifuko ya hifadhi ya jamii asilimia 23.5 na watu binafsi na mashirika madogo asilimia 1.2.

Kielelezo Na.4.1: Deni la Ndani kwa Mkopeshaji, hadi Desemba 2011



Kielelezo Na.4.1: Deni la Ndani kwa Mkopeshaji, hadi Desemba 2011



Deni la Nje

107. Hadi kufikia Disemba 2011, deni la Taifa la nje lilikuwa Dola za Kimarekani 8,959.6 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 8,363 milioni mwishoni wa mwezi Disemba 2010, hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Kati ya hizo, dola za Kimarekani 7,133 milioni zilikuwa ni deni la Serikali na dola 1,826.6 milioni ni deni la sekta binafsi. Aidha, deni la Serikali la nje liliongezeka kwa asilimia 9.2 katika kipindi hicho ikilinganishwa na dola za Kimarekani 6,529.6 milioni mwishoni wa mwezi Disemba 2010. Kuongezeka kwa deni kulitokana na mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, malimbikizo ya riba kwa mikopo ya nje kwa nchi zinazotakiwa kutoa msamaha wa madeni lakini bado hazijatoa.

Deni la Nje kwa Wakopeshaji

108. Mchanganuo wa deni la Serikali la nje kwa wakopeshaji unaonesha kwamba, wakopeshaji wakubwa ni mashirika ya fedha ya kimataifa. Hadi kufikia Desemba 2011, mashirika ya fedha ya kimataifa yalichangia asilimia 67 ikilinganishwa na asilimia 72 mwaka 2010, mikopo kutoka nchi marafiki zilichangia asilimia 25 sawa na mwaka 2010 na mikopo yenye masharti ya kibiashara ilichangia asilimia 8. Serikali imedhamiria kuendelea kukopa kutoka

vyanzo nafuu na kuhakikisha kwamba mikopo yote hasa ya kibiashara inatumika kugharamia miradi ya maendeleo.

Kielelezo Na.4.2: Deni la Nje kwa Mkopeshaji, hadi Desemba 2011



MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na. 25 — Sh. milioni

	2006/07 Halisi	2007/08 Halisi	2008/09 halisi	2009/10 halisi	2010/11 Halisi	2011/12 Bajeti	2011/12 Matokeo hadi Machi	2011/12 Matarajio hadi Juni
A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri)	2739022	3634581	4293075	4661540	5736266	7126448	5157554	7036821
MAPATO YA NDANI	2739022	3634581	4293075	4661540	5577986	6775952	5037554	6836821
1. Mapato yatokanayo na Kodi	2529439	3359250	4043674	4427834	5293277	6214714	4765452	6294194
Ushuru wa Forodha na Excise Duty	765644	965498	1130860	1214626	1512135	1686789	1159933	1641299
Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	861050	1110951	1333789	1488452	1632863	2217480	1527166	2127154
Bidhaa toka nje	431614	550289	641392	729040	905611	1181936	796208	1124338
Bidhaa za ndani	429436	560661	692397	759412	727252	1035544	730958	1002816
Kodi ya Mapato	790877	1028902	1257861	1388778	1719790	1910582	1644209	2073193
Kodi nyingine	218581	382792	462544	499497	601448	627862	550239	653299
Marejesho (Refunds Accounts)	-106713	-128893	-141380	-163519	-172959	-228000	-116095	-200752
2. Mapato yasiyotokana na Kodi	209583	275331	249401	233707	284709	561238	272102	542627
3. Mapato ya Halmashauri					158280	350497	120000	200000
B. JUMLA YA MATUMIZI	4474680	5208996	6811827	8173749	9439407	12639939	7084574	12979555
1. Matumizi ya Kawaida	3137469	3398024	4681459	5562443	6690370	7714330	4703330	8619469
2. Matumizi ya Maendeleo	1337211	1810972	2130368	2611306	2749037	4925609	2381243	4360086
Fedha za ndani	503291	567421	906023	1004530	984555	1871472	1118370	1471472
Fedha za nje	833920	1243551	1224345	1606776	1764482	3054137	1262873	2888613
C. NAKISI/SALIO (A-B)	-1735658	-1574415	-2518752	-3512209	-3703141	-5513491	-1927020	-5942734
D. KUZIBA NAKISI	1735660	1574415	2518752	3512209	4423391	6324392	2518493	5636935
1. Fedha kutoka nje	1689337	2302805	2201485	2784944	2776309	5128368	2371384	4615832
Ruzuku	971547	1573195	1257283	1405288	1627425	2717928	1385219	2634090
Basket support	47331	200628	151370	194071	220681	296000	105729	252000
Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL	266946	365038	331315	558320	173806	168623	163525	134742
Mikopo ya miradi	433203	209342	488795	695597	643395	741000	367386	778000
Mikopo ya masharti ya kibiashara					153948	1271634	409375	931000
Kulipia madeni ya nje (Amortization Forei	-29690	-45399	-27278	-68331	-42946	-66817	-59850	-114000
2. Fedha za Ndani	46323	-728390	317267	727265	1647081	1196025	147109	1021103
Mikopo isiyo ya mabenki	212475	-19795	1108	-24754	337494	0	0	0
Mikopo ya mabenki	25533	-316755	212567	593023	906837	393360	449635	402000
Mikopo ya ndani (Rollover)				714315	720249	810902	518350	810902
Mapato ya Ubinafsishaji	0	0	45000	9659	0	0	0	0
Marekebisho (Adjustment to Cash)	-60370	-78308	275298	595034	162629	0	-629077	0
Kulipia madeni ya ndani (amortization)	0	-14648	0	-723776	0	-8237	-8237	-8237
Expenditure float	-131315	-298884	-216706	-436236	-480127	0	-183562	-183562

Chanzo: Wizara ya Fedha


MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI
Sh. milioni
14000000
12000000
10000000
8000000
6000000
4000000
2000000
0
-2000000
-4000000
-6000000
-8000000
2006/07
2007/08
2008/09
2009/10
2010/11
2011/12
MAPATO YA NDANI
B. JUMLA YA MATUMIZI
C. NAKISI/SALIO (A-B)

MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI

Jedwali Na. 26 Sh.milioni

	2008/2009			2009/2010			2010/2011			2011/2012*		
	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
1 HUDUMA ZA KAWAIDA.	**1985848**	**516184**	**25221913**	**2895011**	**717801**	**3612812**	**3575949**	**959512**	**4535460**	**4100600**	**1026806**	**5127405**
1.1 Utawala	1,811,197	432,437	19264490	2,695,305	613,601	3308906	3,311,734	822,100	4133834	3,872,620	881,446	4754066
1.2 Misaada ya kiuchumi kutoka nje	10,179	0	89445	6,826	0	6826	7,261	0	7261	13,500	39,025	52525
1.3 Huduma za utafiti	19,727	5,495	1311092	21,751	14,586	36337	22,934	42,731	65665	23,623	79,524	103148
1.4 Huduma	141,296	70,470	4426489	163,031	79,588	242619	175,065	85,041	260106	179,622	6,909	186530
1.5 Huduma za utawala zisizotajwa hapo juu	3,448	7,782	130397	8,098	10,026	18124	58,955	9,640	68594	11,235	19,901	31136
2 ULINZI	**331524**	**55879**	**3840174**	**393868**	**33650**	**427518**	**459665**	**145304**	**604970**	**529513**	**156193**	**665805**
2.1 Utawala	287,446	8,959	3,743,225	372,082	33,650	405,732	459,355	31,104	490459	529,260	19,901	529260
2.2 Misaada ya nje ya ulinzi	0	0	0	0	0	0	213	114,200	114413	149	128,798	128946
2.3 Utafiti na maendeleo ya ulinzi	242	46,920	47,162	360	0	360	98	0	98	104	7,494	7598
2.4 Huduma za ulinzi zisizotajwa hapo juu	43,837	0	49,787	21,426	0	21,426	0	0	0	0	0	0
3 USALAMA	**226497**	**35841**	**2158861**	**268311**	**63957**	**332267**	**339889**	**54987**	**394876**	**401467**	**38026**	**439493**
3.1 Polisi na zimamoto	140,819	14,878	1,346,685	162,538	25,371	187,909	210,770	17,718	228,488	228,048	4,955	233,003
3.2 Mahakama	49,298	8,812	413,046	52,882	18,433	71,315	67,379	7,661	75,040	88,710	1,000	89,710
3.3 Magereza	10,453	800	79,064	8,602	800	9,402	6,752	800	7,552	7,359	26,809	34,168
3.4 Huduma za usalama zisizotajwa hapo juu	25,927	11,350	320,065	44,289	19,353	63,642	54,988	28,809	83,796	77,350	5,263	82,613
4 ELIMU	**500915**	**105614**	**5286541**	**406638**	**135302**	**541939**	**551792**	**145376**	**697169**	**562972**	**319116**	**882088**
4.1 Elimu ya msingi	6,027	7,925	571,271	6,977	3,889	10,866	2,839	3,115	5,955	1,355	12,400	13,755
4.2 Elimu ya sekondari	145,276	26,879	1,138,879	2,306	550	2,856	1,732	14,680	16,412	1,120	117,752	118,872
4.3 Elimu ya juu	302,705	45,570	2,968,629	338,445	113,112	451,557	483,067	113,213	596,279	480,788	0	480,788
4.4 Elimu isiyo pambanuliwa	0	17,213	66,516	946	4,300	5,246	3,315	2,295	5,610	2,260	1,192	3,452
4.5 Huduma za ziada kwa elimu	0	0	0	184	0	184	125	0	125	122	10,294	10,416
4.6 Huduma za elimu zisizotajwa hapo juu	46,908	8,027	541,245	57,779	13,450	71,230	60,715	12,073	72,789	77,326	177,478	254,805
5 AFYA	**221093**	**187226**	**3728935**	**236500**	**255412**	**491912**	**242351**	**389284**	**631635**	**233180**	**112408**	**345589**
5.1 Huduma za hospitali	34,573	146,037	1,291,535	36,466	190,201	226,667	35,163	304,310	339,472	31,847	111,209	143,056
5.2 Kliniki, matibabu, huduma za meno n.k.	179,284	40,939	2,079,907	191,027	64,873	255,900	198,311	84,474	282,785	193,435	0	193,435
5.3 Huduma za afya	0	250	160,519	0	338	338	0	500	500	0	0	0
5.4 Madawa na vifaa	3,513	0	46,978	5,398	0	5,398	8,878	0	8,878	7,898	1,199	9,098
5.5 Utafiti wa afya	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
5.6 Huduma za afya zisizotajwa hapo juu	3,723	0	149,995	3,610	0	3,610	0	0	0	0	0	0
6 USALAMA, USTAWI NA HUDUMA ZA JAMII	**70275**	**7928**	**843817**	**99366**	**13633**	**112999**	**94725**	**9255**	**103980**	**103466**	**10498**	**113964**
6.1 Usalama wa jamii	1,966	290	57,616	1,800	590	2,390	1,494	738	2,231	591	4,337	4,928
6.2 Ustawi na huduma za jamii	64,940	7,112	757,473	95,620	12,665	108,285	91,771	5,663	97,434	101,901	3,052	104,953
6.3 Huduma nyingine za jamii zisizotajwa hapo juu	3,369	526	28,727	1,947	378	2,325	1,460	2,855	4,315	974	3,109	4,083
7 NYUMBA NA HUDUMA ZA JAMII	**20337**	**144471**	**2315415**	**26179**	**215862**	**242040**	**33629**	**243760**	**277389**	**28450**	**417765**	**446215**
7.1 Nyumba na ustawi wa jamii	5,620	586	254,945	8,143	607	8,750	8,623	477	9,101	10,574	398,634	409,208
7.2 Usambazaji wa Maji	7,032	140,988	1,875,636	8,763	205,889	214,652	8,868	224,410	233,278	9,330	0	9,330
7.3 Usafi wa mazingira	6,367	2,896	181,600	7,345	9,365	16,711	4,446	18,872	23,318	6,470	18,301	24,772
7.4 Umeme wa barabarani	0	0	0	0	0	0	11,693	0	11,693	2,076	829	2,906
7.5 Huduma za nyumba na za jamii zisizotajwa hapo juu	1,318	0	3,234	1,928	0	1,928	0	0	0	0	0	0
8 HUDUMA ZINGINE ZA JAMII	**9715**	**7926**	**17641**	**13434**	**8939**	**22373**	**26413**	**9218**	**35631**	**28389**	**302043**	**330432**
8.1 Utamaduni, burdani, dini na huduma zingine	9,715	7,926	17,641	13,434	8,939	22,373	26,413	9,218	35,631	28,389	302,043	330,432

Jedwali hili linaendelea ukurasa unaofuata....

...Jedwali Na. 26 linaendelea

	2008/09			2009/10			2010/11*			2011/12*		
	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
9 MAFUTA NA UMEME	**33127**	**116822**	**149948**	**32801**	**153547**	**186348**	**36735**	**166453**	**203188**	**39053**	**102056**	**141109**
9.1 Mafuta	33,127	116,822	149,948	32,801	153,547	186,348	36,735	166,453	203,188	39,053	102,056	141,109
9.2 Umeme	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
9.3 Huduma zingine za mafuta na umeme	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
10 KILIMO, MISITU, UVUVI NA UWINDAJI	**177264**	**80511**	**257775**	**178486**	**161972**	**340457**	**192442**	**147366**	**339808**	**191700**	**31657**	**223357**
10.1 Kilimo	127,232	55,631	182,863	122,722	117,640	240,362	141,708	116,765	258,473	133,596	0	133,596
10.2 Misitu	11,681	6,481	18,163	14,754	12,399	27,153	16,420	5,473	21,893	14,263	4,970	19,233
10.3 Uvuvi na uwindaji	17,116	8,648	25,764	19,888	17,999	37,887	20,764	13,309	34,073	24,991	9,206	34,197
10.4 Utafiti wa kilimo	14,700	9,751	24,450	14,621	13,133	27,754	12,926	11,321	24,247	18,145	448	18,594
10.5 Huduma zingine za kilimo, misitu, uvuvi na uwindaji	6,535	0	6,535	6,501	800	7,301	624	498	1,122	704	17,033	17,737
11 MADINI, VIWANDA NA UJENZI	**7450**	**3729**	**11179**	**18627**	**20295**	**38923**	**27717**	**19394**	**47110**	**32240**	**800**	**33040**
11.1 Madini	5,544	1,537	7,081	13,590	16,095	29,685	21,121	15,580	36,701	24,417	800	25,217
11.2 Viwanda	192	392	584	497	1,200	1,697	434	814	1,247	688	0	688
11.3 Ujenzi	1,715	1,800	3,514	4,540	3,000	7,540	5,653	3,000	8,653	6,566	0	6,566
11.4 Huduma zingine za madini, viwanda na ujenzi	0	0	0	0	0	0	509	0	509	570	0	570
12 USAFIRI NA MAWASILIANO	**219957**	**219191**	**439148**	**280063**	**567736**	**847800**	**303075**	**871297**	**1174372**	**255770**	**1399898**	**1655668**
12.1 Usafiri wa Barabara	166,065	210,883	376,948	552	0	552	3,021	0	3,021	3,122	1,200	4,322
12.2 Usafiri majini	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
12.3 Huduma za reli	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
12.4 Usafiri wa anga	0	0	0	0	0	0	0	0	0	250	1,376,888	1,377,138
12.5 Usafirishaji kwa mabomba	0	0	0	0	0	0						
12.6 Huduma ya usafirishaji	40,914	3,850	44,764	257,226	539,668	796,894	280,240	854,967	1,135,206	231,889	3,650	235,539
12.7 Mawasiliano	11,561	3,580	15,141	14,234	2,100	16,334	11,729	5,917	17,646	11,741	12,270	24,011
12.8 Huduma zingine za usafiri na mawasiliano	1,417	878	2,295	8,051	25,968	34,019	8,086	10,413	18,499	8,768	5,891	14,659
13 HUDUMA ZINGINE ZA KI - UCHUMI	**224295**	**219400**	**443695**	**244652**	**441795**	**686446**	**99669**	**639369**	**739038**	**127564**	**1021234**	**1148798**
13.1 Biashara - maghala, hoteli na migahawa	6,211	3,077	9,288	9,520	4,867	14,387	9,795	7,470	17,264	9,037	63	9,099
13.2 Utalii	6,074	1,753	7,827	6,127	4,444	10,571	11,521	62	11,583	10,964	408,310	419,274
13.3 Huduma za miradi	194,163	145,816	339,978	204,160	235,445	439,605	52,570	333,869	386,439	78,956	1,401	80,357
13.4 Huduma za uchumi na biashara mbali na zinazohusu	9,338	13,337	22,675	10,837	2,275	13,112	12,180	2,523	14,703	11,911	585	12,496
13.5 Huduma za kazi	3,048	2,934	5,981	4,693	5,010	9,704	4,986	778	5,765	7,900	0	7,900
13.6 Huduma nyinginezo za maendeleo	5,461	52,484	57,945	9,314	189,753	199,067	8,618	294,666	303,285	8,796	610,876	619,671
14 MATUMIZI MENGINEYO	**788840**	**4211**	**793051**	**1613418**	**12051**	**1625469**	**1829578**	**23181**	**1852759**	**1984948**	**6859**	**1991806**
14.1 Deni la Taifa	693,748	0	693,748	1,528,094	0	1,528,094	1,783,211	0	1,783,211	1,938,483	6,859	1,945,342
14.2 Huduma za Fedha	94,218	4,211	98,429	84,483	12,051	96,534	45,805	10,265	56,070	45,907	0	45,907
14.3 Malipo ya uzeeni	875	0	875	842	0	842	562	12,916	13,478	557	0	557
JUMLA	**4,817,137**	**1,704,934**	**45,508,092**	**6,707,354**	**2,801,950**	**9,509,304**	**7,813,631**	**3,823,755**	**11,637,386**	**8,619,311**	**4,945,359**	**13,544,770**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Makadirio

SURA YA 5

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

Ujazi wa Fedha na Karadha

109. Mwaka 2010/11, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka na kufikia shilingi 4,927.1 bilioni kutoka shilingi.4,134.7 bilioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kwa asilimia 19.4 kutoka shilingi 7,287.5 bilioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 8,698.7 bilioni mwaka 2010/11. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia shilingi 11,957.9 bilioni kutoka shilingi 9,801.4 bilioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 22.0. Kwa ujumla, ukuaji wa fedha kwa mwaka 2010/11 ulikuwa mdogo ukilinganisha na ule wa mwaka 2009/10.

110. Hadi kufikia mwezi Desemba 2011, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikua kwa asilimia 15.0 ikiwa ni chini ya lengo la asilimia 21.3 na ukuaji wa asilimia 21.8 Desemba 2010. Vile vile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 18.2 Desemba 2011 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 25.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2010 na lengo la asilimia 20.7. Kasi ndogo ya ukuaji wa ujazi wa fedha ulitokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni kwenye benki ukilinganisha na ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Katika kipindi hiki, rasilimali katika fedha za kigeni (NFA) ilikua kwa asilimia 3.5 tu ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 23.2 Desemba 2010, hususan kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje.

111. Karadha nchini iliongezeka kwa asilimia 37.4 kutoka shilingi 6,164.7 bilioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 8,470.5 bilioni mwaka 2010/11. Aidha, hadi Desemba 2011, karadha ziliongezeka na kufikia shilingi 9,053.9 bilioni ikilinganishwa na shilingi 6,790.4 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na ukuaji wa asilimia 33.3.

Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

112. Kwa mwaka ulioishia Desemba 2011, kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 27.6 ikilinganishwa na asilimia 20.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na kupungua kwa ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni kwenye benki na kupungua kwa mikopo ya serikali kutokana na kuimarika kwa mapato ya ndani.

113. Sehemu kubwa ya mikopo ilielekezwa katika shughuli binafsi ambazo zilipata wastani wa asilimia 21.1 ya mikopo yote iliyotolewa kwa sekta binafsi. Shughuli nyingine zilizonufaika na mikopo hiyo ni pamoja na biashara (asilimia 20.6), uzalishaji viwandani (asilimia 12.8) na shughuli za kilimo (asilimia 12.6).

114. Mwaka 2011, dhamana za Serikali ziliouzwa zilipungua kutoka mauzo yenye thamani ya shilingi 3,124.3 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 2,268.7 bilioni, sawa na upungufu wa asilimia 27.4. Vile vile, Serikali iliuza hati fungani zenye thamani ya shilingi 618.1bilioni ikilinganishwa na shilingi 714 bilioni zilizouzwa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 13.4.

Amana Katika Benki za Biashara

115. Mwaka 2011, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 16.3 kufikia shilingi 11,342.4 bilioni kutoka shilingi 9,748.7 bilioni mwaka 2010. Kati ya hizo, sekta binafsi ilichangia shilingi 10,715.8 bilioni sawa na asilimia 94.5 ya amana zote na Serikali ilichangia asilimia 5.5 iliyobaki. Ongezeko hili lilitokana na kuboreshwa kwa usalama wa kuweka fedha kwenye benki kulikochangiwa na usimamizi madhubuti wa Benki Kuu pamoja na jitihada ambazo benki zimechukua katika kuweka vivutio mbalimbali kwa wateja. Hatua za msingi zilizochukuliwa na benki ni pamoja na kuongeza matawi sehemu mbalimbali nchini, kubuni na kuanzisha huduma mbalimbali za kibenki kwa njia ya simu za mkononi, na mashine za kuweka na kutoa fedha (ATM). Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote uliongezeka na kufikia asilimia 32.8 mwaka 2011 kutoka asilimia 30.0 mwaka 2010 hasa kutokana na kuimarika kwa dola ya Marekani dhidi ya sarafu za mataifa mengine ikiwemo shilingi ya Tanzania.

Mwenendo wa Viwango vya Riba

116. Mwaka 2011, mwenendo wa riba za amana na zile za mikopo ziliimarika ukilinganisha na zilivyokuwa mwaka 2010 kutokana na kuongezeka kwa ushindani katika taasisi za fedha.Wastani wa riba za amana za mwaka mmoja uliongezeka na kufikia asilimia 9.14 mwezi Desemba 2011 kutoka asilimia 7.10 mwezi Desemba 2010. Aidha, kiwango cha riba za mikopo ya mwaka mmoja kilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.37 mwezi Desemba 2010 hadi kufikia asilimia 13.73 mwezi Desemba 2011. Hivyo, tofauti kati ya wastani wa viwango vya riba za amana na za mikopo za mwaka mmoja ilipungua kutoka asilimia 7.26 mwezi Desemba 2010 hadi asilimia 4.59 Desemba 2011. Katika kipindi hicho cha marejeo, riba za dhamana za Serikali ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.2 ikilinganishwa na asilimia 6.32 Desemba 2010.

Maboresho ya Sekta ya Fedha

117. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza programu ya mageuzi ya sekta ya fedha ili kuhakikisha kwamba sekta hii inachangia kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kukuza pato la Taifa. Kanuni zinazohusiana na masuala ya mikopo kwa ajili ukodishaji wa vifaa, na mikopo ya nyumba zilichapishwa kwenye gazeti la Serikali la tarehe 29, Aprili 2011. Aidha, Serikali kupitia kampuni iliyoanzishwa ya utoaji mikopo ya nyumba (TMRC) ilianza utekelezaji wa mradi wa kutoa mikopo kwa ajili ya makazi mwezi Januari, 2011 . Vile vile, utafiti juu ya soko la sekta ya nyumba ulianza mwezi Septemba 2011 wakati ambapo utoaji wa mikopo ya nyumba ulianza rasmi mwezi Novemba, 2011.

118. Mwaka 2011, Serikali iliendelea na mchakato wa uanzishaji wa chombo/ taasisi ya utoaji wa taarifa sahihi zinazohusu waombaji wa mikopo (Credit Rerefence Bureau) na taarifa sahihi za wakopaji (Credit Reference Databank). Mkataba ulisainiwa mwezi Oktoba, 2011 na mshauri elekezi alishaanza zoezi la kuweka vifaa/mitambo na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa chombo hicho. Vile vile, mchakato wa kuandaa mfumo wa hifadhi (database) ya taarifa za wakopaji ulianza mwezi Januari, 2012. Hii ni pamoja na kupitia mifumo ya sheria zilizopo zinazohusiana na taarifa za wakopaji, pamoja na jaribio la kukusanya taarifa za

wakopaji kwenye mabenki. Kuanzishwa kwa Chombo hiki kutazisaidia benki kuweza kufuatilia mwenendo na historia ya taarifa sahihi za wakopaji ambazo zimekuwa ni kikwazo kimojawapo katika kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za kifedha nchini.

119. Mwaka 2011, taarifa kuhusu utafiti wa uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilikamilika na mapendekezo yaliyotolewa yaliridhiwa na Serikali mwezi Januari, 2012. Mchakato kwa ajili ya uanzishaji wa benki hiyo unaendelea kama ilivyopangwa chini ya kamati maalum iliyoundwa kufuatilia utekelezaji huo. Benki hii inategemewa kuanza kazi rasmi mwezi Desemba, 2012.

Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma

120. Idadi ya wanachama wanaochangia katika Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma iliongezeka hadi wanachama 180,049 mwaka 2011 kutoka wanachama 160,068 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.5. Vilevile, michango ya wanachama ikijumuisha faini iliongezeka na kufikia shilingi 188 bilioni mwaka 2011 kutoka shilingi 147.7 bilioni mwaka 2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 27.3. Aidha, katika kipindi kama hicho, malipo ya pensheni kwa wastaafu yalikuwa shilingi 71.9 bilioni ikilinganishwa na shilingi 63.8 bilioni zilizolipwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.7. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa idadi ya wastaafu, kuongezeka kwa malipo ya mkupuo yaliyofanywa na Mfuko kwa wafanyakazi waliostaafu wa Mashirika mbalimbali, na kuongezeka kwa wafanyakazi wanaoacha kazi kufuatia Taasisi zao kurekebishwa au kufungwa. Hadi kufikia Desemba 2011, thamani ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma iliongezeka na kufikia shilingi 896.1 bilioni ikilinganishwa na shilingi 722.5 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 24.0.

121. Mwaka 2011, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma uliendelea kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali vikiwemo amana za mabenki, dhamana, hisa za makampuni na majengo. Hadi kufikia Desemba 2011, thamani ya uwekezaji kwenye vitega uchumi vya mfuko ilikuwa na jumla ya shilingi 872.3 bilioni ikilinganishwa na shilingi 706.9 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Jedwali Na. 5.1 linaonesha mchanganuo wa

uwekezaji. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi 35.2 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 79.8 bilioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 126.7. Hii imetokana na kuongezeka kwa thamani ya hisa za makampuni katika soko la mitaji.

Jedwali Na. 5.1: Maeneo ya Uwekezaji (Tshs. Bilioni)

Eneo la Uwekezaji	**2010 (Des)**	**2011 (Des)**	**Badiliko (%)**
Amana za Benki na Dhamana	452.77	573.34	26.63
Hisa za Makampuni	125.9	165.3	31.52
Majengo	89.26	90.75	1.67
Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja	38.9	42.9	10.28
Jumla	**706.83**	**872.29**	**23.41**

Chanzo: Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma

Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma

122. Mwaka 2010/11, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma ulifanya zoezi la usajili wa wanachama wa Mfuko ambao hawakusajiliwa katika mikoa ya Shinyanga, Mbeya, Rukwa, Iringa, Tabora, Mtwara, Ruvuma, Lindi, Kagera, Mara, Manyara, Arusha na Mwanza. Katika zoezi hili, jumla ya wanachama 21,398 walisajiliwa ikiwa ni asilimia 58.2 ya lengo la kusajili wanachama 36,798 kwa kipindi hicho. Idadi hii, inafanya jumla ya wanachama wa Mfuko waliosajiliwa hadi kufikia Juni 2011 kuwa 198,823. Aidha, michango kutoka kwa wanachama wa Mfuko ilikuwa shilingi 392,172.15 milioni mwaka 2010/11.

123. Mwaka 2010/11, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya jumla ya shilingi 282,006.3 milioni ikilinganishwa na mafao ya shilingi 145,298.9 milioni yaliyolipwa mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 94.1. Ongezeko hili lilitokana na kuwepo kwa idadi kubwa ya watumishi waliostaafu kwa hiari au kuacha kazi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kisiasa. Vile vile,

thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 22.6 kufikia shilingi 897.97 bilioni Juni 2011 kutoka shilingi 732.38 bilioni Juni 2010.

124. Mwaka 2010/11, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma uliendelea kuwekeza katika vitega uchumi mbalimbali kama vile hatifungani, hisa za makampuni, amana za mabenki, mikopo, majengo, dhamana za Serikali na miradi maalum ya Serikali. Jumla ya thamani ya uwekezaji wa Mfuko kwa mwaka 2011/12 ilikuwa shilingi 568,139.20 milioni. Kati ya hizo, shilingi 387,267.67 milioni (sawa na asilimia 68.2 ya uwekezaji wote) ziliwekezwa kwenye amana za mabenki ikifuatiwa na uwekezaji katika majengo ambao ulikuwa shilingi 98,936.01 milioni (asilimia 17.4). Aidha, hadi kufikia Juni 2011, mapato yaliyotokana na uwekezaji yalikuwa shilingi 59,723.44 milioni ukilinganisha na shilingi 41,094.2 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 45.3. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa udhamini wa Mfuko katika kugharamia miradi ya Serikali.

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii

125. Mwaka 2010/11, Mfuko wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii ulikuwa na jumla ya wanachama 521,629 ikilinganishwa na wanachama 506,218 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 3.04. Aidha, Mfuko ulikusanya michango kutoka kwa wanachama yenye thamani ya shilingi 394,681.61 milioni mwaka 2010/11 ikilinganishwa na shilingi 295, 787.14 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 33.43. Ongezeko hili lilitokana na usajili wa wanachama wapya 98,894, uliotokana na usajiri wa waajiri wapya 1,995 kuwasilisha michango kwa wakati.

126. Mafao yaliyotolewa kwa wanachama yalikuwa shilingi 136,596.50 milioni mwaka 2010/11 ikilinganishwa na shilingi 110,135.33 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 24.03. Aidha, idadi ya wanachama waliopata mafao iliongezeka hadi kufikia wanachama 222,776 katika mwaka 2010/11, kutoka wanachama 138,999 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 60.27. Kuongezeka kwa wanachama waliolipwa mafao, kulitokana na wanachama waliopata fao la matibabu pekee, ambao walikuwa 163,944, sawa na asilimia 35.89 ya wanachama wote waliolipwa mafao katika mwaka 2010/11.

127. Mwaka 2010/11, thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi iliongezeka hadi shilingi 1,216,624.46 milioni kutoka shilingi 1,029,206.18 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 18.21. Thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka hadi shilingi 271,171.36 milioni mwaka 2010/11, kutoka shilingi 185,316.8 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 45.92. Mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi yalikuwa shilingi 94,668.47 milioni mwaka 2010/11 kutoka shilingi 92,451.94 milioni, mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 2.40. Kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi, kulitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika miradi ya maendeleo katika majengo, mikopo ya muda mrefu, amana za muda maalumu na dhamana za Serikali.

128. Thamani halisi ya mali za Mfuko kwa ajili ya mafao iliongezeka kwa shilingi 224,011.77, kutoka shilingi 1,129,179.92 milioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 353,191.69 milioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 7.70.

Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali

129. Mwaka 2010/11, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali iliongezeka hadi wanachama 41,879 kutoka wanachama 35,279 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 18.7. Ongezeko hili lilichangiwa na uandikishaji wa wanachama wengi kutoka sekta isiyo rasmi. Vile vile, michango kutoka kwa wanachama iliongezeka hadi shilingi 25,688.9 milioni mwaka 2010/11 kutoka shilingi 16,321.5 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 57.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wanachama na kuanzishwa kwa njia mbadala za ukusanyaji michango, zikiwemo matumizi ya simu za mkononi. Katika kipindi hicho, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka kwa asilimia 10.6 kufikia shilingi 3,675.5 milioni ikilinganishwa na shilingi 3,323.6 milioni zilizolipwa mwaka 2009/10.

130. Mwaka 2010/11, thamani ya uwekezaji wa Mfuko iliongezeka kwa asilimia 24.0 na kufikia shilingi 101,272.5 milioni ikilinganishwa na shilingi 81,673.5 milioni zilizowekezwa mwaka 2009/10. Aidha, mwaka 2010/11,

mapato kutokana na uwekezaji yalikuwa shilingi 9,809.3 milioni ikilinganishwa na mapato ya shilingi 7,693.6 milioni yaliyopatikana mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 27.5. Hii ilitokana na tahadhari kubwa iliyochukuliwa katika kuchagua maeneo ya uwekezaji yanayoweza kuleta faida kubwa na yenye kupunguza uwezekano wa kupata hasara.

131. Thamani ya rasilimali halisi za Mfuko ziliongezeka kutoka shilingi 91,282.3 milioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 119,404.4 milioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Vile vile, thamani ya rasilimali zote za Mfuko ziliongezeka kwa asilimia 31.0 kutoka shilingi 91,487.5 milioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 119,829.0 milioni mwaka 2010/11.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

132. Mwaka 2010/11, idadi ya wanachama wanaochangia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iliongezeka na kufikia 468,611 kutoka wanachama 373,326 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 25.5. Ongezeko hili lilitokana na marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (1999) ambayo yamewajumuisha wananchi wanaohitaji huduma za Mfuko lakini hawakuwa katika mfumo rasmi wa ajira kulingana na matakwa ya sheria iliyoanzisha Mfuko. Aidha, michango kutoka kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi 90,084.06 milioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 134,890.98 milioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 49.7. Hii ilitokana na ongezeko la wanachama wapya katika Mfuko na nyongeza ya mishahara inayofanywa na Serikali kila mwaka.

133. Hadi kufikia Juni 2011, Mfuko ulisajili jumla ya vituo 5,673 vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na vituo 5,576 vilivyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 1.7. Kati ya vituo hivyo vilivyosajiliwa mwaka 2011, vituo 4,661 sawa na asilimia 82.5 ni vya Serikali, vituo 655 (asilimia 11.5) ni vya mashirika ya dini, vituo 26 (asilimia 0.5) ni vya watu binafsi na vituo 331 (asilimia 5.8) ni maduka ya dawa.

134. Mwaka 2010/11, Mfuko uliendelea kutoa huduma mbalimbali za mafao kwa wanachama wake kupitia vituo vilivyosajiliwa vya Serikali, binafsi na

mashirika ya dini. Hadi kufikia Juni 2011, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi 44,351.55 milioni ikiwa ni asilimia 96.2 ya madai ya shilingi 46,125.61 milioni ikilinganishwa na mafao yenye thamani ya shilingi 25,154.08 milioni sawa na asilimia 90.4 ya madai ya shilingi 27,825.31 milioni yaliyopokelewa mwaka 2009/10. Aidha, malipo yaliyofanyika mwaka 2010/11 yaliongezeka kwa asilimia 76.3 kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya kadi za bima ya afya kufuatia zoezi la uhamasishaji kwa wananchi lililofanywa na Mfuko juu ya umuhimu wa matumizi ya kadi za bima, kuongezeka kwa vituo vya afya vilivyosajiliwa, kuimarika kwa ubora wa huduma za afya na kuongezeka kwa mwamko wa wananchi juu ya umuhimu wa kupima na kupata matibabu stahiki.

135. Mwaka 2010/11, Mfuko uliendelea kuwekeza kwenye dhamana, hatifungani za Serikali, amana za mabenki na hisa za makampuni. Katika kipindi hicho, mapato yatokanayo na vitega uchumi yaliongezeka na kufikia shilingi 25,065.08 milioni kutoka shilingi 17,115.73 milioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 46.4. Ongezeko hili lilitokana na hatua ya Mfuko kutumia kikamilifu fursa za uwekezaji zilizojitokeza katika kipindi hicho.

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa

136. Mwaka 2010/11, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa iliongezeka kwa asilimia 9.1 na kufikia wanachama 80,529 ikilinganishwa na wanachama 73,833 mwaka 2009/10. Aidha, michango kutoka kwa wanachama ilikuwa shilingi 80.51 bilioni katika mwaka 2010/11 ikilinganishwa na shilingi 54.24 bilioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 48.4. Vile vile, mafao yaliyolipwa kwa wanachama mwaka 2010/11 yalikuwa shilingi 26.50 bilioni ikilinganishwa na shilingi 22.5 bilioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 17.8.

137. Thamani ya uwekezaji katika vitega uchumi iliongezeka kutoka shilingi 265.9 bilioni mwaka 2009/10 hadi shilingi 366.0 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 31.9. Aidha, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka kutoka shilingi 133.5 bilioni mwaka 2009/10, hadi shilingi 145.5 bilioni mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 9.0.

138. Mwaka 2010/11, mapato kutokana na uwekezaji katika vitega uchumi vya Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 9.2 na kufikia shilingi 28.63 bilioni kutoka shilingi 26.22 bilioni mwaka 2009/10. Hii ilitokana na kuongezeka kwa shughuli za uwekezaji katika mitaji mbalimbali ikiwemo mali zisizohamishika, mikopo ya muda mrefu, amana za muda maalum na dhamana za Serikali. Aidha, thamani halisi ya mali za Mfuko ilikuwa shilingi 450.19 bilioni mwaka 2010/11 ikilinganishwa na shilingi 361.96 bilioni mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 24.4.

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

139. Mwaka 2011, kulikuwa na ongezeko la kampuni moja iliyoandikishwa kufanya biashara ya bima nchini, na hivyo kufanya idadi ya makampuni yaliyoandikishwa kufanya biashara hiyo kufikia 26. Mgawanyo wa huduma zitolewazo na makampuni hayo ni kama ifuatavyo: Kampuni 21 ziliandikishwa kufanya biashara ya bima ya kawaida pekee; kampuni mbili biashara ya bima za maisha pekee na kampuni tatu biashara ya bima za maisha na kawaida. Aidha, mauzo katika soko la bima kwa mwaka 2011 yalikua kwa asilimia 19.2 kufikia mauzo ya shilingi 342.1 bilioni ikilinganishwa na shilingi 286.9 bilioni mwaka 2010. Bima za kawaida zilichangia asilimia 89.2 ya mauzo yote wakati bima za maisha zilichangia asilimia 10.8 ya jumla ya mauzo yote. Mauzo ya bima za kawaida yalikua kwa asilimia 19.4 kufikia shilingi 305.3 bilioni mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 255.7 bilioni mwaka 2010. Vile vile, mauzo ya bima za maisha yalikua kwa asilimia 18.0 kufikia shilingi 36.8 bilioni ikilinganishwa na mauzo ya shilingi 31.2 bilioni mwaka 2010, ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa Makampuni yanayotoa huduma za bima ya maisha, uelewa wa watu kuhusu umuhimu wa bima ya maisha na uimara wa soko la bima ya maisha.

140. Hadi kufikia Desemba 2011, makampuni ya bima za kawaida yalipata hasara yenye thamani ya shilingi 9.2 bilioni ikilinganishwa na hasara ya shilingi 2.0 bilioni mwaka 2010. Hasara hizi zimetokana na ongezeko la madai yenye thamani kubwa na kupanda kwa gharama za uendeshaji. Thamani ya mali za makampuni ya bima kwa mwaka 2011 zilifikia shilingi 420.6 bilioni ikilinganishwa na mali za shilingi 355.7 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko

la asilimia 18.3. Madeni ya makampuni ya bima yaliongezeka na kufikia shilingi 292.8 bilioni mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 247.8 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia18.2.

Jedwali Na. 5.2: Thamani za Mali na Madeni ya Makampuni ya Bima (Shs. Milioni)

Maelezo	**2007**	**2008**	**2009**	**2010**	**2011**
Jumla ya Mali	212,458	289,456	320,611	355,710	420,643
Ukuaji (%)	13.53	26.60	9.72	10.95	18.25
Jumla ya Madeni	133,081	202,238	219,022	247,789	292,845
Ukuaji (%)	16.32	34.20	7.66	13.13	18.18
Ziada ya Mali	79,377	87,218	101,589	107,921	127,798
Ukuaji (%)	8.85	8.99	14.15	6.23	18.42

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

Soko la Hisa la Dar es Salaam

141. Idadi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) ziliongezeka kutoka kampuni 15 mwaka 2010 hadi kampuni 18 mwaka 2011. Kampuni mpya zilizoorodheshwa mwaka 2011 ni National Media Group, African Barrick Gold na Precision Air. Aidha, idadi ya wawekezaji iliongezeka kutoka 174,013 mwaka 2010 hadi wawekezaji 180,882 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Vile vile, thamani ya hisa zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam zilikuwa shilingi 11,577.1 bilioni mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 4,895.5 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 136. Hii ilitokana na ongezeko la kampuni zilizoorodheshwa na kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji.

142. Soko la Hisa la Dar es Salaam liliuza na kununua jumla ya hisa zenye thamani ya shilingi 50.95 bilioni mwaka 2011 ikilinganishwa na shilingi 35.7 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 42.7. Aidha, katika kipindi hicho, fahirisi katika Soko ilikua kutoka 1,163.89 mwaka 2010 hadi 1,303.23 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 12.0.

143. Mwaka 2011, hatifungani za Serikali ziliorodheshwa sokoni zilipungua kwa asilimia 61.9 kufikia shilingi 615.4 bilioni ikilinganishwa na shilingi 1,615.8 bilioni zilizoorodheshwa mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na kuanguka kwa soko la hatifungani katika nusu ya pili ya mwaka 2011. Aidha, thamani ya hatifungani zilizouzwa na kununuliwa ziliongezeka na kufikia shilingi 423.5 bilioni mwaka 2011 kutoka shilingi 205.8 bilioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 105.8. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uhamasishaji na elimu inayotolewa kwa umma kuhusu masoko ya mitaji, dhamana na uwekezaji.

Jedwali Na. 5.3: Muhtasari wa Utendaji wa Soko la Hisa la Dar es Salaam

Kigezo cha Soko	**2010**	**2011**	**Badiliko (%)**
Jumla ya Hisa zote zilizotolewa sokoni	6,981,012,160	7,742,072,981	10.9%
Thamani ya Hisa zote zilizouzwa/kununuliwa (Shs. Milioni)	35,986	50,955	41.6%
Thamani ya Hisa zote zilizoorodheshwa (Shs. Milioni)	4,895	11,577	136.5%
Idadi ya hisa zilizouzwa na kununuliwa	190,387,510	133,403,198	-29.9%
Idadi ya Maafikiano	11,336	12,209	7.7%
Fahirisi	1,164	1,303	12.0%
Idadi ya wenye akaunti za CDS - Watanzania	173,798	180,558	3.9%
Idadi ya wenye akaunti za CDS - Wageni	215	324	50.7%

Chanzo: Soko la Hisa la Dar es Salaam

Benki ya Posta

144. Mwaka 2011, amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi 120,485 milioni kutoka shilingi 107,327 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.3. Ongezeko la amana lilitokana na kupanuka kwa wigo wa kutolea huduma kwa wateja hususan matumizi ya mtandao wa ATM za Umoja Switch. Sambamba na ongezeko la amana, idadi ya wateja waliojiunga na Benki iliongezeka kutoka wateja 582,772 mwaka 2010 hadi wateja 612,005 kufikia mwishoni mwa Desemba 2011, sawa na ongezeko la asilimia 5.0.

145. Mwaka 2011, Benki ya Posta iliendelea kuwekeza rasilimali zake katika dhamana za Serikali, mabenki mengine na dhamana za makampuni binafsi. Thamani ya vitega uchumi vyote hadi Desemba 2011 iliongezeka na kufikia shilingi 121,002 milioni kutoka shilingi 112,758 milioni mwaka 2010, likiwa ni ongezeko la asilimia 7.3.

Jedwali Na. 5.4: Thamani ya Uwekezaji katika Vitega Uchumi (Shs. Milioni)

Kitega Uchumi	**Desemba 2010**	**Desemba 2011**	**Ongezeko (%)**
Amana katika mabenki mengine	3,348	4,988	49
Dhamana za Serikali	16,876	16,113	-4.5
Dhamana za Serikali za muda mrefu	26,036	33,348	28.1
Dhamana za Makampuni Binafsi	1,373	1,273	-7.3
Mikopo ya aina zote	64,635	65,004	0.6
Amana za Ziada za TPC	490	276	-43.7
Jumla	**112,758**	**121,002**	**7.3**

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

146. Mwaka 2011, uwekezaji katika mikopo uliongezeka na kufikia shilingi 65,004 milioni kutoka shilingi 64,635 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 0.6. Ongezeko dogo la utoaji wa mikopo lilitokana na Benki kutokuwa na mtaji wa kutosha pamoja na kuzingatia vigezo vya Benki Kuu kuhusu ulinganishi wa mali hatarishi na mtaji (Risk Weighted Assets to Core Capital). Mchanganuo wa aina ya mikopo iliyotolewa ni kama inavyooneshwa katika jedwali Na.5.5.

Jedwali Na.5.5: Mchanganuo wa Mikopo katika Benki ya Posta (Shs. Milioni)

Aina ya Mikopo	**2010**	**2011**	**Badiliko (%)**
Mikopo ya Biashara	4,245	4,818	13.5
Mikopo ya Watumishi	58,537	58,221	-0.5
Mikopo midogo midogo	1,598	1,534	-4.0
Mikopo ya Uwezeshaji	255	431	69.0
Jumla	**64,635**	**65,004**	**0.6**

Chanzo: Benki ya Posta

147. Mapato ya Benki ya Posta kwa mwaka 2011 yaliongezeka hadi kufikia shilingi 23,849 milioni ikilinganishwa na mapato ya shilingi 20,122 milioni ya mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 18.5. Kutokana na ongezeko hilo la mapato, Benki ilipata faida ya shilingi 2,267 milioni baada ya malipo ya kodi ikilinganishwa na faida ya shilingi 465 milioni kwa mwaka 2010. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mikopo, kuongezeka kwa riba katika dhamana za Serikali na kubana matumizi katika baadhi ya shughuli za Benki. Aidha, Benki ilipata mapato kutokana na kuingia mkataba wa kukusanya kodi za ndani kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 27

Sh. Bilioni

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba									Badiliko 2010-2011	
	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	Kiasi	%
Ujazi wa fedha, maana finyu zaidi (M0)*	**563.5**	**694.5**	**890.0**	**1034.0**	**1162.5**	**1438.6**	**1566.8**	**1897.1**	**2235.8**	**338.7**	**17.9%**
Ujazi wa fedha, maana finyu (M1)	**1107.2**	**1359.0**	**1791.3**	**2006.8**	**2590.5**	**3158.3**	**3590.8**	**4521.4**	**5572.0**	**1050.6**	**23.2%**
Amana za Akiba na za muda maalum	738.9	852.0	1169.1	1447.7	1804.1	2310.2	3012.6	3520.7	3676.0	**155.2**	**4.4%**
Ujazi wa fedha, maana pana (M2)	**1846.1**	**2211.0**	**2960.4**	**3454.5**	**4394.6**	**5468.5**	**6603.4**	**8042.1**	**9247.9**	**1205.8**	**15.0%**
Amana za fedha za kigeni	932.8	942.7	1290.3	1710.0	1829.0	1990.3	2176.7	2970.5	3773.4	**802.9**	**27.0%**
Ujazi wa fedha, maana pana zaidi (M3)	**2778.8**	**3153.8**	**4250.7**	**5164.5**	**6223.6**	**7458.8**	**8780.1**	**11012.6**	**13021.3**	**2008.7**	**18.2%**
Akiba halisi ya mali za kigeni (Foreign Assets)	**2302.7**	**2498.8**	**2665.1**	**3617.4**	**3641.9**	**4086.8**	**4939.5**	**6086.3**	**6296.4**	**210.1**	**3.5%**
Amana Halisi Nchini	**1412.4**	**1873.0**	**3074.6**	**3637.0**	**5172.9**	**5904.8**	**6578.0**	**7650.7**	**8589.4**	**938.7**	**12.3%**
Karadha Nchini	1820.3	2258.6	3335.3	4117.4	5422.5	6753.9	7857.6	9522.9	10958.1	**1435.2**	**15.1%**
Mikopo kwa serikali	827.7	945.9	1681.1	1807.3	2271.3	2197.8	2865.8	3531.0	3335.7	**-195.3**	**-5.5%**
Mikopo kwa sekta isiyo serikali	992.5	1312.7	1654.3	2310.1	3151.2	4556.2	4991.9	5991.9	7622.3	**1630.4**	**27.2%**
Amali halisi nyinginezo (net other items)	-407.9	-385.6	-260.7	-480.4	-249.7	-849.2	-1279.6	-1872.2	-2368.7	**-496.4**	**26.5%**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya benki

VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 28

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba							
	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Ujazi wa fedha, maana finyu zaidi (M0)*	**23.2%**	**28.1%**	**16.2%**	**12.4%**	**23.8%**	**8.9%**	**21.1%**	**17.9%**
Ujazi wa fedha, maana finyu (M1)	**22.7%**	**31.8%**	**12.0%**	**29.1%**	**21.9%**	**13.7%**	**25.9%**	**23.2%**
Amana za Akiba na za Muda Maalum	15.3%	37.2%	23.8%	24.6%	28.1%	30.4%	16.9%	4.4%
Ujazi wa fedha, maana pana (M2)	**19.8%**	**33.9%**	**16.7%**	**27.2%**	**24.4%**	**20.8%**	**21.8%**	**15.0%**
Amana za fedha za kigeni	1.1%	36.9%	32.5%	7.0%	8.8%	9.4%	36.5%	27.0%
Ujazi wa fedha, maana pana zaidi (M3)	**13.5%**	**34.8%**	**21.5%**	**20.5%**	**19.8%**	**17.7%**	**25.4%**	**18.2%**
Akiba halisi ya mali za kigeni (Foreign Assets)	**8.5%**	**6.7%**	**35.7%**	**0.7%**	**12.2%**	**20.9%**	**23.2%**	**3.5%**
Amana Halisi Nchini								
Karadha Nchini	32.6%	64.2%	18.3%	42.2%	14.1%	11.4%	16.3%	12.3%
Mikopo kwa serikali	24.1%	47.7%	23.4%	31.7%	24.6%	16.3%	21.2%	15.1%
Mikopo kwa sekta isiyo serikali	14.3%	77.7%	7.5%	25.7%	-3.2%	30.4%	23.2%	-5.5%
Amali halisi nyinginezo (other items net)	32.3%	26.0%	39.6%	36.4%	44.6%	9.6%	20.0%	27.2%

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabenki

MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na.29

	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Shs/Dola mwisho wa mwaka	976.65	1,063.62	1,042.96	1,165.51	1,261.64	1,132.09	1,280.30	1,313.29	1,453.54	1,566.66
Badiliko la thamani ya shilingi (%)		-8.2	-1.9	11.8	8.2	-10.3	13.1	2.6	10.7	7.8
Shs/Dola wastani wa mwaka	965.57	1,042.26	1,089.52	1,132.23	1,254.17	1,239.50	1,196.77	1,319.86	1,432.25	1,579.50
Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%)		-7.4	4.5	3.9	10.8	-1.2	-3.4	10.3	8.5	10.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Jedwali Na. 30

Aina ya Shughuli	**Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Milioni)**				Ukuaji (%)	Mchango (%)
	2008	**2009**	**2010**	**2011**		
Uzalishaji katika Kilimo	515936.0	467097.1	691210.3	912331.8	32.0	12.3
Huduma za Kifedha	122001.1	105843.7	142600.1	177691.8	24.6	2.4
Madini na Uchimbaji Mawe	37727.8	18926.3	33943.7	39175.7	15.4	0.5
Viwanda	612670.6	565775.5	786470.6	928746.6	18.1	12.6
Majengo na Ujenzi	142992.8	148713.4	182071.6	320938.2	76.3	4.3
Uchukuzi na Mawasiliano	320600.6	457407.2	533990.3	545243.5	2.1	7.4
Biashara	737092.1	926626.3	1014177.8	1523962.2	50.3	20.6
Utalii	29165.5	27097.6	37665.7	49730.4	32.0	0.7
Mahoteli na Migahawa	150978.4	187204.6	263046.3	361039.7	37.3	4.9
Umeme	183487.0	193609.6	156528.3	166672.8	6.5	2.3
Watu Binafsi	928491.7	1063142.9	1242763.5	1557495.5	25.3	21.1
Sekta Nyinginezo	595327.5	644369.9	713954.0	815729.5	14.3	11.0
Jumla	**4376471.1**	**4805814.0**	**5798422.1**	**7398757.6**	**27.6**	**100.0**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA

Jedwali Na.31 — Sh. Bilioni

	Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba											Badiliko
	2001	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2010/11 (%)
Amana za Sekta Binafsi												
Amana za Hundi/Zinazaohamishika	339.8	441.4	541.7	662.3	898.1	969.5	1,424.8	1,715.7	2,019.4	2,617.8	3,329.5	27.2
Amana za Akiba na za Muda Maalum	548.5	623.3	735.1	848.9	1,165.9	1,444.5	1,803.9	2,307.9	3,011.9	3,505.2	3,664.2	4.5
Amana za fedha za kigeni	563.3	764.3	921.3	934.8	1,289.0	1,709.9	1,828.6	1,989.3	2,158.8	2,926.4	3,722.0	27.2
Jumla	**1,451.6**	**1,828.9**	**2,198.1**	**2,446.0**	**3,353.0**	**4,123.9**	**5,057.3**	**6,012.9**	**7,190.1**	**9,049.5**	**10,715.8**	18.4
Amana za Serikali	80.0	102.8	125.2	152.1	206.6	230.1	325.2	401.7	662.6	699.3	626.6	-10.4
Jumla za Amana zote	**1,531.5**	**1,931.7**	**2,323.3**	**2,598.0**	**3,559.6**	**4,354.0**	**5,382.5**	**6,414.5**	**7,852.7**	**9,748.7**	**11,342.4**	16.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA

Jedwali Na. 32 — Asilimia

Aina ya Riba	Kipindi Kinachoishia Mwezi Desemba								
	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Riba ya Benki Kuu (Bank rate)	12.34	14.42	19.33	20.07	16.40	15.99	3.70	7.58	12.00
Riba za Amana									
Amana za akiba	2.45	2.60	2.60	2.59	2.65	2.74	2.83	2.43	2.90
Amana za muda maalum	3.87	4.39	5.28	7.17	8.37	6.63	6.36	6.09	7.12
Riba za mikopo									
Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja	15.65	14.23	15.65	15.67	15.01	13.56	13.96	14.37	13.73
Mikopo ya muda wa kati na mrefu	13.83	14.80	14.98	16.36	15.31	16.05	14.38	14.92	14.21
Riba za Hawala za Hazina									
Siku 91	7.57	9.63	14.70	14.39	9.90	11.20	6.06	5.24	12.61
Siku 182	7.61	9.87	14.71	14.95	10.15	12.13	6.59	6.20	16.39
Siku 364	7.93	10.67	15.72	15.61	12.95	12.79	8.83	7.67	18.66

Chanzo:Benki Kuu ya Tazania

SURA YA 6

RASILIMALI WATU

Idadi ya Watu na Maendeleo

148. Mwaka 2011, Serikali iliendelea na zoezi la maandalizi ya sensa ya watu na makazi itakayofanyika tarehe 26 Agosti, 2012. Maandalizi ya zoezi hili yamekuwa yakifanyika chini ya uratibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Hadi sasa mambo yafuatayo yamefanyika: kutenga maeneo ya kuhesabia watu ambapo hadi mwezi Machi 2012, kazi hii ilikuwa imekamilika katika mikoa 27 kati ya 30 nchi nzima; utayarishaji wa madodoso na miongozo ambayo lengo lake ni kukusanya taarifa muhimu za sensa kama vile demografía, ulemavu, elimu, vifo, hali ya makazi na umiliki wa rasilimali, shughuli za kiuchumi, uhamaji na uhamiaji; sensa ya majaribio ambayo ilifanyika Oktoba 2011 katika maeneo 44 ya kuhesabia watu ikiwa na lengo la kupima kama dodoso linaeleweka kwa wananchi ili kubaini kasoro zinazohitaji kurekebishwa kabla ya sensa yenyewe; na zoezi la uhamasishaji wa umma na wadau wengine ambalo linaendelea hadi sensa itakapokamilika kwa kutumia semina, warsha kongamano, machapisho mbalimbali na pia vyombo vya habari.

149. Idadi ya watu Tanzania kwa mwaka 2011 ilikadiriwa kuwa 44,484,857 ikilinganishwa na watu 43,187,823 mwaka 2010. Kati ya hao, wanawake walikuwa 22,570,628, sawa na asilimia 50.7 na wanaume walikuwa 21,914,229, sawa na asilimia 49.3. Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na jumla ya watu 43,169,305 sawa na asilimia 97.0 ambapo Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 1,315,552 sawa na asilimia 3.0 ya watu wote. Mgawanyo wa watu unaonesha kuwa watu 32,609,462, sawa na asilimia 73.3 ya watu wote, wanaishi vijijini wakati watu 11,875,395, sawa na asilimia 26.7 wanaishi mijini. Makadirio haya yanatokana na maoteo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002.

150. Mwaka 2011, mchanganuo wa idadi ya watu kulingana na umri unaonesha kuwa watu wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa 7,974,308 sawa na asilimia 17.9 ya watu wote. Kati ya hao, wavulana walikadiriwa kuwa

4,020,794 na wasichana 3,953,514. Idadi ya watu wenye umri kati ya miaka mitano hadi 14 ilikuwa 11,768,537, sawa na asilimia 26.5 ya watu wote. Kati ya hao, wavulana walikuwa 5,905,655 na wasichana 5,862,882. Aidha, jumla ya watu 19,742,845 ambao ni sawa na asilimia 44.4 ya watu wote walikadiriwa kuwa na umri chini ya miaka 15. Kati ya hao, wanaume walikadiriwa kuwa 9,926,449 na wanawake 9,816,396. Idadi ya watu waliokuwa na umri kati ya miaka 15 hadi 24 walikadiriwa kuwa 8,843,197, sawa na asilimia 19.9 ya watu wote. Kati ya hao, 4,408,579 walikuwa ni wanawake na wanaume 4,434,618. Idadi ya watu wenye umri kati ya miaka 25 hadi 64 ilikadiriwa kuwa 14,539,109 sawa na asilimia 32.7 ya watu wote. Idadi ya watu wenye miaka kati ya 15 hadi 64, ambao ndio nguvukazi, ilikuwa 23,382,306, sawa na asilimia 52.6 ya watu wote. Kati ya hao, 12,036,168 walikuwa ni wanawake na wanaume walikuwa 11,346,138. Wazee wenye umri wa miaka 65 au zaidi walikuwa 1,359,706 sawa na asilimia 3.1 ya watu wote. Kati ya hao, wanawake walikuwa 718,064 na wanaume ni 641,642.

Kielelezo Na. 6.1: Mchanganuo wa Idadi ya Watu Kulingana na Umri



151. Kutokana na makadirio ya idadi ya watu ya mwaka 2011, msongamano wa watu ulikadiriwa kuwa watu 50 kwa kila kilometa moja ya mraba. Kwa

upande wa Tanzania Bara, msongamano wa watu ulikuwa ni watu 49 wakati upande wa Tanzania Zanzibar ulikuwa ni watu 535 kwa kila kilometa moja ya mraba. Mgawanyiko wa watu kimkoa unaonesha kuwa mkoa wenye msongamano mkubwa zaidi wa watu ni Dar es Salaam, ambao ulikadiriwa kuwa na watu 2,294 kwa kila kilometa moja ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza watu 186, Kilimanjaro watu 126 na Mara watu 87 kwa kila kilometa moja ya mraba. Mkoa uliokuwa na kiwango kidogo zaidi cha msongamano wa watu ulikuwa ni Lindi, ambao ulikuwa na watu 14 kwa kila kilometa moja ya mraba ukifuatiwa na Ruvuma watu 22 na Rukwa watu 23 kwa kila kilometa moja ya mraba. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na watu wengi zaidi waliokadiriwa kuwa 2,152 kwa kila kilometa ya mraba wakati ambapo mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na msongamano mdogo wa watu waliokadiriwa kuwa 135 kwa kila kilometa moja ya mraba.

152. Mtawanyiko wa watu kimkoa unaonesha kuwa mkoa wa Shinyanga uliendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya watu. Mwaka 2011, mkoa wa Shinyanga ulikuwa na watu 3,998,664 sawa na asilimia 9.3 ya watu wote Tanzania Bara, ukifuatiwa na Mwanza watu 3,669,380 (asilimia 8.5) na Dar es Salaam watu 3,194,903 (asilimia 7.4). Idadi kubwa ya watu mkoani Shinyanga ilitokana na kiwango kikubwa cha uzazi kilichokadiriwa kufikia watoto 7.4 kwa mwanamke mmoja. Mkoa wa Lindi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu mwaka 2011 waliokadiriwa kufikia 941,885, sawa na asilimia 2.2 ya watu wote Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, mkoa uliokuwa na watu wengi zaidi ulikuwa ni Mjini Magharibi (495,054) na mkoa uliokuwa na idadi ndogo ya watu ulikuwa ni Kusini Unguja (115,035). Idadi ndogo ya watu katika mikoa ya Lindi na Kusini Unguja ilitokana na kiwango kidogo cha uzazi pamoja na watu kuhamia mikoa mingine kufuata fursa za kiuchumi na huduma za kijamii.

Nguvukazi na Ajira

153. Kulingana na matokeo ya Utafiti wa Nguvukazi na Ajira ya mwaka 2006, nguvukazi nchini ilikuwa watu milioni 18.8 ambapo milioni 9.0 walikuwa wanaume na milioni 9.7 walikuwa wanawake. Vile vile, matokeo hayo yanaonesha kuwa watu milioni 16.6 walikuwa wameajiriwa na milioni 2.2

walikuwa hawajaajiriwa. Kati ya walioajiriwa, watu milioni 8.5 walikuwa wanawake na wanaume milioni 8.0. Wanaume 967,847 hawakuwa wameajiriwa na wanawake ni 1,226,545. Kilimo kiliendelea kuwa ajira kuu ya watu nchini.

154. Utafiti wa nguvukazi na Ajira wa mwaka 2006 ambao ndio hutoa takwimu za hali ya sekta ya ajira nchini, ndio utafiti uliofanyika miaka ya karibuni na hakuna tafiti nyingine zilizofanyika. Utafiti huo unapaswa kufanyika kila baada ya miaka mitano kulingana na upatikanaji wa fedha, hata hivyo kulingana na maoteo ya sensa ya watu na makazi, inaonyesha kuwa nguvukazi ya taifa (miaka 15-64) ni watu millioni 19.2 kwa mwaka 2010.

155. Mwaka 2011, Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) ilitoa huduma za ajira kwa wateja 2,619. Kati ya hao, 1,841 walikuwa wanaume sawa na wasilimia 70.3 na 778 walikuwa wanawake sawa na asilimia 29.7. Aidha, Wakala uliendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wanaotafuta ajira kwa kuwapa mbinu za ujasiriamali ili kuboresha uwezo wao wa kuajiriwa. Aidha, Wakala ulitoa mwongozo wa kitaalam uanobainisha mbinu mbalimbali za kutafuta kazi na ushauri juu ya masuala yanayohusu ajira.

156. Mwaka 2011, TaESA iliweza kufanya mawasiliano na waajiri mbalimbali ambapo jumla ya nafasi 543 za kazi zilipatikana na fursa za ajira 819. Wakala pia uliendelea kuendesha mafunzo kwa wanaotafuta ajira juu ya mbinu mbalimbali za kutafuta ajira, kufaulu usaili, taarifa za soko la ajira na ushauri juu ya masuala yanayohusu huduma za ajira.

IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2005-2011

Jedwali 33

Mkoa	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011**
Dodoma	1,786,073	1,896,786	1,951,071	2,004,544	2,058,630	2111764	2163817
Arusha	1,427,904	1,475,489	1,522,975	1,570,394	1,617,728	1664780	1711624
Kilimanjaro	1,435,847	1,503,014	1,535,975	1,569,212	1,602,530	1635870	1669174
Tanga	1,716,271	1,753,284	1,837,661	1,880,389	1,923,468	1966908	2010480
Morogoro	1,881,113	1,929,087	1,975,160	2,021,713	2,068,426	2115275	2162197
Pwani	944,145	968,637	991,586	1,014,968	1,038,654	1062574	1086658
Dar es Salaam	2,799,241	2,801,675	2,881,548	2,961,150	3,040,118	3118132	3194903
Lindi	816,815	851,764	869,522	887,434	905,480	923607	941884
Mtwara	1,176,112	1,220,248	1,246,089	1,271,912	1,297,751	1323568	1349235
Ruvuma	1,192,680	1,235,161	1,268,738	1,303,330	1,338,800	1375017	1412084
Iringa	1,553,392	1,617,696	1,649,200	1,679,828	1,709,225	1737382	1764285
Mbeya	2,201,206	2,346,388	2,423,635	2,502,258	2,581,792	2662156	2743084
Singida	1,150,367	1,222,810	1,258,545	1,294,584	1,330,931	1367481	1404065
Tabora	1,887,507	2,004,115	2,086,048	2,170,926	2,258,664	2349374	2443049
Rukwa	1,251,697	1,302,278	1,349,579	1,398,866	1,450,118	1503184	1558200
Kigoma	1,910,592	1,970,750	1,601,020	1,669,078	1,740,111	1814158	1891173
Shinyanga	3,060,176	3,277,784	3,411,023	3,549,342	3,692,941	3841787	3998664
Kagera	2,206,814	2,210,217	2,293,093	2,379,637	2,469,904	2563870	2661671
Mwanza	3,196,714	3,168,904	3,265,729	3,364,378	3,464,566	3566263	3669380
Mara	1,461,270	1,572,068	1,631,031	1,692,449	1,756,442	1822866	1891907
Manyara	1,141,376	1,198,051	1,241,994	1,288,280	1,337,015	1388295	1441771
Tanzania Bara	**36,197,312**	**37,526,206**	**38,291,222**	**39,474,672**	**40,683,294**	**41,914,311**	**43,169,305**
Kaskazini Unguja	146,221	155,066	160,175	165,544	171,150	177095	183209
Kusini Unguja	99,678	103,191	105,456	107,811	110,183	112612	115035
Mjini Magharibi	441,446	461,759	447,716	459,502	471,341	483205	495054
Kaskazini Pemba	196,221	216,174	224,951	234,142	243,759	253999	264677
Kusini Pemba	186,651	207,348	216,479	226,055	236,072	246601	257577
Zanzibar	**1,070,217**	**1,143,538**	**1,154,777**	**1,193,054**	**1,232,505**	**1,273,512**	**1,315,552**
Tanzania	**37,267,529**	**38,669,744**	**39,445,999**	**40,667,726**	**41,915,799**	**43,187,823**	**44,484,857**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

** Makadirio kulingana na takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2002

SEHEMU YA PILI

UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

SURA YA 7

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini

157. Mwaka 2011, miradi iliyosajiliwa na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji iliongezeka kwa asilimia 62.2 kutoka miradi 509 yenye thamani ya shilingi 7,092,618.68 milioni mwaka 2010 na kufikia miradi 826 yenye thamani ya shilingi 10,909,404.80 milioni. Kati ya miradi hii, miradi 689 ilikuwa mipya na miradi 136 ilikuwa ya upanuzi na ukarabati. Aidha, miradi inayomilikiwa na wawekezaji wa ndani ilikuwa 462, wawekezaji wa nje miradi 172 na miradi ya ubia ilikuwa 191. Fursa za ajira zilizotokana na miradi hii zilifikia 79,101 kutoka fursa za ajira 43,640 mwaka 2010.

158. Mwaka 2011, shughuli za utalii ziliongoza kwa kuvutia wawekezaji wengi zikiwa na miradi 222 yenye thamani ya shilingi 798, 243.23 milioni na fursa za ajira 9,349, zikifuatiwa na shughuli za uzalishaji viwandani zilizokuwa na miradi 206 yenye thamani ya shilingi 1,074,548.8 milioni na fursa za ajira 19,779. Uwekezaji katika maeneo mengine ulikuwa ni kama ifuatavyo: usafirishaji miradi 143 yenye thamani ya shilingi 1,103672.0 milioni na fursa za ajira 15,336; majengo ya biashara miradi 130 yenye thamani ya shilingi 1,484,356.0 milioni na fursa za ajira 16,493; kilimo miradi 53 yenye thamani ya shilingi 1,012,198.4 milioni na fursa za ajira 8,968; rasilimali watu miradi 29 yenye thamani ya shilingi 385,107.2 milioni na fursa za ajira 2,239; huduma kwa wateja miradi 12 yenye thamani ya shilingi 35,720.0 milioni na fursa za ajira 962; mawasiliano miradi 8 yenye thamani ya shilingi 413,956.8 milioni na fursa za ajira 503; taasisi za fedha miradi 7 yenye thamani ya shilingi 132,954.4 milioni na fursa za ajira 843; miundombinu ya kiuchumi miradi minne yenye thamani ya shilingi 3,772,776.8 milioni na fursa za ajira 3,543; nishati miradi mitatu yenye thamani ya shilingi 469,711.2 milioni na fursa za ajira 120; utangazaji miradi mitatu yenye thamani ya shilingi 23,134.4 milioni na fursa za ajira 390; kompyuta miradi mitatu yenye thamani ya shilingi 9,393.6 milioni na fursa za ajira 72; maliasili miradi miwili yenye thamani ya shilingi 8,512.0 milioni na fursa za ajira 313; na

bidhaa za petroli na madini mradi mmoja wenye thamani ya shilingi 85,120.0 milioni na fursa za ajira 191.

Mchanganuo wa Miradi Kimkoa

159. Mwaka 2011, mkoa wa Dar es salaam uliongoza kwa kusajili miradi mingi ya uwekezaji ukifuatiwa na mkoa wa Arusha, ikiwa imesajili miradi 460 na 119 kwa mtiririko huo. Uwekezaji katika mikoa mingine ulikuwa kama ifuatavyo: Pwani miradi 45; Mwanza 40; Iringa 29; Tanga 23; Kilimanjaro 20; Mbeya, 18; Morogoro 16; Mtwara 10; Ruvuma na Dodoma miradi 7 kila mmoja; Rukwa na Shinyanga miradi 6 kila mmoja; Tabora na Kagera miradi mitano kila mmoja; Manyara miradi minne; Kigoma, Lindi, Mara na Singida miradi mitatu kila mkoa. Aidha, kituo hiki kilishughulikia maombi 13,566 ikilinganishwa na maombi 10,822 mwaka 2010, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 7.1.

Jedwali Na 7.1: Maombi Yaliyoshughulikiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Huduma	**2009**	**2010**	**2011**
Uhamiaji: Daraja A	327	276	288
Daraja B	2578	2,386	2,247
Kazi	3473	3,284	2,542
Usajili wa Makampuni	104	49	43
Leseni za Bishara	62	75	100
Ardhi	2191	1,677	4292
Kodi	3968	3,351	4342
Jumla	**12703**	**10,822**	**13,566**

Chanzo: Kituo cha Taifa cha Uwekezaji

Uwekezaji Mitaji ya Kigeni ya moja kwa moja

160. Mwaka 2011, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja iliongezeka kwa asilimia 97 na kufikia dola za Kimarekani 854.2 milioni ikilinganishwa na dola za Kimarekani 433.9 milioni mwaka 2010. Ongezeko hili kubwa lilitokana na uwekezaji mkubwa wa utafutaji wa gesi katika mkoa wa Mtwara ambao uligharimu zaidi ya dola za Kimarekani 300 milioni.

Jedwali Na. 7.2: Uwekezaji Mitaji ya Kigeni ya Moja kwa Moja, 1995-2011

Mwaka	Thamani ya Mitaji iliyowekezwa (Dola za Kimarekani Milioni)
1995	150.9
1996	148.6
1997	157.8
1998	172.2
1999	516.7
2000	463.4
2001	467.2
2002	387.6
2003	308.2
2004	330.6
2005	447.6
2006	616.6
2007	653.4
2008	744.0
2009	558.4
2010	433.9
2011	854.2*

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

*Makisio

Uboreshaji wa Mazingira Wezeshi kwa Sekta Binafsi

161. Mwaka 2011, Serikali ilianza utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji ulioidhinishwa mwaka 2010. Kupitia Mpango huu, Serikali ilipitisha kanuni za mawasilisho na malipo ya kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mauzo kufanyika kwa njia ya mtandao kupitia gazeti la Serikali Na. 242 na 241 kwa mtiririko huo. Utaratibu huu umeongeza ufanisi kwa kuondoa usumbufu na upotevu wa muda katika ulipaji wa kodi. Hadi sasa zaidi ya asilimia 75 ya walipa kodi wakubwa na walipa kodi wengine 2,795 wanafanya mawasilisho yao kwa njia ya mtandao. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianzisha mfumo unaounganisha usimamizi wa kodi (*Asycuda*, *ITAX*) na benki za biashara ili kurahisisha ulipaji wa kodi. Hadi sasa, mfumo huu umeunganisha jumla ya benki 25. Aidha, Mamlaka inatumia huduma za M-Pesa (Vodacom) na “NMB mobile” kwa ajili ya kulipia kodi ya majengo na kodi ya mapato.

162. Mwaka 2011, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania iliendelea na jitihada za kuondoa urasimu katika mchakato mzima wa kuondoa mizigo bandarini. Serikali ilianzisha utaratibu wa kuwasilisha nyaraka kwa njia ya mtandao kabla ya mizigo kuwasili. Utaratibu huu: umewawezesha wadau kuwasilisha nyaraka zao mahali popote palipo na mtandao; umeondoa tatizo la kuwasilisha nyaraka mara mbili au zaidi kwa Kampuni ya ukaguzi wa mizigo bandarini (TISCAN) na Kitengo cha Forodha; umeondoa tatizo la mrundikano na upotevu wa nyaraka kwenye mchakato mzima wa kuondoa mizigo bandarini; na umepelekea kupungua kwa muda na gharama za uagizaji na usafirishaji mizigo nje ya nchi. Aidha, Serikali ilianzisha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za kutathimini mapato ya forodha. Vile vile, Serikali ilitenga eneo kwa ajili ya kujenga bandari kavu itakayowaweka pamoja wadau wote wa bandari na mchakato wa kuanza ujenzi unaendelea. Serikali pia imeondoa vizuizi vya usafirishaji mizigo ndani ya nchi kutoka 50 vilivyokuwepo kufikia 15, isipokuwa vile vya kupima uzito karibu na madaraja na vituo vya kodi.

163. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kuboresha mfumo wa umilikaji wa mali ikiwemo maboresho ya sheria, usimamizi na matumizi ya teknologia ya kisasa katika kusajili mali. Lengo ni kupunguza muda katika mchakato mzima wa kusajili mali kutoka siku 73 zilizokuwepo hadi siku 45. Katika mwaka 2011, hatua za mwisho katika kusaji mali zilipungua kutoka siku 14 mpaka siku 9. Serikali pia iliweka mazingira mazuri katika kusaidia upatikanaji wa mikopo ikiwemo kupitisha kanuni zitakazosaidia kuongeza upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na ya riba nafuu na kusimamia mikopo ya ukodishaji vifaa (Financial Leasing Regulations 2011). Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kuanziasha kitengo huru kitakachohusika na usimamizi wa mifuko ya Serikali ya Dhamana ya Mikopo.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi

164. Mwaka 2011, Serikali kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 7.1 bilioni ikilinganishwa na shilingi 4.6 bilioni

zilizotolewa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 54.4. Mikopo hiyo ilitolewa kupitia vyama 30 vya akiba na mikopo (SACCOS) katika mikoa ya Pwani, Dodoma, Lindi, Manyara, Mtwara, Rukwa, Ruvuma, Singida na Tanga. Marejesho ya mikopo hiyo yalikuwa asilimia 96 ya mikopo yote iliyotolewa. Mikopo hiyo iliwawezesha wajasiriamali kuanzisha miradi midogo midogo na kununua zana za kilimo zikiwemo trekta za mikono (power tillers) na pembejeo za kilimo.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira

165. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira. Hadi kufikia Desemba 2011, Serikali kupitia Mpango huo ilikuwa imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 49.23 bilioni kwa wajasiriamali 72,912 kupitia asasi za kifedha 12 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi 47.14 bilioni iliyotolewa kwa wajasiriamali 72,179 mwaka 2010. Aidha, kiasi cha shilingi 39.28 bilioni kilirejeshwa, sawa na asilimia 83.3 ya mikopo iliyoiva.

Utoaji na Upatikanaji wa Mikopo Kupitia Mifuko Mbalimbali

166. Mwaka 2011, Serikali kupitia mfuko wa Rais wa kutoa mikopo kwa wananchi wa kipato cha chini ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 6.8 bilioni kwa walengwa 167,372 ili kuwawezesha kuanzisha na kuimarisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, asilimia 65 ya mikopo iliyoiva ilirejeshwa.

167. Mwaka 2011, Benki Kuu ya Tanzania kupitia Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya mauzo nje ya nchi ilitoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi 448,590,063,693 kwa asasi za fedha ili kuziwezesha kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wanaouza bidhaa nje ya nchi. Kutokana na dhamana hiyo, asasi hizo ziliweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 584,946,840,280 . Aidha, asilimia 80 ya dhamana ya mikopo hii ilitumika kusaidia shughuli za kilimo. Vile vile, Serikali kupitia Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa wafanyabiashara wa kati na wadogo ilitoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi 3,135,659,876 kwa asasi za kifedha. Asasi za kifedha kwa upande wake ziliweza kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 6,505,912,000 kwa wafanyabiashara kupitia dhamana hizo.

168. Mwaka 2011, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo kwa Wajasiriamali unaosimamiwa na shirika la kuhudumia viwanda vidogo ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 26.0 bilioni kwa walengwa 51,019. Mikopo hiyo iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 153,185. Aidha, kiwango cha marejesho ya mkopo kilikuwa asilimia 90.4 ya mikopo iliyoiva.

169. Mwaka 2011, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 1.7 bilioni kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15-35. Kati ya mikopo iliyofikia muda wa marejesho, ni kiasi cha shilingi 0.25 bilioni tu (asilimia 14.7) kilichorejeshwa. Kiwango hiki kinadhihirisha kuwa kuna changamoto kubwa katika urejeshaji wa mikopo katika Mfuko huu. Aidha, mikopo yenye thamani ya shilingi 40.2 bilioni kilitolewa kwa wafanyabiashara 84,315 kupitia Mradi wa kuhudumia Biashara Ndogondogo (SELF). Mradi huu unatekeleza jukumu la kujenga uwezo na kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo hususan, walioko vijijini. Kati ya wafanyabiashara waliopata mkopo wanawake walikuwa asilimia 58. Marejesho ya mikopo hii ilikuwa ni asilimia 92.5.

170. Mwaka 2011, Serikali kupitia mfuko wa kuwezesha wakulima ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 49.45 bilioni kwa wakulima na wasambazaji wa pembejeo za kilimo. Kiasi cha mikopo kilichorejeshwa ni shilingi 14.6 bilioni sawa na asilimia 29.5 ya mikopo iliyotolewa, hii inatokana na muda wa marejesho kwa baadhi ya mikopo kuwa mrefu (miaka 5) hususan kwenye mikopo ya zana za kilimo ikiwemo matrekta.

KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI ILIYOPITISHWA

Jedwali Na.34

Sekta	2010								2011							
	A	B	C	D	E	F	G	H	A	B	C	D	E	F	G	H
Kilimo na Ufugaji	23	21	2	12	6	5	5169	663,710.6	53	47	6	21	17	15	8968	1,012,198.4
Maliasili	1	1	0	0	1	0	100	4,494.0	2	2	0	0	0	2	313	8,512.0
Utalii	103	84	19	66	22	15	5452	417,083.9	222	177	45	142	31	49	9349	798,243.2
Uzalishaji Viwandani	183	162	21	68	76	39	14327	705,299.1	206	173	33	83	64	59	19779	1,074,548.8
Bidhaa za Petroli na Madini	0	0	0	0	0	0	0	-	1	1	0	0	0	1	191	85,120.0
Ujenzi	0	0	0	0	0	0	0	-	0	0	0	0	0	0	0	-
Majengo ya Biashara	92	85	7	43	30	19	5078	1,925,186.1	130	113	16	81	23	25	16493	1,484,356.0
Usafirishaji	62	44	18	37	13	12	7197	436,513.1	143	116	27	96	24	23	15336	1,103,672.0
Huduma	19	19	0	4	10	5	4717	213,127.6	12	12	0	3	5	4	962	35,720.0
Kompyuta	1	1	0	0	0	1	43	1,218.0	3	3	0	1	1	1	72	9,393.6
Asasi za Fedha	4	2	2	0	0	4	86	2,294.6	7	5	2	1	2	4	843	132,954.4
Mawasiliano	5	5	0	2	1	2	529	260,008.0	8	6	2	2	0	6	503	413,956.8
Rasilimaliwatu	3	3	0	1	1	1	45	20,921.6	29	24	5	26	3	0	2239	385,107.2
Nishati	8	6	2	5	0	3	412	2,277,800.0	3	3	0	1	1	1	120	569,711.2
Miundombinu ya kiuchumi	1	1	0	1	0	0	22	6,076.0	4	4	0	2	1	1	3543	3,772,776.8
Utangazaji	4	4	0	3	0	1	463	158,886.0	3	3	0	3	0	0	390	23,134.4
Jumla	509	438	71	242	160	107	43640	7,092,618.6	826	689	136	462	172	191	79101	10,909,404.8

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

A Jumla ya Miradi Iliyopitishwa
B Miradi Mipya
C Miradi ya Zamani (Upanuzi na Ukarabati)
D Miradi ya Nchini
E Miradi ya Nje
F Miradi ya Ubia
G Jumla ya Ajira
H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (Million Tsh.)

SURA YA 8

MASUALA MTAMBUKA

UKIMWI

171. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI kwa kutoa huduma za tiba na matunzo kwa wagonjwa wa UKIMWI, ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari. Aidha, Serikali iliendelea kuboresha huduma hizi kwa kuhakikisha kuwa dawa za kupunguza makali ya VVU zinapatikana katika vituo vya kutoa huduma. Mwaka 2011, jumla ya vituo 1,100 vilikuwa vinatoa huduma za matunzo na matibabu kwa walengwa kwenye hospitali zote za rufaa, mikoa, wilaya na baadhi ya vituo vya afya na zahanati nchini kote. Vile vile, vituo vinavyotoa huduma ya unasihi na upimaji viliongezeka kwa asilimia 2.9 kutoka vituo 2,137 mwaka 2010 hadi vituo 2,200 mwaka 2011.

172. Mwaka 2011, watu 14,992,976 walipata ushauri nasaha na kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari ikilinganishwa na watu 8,890,207 mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa watoa mafunzo mbalimbali ya ushauri nasaha pamoja na kuongezeka kwa vituo vya kutoa ushauri nasaha na vipimo. Idadi ya watoa huduma iliongezeka kutoka 5,240 mwaka 2010 hadi 9,880 mwaka 2011. Aidha, mwaka 2011, idadi ya watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na wanaopata dawa za kupunguza makali ya virusi iliongezeka kwa asilimia 24.6 kutoka watu 313,384 mwaka 2010 mpaka watu 390,390 mwaka 2011. Kati ya hao, 29,918 ni watoto chini ya miaka 15.

Mazingira

173. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Mazingira ya mwaka 1997 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191. Katika kipindi hiki, kanuni mbili kwa ajili ya kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ziliandaliwa na hivyo kufanya sheria iwe na kanuni 17 kati ya kanuni 29 zinazohitajika ikilinganishwa na kanuni 15 mwaka 2010. Kanuni hizi ni Kanuni za Usimamizi Endelevu wa Ardhi Oevu na Kanuni za Usimamizi wa Ukanda wa Pwani. Aidha, mwaka 2011, miongozo mitatu ya kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliandaliwa. Miongozi hiyo ni: Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Mazingira; Mwongozo wa Uendeshaji

wa Baraza la Rufaa la Mazingira; na Mwongozo wa Kujumuisha Masuala ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Sera na Mipango ya Kisekta.

174. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kuwahimiza wawekezaji kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika uwekezaji kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla na baada ya kutekeleza miradi yao. Katika kipindi hiki, jumla ya miradi ya maendeleo 467 ya uwekezaji ilisajiliwa kwa ajili ya kufanyiwa TAM. Kati ya miradi hiyo, miradi 163 ilipata hati za TAM baada ya kukidhi vigezo ikilinganishwa na miradi 220 mwaka 2010. Aidha, kati ya miradi iliyopewa hati za TAM mwaka 2011, miradi 44 ilikuwa ya mawasiliano; 36 ya viwanda; 28 ya nishati; 17 ya miundombinu; 16 ya ujenzi na uendelezaji kwenye vivutio vya utalii; 12 maji; 7 ya uchimbaji wa madini; na miradi mitatu ilikuwa ya misitu na kilimo.

175. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali kwa ajili ya kuhifadhi baoanuwai. Miradi hii ni pamoja na: Mradi wa Kuhifadhi Mazingira katika maeneo ya mfumo wa ikolojia wa Gombe Kigoma na Masito Mpanda ambao unatekelezwa katika eneo la kilomita za mraba 12,047; Mradi wa Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Kihansi; na Mradi wa kuhifadhi Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika ambao unatekelezwa katika mikoa ya Kigoma na Rukwa. Katika utekelezaji wa mradi huu, miti 170,000 ilipandwa mwaka 2011 ili kuongoa maeneo yaliyoharibika sana, vikundi 19 vya uvuvi shirikishi viliundwa ili kuhamasisha uvuvi endelevu, mialo minne ya kisasa ilijengwa na vikundi vya jamii vinavyofanya shughuli mbadala za kiuchumi katika vijiji 6 vya mfano vilianzishwa.

176. Mwaka 2011, katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Mkakati huu wa miaka mitano unaweka mikakati ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kusaidia kupunguza gesijoto. Aidha, mwaka 2011, Serikali iliendelea kutekeleza miradi miwili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Miradi hii ni: Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika sekta za kilimo, maji, afya, wanyapori, misitu mifugo na ardhi na Mpango wa kupunguza uzalishaji wa ukaa itokanayo na ukataji wa miti na uharibifu wa misitu

177. Mwaka 2011, Serikali kupitia Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari ya Pwani iliendelea kufadhili jamii za pwani kutekeleza miradi ya uzalishaji. Katika kutekeleza hilo, jumla ya miradi 56 yenye thamani ya shilingi 780,295,425.0 ilifadhiliwa katika Halmashauri ya Wilaya za Mtwara D.C. (22), Manispaa ya Temeke (17), Lindi Manispaa (8), Jiji la Tanga (1), Bagamoyo (3), Lindi Wilaya (1) na Mtwara Mikindani (4). Jumla ya wananchi 1,066, walifaidika na miradi hii wakiwemo wanaume 511 na wanawake 555. Aidha, uchambuzi wa miradi 32 ya utunzaji wa mazingira kutoka hifadhi za bahari na maeneo tengefu ulifanyika na mapendekezo kwa ajili ya kupewa fedha za kuwezesha utekelezaji wake umekamilika;

Utawala Bora

178. Mwaka 2011, Serikali kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea na juhudi zake za kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala bora katika jamii. Aidha, katika mwaka 2011, Tume ilishughulikia jumla ya malalamiko mapya na ya zamani 8,875 ya wananchi. Kati ya hayo, malalamiko 1,042 yalipatiwa ufumbuzi na 7,833 yaliendelea kushughulikiwa, ikilinganishwa na malalamiko 1,003 yaliyohitimishwa mwaka 2010.

179. Mwaka 2011, Mahakama ya Rufaa ilipokea jumla ya mashauri 2,857. Kati ya hayo, mashauri 798 yalisikilizwa na kutolewa maamuzi na mashauri 2,059 yaliendelea kushughulikiwa ikilinganishwa na mashauri 2,624 yaliyopokelewa na Mahakama hiyo mwaka 2010 ambapo mashauri 627 yalikamilishwa na mashauri 1,997 yaliendelea kushughulikiwa. Aidha, Mahakama Kuu ilipokea mashauri mapya 9,453 na kufanya jumla ya mashauri kuwa 20,385 ikilinganishwa na mashauri 10,932 yaliyokuwepo mwaka 2010. Kati ya mashauri hayo, mashauri 9,669 yalisikilizwa na kuhitimishwa mwaka 2011. Vilevile, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi na Wilaya kulikuwa na mashauri 85,323 mwaka 2011, kati ya hayo, mashauri 67,437 yalisikilizwa na kuhitimishwa ukilinganisha na mashauri 62,154 yalipokelewa mwaka 2010 ambapo mashauri 46,977 yalisikilizwa na kuhitimishwa.

180. Mwaka 2011, Serikali iliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa (NACSAP II). Katika utekelezaji wa Mkakati huo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilipokea na kufanyia

uchunguzi kesi za rushwa 399. Kati ya hizo, jumla ya kesi 103 zilikamilika na watuhumiwa walifikishwa mahakamani. Katika kesi zilizofikishwa mahakamani, kesi 48 watuhumiwa walitiwa hatiani na kuadhibiwa na kesi 55 watuhumiwa hawakupatikana na hatia ikilinganishwa na kesi 870 za mwaka 2010 ambapo kati ya kesi hizo, kesi 587 zilifikishwa mahakamani na kesi 64 zilitolewa hukumu.

Jinsia

181. Mwaka 2011, Serikali ilianza mchakato wa kuhuisha Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, ili kuendana na mabadiliko na changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya kiuchumi. Aidha, mwaka 2011, Serikali iliendesha mkutano wa wataalamu na mawaziri kutoka nchi za ukanda wa maziwa makuu kuhusiana na ukatili wa kijinsia. Mkutano huo ulishirikisha wadau kutoka nchi 11 za ukanda wa maziwa makuu. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kutafuta namna ya kuweza kutokomeza ukatili wa kijinsia.

182. Katika kuleta usawa wa jinsia, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa idadi ya wanawake wanaoshiriki katika maamuzi inaboreshwa. Kwa kufanikisha hili, Serikali iliongeza idadi ya viti maalum vya wanawake kwenye bunge kutoka viti 75 katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 mpaka viti 102 katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Aidha, Serikali imepandisha vyeo wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi wakiwemo mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya na makatibu wakuu wa wizara na wakurugenzi katika taasisi mbalimbali. Kufuatia hatua hii, wanawake katika nafasi za maamuzi wameongezeka kutoka asilimia 31 mwaka 2009/10 hadi asilimia 36.4 mwaka 2010/11.

Usalama wa Raia

183. Hali ya usalama nchini kwa ujumla iliendelea kuwa tulivu mwaka 2011 licha ya kuwepo kwa matukio ya uhalifu na makosa ya usalama barabarani. Mwaka 2011, makosa 63,703 ya jinai yaliripotiwa katika vituo vya polisi nchini ikilinganishwa na makosa 62,134 yaliyoripotiwa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 2.5. Hii ilitokana na mikakati iliyotekelezwa na Jeshi la Polisi ya kupambana na uhalifu nchini, ikiwa ni pamoja na kutambua maeneo

yenye mazingira ya uhalifu, kuyapangia ulinzi na kuyafanyia misako ya kushtukiza na ya mara kwa mara.

184. Mwaka 2011, jumla ya matukio 24,078 ya ajali za barabarani nchini yaliripotiwa katika vituo vya Polisi ikilinganishwa na matukio 24,296 yaliyoripotiwa mwaka 2010, sawa na punguzo la ajali kwa asilimia 3.4. Aidha, jumla ya watu 4,013 walikufa na wengine 20,917 kujeruhiwa katika ajali hizo ikilinganishwa na watu 3,687 waliokufa na wengine 22,064 waliojeruhiwa mwaka 2010. Idadi ya vifo vilivyotokana na ajali za barabarani iliongezeka kwa asilimia 8.8 na idadi ya watu waliojeruhiwa ilipungua kwa asilimia 5.2. Idadi ya ajali barabarani ilipungua mwaka 2011 kutokana na juhudi za Serikali katika kufanya operesheni za kuzuia mwendo kasi kwa magari ya abiria, kukamata magari yanayotumia matairi yasiyo na viwango, ukaguzi wa leseni za udereva na magari. Chanzo kikubwa cha ajali za barabarani ni pamoja na uzembe wa madereva; ubovu wa magari; uduni wa miundombinu; uzembe wa waenda kwa miguu, wapanda pikipiki na baiskeli na ulevi.

185. Mwaka 2011, jumla ya wakimbizi 131,243 waliingia nchini ikilinganishwa na wakimbizi 109,286 mwaka 2010. Wakimbizi hawa walitoka katika mataifa ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia na wachache kutoka Rwanda, Uganda, Sudan, Ethiopia na Zimbabwe. Mchanganuo wa idadi ya wakimbizi na nchi wanakotoka ni kama ifuatavyo: Burundi wakimbizi 67549; Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo 61,913; Somalia 1530; na Mataifa mengine wakimbizi 251. Aidha, katika mwaka 2011, jumla ya wakimbizi 279 walirejea nchini Burundi ikilinganishwa na wakimbizi 1,092 mwaka 2010.

186. Mwaka 2011, jumla ya wageni 963,687 waliingia nchini kutoka mataifa mbalimbali ikilinganishwa na wageni 628,795 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 53.3. Aidha, jumla ya wageni 999,090 walitoka nchini mwaka 2011 ikilinganishwa na wageni 775,310 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 28.9. Mwaka 2011, jumla ya hati za ukaazi 17,441 zilitolewa kwa wageni walioingia nchini kufanya shughuli mabalimbali ikilinganishwa na hati za ukaazi 19,550 zilizotolewa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 10.8.

SURA YA 9

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI TANZANIA

Utangulizi

187. Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) awamu ya kwanza ulikamilika Mwezi Juni 2010. Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya kwanza (2005/06 - 2009/10), taarifa za utekelezaji zinazoelezea mafanikio na changamoto zimekuwa zikiandaliwa chini ya Mpango wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA. Taarifa hizi ni pamoja na: Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA; Taarifa ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ambayo huchambua kwa kina matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA; Taarifa itokanayo na maoni ya watu; na taarifa za tafiti na uchambuzi/sensa mbalimbali. MKUKUTA awamu ya pili (MKUKUTA-II) uliandaliwa na kupitishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwezi Oktoba 2010 kwa kuzingatia changamoto na mambo tuliyojifunza wakati wa utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya kwanza.

188. Kama ilivyokuwa katika utekelezaji wa MKUKUTA-I, MKUKUTA II utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2010/11 – 2014/15) na utaendeleza muundo wa nguzo kuu tatu ambazo ni ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; kuboresha maisha na ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji. Aidha, viashiria mbalimbali vya kupima utekelezaji wa MKUKUTA-II vimeainishwa katika nguzo hizo. Uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vya MKUKUTA II katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji ni kama inavyobainishwa hapa chini.

Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

189. Mwaka 2011, uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 6.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Ukuaji huu ni chini ya shabaha ya MKUKUTA-II ya kuwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 8 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2015. Sekta zilizokuwa na ukuaji mkubwa ni pamoja na mawasiliano (asilimia 19.0), fedha (asilimia 10.7), ujenzi (asilimia 9.0), na biashara (asilimia 8.1).

190. Sekta ya kilimo ambayo ndiyo inategemewa na watu wengi zaidi ya asilimia 74 ilikua kwa asilimia 3.6 mwaka 2011 ukilinganisha na asilimia 4.2 ya mwaka 2010. Pamoja na kasi ndogo ya ukuaji, Tanzania imekuwa ikijitegemea kwa chakula kwa miaka mingi ambapo uwiano wa kujitosheleza kwa chakula ulikuwa na wastani wa asilimia 95. Uwiano huo unapatikana kwa kulinganisha uzalishaji wa ndani wa mazao ya chakula na mahitaji ya ndani ya chakula. Katika mwaka 2010/2011, uwiano wa kujitosheleza kwa chakula ulikuwa asilimia 112 ikilinganishwa na asilimia 102 mwaka 2009/2011.

191. Pato la wastani la kila mtu lilikuwa kwa asilimia 12.8 kutoka shilingi 770,464.3 mwaka 2010 hadi kufikia shilingi 869,436.3 mwaka 2011. Maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya nguzo hii yamebainishwa katika taarifa ya utekelezaji wa MKUKUTA ya mwaka 2010/11.

Kuboresha Maisha na Ustawi wa Jamii

192. Katika kipindi cha mwaka 2010/11, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iliendelea kutekeleza programu na maboresho katika sekta za huduma ya jamii kwa lengo la kuimarisha ubora wa maisha na ustawi wa jamii. Vishiria vikuu katika nguzo hii ni vile vinavyohusiana hususan na elimu, afya na maji. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kiashiria cha elimu ni pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji katika shule za awali, sekondari, vyuo vya ufundi na elimu ya juu.

193. Kiwango halisi cha uandikishaji watoto katika elimu ya awali ilifikia asilimia 42.4 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 37.5 mwaka 2010. Hata hivyo, kiwango cha uandikishaji watoto kwa elimu ya msingi kilipungua kidogo kutoka asilimia 95.4 mwaka 2010 hadi asilimia 94.0 mwaka 2011. Kiwango cha kufaulu kiliongezeka kutoka asilimia 49.4 mwaka 2009 hadi asilimia 53.5 mwaka 2010. Kiwango cha kuhitimu katika shule za msingi kiliongezeka kutoka asilimia 53.0 mwaka 2010 hadi asilimia 62.6 mwaka 2011, kati yake kiwango cha wanawake kuhitimu kiliongezeka kutoka asilimia 54.3 hadi asilimia 65.2.

194. Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya na Idadi ya Watu wa Mwaka 2009/10 (TDHS), huduma ya afya ya mama na mtoto wakati wa kujifungua nayo

imeimarika. Wastani wa vifo vya mama wajawazito umepungua kutoka vifo 578 kati ya wamama wajawazito 100,000 mwaka 2004/05 hadi 454 kati ya 100,000 mwaka 2010. Wastani wa vifo vya watoto wachanga ilikuwa vifo 51 kati ya watoto 1000 waliozaliwa hai mwaka 2011 ikilinganishwa na vifo 68 kwa watoto 1000 mwaka 2004-05. Malengo ni kupunguza hadi vifo 38 kati ya watoto 1,000 ifikapo 2015. Wastani wa vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano ilikuwa vifo 81 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2011 ikilinganishwa na vifo 112 kati ya watoto 1,000 mwaka 2004/05. MKUKUTA II unalenga kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano hadi kufikia vifo 54 kati ya watoto 1,000 ifikapo 2015. Kiwango cha maambukizi ya VVU katika kundi la watu wenye umri kati ya miaka 15-24 kilifikia asilimia 2.4 mwaka 2010. Lengo la MKUKUTA-II ni asilimia 1.2 ifikapo mwaka 2015.

195. Kutokana na tafiti ya TDHS 2010, kiwango cha watoto walio na umri chini ya miaka mitano waliodumaa kimepungua kutoka asilimia 38 mwaka 2004/05 hadi asilimia 35 mwaka 2010; Wastani wa watoto walio chini ya miaka mitano wenye uzito mdogo umepungua kutoka asilimia 22 mwaka 2004/05 hadi asilimia 21 mwaka 2010.

196. Idadi ya kaya zilizounganishwa katika mpango wa usambazaji maji mijini imeongezeka kutoka kaya 234,468 mwaka 2009/10 hadi kaya 254,236 mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 8. Usambazaji maji umehusisha makao makuu ya mikoa 19 ya Tanzania Bara ambapo imefikia asilimia 86 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 84 mwaka 2010. Idadi ya watu katika maeneo ya vijijini wanaopata maji katika vyanzo vya maji vilivyohifadhiwa imeongezeka kutoka asilimia 40.4 (Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya mwaka 2007) na kufikia asilimia 47.9 (Utafiti wa Afya na idadi ya Watu mwaka 2009/10).

Utawala Bora na Uwajibikaji

197. Katika kipindi cha utekelezaji wa MKUKUTA awamu ya pili, Serikali iliendelea na juhudi zake za kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma katika ngazi zote za kiutendaji hasa katika Serikali za Mitaa. Katika kipindi hicho, Serikali ilihakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatangaza taarifa za mapato, bajeti na matumizi kwa lengo la kuwawezesha wadau wote kupata taarifa sahihi juu ya matumizi ya rasilimali za

umma kwa lengo la kuleta uwazi. Juhudi hizi zimesaidia kupungua kwa Mamlaka za Serikali zisizoweka taarifa zao kwenye mbao za matangazo kuhusiana na bajeti, mipango, na taarifa za ukaguzi kutoka asilimia 93.2 mwaka 2009/2010 hadi asilimia 87 mwaka 2010/2011.

198. Katika kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, mwaka 2010/11, Serikali ilichunguza jumla ya kesi za rushwa 2,258 na kati ya hizo, uchunguzi wa kesi 598 sawa na asilimia 26 ulikamilika. Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa kuridhisha, mafaili themanini (80) ya kesi yalipelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka na mafaili 92 ya kesi yalipelekwa katika asasi nyingine za Serikali baada ya kujiridhisha kwamba ushahidi ulioletwa haukujitosheleza na haukuendana na sheria ya rushwa ya mwaka 2007. Aidha, katika mwaka 2011, jumla ya kesi 399 za rushwa zilipelekwa mahakamani na kesi 103 zilifanyiwa kazi na kati ya hizo watuhumiwa 48 wa kesi hizo walikutwa na makosa.

199. Katika mwaka 2010/11, Serikali iliendelea kutoa haki za msingi kwa kila raia. Serikali pia inatambua kwamba taarifa za vizazi ni muhimu katika uandaaji wa bajeti na mipango mingine ya maendeleo. Katika mwaka 2011, uandikishaji au usajili wa vizazi na vifo, na talaka, uliongezeka.

Jedwali Na 9.1: Mwenendo wa Usajili wa Vizazi, Vifo na Ndoa

Mwaka	Cheti cha kuzaliwa	Cheti cha Kufariki	Ndoa	Talaka	Wadhamini	Wosia	Kuasili (watoto waliopata walezi wapya)
2008/09	938,775	105,482	73	15,345	247	-	39
2009/10	469,274	47,118	85	17,106	277	83	46
2010/11	625,670	73,810	69	23,108	203	36	33

Chanzo:Wizara ya Fedha

SEHEMU YA TATU

SUALA MAALUM KIMAENDELEO

SURA YA 10

MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO

Utangulizi

200. Tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1980, kumekuwepo na utaratibu wa kuwa na Mipango ya Muda Mrefu na Kati kama miongozo katika kufikia malengo ya maendeleo yaliyowekwa na Taifa. Hata hivyo, kutokana na migogoro ya kiuchumi duniani, sambamba na uwezo mdogo wa nchi kukabiliana na migogoro hiyo, Tanzania ililazimika kuwa na mfumo wa mipango ya muda mfupi ya kipindi cha mwaka mmoja hadi mitatu ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Kutokana na kuwa na mipango ya muda mfupi, ni dhahiri kuwa matarajio na malengo ya muda mrefu hayakuweza kufanikiwa kikamilifu. Kwa kuzingatia muktadha huu, mwaka 2008, Serikali iliazimia kuanzisha tena mipango ya muda mrefu na ile ya kati kama sehemu muhimu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, mwaka 2011, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) ulizinduliwa kwa ajili ya kuongeza kasi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kipindi kilichobaki hadi mwaka 2025. Mpango huu wa Maendeleo ni wa kwanza na matarajio ni kuwa na mipango mingine miwili 2016/17-2020/21, na 2021/22-2025/26.

Maana ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

201. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni mwongozo wa nchi katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kipindi cha muda wa miaka mitano. Katika kipindi hicho, Serikali inajaribu kuelezea dhamira ya dhati ya hatua zitakazochukuliwa kutatua vikwazo vilivyopo katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ili kuinua kipato cha mwananchi na kuleta maendeleo endelevu katika nchi. Kwa kuzingatia maana hiyo, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano - 2011/12-2015/16 utakuwa ndio nyenzo ya utekelezaji wa ajenda ya maendeleo iliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, hususan kuiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za kipato cha kati na hatimaye kuondokana na umaskini. Mpango huu wa kwanza unajielekeza zaidi katika azma ya kufungulia fursa fiche za ukuaji wa uchumi nchini ili kuiwezesha Tanzania kutumia rasilimali asili kama madini na kutumia utajiri wa kijiografia

kama vile bandari, na njia za usafirishaji kwenda nchi jirani katika kukuza uchumi wa nchi.

Historia ya Mipango ya Maendeleo Tanzania

202. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12-2015/16 sio wa kwanza Tanzania kwani historia inatuonesha kuwa mipango kama hii ilikuwapo mara baada ya Tanzania kupata uhuru. Katika miaka ya mwanzo ya uhuru agenda kuu ya maendeleo ya Tanzania iliweka msukumo katika ukuaji wa uchumi na kuondoa umasikini. Lengo la msingi likiwa ni kuhakikisha kuwa Watanzania wengi wananufaika na maendeleo yanayopatikana. Katika kufikia msukumo huu, Tanzania Bara imekuwa na utaratibu wa kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya muda wa kati na mrefu. Mpango wa Kwanza ulikuwa wa miaka mitatu (1961 - 1964), ambao lengo lilikuwa kupinga vita maadui watatu wa msingi katika maendeleo ya Taifa: Ujinga, Umasikini na Maradhi.

203. Kufuatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitatu, sambamba na shabaha ya kumfanya mwananchi kuwa kiini cha maendeleo, mwaka 1964, Serikali ilizindua Mpango Elekezi wa Kwanza wa Miaka Kumi na Tano (1964 – 1980). Utekelezaji wa Mpango huo ulikuwa wa vipindi vitatu mfululizo vya miaka mitano mitano, kwa kuanzia na Mpango wa mwaka 1964-1969. Mpango huu ulifanyiwa marekebisho mwaka 1967 ili kuendana na sera ya Azimio la Arusha. Azimio la Arusha lilifafanua itikadi na dira ya maendeleo ya nchi, na hivyo kuwa msingi wa matayarisho ya Mipango iliyofuata. Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ulitekelezwa kutoka mwaka 1969 hadi 1974, na Mpango wa tatu ambao ungetekelezwa kutoka mwaka 1975 mpaka 1980 haukutekelezwa, hasa kufuatia matatizo ya kiuchumi (ukame, kupanda kwa bei za mafuta na vita dhidi ya Iddi Amini wa Uganda).

204. Mwaka 1981, Serikali ilitayarisha Mpango wa Pili wa Muda Mrefu (1981–2000) uliotakiwa kutekelezwa katika vipindi vinne vya muda wa kati (miaka mitano mitano). Pamoja na dhamira ya Serikali kutekeleza Mpango huu, matatizo ya kudorora kwa uchumi nchini yalisababisha kushindwa kutekeleza Mpango huu ipasavyo. Hivyo, Serikali iliamua kutayarisha Mpango wa Muda Mfupi wa Kunusuru Uchumi (1981/82) ambao ulitarajiwa kuwa wa dharura kukabiliana na tatizo la uhaba wa bidhaa katika soko. Hata hivyo, kuendelea kwa mdororo wa uchumi kufuatia kupanda kwa bei za mafuta, athari za vita

dhidi ya Iddi Amini wa Uganda, na hali ya ukame wa muda mrefu, Serikali iliachana kabisa na utekelezaji wa mipango ya miaka mitano kama njia ya utekelezaji wa Mpango wa muda mrefu na badala yake programu za miaka mitatu za kurekebisha uchumi zilitekelezwa mfululizo kutoka mwaka 1982/83 hadi mwaka 1991/92. Programu ya kwanza ya 1982 – 1985 (Structural Adjustment Program - SAP) ililenga kukabiliana na mtikisiko wa kiuchumi, ambayo ilifuatiwa na programu mbili za kufufua uchumi (Economic Recovery Programs - ERP I&II) mwaka 1986-1989 na 1989–1992 ambayo ilitekelezwa kwa misaada ya washirika wa maendeleo.

205. Kwa ujumla, mabadiliko ya mfumo wa mipango kutoka wa miaka mitano hadi kuwa wa programu maalum za miaka mitatu yaliiondoa nchi katika utaratibu wa utayarishaji wa mipango kuendana na agenda ya Taifa ya maendeleo kuwa mipango ya mahitaji ya wakati. Upangaji wa mipango ukawa wa dharura mara kwa mara ikijikita katika kutatua matatizo ya kiuchumi, hivyo kukosa mwelekeo mkakati wa uwekezaji unaoendana na agenda ya maendeleo ya muda mrefu.

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

206. Kwa kuzingatia kuwa utekelezaji wa programu za kufufua na kurekebisha uchumi hazikuzaa matokeo tarajiwa ya kijamii na kiuchumi, mwaka 1999, Serikali ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ikiwa na lengo la kuiondoa Tanzania kutoka katika nchi zenye kipato cha chini kimaendeleo na kuipeleka hadi kufikia hadhi ya kimaendeleo ya nchi zenye kipato cha kati. Dira ya Taifa imejengeka katika sifa kuu zifuatazo: Maendeleo makubwa ya sekta ya viwanda; uwezo wa kuhimili ushindani; maisha bora na mazuri; utawala bora na wa kisheria; na kuwa na jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza.

207. Utekelezaji wa Dira 2025 ulipangwa kufuata mfumo wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano. Hata hivyo, hili halikuwezekana kwa kuwa, wakati wa kuzinduliwa kwake, Tanzania ilikuwa imeanza utekelezaji wa maboresho ya kisera chini ya programu ya kuzipunguzia madeni nchi maskini duniani. Tanzania ilianza kutekeleza mikakati ya muda mfupi ya kupunguza umaskini (PRS 2000 - 2003), ambayo katika hali ya kukosekana kwa mipango, ilitumika kama nyenzo ya utekelezaji wa Dira. Mkakati huu wa miaka mitatu baadaye uliboreshwa na kubadilishwa jina na kuwa Mkakati (wa miaka mitano)

wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTAI, 2005-2010) na hatimaye MKUKUTA II (2010-2015).

Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano -2011/12-2015/16

208. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) unarejesha utaratibu wa awali katika kuainisha mwelekeo wa kufikia matarajio kimaendeleo katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Mpango huu unawasilisha mabadiliko katika mfumo wa utayarishaji wa mipango kutoka ule unaozingatia mahitaji kwenda katika mfumo unaozingatia fursa. Katika mfumo wa awali, matakwa ya nchi kimaendeleo yanarudishwa nyuma kwa kuwa mipango huzingatia fedha zilizopo wakati katika mfumo huu, fedha ni njia tu ya utekelezaji wa mipango kwa ajili ya kufikia malengo. Mpango huu ni wa kwanza kati ya mitatu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 unaozingatia mtazamo mpya wa kupanga.

Mchakato wa Utayarishaji wa Mpango

209. Mchakato wa kutayarisha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulipitia katika hatua mbalimbali za mapitio, maboresho na miundo iliyopo. Baadhi ya mambo yaliyozingatiwa ni pamoja na mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, MKUKUTA I na utayarishaji wa MKUKUTA II , Mipango na Mikakati ya Kisekta, Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF), Vipaumbele vya utekelezaji (PAPs) vya Wizara, Idara na Wakala, Malengo ya Milenia (MDGs), na mikakati na programu mbalimbali za kikanda na kimataifa, ambazo serikali ya Tanzania imeridhia. Kwa hiyo, Mpango umewianisha vipaumbele vilivyoainishwa katika hatua hizo na kuhakikisha kuwa vinaendana na dhamira ya kufikia malengo ya Dira Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, rasimu ya Mpango wa Uwekezaji wa Umma (MKUU) uliotayarishwa chini ya uratibu wa Wizara ya Fedha uliweka msingi na mwelekeo wa Mpango huu. Mpango huu pia ulizingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa kupitia hotuba yake ya Uzinduzi wa Bunge la 10 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na maelekezo mbalimbali ya kisera ya serikali. Aidha, katika uandaaji wake wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, Idara, Wakala wa serikali, Asasi za Kijamii, Washirika wa Maendeleo, na Sekta Binafsi kwa ujumla wake walishirikishwa kwa namna moja ama nyingine katika maandalizi.

Malengo ya Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16)

210. Lengo kuu la Mpango huu ni Kufungulia Fursa za Ukuaji wa Uchumi wa Taifa ili kuharakisha ujenzi wa uwezo wa nchi kukidhi mahitaji ya msingi kwa kuwa na ukuaji wa uchumi unaohusisha wengi na kujali maskini. Shabaha ya Mpango ni kuwa na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 8 kwa mwaka kutoka ukuaji wa asilimia 7 mwaka 2010, na hatimaye kufikia kiwango cha ukuaji wa angalau asilimia 10 mwaka kati ya 2016 hadi 2025. Lengo hili limekadiriwa kwa kuzingatia mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa kipindi cha miaka kumi na mitano iliyopita na uzoefu wa nchi ambazo zimeweza kufikia hadhi ya uchumi wa kati katika kipindi cha miaka 30 iliyopita.

Kufungulia Ukuaji wa Kiuchumi

211. Ili kufikia lengo la ukuaji wa uchumi, mambo matano muhimu yatahitajika: (i) uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya nishati na usafirishaji; (ii) uwekezaji mkakati kuwezesha kupanua uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na kuharakisha maendeleo ya viwanda ili kuongeza thamani; (iii) kuimarisha maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi; (iv) kuboresha mazingira ya biashara; na (v) maboresho ya mfumo taasisi wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya Mipango. Hii pia itahitaji mabadiliko ya ukuaji kisekta: Kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo itabidi kiongezeka kutoka wastani wa asilimia 4.4 kwa sasa hadi asilimia 6, uzalishaji viwandani kutoka asilimia 8 hadi asilimia 12.1, sekta ya viwanda kwa ujumla kutoka asilimia 8.6 hadi asilimia 9.4 na huduma kutoka asilimia 7.5 hadi 7.8. Katika kuimarisha ukuaji wa uchumi, ni muhimu kujenga uwezo wa ushindani ili kuhakikisha ufanisi katika matumizi ya fursa za kijiografia, utajiri wa maliasili, utulivu wa uchumi, amani na utulivu wa kisiasa. Hata hivyo, kuna haja ya kuratibu kwa karibu maendeleo ya kipato ili kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi unawanufaisha.

Sifa Mahsusi za Mpango

212. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano unawianisha mipango mbalimbali ya maendeleo ya kitaifa katika mfumo mmoja madhubuti ili kutoa mwongozo wa utekelezaji na kuipa Serikali fursa na mifumo rasmi ya kutathmini mchakato wa maendeleo ya Taifa. Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano unatofautiana na mipango/mikakati mingine hasa katika maeneo makuu manne yafuatayo:

i. Kuondokana na utaratibu wa kupanga kukidhi mahitaji ya muda mfupi, ambayo huzingatia upeo wa rasilimali fedha inayoweza kupatikana, na badala yake kuweka mfumo wa kupanga kwa kuzingatia fursa za kimaendeleo, ambao unahitaji uthubutu zaidi ya kikwazo cha rasilimali;
ii. Kuondokana na ubainishaji wa vipaumbele kisekta na badala yake kuwa na vipaumbele vya hatua za kiutekelezaji, ukibainisha kwa kina programu na shughuli za utekelezaji ;
iii. Msukumo unaonekana zaidi katika ukuaji wa uchumi, pasipo kusahau mafanikio yaliyopatikana katika kuboresha upatikanaji wa za huduma za jamii, sawia na kulenga kuboresha rasilimali watu, hatua kwa hatua, hususan, katika kuendeleza ujuzi kwa ajili kukabiliana na ongezeko la mahitaji katika soko la ajira; na
iv. Kuongeza nafasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza uchumi, kwa kuboresha mazingira ya biashara na kuwa na ufanisi katika matumizi ya nguzo za uzalishaji, kuwekeza katika rasilimali watu na maendeleo ya miundombinu, na kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa ya ustawi kijamii na kiuchumi.

Hatua za Kimkakati za Utekelezaji wa Mpango

213. Hatua za kimkakati katika utekelezaji wa Mpango zimejikita katika kubainisha fursa zilizopo; maeneo ya viapumbele; mambo muhimu ya kuzingatia katika utekelezaji wa Mpango; masuala yanayoweza kujitokeza hapo baadae; na kubainisha vikwazo vilivyopo sasa katika uchumi. Kimsingi, Tanzania ina rasilimali nyingi za kimaendeleo ikilinganishwa na nchi jirani na eneo lake la ardhi ni kubwa na lenye rutuba. Kuna hekta milioni 44 za ardhi ifaayo kwa kilimo katika maeneo ya hali tofauti ya hewa, kati ya hizo ni asilimia 24 tu ndizo zinatumika kwa kilimo. Aidha, Tanzania ina fursa nyingi za kuzalisha nishati ya kutosha hasa uzalishaji wa umeme, kwa kutumia gesi asilia ambapo imethibitishwa kuwa Tanzania ina mita za ujazo bilioni 43, tani 1,200 za mashapo ya makaa ya mawe, mashapo ya uranium, nishatijoto ardhi (geothermal), fursa ya nguvu ya umeme wa maji ya uwezo wa kuzalisha 4.7 GW, nguvu ya upepo, jua na rasilimali nyingine mbadala.

214. Tanzania pia imejaliwa kuwa na chokaa yenye ubora kwa uzalishaji wa saruji na mashapo ya phosphate, ambayo yakichanganywa na gesi asilia huweka msingi wa uzalishaji wa mbolea. Rasilimali nyingine ni pamoja na madini ya dhahabu, almasi, Tanzanite, rubi, nikeli, bati, magadi na chuma. Tanzania pia

ina vivutio vya kitalii ikiwa ni pamoja na mbuga za wanyama 15 ambazo ni maarufu duniani, kama vile Hifadhi ya Ngorongoro na Serengeti; Mlima Kilimanjaro, mbuga za akiba 33, maeneo tengefu 43 ya mbuga za uwindaji yaliyodhibitiwa na urithi mkubwa wa vivutio vya utalii wa kiutamaduni. Vile vile kuna hekta milioni 35.3 za misitu na nyika sawia na milioni 13.5 za hifadhi za Taifa na serikali za mitaa za misitu. Hizi ni baadhi tu ya fursa ambazo Tanzania imejaliwa na kama kukiwa na hatua za kimkakati za kuvuna na kutumia rasilimali zilizopo, Tanzania inaweza kufikia malengo ya Dira kabla ya mwaka 2025.

215. Pamoja na fursa zilizobainishwa hapo juu, bado Tanzania inakabiliwa na vikwazo vya msingi ambavyo vikitatuliwa ipasavyo, uchumi wa Tanzania utaweza kukua kwa kasi zaidi na kuvutia wawekezaji hasa katika sekta binafsi na hatimaye kutoa fursa ya kuongeza ajira zaidi na kupunguza umaskini uliokithiri. Vikwazo vinavyokwamisha uchumi wa Tanzania ni vingi ingawa katika uchambuzi uliofanyika hivi karibuni imebainika kuwa baadhi ya vikwazo vikubwa katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania ni kama ifuatavyo:

i. Ukosefu wa umeme wa uhakika na wa kutosha;
ii. Miundombinu duni: hasa mtandao wa usafiri, hususan, barabara za vijijini na zile zinazoingia mijini, reli na bandari;
iii. Upungufu wa nguvu kazi yenye weledi;
iv. Ugumu wa upatikanaji wa hati miliki ya ardhi;
v. Athari za mabadiliko ya tabia-nchi sambamba na ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji;
vi. Uwezo mdogo katika uongezaji thamani kwa mazao na bidhaa za msingi nchini; na
vii. Ugumu wa kupata mitaji, hasa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati.

216. Ili kuweza kukabiliana na vikwazo hivyo, kunahitajika kuzingatia mambo ya msingi ambayo yatachochea mchakato endelevu wa maendeleo ya uchumi katika sekta mbalimbali. Kwa mantiki hii, hatua za awali za jitihada mpya za kufungulia fursa fiche za ukuaji wa uchumi wa Tanzania ni lazima zichukuliwe ili kuweza kujua ni jinsi gani, wapi na kwa wakati gani rasilimali zilizopo ziwekezwe. Sambamba na hili, mahitaji ya kuwezesha kuwepo kwa mazingira wezeshi ya ukuaji endelevu wa uchumi na utulivu wa uchumi jumla ni muhimu. Aidha, kuwepo kwa mazingira mazuri ya kufanya biashara, kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uzalishaji na makazi na

kuimarisha mfumo wa utawala bora na wa kisheria nalo ni japo la msingi katika kufikia malengo ya Mpango.

Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

217. Kwa kuzingatia azma ya Mpango huu, maeneo matano yalichaguliwa kuwa vipaumbele vya Mpango. Maeneo hayo ni:

(i) Miundombinu: *hasa uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya nishati, usafirishaji (bandari, reli, barabara na usafiri wa anga), maji (safi, taka na ya uzalishaji) na TEHAMA;*

218. Hatua kimkakati katika eneo hili zimegawanyika makundi mawili: uendelezaji na usimamizi wa miundombinu msingi; na miundombinu saidizi. Katika eneo la miundombinu ya msingi, hatua za kimkakati zimejikita katika: kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika; kuendeleza sekta ya usafirishaji na uchukuzi kwa maana ya barabara, viwanja vya ndege, reli, na bandari ambapo shabaha kuu hapa ni kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha usafirishaji na uchukuzi katika nchi za Afrika Mashariki na Kati; na kuimarisha miundombinu ya maji safi na majitaka. Kwa upande miundombinu saidizi, hatua kimkakati zitaelekezwa katika uendelezaji TEHAMA.

(ii) Maendeleo ya Viwanda: *hasa vile vinavyotumia malighafi za ndani kama vile viwanda vya nguo, mbolea, saruji, makaa ya mawe, chuma na bidhaa za chuma sambamba na uendelezaji wa kanda maalum za kiuchumi kwa mfumo wa ubia baina ya sekta za umma na binafsi;*

219. Lengo kuu kwa sekta ya viwanda ni kuharakisha mabadiliko ya uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa kuendana na mahitaji ya soko. Msisitizo utakuwa katika kujenga msingi imara kuwezesha maendeleo endelevu ya viwanda na ukuaji wa uchumi unaoongozwa na biashara ya nje. Hatua za kimkakati zitaelekezwa katika kufanya mabadiliko katika sekta ya viwanda ili iendane na maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kuweka mikakati ya kukuza viwanda hasa vya kusindika mazao ya kilimo. Aidha, hatua zitachukuliwa ili kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na msingi wa viwanda kwa kujenga viwanda mama (vya mbolea, saruji, chuma, nguo, sukari, karatasi na bidhaaa za petrol) kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini (makaa ya mawe, chuma, gesi asilia, magadi soda, chokaa, phosphate, mbao, na pamba). Aidha, mkazo katika maendeleo ya uzalishaji viwandani utawekwa katika: kuboresha mazingira ya biashara, hasa kwa viwanda vidogo na vya kati vyenye kutumia

zaidi nguvukazi; kujenga Maeneo Maalumu ya Uchumi (SEZs) na Maeneo Mahsusi ya uzalishaji kwa mauzo ya nje (EPZ) mijini na vijijini ili kuharakisha uwiano wa maendeleo ya sehemu nyingi nchini; na kuhimiza uwekezaji wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi.

(iii) Kilimo, *kwa shabaha ya kuleta mapinduzi ya kilimo kuwezesha kujitosheleza kwa chakula ndani na kwa uuzaji nje ya nchi, uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji hasa katika kanda maalum za kilimo zilizotengwa, na uendelezaji wa mazao yenye thamani kubwa, ikiwa ni pamoja na cha mbogamboga, maua, viungo, zabibu n.k;*

220. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, hatua za kimkakati zitalenga katika: kupanua maeneo na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji; kurahisisha upatikanaji na kuongeza matumizi ya pembejeo na teknolojia za kisasa; kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa mbinu za kisayansi za uzalishaji, kwa kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani; kuboresha upatikanaji wa soko; kuendeleza shughuli za usindikaji wa mazao na uongezaji thamani; na kilimo chenye kuendana na mabadiliko ya tabia-nchi;

(iv) Maendeleo ya rasilimali *watu na ujuzi kwa kutilia mkazo maendeleo ya sayansi, teknologia na ubunifu. Maendeleo ya rasilimali watu yanajumuisha masuala mbalimbali yanayohusiana na uendelezwaji nguvukazi kama vile viwango vya ujuzi, elimu, afya na lishe.*

221. **Elimu na Uendelezaji wa Ujuzi:** Hatua za kimkakati zitalenga katika kuongeza ubora wa elimu kwa ngazi zote, hususani kusaidia upatikanaji wa elimu kwa watu maskini. Aidha, katika uendelezaji stadi na ujuzi wa kazi, Mpango utajielekeza katika kukidhi mahitaji ya rasilimali watu katika sekta muhimu za uzalishaji (kilimo, madini, na viwanda) na miundombinu ya kiuchumi (nishati, TEHAMA, usafiri na utalii).

222. **Afya:** Mpango unaweka msisitizo katika hatua zitakazoweza kukabili changamoto za sekta ya afya. Hatua hizo za kimkakati ni pamoja na: kuongeza upatikanaji wa huduma za afya, kwa misingi ya usawa na mahitaji ya uwiano wa kijinsia; kuboresha ubora wa huduma za afya; kuimarisha usimamizi wa sera na kanuni juu ya huduma za afya; na kuimarisha uendelezaji wa rasilimali watu kwa ajili ya afya na ustawi wa jamii.

(v) Uendelezaji wa huduma wezeshi: *hususan huduma za utalii, biashara na fedha.*

223. Mpango unaweka msisitizo katika hatua zitakazoweza kukabili changamoto zinazojitokeza katika maeneo ya huduma wezeshi za utalii, biashara na fedha. Vipaumbele vimewekwa katika: kuboresha huduma za utalii na mapato yake; kuimarisha uwezo wa kufanya biashara ya kimataifa, ushirikiano wa kiuchumi na mtangamano wa kikanda; na kuimarisha upatikanaji huduma za fedha na utengamavu wa kifedha.

224. Katika miaka mitano ijayo, Mpango umebainisha maeneo makuu ya uwekezaji ambayo yanatokana na vipaumbele vilivyotajwa hapo juu. Maeneo hayo ni: Kwa kuanzia, utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano umebainisha maeneo makuu ya uwekezaji ambayo ni:

i. Ufuaji wa umeme kufikia kiwango cha uzalishaji wa 2,780 MW;
ii. Upanuzi wa uwezo wa bandari ya Dar es Salaam;
iii. Ukarabati wa reli ya kati na kuongeza idadi ya injini na mabehewa ya abiria na mizigo;
iv. Ujenzi wa barabara za mikoa na wilaya katika ukanda wa kilimo wa SAGCOT;
v. Utandazaji wa mkongo wa taifa wa TEHAMA nchi nzima;
vi. Uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji katika ukanda wa SAGCOT;
vii. Utoaji mafunzo katika fani za sayansi, uhandisi na elimu kwa ujumla;
viii. Uendelezaji wa kanda maalum za uchumi (SEZ), hasa kwa bidhaa za elektroniki, zana za kilimo, viwanda vya kusindika (kuongezea thamani) mazao ya kilimo na madini;
ix. Uwekezaji kwa uzalishaji mkubwa wa mbolea; na
x. Uwekezaji katika uzalishaji wa makaa ya mawe na chuma.

Gharama za Utekelezaji za Mpango

225. Ili mpango wowote uweze kutekelezwa ipasavyo, ukusanyaji wa rasilimali fedha za kuugharamia ni suala la msingi. Kwa kipindi cha muda mrefu, Serikali imekuwa ikitegemea vyanzo vya kawaida vya fedha kugharamia bajeti ya matumizi yake ya kawaida na maendeleo. Vyanzo hivyo ni pamoja na: mapato ya kodi za ndani, mapato yasiyo ya kodi (mikopo ya ndani, gawio la hisa, ada, leseni) na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nchi marafiki na mashirika ya kimataifa. Pamoja na vyanzo hivyo vya kawaida vya mapato, Mpango unapendekeza vyanzo na njia mpya za mapato kwa ajili ya kugharamia

Mpango. Vyanzo hivyo ni pamoja na kutenga angalau asilimia 35 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ; Hati-Fungani za Miundombinu na Akiba ikijumuisha Hati Fungani kwa Waishio Ughaibuni, Hatifungani za ndani, Hati-Fungani katika Masoko ya kimataifa; Mifuko ya Pensheni na hifadhi ya jamii; Ruzuku na Michango ya Washirika Maalum; Udhamini wa Serikali kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ; Makubaliano ya Ushirikiano wa Kiuchumi Kikanda na Chini ya Mfumo wa nchi za Kusini; Kodi katika Biashara ya Kifedha; Mfuko wa Taifa wa Mazingira; Utaratibu wa Kuchangia kwa Hiari; Kodi ya ziada katika madini;

226. Kwa kuzingatia maeneo makuu ya uwekezaji katika Mpango, jumla ya shilingi trilioni 43.7 zitahitajika katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Kati ya fedha hizi, wastani wa shilingi trilioni 8.6 zitahitajika kutoka Serikalini na kiasi kilichobaki kitahitajika kutoka sekta binafsi, ubia, wahisani, na wadau wengineo katika maendeleo. Jedwali Na. 10.1 linachanganua gharama za uwekezaji uliobainishwa katika sekta na maeneo ya kisekta.

Jedwali Na. 10.1: Mahitaji ya Fedha kwa Utekelezaji Maeneo ya Vipaumbele; 2011/2012 – 2015/16 (TShs. Milioni)

Sekta	Jumla ya Gharama (TShs. Milioni) Jumla	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16
Kilimo	**4,361,576**	**922,685**	**812,378**	**775,589**	**723,757**	**727,164**
Mazao	2,630,654	457,733	397,292	428,106	455,278	492,240
Misitu	71,563	29,859	8,580	10,607	11,323	11,196
Uvuvi	326,180	90,011	76,670	61,766	52,831	44,902
Mifugo	1,333,179	345,082	329,836	275,110	204,325	178,826
Bidhaa za Viwandani	**1,513,880**	**199,300**	**180,410**	**339,430**	**519,620**	**275,120**
Madini	**1,383,014**	**207,856**	**345,694**	**345,614**	**345,604**	**138,247**
Uchukuzi	**11,293,947**	**2,283,026**	**2,759,728**	**2,228,085**	**2,199,878**	**1,823,235**
Barabara	7,106,765	1,781,924	2,137,284	1,568,408	993,777	625,373
Reli	2,097,359	252,535	272,065	280,385	644,615	647,760
Usafiri wa majini	995,400	119,212	129,124	157,262	237,984	351,818
Usafiri wa Anga	1,094,423	129,355	221,255	222,030	323,502	198,284
Maji	**2,326,256**	**392,985**	**540,090**	**529,032**	**457,898**	**406,251**
Ardhi	**142,645**	**42,139**	**34,239**	**23,139**	**22,139**	**20,989**
Nishati	**14,619,211**	**2,474,127**	**5,010,213**	**3,914,558**	**1,926,846**	**1,293,467**
TEHAMA	**1,606,450**	**408,010**	**453,010**	**298,510**	**176,510**	**270,410**
Elimu	**1,814,629**	**65,076**	**354,546**	**469,054**	**484,101**	**441,853**
Afya	**2,765,911**	**933,033**	**721,435**	**449,005**	**461,881**	**200,557**
Utawala Bora	**1,546,877**	**411,047**	**387,405**	**240,072**	**185,310**	**323,043**
Utalii, Biashara na Huduma za Fedha	**1,130,853**	**169,428**	**110,464**	**105,999**	**264,322**	**80,639**
Utalii	185,818	18,250	53,696	43,968	36,918	32,985
Biashara	89,370	17,568	17,914	17,916	18,010	17,962
Huduma za Fedha	855,665	133,610	38,854	44,115	209,394	29,692
Ajira	**7,200**	**1,710**	**1,230**	**1,400**	**1,400**	**1,460**
Jumla	**43,656,784**	**8,376,812**	**11,771,988**	**9,775,372**	**7,659,872**	**6,072,743**

Chanzo: Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango

Mfumo wa Utekelezaji

227. Mpango ya Maendeleo wa Miaka Mitano utatekelezwa kupitia mipango ya mwaka mmoja mmoja ambayo itapambanua programu na miradi ya uwekezaji katika sekta mbalimbali. Ofisi ya Rais Tume ya Mipango (ORTM) itaandaa vigezo vitakavyotumika kuchagua miradi ya Mpango wa mwaka. Kwa

upande wake, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za serikali, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa zitawasilisha mapendekezo ya mipango ya mwaka ORTM. Mipango hii ni lazima iidhinishwe na kamati husika zilizopo katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kabla ya kuwasilishwa ORTM. Miradi yote ya kimkakati ya uwekezaji kitaifa itachambuliwa na kuidhinishwa na ORTM na Wizara ya Fedha ili kuiwezesha kuingizwa katika mipango ya mwaka na kutengewa rasilimali.

Utekelezaji na Uratibu wa Mpango wa Mwaka

228. Jukumu la utekelezaji na uratibu wa mpango litabaki kuwa la Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais Tume ya Mipango itakuwa na jukumu la kuongoza uratibu, usimamizi na tathmini katika ngazi ya kitaifa, hususan kwa programu na miradi ya kimkakati ya uwekezaji kitaifa. Kazi mahsusi za, na wajibu wa taasisi na viongozi katika utekelezaji wa Mpango ni kama ifuatavyo:

Wajibu na kazi za ORTM

229. Usimamizi thabiti wa utekelezaji wa mpango katika ngazi ya kitaifa utaongozwa na Ofisi ya Rais, Tume ya mipango. Aidha, Mwongozo wa utayarishaji mipango na bajeti utatolewa kwa pamoja kati ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitapaswa kuzingatia mwongozo huu katika uandaaji wa mipango na bajeti zao. Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango itawajibika kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mipango ya nusu mwaka katika ngazi ya kitaifa kwa ajili ya kujua hatua zilizofikiwa. Tume ya Mipango mbali na kutoa fikra za kimkakati na ushauri kwa Serikali katika usimamizi wa uchumi na utayarishaji na utekelezaji wa mipango, itashauri katika kuwezesha upatikanaji wa rasilimali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Wajibu na Kazi za Wizara ya Fedha

230. Jukumu la msingi la Wizara ya Fedha litabaki kuwa ni: ukusanyaji wa rasilimali kwa mahitaji ya utekelezaji wa majukumu ya serikali; kuratibu mahusiano ya kifedha ndani ya serikali na kimataifa; kushirikiana na ORTM katika kuanzisha kamati ya pamoja ili kuhakikisha kwamba mipango ya mwaka

inashabihiana na mfumo wa bajeti; kutoa mwongozo wa utayarishaji na usimamizi wa bajeti ambayo itafuatwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali na Serikali za Mitaa; na kushirikiana na ORTM katika kubainisha vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya kugharimia programu za maendeleo.

Wajibu na kazi za Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa

231. Utekelezaji wa vipaumbele, programu na miradi iliyobainishwa katika mpango utakuwa ni wajibu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Asasi Zisizo za Kiserikali. Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitabuni miradi na programu mahsusi ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Uchaguzi wa miradi na programu za Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango ili kuwezesha Tume ya Mipango kutekeleza wajibu wake wa kufanya tathmini na ufuatiliaji.Serikali za mitaa na Wizara za Kisekta zitakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba vipaumbele vilivyoainishwa na jamii na sekta kwa mtiririko huo, vinashabihiana na vipaumbele vya kitaifa.

Hitimisho

232. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/12-2015/16 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mpango huu utatekelezwa chini ya dhana ya kufungulia fursa fiche za ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi. Matarajio ni kuwa na mipango mingine miwili ya vipindi vya miaka mitano mitano (2016/17-2020/21, na 2021/22-2025/26). Utekelezaji wa mipango hii unalenga kubadilisha muundo wa uchumi kutoka ule unaotegemea kilimo kwenda kwenye uchumi wa hadhi ya kipato cha kati ukiongozwa na maendeleo ya viwanda. Mafanikio ya Mpango huu yatatokana na juhudi za pamoja kati ya serikali na wananchi, sekta binafsi, washirika wa maendeleo, asasi za kiraia katika kutimiza kikamilifu wajibu wao wa kutekeleza vipaumbele vilivyobainishwa katika maeneo yanayowahusu.

SEHEMU YA NNE

MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

SURA YA 11

KILIMO NA USHIRIKA

Kiwango cha Ukuaji

233. Mwaka 2011, shughuli za kiuchumi za kilimo ambazo hujumuisha mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikua kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2010. Aidha, shughuli ndogo za kiuchumi za mazao; mifugo; na misitu na uwindaji zilikua kwa asilimia 3.5, 3.9 na 3.5 mwaka 2011 ikilinganishwa na ukuaji halisi wa asilimia 4.4, 3.4 na 4.1 mwaka 2010, kwa mtiririko huo. Kwa upande mwingine, shughuli za kilimo zilichangia asilimia 23.7 ya Pato la Taifa mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 24.1 mwaka 2010. Mchango wa shughuli ndogo za mazao na mifugo katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 17.8 na 3.8 mwaka 2010 hadi asilimia 17.4 na 3.7 mwaka 2011, kwa mtiririko huo. Hata hivyo, mchango wa shughuli ndogo za misitu na uwindaji katika Pato la Taifa uliongezeka kufikia asilimia 2.5 mwaka 2011 kutoka asilimia 2.4 mwaka 2010.

Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

234. Mwaka 2011, uzalishaji wa mazao ya chakula hususan ngano, mihogo, maharage, ndizi na viazi uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2010 kutokana na hali nzuri ya hewa na mtawanyiko mzuri wa mvua kwa ustawi wa mazao. Uzalishaji wa zao la ngano uliongezeka kutoka tani 62,000 mwaka 2010 hadi tani 113,000 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 82.3. Aidha, uzalishaji wa zao la mihogo uliongezeka hadi tani 1,549,000 mwaka 2011 kutoka tani 1,464,000 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Uzalishaji wa zao la maharage/mikunde uliongezeka kutoka tani 1,254,000 hadi tani 1,632,000, sawa na ongezeko la asilimia 30.1. Uzalishaji wa zao la ndizi uliongezeka kutoka tani 975,000 hadi tani 1,048,000, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Vile vile, uzalishaji wa zao la viazi vitamu uliongezeka kutoka tani 1,231,000 hadi tani 1,710,000, sawa na ongezeko la asilimia 38.9. Hata hivyo, uzalishaji wa mahindi, mchele na mtama/ulezi ulipungua mwaka 2011 ikilinganishwa na mwaka 2010. Uzalishaji wa mahindi ulipungua kutoka tani 4,475,416 hadi tani 4,340,823, sawa na upungufu wa asilimia 3.0. Uzalishaji wa zao la mchele ulipungua kwa asilimia 14.1 kutoka tani 1,700,000 hadi tani 1,461,000.

Uzalishaji wa zao la mtama/ulezi ulipungua kutoka tani 1,161,000 hadi tani 1,119,000, sawa na upungufu wa asilimia 3.6. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya chakula ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula 2008 – 2011 (Tani 000)

Zao	2008	2009	2010r	2011p	Badiliko (%) 2009/10
Mahindi	3,555	3,324	4,475	4,341	-3.0%
Mchele	875	886	1,700	1,461	-14.1%
Ngano	92	94	62	113	82.3%
Mtama/Ulezi	1,064	204	1,161	1,119	-3.6%
Mihogo	1,797	1,759	1,464	1,549	5.8%
Maharage/Mikunde	1,125	1,184	1,254	1,632	30.1%
Ndizi	982	991	975	1,048	7.5%
Viazi vitamu	1,379	1,381	1,231	1,710	38.9%

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.
r Takwimu zimerekebishwa
p: Takwimu za muda

Uzalishaji wa Mazao ya Biashara

235. Mwaka 2011, uzalishaji wa mazao ya biashara hususan pamba, mkonge, korosho, chai na sukari uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2010. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo yanayolima mazao haya; na matumizi ya mbegu bora, madawa na mabomba ya kunyunyuzia dawa. Aidha, sababu mahsusi ni pamoja na ufufuaji wa mashamba ya chai katika wilaya za Rungwe na Korogwe; upanuzi wa mitambo ya kuzalisha sukari; kuanza kwa uvunaji wa mkonge kwa wakulima wadogo; na utumiaji wa viuatilifu vya udhibiti wa visumbufu vya mikorosho kwa wakati unaotakiwa.

236. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa mazao ya kahawa, pareto na tumbaku ulipungua mwaka 2011 ikilinganishwa na mwaka 2010. Uzalishaji wa zao la kahawa ulipungua kutoka tani 60,575 mwaka 2010 hadi tani 32,304, sawa na upungufu wa asilimia 88. Kupungua kwa uzalishaji kulitokana na kupungua kwa mvua za vuli, mabadiliko ya vipindi vya mvua katika mikoa ya Kagera na Mbeya na matumizi duni ya pembejeo. Uzalishaji wa pareto ulipungua kwa

asilimia 9.6 kutoka tani 5,000 mwaka 2010 hadi tani 4,560 mwaka 2011. Upungufu huu ulitokana na mbegu/miche bora kutotosheleza mahitaji ya wakulima. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya biashara ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 11.2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara 2008-2011 (Tani).

Zao	2008	2009	2010	2011	Badiliko (%) 2010/11
Pamba	200,662	267,004	163,644	250,000	35
Tumbaku	55,356	60,900	130,000	123,904	(4.9)
Sukari	276,605	279,850	317,000	304,135	13.37
Chai	34,770	33,160	55,699.13	32,812	3.55
Pareto	1,500	3,320	5,000	4,560	(9.64)
Kahawa	58,052	40,000	60,575	32,304	(88)
Mkonge	33,000	26,363	35,000	33,406	27.88
Korosho	99,107	74,169	121,070	160,000	24.33

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta

237. Mwaka 2011, uzalishaji wa mazao ya mafuta yakiwemo alizeti, karanga, na ufuta uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2010. Ongezeko hilo lilitokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo yanayozalisha kwa wingi mazao hayo na kuendelea kupanuka kwa wigo wa soko la ufuta. Hata hivyo, uzalishaji wa soya ulikuwa pungufu kwa asilimia 42.0 kutokana na muitiko mdogo wa wakulima kutokana na kukosa soko la uhakika.Mchanganuo wa uzalishaji wa mazao ya mafuta ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta 2008 – 2011 (Tani)

Zao	2008	2009	2010	2011	Badiliko (%) 2010/11
Alizeti	418,317	466,831	348,877	786,902	126
Karanga	396,769	385,480	320,582	651,397	103
Ufuta	46,767	115,295	65,557	357,162	445
Soya	3,450	3,900	4,300	2,500	-42

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo

238. Mwaka 2011, jumla ya matrekta makubwa mapya 3,183 yaliingizwa nchini ikilinganishwa na matrekta 1,586 mwaka 2010. Ongezeko la matrekta makubwa lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matrekta nchini kufuatia kuongezeka kwa fursa ya kupata mikopo ya kununua matrekta hayo kutoka taasisi mbalimbali kama vile Mfuko wa pembejeo na Benki ya Rasilimali na kuendelea kuingizwa kwa wingi kwa matrekta makubwa kupitia mradi wa SUMA JKT. Mwaka 2011, SUMA JKT peke yao waliingiza nchini matrekta makubwa 1,190. Aidha, idadi ya matrekta madogo (*Power Tillers*) yaliyoingizwa nchini mwaka 2011 yalikuwa 699 ikilinganishwa na matrekta madogo 2,553 mwaka 2010.

Kilimo cha Umwagiliaji

239. Mwaka 2011, eneo la jumla ya hekta 54,000 za umwagiliaji lilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu ikilinganishwa na hekta 90,000 zilizofanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2010. Idadi hii inafanya jumla ya eneo lililofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu kufikia jumla ya hekta 419,744 ikilinganishwa na hekta 365, 744 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 14.8. Jumla ya hekta 345,690 za umwagiliaji ziliendelezwa kwa kujengewa miundombinu ya umwagiliaji ikilinganishwa na hekta 331,490 zilizoendelezwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Aidha, miundombinu ya mabwawa 8 ya kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji ilijengwa/ilikarabatiwa mwaka 2011.

240. Mwaka 2011, idadi ya kaya zilizonufaika na miundombinu iliyoboreshwa ya skimu za umwagiliaji iliongezeka na kufikia kaya 440,892 kutoka kaya 351,720 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 25.4. Idadi ya

vikundi vya umwagiliaji vilivyoundwa na kusajiliwa ili kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinakuwa endelevu ilifikia vikundi 250 mwaka 2011 ikilinganishwa na vikundi 210 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 19.0. Jumla ya wakulima 350 na wataalam 96 katika ngazi mbalimbali walipatiwa mafunzo juu ya namna ya kuendeleza teknolojia sahihi za umwagiliaji na matumizi bora ya maji kwa umwagiliaji ikilinganishwa na wakulima 510 na wataalam 30 mwaka 2010.

Huduma za Ugani na Mafunzo

241. Mwaka 2011, wataalam wapya wa ugani 2,793 waliajiriwa katika Halmashauri za Wilaya nchini ikilinganishwa na wataalam 1,738 na hivyo kufanya idadi ya wataalam wa ugani kufikia 7,974 ikilinganishwa na wataalam wa ugani 5,181 mwaka 2010. Kati ya hao, 1,927 walikuwa wataalam wa ngazi ya stashahada na waliobaki ni wa ngazi ya astashahada

242. Mwaka 2011, maafisa ugani 33 wa shamba darasa kutoka Halmashauri 10 za mikoa ya Mara, Mwanza, Kigoma, Kagera, Tabora na Shinyanga walipatiwa mafunzo rejea ya wakufunzi wawezeshaji (*Training of Trainers – TOT*). Aidha, Serikali ilitoa mafunzo ya wakufunzi wawezeshaji katika kilimo cha mpunga kwa maafisa ugani 25 kutoka Halmashauri 20 za Igunga, Nzega, Bahi, Bagamoyo, Rufiji, Kilombero, Mvomero, Kilosa, Kahama, Shinyanga, Sengerema, Misungwi, Kwimba, Bukombe, Maswa, Kibondo, Magu, Mbarali, Kyela na Iringa kupitia Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji. Mwaka 2011, Vituo 73 vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (*Ward Agriculture Resource Centre – WARCs*) vilijengwa na vituo 64 vilikarabatiwa. Wakulima 23,200 walipatiwa mafunzo kupitia mfumo wa mkulima kumfundisha mkulima (*Farmer – to Farmer Extension*) ambao wanaendelea kuwafundisha wakulima wenzao mbinu bora za kilimo. Aidha, mwaka 2011, Serikali kupitia mradi wa DADPS iliendelea kuboresha huduma za ugani ambapo pikipiki 1,612 na baiskeli 3,389 zilinunuliwa; nyumba mpya 78 zilijengwa na nyumba 156 zilikarabatiwa.

Shughuli za Utafiti

243. Mwaka 2011, mbegu mpya 7 za mazao ya chakula ziligunduliwa na kupitishwa ili ziweze kutumika na wakulima. Mbegu hizo mpya na bora ni kwa mazao matatu ya chakula ambayo ni ulezi (aina mbili), maharage na muhogo

(aina nne). Aidha, mwaka 2011, uzalishaji wa mbegu mama kwa aina za mbegu mpya kwa ajili ya kuzalisha mbegu za msingi uliendelea, ambapo kilo 12,361 za nafaka na jamii ya mikunde zilizalishwa kama ilivyoainishwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 11.4: Uzalishaji wa Mbegu Mama (Tani)

Mbegu mama	**2010**	**2011**
Jamii ya nafaka	13.13	6.53
Jamii ya mikunde	11.53	5.84
Jamii ya mafuta	4.3	-
Pamba	1.48	-
*Muhogo (Vipingili)	27.6 (milioni)	-

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.
*Jamii ya mizizi vipando
-Takwimu hazikupatikana

Mfuko wa Pembejeo

244. Mwaka 2011, Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo ilitoa mikopo 6 ya matrekta madogo ya mikono ikilinganishwa na mikopo 30 iliyotolewa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 80. Aidha, mikopo 93 ya matrekta makubwa ilitolewa mwaka 2011 ikilinganishwa na mikopo 89 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Vile vile, mwaka 2011 Serikali ilitoa mikopo 32 kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo ikilinganishwa na mikopo 46 iliyotolewa mwaka 2010. Upungufu huu ulitokana na ufinyu wa bajeti ambao ulipelekea kushindwa kukidhi maombi yaliyopokelewa. Serikali pia ilitoa mkopo mmoja mwaka 2011 kwa ajili ya zana za umwagiliaji na mkopo mwingine mmoja kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao.

Utoaji wa Ruzuku za Pembejeo

245. Mwaka 2011, jumla ya vocha 5,340,000 zilikuwa zimesambazwa kwa kuzingatia mahitaji ya ngazi ya Taifa, Mkoa, Wilaya hadi ngazi ya kijiji. Ruzuku iliendelea kutolewa kwa mikoa 20 kama ilivyokuwa mwaka 2010. Idadi ya kaya zilizonufaika na ruzuku ya pembejeo ziliongezeka kutoka kaya 1,500,000 mwaka 2010 hadi kaya 2,000,000 mwaka 2011. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa maduka ya pembejeo za kilimo hadi ngazi ya kijiji

kufuatia kuhamasika kwa mawakala wa pembejeo za kilimo kupitia utaratibu wa vocha. Aidha, hadi Februari 2011, upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora ulikadiriwa kufikia tani 27,772.6 sawa na asilimia 92.6 ya mahitaji yote ya tani 30,000 kwa mwaka. Vile vile, upatakanaji wa mbolea hadi Februari 2011 ulikuwa tani 298,453 sawa na asilimia 62 ya mahitaji yote ambayo ni tani 485,000 kwa mwaka. Kupungua kwa upatikanaji wa mbolea kulitokana na gharama kubwa za uagizaji kwani takribani asilimia 90 ya mbolea inayotumika nchini inaagizwa kutoka nje. Kutokana na utaratibu huo, tija katika uzalishaji wa mazao ya mahindi iliongezeka. Utoaji wa ruzuku za pembejeo umeainishwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 11.5: Utoaji Ruzuku za Pembejeo

Aina ya Pembejeo	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11
Mbolea (MT)	89,820	141,050	150,055	200,000
Mbegu bora (MT)	1,071	7,180	15,525.20	21,150
Madawa ya Korosho	Lita 50,000 na Tani 1,100	Lita 386,649 na Tani 154	Tani 64,000	Tani 64,000
Madawa ya Pamba – (Acre-pack)	1,200,000	1,200,000	4,653,900	4,653,900
Miche ya Kahawa	5,000,000	10,000,000	10,400,000	8,226,091
Miche ya Chai	5,000,000	8,112,515	7,700,000	11,481,528
Mbegu bora ya Pamba (MT) - Tani			7,180	15,370

Chanzo: Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika

MIFUGO

Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake

246. Mwaka 2011, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na kuku uliongezeka na kufikia tani 503,496 kutoka tani 449,673 zilizozalishwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mazao yake na kupanuka kwa wigo wa masoko.

247. Mwaka 2011, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) iliuza jumla ya ng'ombe wa nyama 8,722 wenye thamani ya shilingi 2.6 bilioni ikilinganishwa na ng'ombe wa nyama 7,597 wenye thamani ya shilinigi 2.4 bilioni waliouzwa mwaka 2010. Ongezeko hilo lilitokana na kuanzisha kwa Programu ya Unenepeshaji mifugo.

248. Mwaka 2011, uzalishaji wa maziwa nchini uliongezeka kwa asilimia 5.2 hadi lita 1.74 bilioni kutoka lita 1.65 bilioni mwaka 2010. Kati ya hizo, lita milioni 608 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita 1.13 bilioni zilitokana na ng'ombe wa asili. Aidha, usindikaji wa maziwa uliongezeka na kufikia lita 112,400 kwa siku mwaka 2011 ikilinganishwa na lita 105,380 kwa siku mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Mwaka 2011, jumla ya dozi 150,000 za mbegu bora zilizalishwa ikilinganishwa na dozi 110,000 zilizozalishwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 36. Vile vile, idadi ya ng'ombe waliohamilishwa iliongezeka kutoka ng'ombe 73,900 mwaka 2010 hadi ng'ombe 76,800 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 4.

249. Uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai 2.9 bilioni mwaka 2010 hadi mayai 3.34 bilioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 15. Aidha, jumla ya vifaranga 38.4 milioni vya kuku wa nyama na mayai vilizalishwa nchini mwaka 2011 ilinganishwa na vifaranga 35.6 milioni mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 7.9

250. Mwaka 2011, tani 48.0 za mbegu bora za aina mbalimbali za malisho zilizalishwa katika mashamba ya Serikali ikilinganishwa na tani 45.0 zilizozalishwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 6.7. Aidha, uzalishaji wa hei kutoka katika mashamba ya Serikali uliongezeka kwa asilimia 15.5 hadi marobota 350,000 ikilinganishwa na marobota 303,000 yaliyozalishwa mwaka 2010. Vile vile, jumla ya marobota 420,000 ya hei yalizalishwa na sekta binafsi ikilinganishwa na marobota 418,831 yaliyozalishwa mwaka 2010. Mwaka 2011, tani 852,000 za aina mbalimbali ya vyakula vya mifugo zilizalishwa ikilinganishwa na tani 801,727 zilizozalishwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 6.

Jedwali Na. 11.6: Uzalishaji wa Mazao Yatokanayo na Mifugo

Mazao	Uzalishaji/Kipimo	2007	2008	2009	2010	2011	% Badiliko
Nyama:							
Ng'ombe	Tani	180,629	218,976	225,178	243,943	262,606	7.7
Mbuzi/Kondoo	Tani	80,936	81,173	82,884	86,634	103,709	19.7
Nguruwe	Tani	31,721	33,307	36,000	38,180	43,647	14.3
Kuku	Tani	77,280	77,250	78,168	80,916	93,534	15.6
Jumla		**370,566**	**410,706**	**422,230**	**449,673**	**503,496**	**12.0**
Maziwa:							
Ng'ombe asilia	Lita (000)	945,524	980,000	1,012,436	997,261	1,135,422	13.9
Ng'ombe wa kisasa	Lita (000)	475,681	520,000	591,690	652,596	608,800	-6.7
Jumla		**1,421,205**	**1,500,000**	**1,604,126**	**1,649,857**	**1,738,683**	**5.4**
Mayai	Idadi	2,230,900	2,690,000	2,806,350	2,917,875	3,339,566	14.5
Uzalishaji Vyakula vya Mifugo	Tani	-	-	801,827	720,711	852,000	18.2

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

251. Mwaka 2011, idadi ya mifugo nchini ilikadiriwa kufikia ng'ombe 21.3 milioni, mbuzi 15.2 milioni, na kondoo 6.4 milioni ikilinganishwa na ng'ombe 19.2 milioni, kondoo 3.6 milioni na mbuzi 13.7 milioni mwaka 2010. Aidha, idadi ya nguruwe ilikuwa 1.9 milioni na kuku 58 milioni kama ilivyokuwa mwaka 2010. Viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo kwa mtu kwa mwaka kwa sasa ni wastani wa kilo 12 za nyama, lita 44 za maziwa na mayai 75. Hata hivyo, viwango hivi ni vidogo ikilinganishwa na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

Biashara ya Mifugo na Mazao yake

252. Mwaka 2011, idadi ya mifugo iliyouzwa minadani iliongezeka hadi kufikia ng'ombe 925,097, mbuzi 704,987 na kondoo168,313 wenye thamani ya shilingi 423.9 bilioni ikilinganishwa na ng'ombe 857,208, mbuzi 682,992 na kondoo 122,035 waliokuwa na thamani ya shilingi 382.4 bilioni mwaka 2010. Ongezeko hilo la idadi ya mifugo iliyouzwa lilitokana na kuimarishwa kwa huduma za minada, kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika miji na masoko maalum kama maduka ya kisasa, hoteli na migodi.

253. Mwaka 2011, jumla ya ng'ombe 1,041 na mbuzi 657 wenye thamani ya shilingi 9.65 bilioni waliuzwa katika nchi za Comoro, Rwanda na Kenya ikilinganishwa na jumla ya ng'ombe 2,970 na mbuzi 302 wenye thamani ya shilingi 2.89 bilioni waliouzwa mwaka 2010. Aidha, jumla ya tani 20.3 za nyama ya ng'ombe, tani 286 za nyama ya mbuzi na tani 97 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi 1.6 bilioni ziliuzwa katika nchi za Oman na Kuwait ikilinganishwa na tani 36.9 za nyama ya ng'ombe, tani 122 za nyama ya mbuzi na tani 34.6 za nyama ya kondoo zilizouzwa katika nchi za Comoro, Burundi, Oman, Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu (UEA), Muscat, Malawi, Kenya na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo mwaka 2010.

254. Mwaka 2011, jumla ya vipande milioni 2.5 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.4 vya mbuzi na 200,000 vya kondoo vilikusanywa. Kati ya hivyo, vipande 1,719,506 vya ngozi ya ng'ombe, 2,111,176 vya mbuzi na 83,600 vya kondoo viliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi 17.4 bilioni ikilinganishwa na vipande 739,315 vya ngozi ya ng'ombe, vipande 1,900,000 vya ngozi ya mbuzi na vipande 176,400 vya ngozi ya kondoo vilivyouzwa nje mwaka 2010 kwa thamani ya shilingi 8.2 bilioni. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa bei na mahitaji ya ngozi na kuimarika kwa soko la ngozi duniani.

255. Mwaka 2011, idadi ya vipande vya ngozi iliyosindikwa iliongezeka na kufikia vipande 782,447 vya ng'ombe, vipande 1,535,562 vya ngozi ya mbuzi na vipande 61,200 vya ngozi ya kondoo vyenye thamani ya shilingi 10.6 bilioni ikilinganishwa na vipande 275,000 vya ngozi ya ng'ombe na vipande 1,440,000 vya ngozi ya mbuzi vilivyokuwa na thamani ya jumla ya shilingi 6.2 bilioni mwaka 2010.

Jedwali Na. 11.7: Ukusanyaji, Uuzaji wa Ngozi Ndani na Nje ya Nchi na Madaraja ya Ngozi Hizo

A. UKUSANYAJI WA NGOZI				
Mwaka	**Ngozi za Ng'ombe**	**Ngozi za Mbuzi**	**Ngozi za Kondoo**	**Thamani Tshs.'000**
2002	1,400,000	700,000	350,000	4,500,000
2003	1,400,000	800,000	460,000	5,500,000
2004	1,600,000	1,200,000	650,000	6,500,000
2005	1,600,000	1,500,000	750,160	5,500,000
2006	1,660,000	1,400,000	950,000	6,800,000
2007	1,980,000	1,520,000	1,200,000	8,700,000
2008	2,500,000	1,900,000	1,500,000	13,500,000
2009	1,650,000	2,990,000	1,250,000	10,900,000
2010	1,500,000	2,400,000	650,000	8,500,000
2011	2,500,000	2,400,000	200,000	16,100,000

B. UUZAJI NGOZI NJE				
Mwaka	**Ngozi za Ng'ombe**	**Ngozi za Mbuzi**	**Ngozi za Kondoo**	**Thamani Tshs.'000**
2002	1,200,000	511,700	165,000	4,000,000
2003	1,300,000	600,000	300,000	4,600,000
2004	1,774,000	1,431,000	488,000	5,712,000
2005	1,400,000	1,200,000	597,155	4,025,400
2006	1,363,721	1,216,740	861,770	7,500,000
2007	1,700,000	1,055,000	925,530	16,200,000
2008	2,300,000	1,600,000	1,100,000	21,500,000
2009	982,668	2,700,000	769,936	12,800,000
2010	739,315	1,912,182	176,400	8,191,803
2011	1,719,506	2,111,176	83,600	17,400,000

Chanzo: Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, 2011

USHIRIKA NA MASOKO

Maendeleo ya Ushirika

256. Mwaka 2011, Serikali iliendelea na utekelezaji wa programu ya mageuzi na maboresho ya Ushirika nchini (Cooperative Reform and Mordenization Programme) ili kuimarisha vyama vikuu vya ushirika na kuviwezesha kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi hususan waliopo vijijini. Utekelezaji wa programu hii ulipelekea kuongezeka kwa idadi ya vyama vya ushirika kutoka vyama 9,596 mwaka 2010 hadi kufikia vyama 9,693 mwaka 2011.

257. Mwaka 2011, idadi ya Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) iliongezeka na kufikia 5,346 kutoka vyama 5,314 mwaka 2010. Vile vile, idadi ya wanachama iliongezeka kwa asilimia 5.7 na kufikia wanachama 970,655 kutoka wanachama 917,889 mwaka 2010. Aidha, hisa, akiba na amana za wanachama ziliongezeka kutoka shilingi 236.8 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 399.0 bilioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 68.5. Mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka shilingi 539.2 bilioni mwaka 2010 hadi shilingi 627.2 bilioni mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 16.3.

Jedwali Na. 11.8: Maendeleo ya Ushirika

Aina ya ushirika	Mwaka		Badiliko %
	2010	2011	
SACCOS	5,314	5,346	0.6
AMCOS	2,819	2,871	1.8
Ushirika wa Umwagiliaji	113	116	2.7
Ushirika wa aina nyingine	1,309	1,319	0.8
Vyama vikuu/Apex/TFC	41	41	0
Jumla	9,596	9,693	0.7

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mwenendo wa Bei za Mazao ya Biashara

258. Mwaka 2011, wastani wa bei ya kahawa aina ya Mild Arabica katika soko la nje ilipanda hadi dola za kimarekani 4.38 kwa kilo kutoka dola za kimarekani 3.17, sawa na ongezeko la asilimia 38.2. Kahawa aina ya Hard Arabica iliuzwa kwa dola za kimarekani 2.60 kwa kilo kutoka dola za kimarekani 1.95 kwa kilo mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 33. Aidha, kahawa aina ya Robusta iliuzwa kwa dola za kimarekani 1.52 mwaka 2011 kutoka dola za kimarekani 1.25 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 22. Bei ya mkonge ilipanda kutoka dola za kimarekani 0.91 kwa kilo mwaka 2010 hadi dola za kimarekani 1.26 kwa kilo mwaka 2011. Wastani wa bei ya kilo ya chai ulishuka kutoka dola za kimarekani 1.99 mwaka 2010 hadi kufikia dola za kimarekani 1.68 kwa kilo mwaka 2011.

Jedwali Na.11.9: Mwenendo wa Wastani wa Bei za Mazao ya Biashara Katika Soko la Dunia

Mwaka	**Zao**						
	Kahawa -Mild Arabica	Kahawa -Hard Arabica	Kahawa-robusta	Chai	Pamba	Mkonge	Karafuu
	Bei (USD /Kg)						
2008	2.71	1.70	1.57	1.38	1.92	0.97	3.97
2009	2.34	1.76	1.49	1.59	1.99	1.21	4.02
2010	3.17	1.95	1.25	1.99	1.99	0.91	4.33
2011	4.38	2.60	1.52	1.68	-	1.26	-

Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara

UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 35

Msimu[1]	Miwa				Sukari		
	Wakulima					iliyotumika[3]	
	Umma (000 Tani)	Binafsi (000 Tani)	Jumla (000 Tani)	Bei[2] (Sh./Tani)	Iliyozalishwa Tani	Jumla Tani	Kilo kwa kila mtu[4]
1977/78	1008	116	1124	96.20	132979	111546	6.69
1978/79	1169	197	1366	96.20	114267	127712	7.42
1979/80	1180	210	1390	101.20	122530	112282	6.34
1980/81	854	193	1047	106.20	114667	115961	6.37
1981/82	1135	203	1338	137.30	124326	120629	6.44
1982/83	1090	113	1203	170.00	101996	93179	4.84
1983/84	1372	160	1532	238.00	131525	108369	5.48
1984/85	1148	105	1253	323.70	108102	111433	5.48
1985/86	1003	104	1107	352.30	100287	95379	4.56
1986/87	991	72	1063	463.00	94815	109462	5.09
1987/88	997	102	1099	600.00	101266	96271	4.35
1988/89	787	91	878	750.00	96227	126771	5.29
1989/90	963	98	1061	1748.45	111236	190750	5.47
1990/91	1068	116	1184	2525.90	118560	212585	5.93
1991/92	967	114	1081	3476.85	108480	202478	6.07
1992/93	1098	273	1371	5267.67	121414	204126	6.11
1993/94	1105	362	1467	6200.00	123949	139829	5.38
1994/95	914	370	1284	8600.00	104624	238424	5.38
1995/96	997	372	1369	8900.00	116810	268910	..
1996/97	951	347	1298	9500.00	116100	275700	5.54
1997/98	808	176	984	10500.00	116100	271790	5.70
1998/99	948	320	1268	12500.00	113622	101272	5.87
1999/00	907	341	1248	12500.00	116927	100127	6.70
2000/01	1050	284	1334	14000.00	135534	122534	10.00
2001/02	1134	389	1523	14700.00	164498	142398	10.10
2002/03	1402	411	1813	15000.00	190120	167300	10.42
2003/04	1672	670	2342	16800.00	223839	290711	10.90
2004/05	1594	752	2346	20568.00	229617	328005	10.90
2005/06	1545	956	2501	22383.00	263317	343292	12.00
2006/07	1430	611	2041	29000.00	192095	366708	12.00
2007/08	1967	799	2766	32767.00	265434	382518	13.00
2008/09	2056	693	2749	32770.51	279850	396113	13.40
2009/10	1972	598	2570	42046.00	263461	398070	13.68
2010/11	2357	661	3019	43865.00	304135	410259	12.00
Badiliko (%)							
09/10-10/11	-0.16	-0.10	-0.15	-0.04	-0.13	-0.03	0.14
ɔngezeko (%)							
77/78-10/11	1.34	4.70	1.69	454.98	1.29	2.68	0.79

Chanzo: Bodi ya Sukari Tanzania

1 Msimu ni Kati ya Julai na Juni

2 Bei ya Mimea ni ile iliyo na asilimia 10.5 za Sycrose

3 Ni pamoja na Sukari iliyopelekwa Zanzibar

4 Ni kwa Tanzania bara

* Sukari yote huzalishwa na wakulima/mashirika binafsi

PAMBA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 36

Msimu [1]	Pamba yenye mbegu					Pamba iliyoondolewa mbegu					
	Uzalishaji Kiasi (tani)			Bei ya wastani (Shs/Kilo)		Kiasi (tani)			Mauzo nchini		
									Kiasi (tani)	Bei ya wastani (Shs/tani)	
	AR	BR	Jumla	AR	BR	AR	BR	Jumla	Jumla [2]	AR	BR
1976/77	176894	17800	194694	2.00	1.00	61549	6074	67623	8146	9487	7230
1977/78	153292	14790	168082	2.30	1.15	46555	5821	52376	14422	12186	9370
1978/79	152267	14248	166515	2.40	1.20	51072	4696	55768	14253	12340	8810
1979/80	162087	18367	180454	3.00	1.30	52546	3931	56477	17284	13750	11040
1980/81	166233	8344	174577	3.20	1.50	54189	2962	57151	15634	13750	11040
1981/82	126799	6127	132926	3.70	1.70	42439	2153	44592	14070	15480	11730
1982/83	124559	3351	127910	4.70	2.50	40521	2381	42902	12660	15420	11730
1983/84	136151	4647	140798	6.00	3.70	41779	2175	43954	11771	15867	12038
1984/85	152355	4490	156845	8.40	4.50	50858	1154	52012	16236	26000	17400
1985/86	97384	8515	105899	13.00	7.00	29715	17775	47490	13247	52250	37350
1986/87	210454	4115	214569	16.90	9.10	55108	2338	57446	11389	52250	37350
1987/88	252177	2738	254915	19.45	9.10	67057	659	67716	13247	81350	67250
1988/89	184524	4720	189244	22.35	10.00	61552	1880	63432	11084	175000	140000
1989/90	112333	572	112905	28.00	11.00	37652	192	37844	13184	225000	190000
1990/91	148124	1017	149141	41.00	14.00	48880	341	49221	300000	300000	240000
1991/92	26841	32	26873	70.00	28.00	90706	11	90717	14301	325000	255000
1992/93	281984	22000	303984	60.00	28.00	85784	..	85784	4405	542916	..
1993/94	125434	..	125434	120.00	..	42695	..	42695	..	..	..
1994/95	125434	..	125434	120.00	..	42695	..	42695	..	..	..
1995/96	221148	..	221148	207.00	..	84782	..	84782	..	..	..
1996/97	251751	74	251751	170.00	..	85162	25	85187	..	..	..
1997/98	202217	..	202217	180.00	..	67780	..	67780	..	..	..
1998/99	105853	..	105853	185.00	..	35480	..	35480	..	..	..
1999/00	100500	..	100500	123.00	..	33686	..	33686	..	..	..
2000/01	123558	..	123558	180.00	..	41415	..	41415	..	..	..
2001/02	148180	..	148180	165.00	..	49668	..	49415	..	..	..
2002/03	187908	781	188689	180.00	50	62983	262	63245	..	..	..
2003/04	139756	213	139969	280.00	100	46843	72	46915	..	..	..
2004/05	341589	..	341589	250.00	0	114496	..	114496	..	..	..
2005/06	376591	..	376591	220.00	0	126228	..	126228	..	..	..
2006/07	130585	..	130585	350.00	0	43770	..	43770	..	..	..
2007/08	200662	-	200662	450		70773	-	70773	37488	..	..
2008/09	368697	0	368697	480	0	123582	0	123582	66554	..	..
2009/10	267644	0	267644	480	0	54851	0	54851	..	..	..
2010/11	163518	0	163518	900	0	54809	0	54809	..	..	..
Badiliko (%) 2009/10-2010/11*	-0.39		-0.27	0.00		-0.56		-0.56			
Ongezeko (%) 77/78-10/11*	-0.08		-0.16	449.00		-0.11		-0.19			

Chanzo: Bodi ya Mauzo ya Pamba

[1] Msimu ni kati ya Juni na Mei

[2] Ni jumla ya AR na BR

.. Takwimu hazikupatikana

ENEO LILILOPANDWA MICHAI NA MAJANI MABICHI YALIYOPATIKANA

Jedwali Na. 37

Msimu [1]	Eneo lililopandwa (hekta): mashamba			Majani Mabichi yaliyopatikana (tani)						Bei kwa mkulima (Shs/Kilo)	Mauzo[2] Nchini (tani)
				Kiumilikaji: mashamba			Kikanda: mashamba				
	Makubwa	Madogo	Jumla	Makubwa	Madogo	Jumla	Kaskazini	Kusini	Jumla		
1976/77	9023	9217	18240	59300	13679	72979	27841	45138	72979	0.90	2994
1977/78	9214	9334	18548	65933	22598	88531	32784	55747	88531	1.50	4168
1978/79	9268	9280	18548	60062	24230	84292	27177	57115	842292	1.50	3735
1979/80	9268	9289	18557	61294	21780	83074	27249	55825	83074	1.50	4376
1980/81	9268	9289	18557	59603	18800	78403	25267	53136	78403	1.50	5487
1981/82	9268	9289	18557	59603	18800	78403	25267	53136	78403	1.50	5487
1982/83	9268	9365	18633	56023	18540	74563	22622	51941	74563	1.50	6735
1983/84	9699	9177	18876	65309	18931	84240	22869	61371	84240	2.80	3763
1984/85	9699	9177	18876	51443	21493	72936	18346	54590	72936	2.80	4286
1985/86	9699	9177	18876	55680	21550	77230	22369	54861	77230	4.10	4714
1986/87	9699	9177	18876	52271	19201	71472	17564	53908	71472	4.90	6346
1987/88	9699	9177	18876	46752	17942	64694	12333	52361	64694	7.60	4556
1988/89	9699	9177	18876	45771	17851	63622	12749	50883	63632	9.90	4260
1989/90	9699	9177	18876	52194	18874	71068	18099	52969	71068	13.40	3559
1990/91	9699	9177	18876	70442	22434	92876	23531	69345	92876	17.00	3491
1991/92	9699	9177	18876	62994	20229	83223	19296	63927	83223	28.00	2750
1992/93	9699	9197	18896	80896	19934	100830	32218	68412	100630	45.00	3278
1993/94	10029	9197	19226	81159	21231	102390	32148	70242	102390	45.00	11124
1994/95	10149	9197	19346	93608	22641	116249	36825	79424	116249	50.00	..
1995/96	10652	9332	19984	79968	13803	93771	25935	67836	93771	55.00	2350
1996/97	11113	9451	20564	83126	7803	90929	21992	68937	93771	55.00	..
1997/98	11416	9451	20867	113448	7100	120548	30137	90411	120548	55.00	..
1998/99	11416	9451	20867	98800	7000	105800	26450	79350	150800	55.00	..
1999/2000	..	..	..	99848	6092	105940	24439	81502	105941	55.00	..
2000/2001	10811	10364	21175	109007	9728	118735	29419	89316	118735	65.00	2386
2001/2002	10811	10364	21175	97297	13999	111296	22794	88502	111296	80.00	2683
2002/2003	11097	9762	20889	100677	31718	132395	28679	103716	132395	85.00	3158
2003/2004	11485	10801	22286	95986	31993	127979	26384	101595	127979	86.00	3225
2004/2005	11271	11442	22713	94172	39246	133418	20649	112769	133418	86.00	4004
2005/2006	11310	10977	22287	91337	31881	123218	29046	94172	123218	93.00	3881
2006/2007	11271	11956	23227	109632	49024	158656	39673	118983	158656	100.00	4737
2007/08	11272	11449	22722	97310	51160	148470	33456	115015	148471	111.00	4253
2008/09	11271	11449	22722	100644	41167	141811	31677	110134	141811	118.00	4464
2009/10	11272	11449	22722	106021	44716	150737	33309	117428	150737	124.00	5084
2010/11	11272	11449	22722	95511	47616	143127	112368	30759	143127	152.00	6065
Badiliko (%)											
2009/10-2010/11	0.00	0.00	0.00	-0.10	0.06	-0.05	2.37	-0.74	-0.05	0.23	0.19
Ongezeko (%)											
76/77-2010/11	0.25	0.24	0.25	0.61	2.48	0.96	3.04	-0.32	0.96	167.89	1.03

Chanzo: Bodi ya Chai Tanzania

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Chai iliyotengenezwa

.. Takwimu hazikupatikana

KAHAWA ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 38

Msimu[1]	Iliyonunuliwa (Tani)				Bei (Sh./kilo)			Mauzo nchini[+]	
	ARABICA		ROBUSTA	JUMLA	ARABICA		ROBUSTA	KIASI	THAMANI
	Laini	Ngumu			Laini	Ngumu	Maganda	(Tani)	(shs'000)
1976/77	35263	2424	10995	48682	15.00	11.00	8.90	1625	9516
1977/78	38222	2851	12023	53096	10.89	17.50	5.27	758	6300
1978/79	33853	2551	12946	49350	9.07	14.16	4.64	587	8232
1979/80	30850	2968	14216	48034	11.42	13.32	5.55	336	5541
1980/81	52301	3223	11237	66761	12.36	10.50	4.50	687	7012
1981/82	36090	3753	10947	50790	14.90	10.50	5.93	997	13072
1982/83	38852	2216	12728	53796	15.17	10.55	10.55	1020	20170
1983/84	36436	1729	11509	49674	22.87	16.35	16.35	1730	25716
1984/85	36270	1974	10836	49080	29.68	15.07	15.07	895	36418
1985/86	41042	2820	11285	55147	45.80	20.90	20.90	1408	94117
1986/87	39060	2702	16975	58737	50.75	29.00	29.00	1146	96626
1987/88	32804	2514	10389	45707	66.00	37.70	37.00	1122	120638
1988/89	41230	2280	11620	55130	90.00	51.00	51.00	1220	229322
1989/90	34945	1702	16427	53074	165.00	66.50	55.00	783	144998
1990/91	31304	1416	11403	44123	165.00	66.50	60.50	783	151088
1991/92	37065	1926	8996	47987	230.00	100.00	70.00	1140	2558.76
1992/93	36901	2128	12217	51246	316.00	123.00	100.00	765	128200
1993/94	26361	2448	7577	36386	923.00	904.00	700.30	..	..
1994/95	27137	1542	7157	35836	1965.00	1481.10	1453.60	..	..
1995/96	35142	2096	9710	46948	1229.30	1301.60	1169.00	..	..
1996/97	32933	1279	9279	43491	..	..	..	..	..
1997/98	19789	1894	9165	30848	..	..	..	..	..
1998/99	23605	2590	13523	39718	1936.00	1064.00	1040.00	..	..
1999/00	18171	3593	1078	32842	1486.60	1894.80	476.47	..	..
2000/01	37176	3805	17007	57988	..	..	..	..	..
2001/02	38000	3500	12000	53500	..	..	..	..	..
2002/03	37294	4766	34368	76428	..	..	..	..	..
2003/04	20716	1850	16138	38704	1800.00	1200.00	600.00	38704	46670
2004/05	23870	888	9133	33891	2593.50	1976.00	1235.00	33891	62566
2005/06	24116	1362	8856	34334	1200.00	420.00	270.00	33300	79304246
2006/07	33345	2417	19076	54838	2840.00	1796.00	1616.00	548	1298675
2007/08	26330	1588	15606	43524	2995.00	1875.00	1734.00	43523	89,099
2008/09	37207	1727	29643	68577	2887.00	2172.00	1836.00	68577	165615552
2009/10	22217	915	11467	34599	3988.00	2475.00	1563.00	34599	108741091
2010/11	30309	2013	24348	56670	4500.00	1300.00	1200.00	56670	264143599
Badiliko (%)									
2009/10-10/11	0.36	1.20	1.12	0.64	0.13	-0.47	-0.23	0.64	1.43
Ongezeko (%)									
1976/77-10/11	-0.1	-0.2	1.2	0.2	299.0	117.2	133.8	33.9	27756.8

Chanzo: Bodi ya Kahawa Tanzania

+ Kahawa iliyosafishwa

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

2 Ni ya muda

.. Takwimu hazikupatikana

ENEO LILILOPANDWA MKONGE NA KATANI ILIYOPATIKANA

Jedwali Na. 39

Msimu[1]	Eneo (Hekta)			Katani iliyopatikana		Mauzo nchini[+]	
	Uliokomaa	Usiokomaa	Jumla	Kiasi (tani)	Bei kwa Mkulima (shs/tani)	Kiasi (tani)	Thamani (Sh. milioni)
1977/78	11626	38626	150252	91873	2474	25104	57.7
1978/79	107371	32589	139960	81384	2549	32023	95.6
1979/80	106866	26024	132890	85978	3135	35730	125.4
1980/81	99771	21642	121413	73753	3749	19687	68.0
1981/82	82257	17998	100255	60635	3784	30851	117.4
1982/83	85314	15720	101034	46187	4797	22384	94.9
1983/84	69799	13121	82920	38255	6410	12573	70.0
1984/85	62307	11796	74103	32247	7213	13075	88.3
1985/86	67606	13606	81212	30151	16099	19842	200.0
1986/87	67606	13606	81212	33170	19472	16477	407.0
1987/88	32932	20866	53798	33268	38750	20635	862.0
1988/89	47651	30584	78235	32265	64604	22661	1464.0
1989/90	48826	33780	82606	33743	94003	25563	2403.0
1990/91	49374	36240	85614	36001	89633	10398	932.0
1991/92	49374	36240	85614	24309	89203	17644	1582.2
1992/93	49374	36240	85614	21221	107079	18067	1517.6
1993/94	54485	24608	79093	29002	163540	17694	4031.0
1994/95	52953	25757	78710	24716	216026	18206	2629.0
1995/96	52018	27153	79171	28902	370807	18719	2549.0
1996/97	50459	28507	78967	25022	..	18606	3374.0
1997/98	48745	29997	78742	22180	..	18819	..
1998/99	151869	33997	185666	23229	..	6712	2146.0
1999/00	34645	7942	42587	41084	..	16033	5617.8
2000/01	34645	11473	46118	23542	368077	7569	2786.0
2001/02	34645	11473	46118	23641	337732	4947	1671.0
2002/03	39462	10611	50073	23280	450000	6300	2835.0
2003/04	29493	12204	41697	26758	540000	6370	4027.0
2004/05	45079	14500	59579	27794	617342	8213	5070.0
2005/06	26384	13264	39649	30934	810000	10767	8613.0
2006/07	28273	13608	41882	33327	975000	11010	10152.0
2007/08	28577	15622	44199	34057	1000000	16997	15800.0
2008/09	35751	18023	53774	25996	1000000	11496	10100
2009/10	30556	11849	42405	24092	1200000	12761	10375
2010/11	31117	12169	43286	25090	1300000	11617	13154
Badiliko (%)							
2009/10-10/11	1.8%	2.7%	2.1%	4.1%	8.3%	-9.0%	26.8%
Ongezeko (%)							
1977/78- 10/11	162.82%	-69.32%	-71.78%	-73.78%	48404.45%	-49.17%	17880.94%

Chanzo: Bodi ya Katani

+ Katani aina ya Line fibre, Tow na Flume Tow

1 Msimu ni kati ya Julai na Juni

.. Takwimu hazikupatikana

TUMBAKU ILIYONUNULIWA NA MAUZO NCHINI

Jedwali Na. 40

Msimu[1]	Iliyonunuliwa (tani)				Bei (shs/kg)			Mauzo Nchini[+]			
	Mvuke	Moshi	Hewa	Jumla	Mvuke	Moshi	Hewa	Kiasi (tani)		Thamani (shs.mil.)	
								Mvuke	Moshi	Mvuke	Moshi
1977/78	14451	2653	33	17137	7.40	5.20	4.80	3694	433	56.10	6.10
1978/79	14403	2654	30	17087	7.40	5.20	4.80	3254	1212	54.90	13.30
1979/80	13005	4195	34	17234	8.80	6.25	6.50	2829	1197	51.80	19.30
1980/81	12972	3670	33	16675	10.50	6.25	6.50	2981	958	57.70	43.40
1981/82	12164	4060	40	16264	12.60	7.70	6.80	3515	685	61.60	10.80
1982/83	9576	3987	52	13615	18.00	11.50	10.00	4048	462	99.00	31.10
1983/84	9009	1963	40	11012	18.00	11.50	10.00	3571	583	114.50	19.30
1984/85	10554	2726	36	13316	25.20	16.10	14.00	4417	333	179.80	13.20
1985/86	12113	415	21	12549	37.90	23.30	20.30	2302	281	126.30	13.80
1986/87	15009	1422	14	16445	49.25	30.30	26.40	4040	256	452.40	32.50
1987/88	11111	1802	8	12921	63.00	39.00	34.00	4069	259	651.90	45.10
1988/89	10187	1355	12	11554	75.60	48.75	37.32	4383	537	1074.10	88.20
1989/90	8461	3342	5	11808	93.04	76.49	40.25	8027	1057	2554.50	392.00
1990/91	10718	5733	8	16459	117.00	91.00	61.00	3845	531	4319.40	301.30
1991/92	18754	4566	2	23322	264.61	157.65	106.54	5364	172	7457.90	114.40
1992/93	18756	4566	2	23324	313.95	221.28	234.20	5372	209	7463.40	255.00
1993/94	21838	3953	6	25797	343.97	253.00	286.00	3164	285	4540.60	1120.00
1994/95	18269	4362	19	22650	564.58	353.30	373.22	18260	4360	10309.00	1984.00
1995/96	23415	5183	-	28598	561.00	455.00	-	1319	183	1785.00	1331.00
1996/97	27101	8279	-	35380	632.00	551.00	-	2914	86	1236.00	1332.00
1997/98	42041	9054	-	51095	714.00	477.00	-	2647	117	1890.00	1320.00
1998/99	32041	5482	-	37957	530.00	454.00	-	979	69	2077.00	2435.00
1999/00	18232	6202	-	24434	603.00	566.00	-	-	-	-	-
2000/01	18231	6578	-	24809	543.00	556.00	-	2176	3392	5669.00	-
2001/02	25905	1799	-	27704	519.00	428.00	-	1595	348	4996.00	-
2002/03	23074	4798	-	27872	563.00	547.00	-	2325	45	5940.00	-
2003/04	30124	3422	-	43547	725.00	680.00	-	2245	136	6862.00	-
2004/05	41394	5983	74	47451	918.11	781.93	729.23	3144	252	6881.00	427.00
2005/06	50494	5228	741	56464	983.00	735.00	635.00	3486	168	9335.00	392.00
2006/07	49576	1038	170	50784	1264.00	881.00	960.00	3685	0	14302.00	0.00
2007/08	52597	2474	286	55357	1144.000	849.000	957.000	4057	231	15392	801
2008/09	56,663	3641	437	60,741	2,741	1,659	1,698	5,544	0	26,167	0
2009/10	88,808	4901	497	94,202	2,946	1,691	1,773	2,210	148	9,699	590
2010/11	116,886	3685	-	120,572	1,960	1,540	-	1,877	0	11,815	0
Badiliko (%)											
09/10 - 10/11	0.32	-0.25	-1.00	0.28	-0.33	-0.09	-1.00	-0.15	-1.00	0.22	-1.00
Ongezeko (%)											
77/78-10/11	7.09	0.39	-1.00	6.04	263.86	295.15	-1.00	-0.49	-1.00	209.61	-1.00

Chanzo: Bodi ya Tumbaku Tanzania

+ Mauzo ya Tumbaku Moshi ni pamoja na Tumbaku Hewa

1 Msimu ni kati ya April na Machi

- Takwimu hazikupatikana

MAUA YA PARETO YALIYONUNULIWA NA MAUZO YA BIDHAA ZA PARETO NCHINI

Jedwali Na. 41

Msimu [1]	Maua yaliyonunuliwa (tani)				Mauzo Nchini: Kiasi (tani)			Mauzo Nchini: Thamani (Sh.'000)		
	Kaskazini	Kusini	Jumla	Bei [2] (Sh./kg)	Utomvu (Crude Extract)	Poda	Dawa (Dry Mack)	Utomvu (Crude Extract)	Poda	Dawa (Dry Mack)
1977/78	173	2379	2552	4.00	1.4	89.0	1609.0	332.00	880.00	555.00
Jasi	Tani	2500	2024	4226	9498	11820	74	650	84	126	99
Grafiti	Tani	-	-				-	-	-	-	-
Fedha	000Grams	12381	9835	8231	12040	10399	5317	6680	4961	7673	11615
Shaba	0001b	7222	6288	4452	11742	7531	21063	21063	11499	36710	30202
Madini ya viwandani	Tani	-	-				-	-	-	-	-
Bauxite	Tani	5003	20600	122920	39326000	37700000	571	480	2127	1050	1385
Jumla ('000 US $)							**983282**	**1076423**	**1103414**	**1508713**	**1940836**

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

** Takwimu zimerekebishwa

SURA YA 14

VIWANDA NA BIASHARA

Kiwango cha Ukuaji

294. Mwaka 2011, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za uzalishaji bidhaa za viwandani kilikuwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 7.9 mwaka 2010. Mchango wa shughuli za kiuchumi za uzalishaji bidhaa za viwandani katika Pato la Taifa uliendelea kuongezeka kutoka asilimia 9.0 mwaka 2010 hadi asilimia 9.3 mwaka 2011.

.

Viwanda Vidogo

295. Mwaka 2011, Serikali ilikamilisha zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo (SMEs baseline Survey 2011). Matokeo ya zoezi hilo yalibainisha kuwa kuna vikundi vya wajasiriamali zaidi ya milioni 2.7 ikilinganishwa na vikundi milioni 2.0 vilivyokuwepo mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 35.0. Kati ya vikundi hivyo vya wajasiriamali, zaidi ya asilimia 98 vipo katika sekta isiyo rasmi. Aidha, kutokana na matokeo ya utafiti huo, mchango wa sekta ya biashara na viwanda vidogo na vya kati katika pato la taifa uliongezeka kutoka asilimia 30 mwaka 2010 hadi asilimia 35 mwaka 2011. Matokeo ya utafiti yalibainisha pia kuwa sekta hii ilitoa ajira kwa watu milioni 5.1.

Gharama za Uzalishaji

296. Mwaka 2011, gharama za uzalishaji bidhaa ziliongezeka kwa asilimia 40 hadi shilingi 2,914,708 milioni kutoka shilingi 2,081,934 milioni mwaka 2010. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa vyakula, vinywaji, tumbaku, chuma, sigara na kemikali kutokana na mfumuko wa bei na ukosefu wa nishati ya umeme wa uhakika.

Uzalishaji katika baadhi ya Viwanda Nchini

297. Mwaka 2011, uzalishaji katika baadhi ya viwanda kama vile konyagi, sigara, kamba za katani, nguo, pombe ya kibuku, bia na chuma uliongezeka. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo katika

soko la ndani. Uzalishaji wa konyagi uliongezeka kwa asilimia 11.2 kutoka lita 11,186,000 mwaka 2010 hadi lita 12,437,000 mwaka 2011. Aidha, uzalishaji wa pombe ya kibuku uliongezeka kwa asilimia 15.9 kutoka lita 21,037,000 mwaka 2010 hadi lita 24,391,000 mwaka 2011. Uzalishaji wa mabati uliongezeka kwa asilimia 0.8 kutoka tani 71,276 mwaka 2010 hadi tani 71,881 mwaka 2011.

298. Uzalishaji wa unga wa ngano uliongezeka kutoka tani 444,242 mwaka 2010 hadi tani 445,227 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Uzalishaji katika viwanda vya bia uliongezeka kutoka lita milioni 243 mwaka 2010 hadi kufikia lita milioni 305 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 25.7. Uzalishaji wa sigara ulipanda kwa asilimia 6.3 kutoka sigara milioni 6,181 mwaka 2010 hadi kufikia sigara milioni 6,569 mwaka 2011. Uzalishaji katika viwanda vya kusindika ngozi uliongezeka kutoka futi za mraba milioni 39.7 mwaka 2010 hadi kufikia futi za mraba milioni 40.2 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 1.3.

299. Uzalishaji wa nguo uliongezeka kutoka mita za mraba 103,177,000 mwaka 2010, hadi mita za mraba 111,243,000 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Uzalishaji wa chuma uliongezeka kutoka tani 33,384 mwaka 2010 hadi kufikia tani 34,881 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Aidha, uzalishaji wa kamba za katani uliongezeka kutoka tani 6,872 mwaka 2010 hadi tani 7,091 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asailimia 3.2. Aidha, uzalishaji wa bidhaa nyingine kwa mwaka 2011 ulikuwa: mahindi tani 15,068; sukari tani 201,766; sabuni tani 158,956; na vinywaji baridi lita 497,189,000.

Biashara ya Ndani

300. Shughuli za kiuchumi za biashara zinajumuisha uuzaji wa jumla, reja reja na matengenezo. Mwaka 2011, kasi ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi za biashara na matengenezo ilipungua kidogo na kuwa asilimia 8.1 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2010. Aidha, mchango wa shughuli za biashara na matengenezo katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 12.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2010.

Maonesho ya Biashara ya Kimataifa

301. Mwaka 2011 nchi zilizoshiriki katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere zilikuwa 17 idadi hii ni sawa na ya mwaka 2010. Aidha, makampuni ya nje yaliyoshiriki yalikuwa 141, ikilinganishwa na makampuni ya nje 350 mwaka 2010, sawa na upungufu wa makampuni ya nje 209. Upungufu huu ulitokana na athari za kudorora kwa uchumi wa dunia na kuzuka kwa migogoro ya kisiasa katika nchi za Kiarabu.

302. Mwaka 2011, washiriki wa ndani walikuwa 1041 ukilinganisha na washiriki 2150 mwaka 2010, hii ni sawa na upungufu wa washiriki wa ndani 759. Upungufu huu ulitokana na nchi au makampuni kuchukua maeneo makubwa na kufanya washiriki wengine kukosa nafasi. Hata hivyo idadi ya watu waliotembelea maonesho ya mwaka 2011 iliongezeka kutoka watu 761,601 mwaka 2010 hadi 819,273, sawa na ongezeko la asilimia 7.6. Aidha, katika mwaka 2011, Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere yalifikia viwango vya juu vya ubora kimataifa kwa kutunukiwa cheti safi kutoka Shirikisho la Maonesho ya Biashara Duniani (UFI).

303. Mwaka 2011, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ilihamasisha wajasiriamali kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam na Maonesho ya Kisekta. Aidha, Wizara iliwahamasisha na kuwawezesha wajasiriamali kushiriki maonyesho mbalimbali ya kimataifa kama vile Maonesho ya Biashara ya Nairobi (Nairobi International Trade Fair); African Commodity Exhibition (ACE) Yiwu, China; Maonesho ya Kimataifa ya Msumbiji; Maonesho ya Kimataifa ya Malawi; na Maonesho ya EXPO 2010 yaliyofanyika Shanghai, China.

MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 58

Mwaka	Kutoka Nje	Uuzaji nje	Utengenezaji	Tani	
				Tani	Badiliko%
1980	30555	11110	305811	325256	-4%
1981	49325	7751	389953	431527	33%
1982	27541	16010	333531	345062	-20%
1983	42428	20639	246919	268708	-22%
1984	16895	18974	368644	366565	36%
1985	111341	16424	375957	470874	28%
1986	42028	6558	434898	470368	0%
1987	1383	11146	498261	488498	4%
1988	9076	65765	590927	534238	9%
1989	2145	29035	594791	567901	6%
1990	2544	131469	663900	534975	-6%
1991	2800	67766	1022580	957614	79%
1992	3080	63065	677388	617403	-36%
1993	3600	102282	748850	650168	5%
1994	3160	53706	686200	617272	-5%
1995	4000	72092	739156	671064	9%
1996	1309	104811	725755	622253	-7%
1997	2804	100165	621159	523798	-16%
1998	14388	50718	777620	741290	42%
1999	11418	29097	832602	814923	10%
2000	7281	30497	833092	809882	-1%
2001	56395	53517	900430	903308	12%
2002	149079	37203	1026082	1137958	26%
2003	166446	34396	1186434	1318484	16%
2004	125007	37655	1280851	1368203	4%
2005	120200	40430	1375222	1454992	6%
2006	92711	98	1421460	1514073	4%
2007	101827	52170	1629890	1679547	11%
2008	356468	99688	1755862	2012642	20%
2009	516182	57569	1940845	2399458	19%
2010	566828	189321	2312055	2689562	12%
2011*	768343	217944	2408765	2959164.02	10%

Chanzo: Ofisi ya Taifa Takwimu

* Za Awali (Provisional)

UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na.59

Aina ya Bidhaa	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	Badiliko(%) 2010-2011
Biskuti & tambi	Tani	2284	5906	10214	10912	10565	11273	15435	15200	7435	12053	62.1%
Unga wa ngano	Tani	219118	355616	338076	368019	434160	406336	287925	368885	444242	439926	-1.0%
Konyagi	000 Lita	2937	3670	4105	4489	5365	5622	4049	10201	11186	15432	38.0%
Bia	000 Lita	175870	194100	202628	216604	299036	310194	291178	284906	242689	323393	33.3%
Chibuku	000 Lita	19400	14825	10119	11106	11559	10320	10235	16141	21037	23474	11.6%
Sigara	Milioni	3778	3920	4219	4445	5095	5821	6101	5831	6181	6630	7.3%
Nguo	000 M^2	106305	116714	111637	99134	146600	139000	140531	91501	103177	101820	-1.3%
Kamba za katani	Tani	5901	6839	5161	5943	5854	7012	7783	7913	6872	6976	1.5%
Nyavu za uvuvi	Tani	30	41	260	274	119	156	-	64	247	164	-33.6%
Mazulia	000 M^2	-	-	-	-	-	-	-	37152	-		
Tabaka za mbao	M^2	304	32609	40248	37941	44310	45147	44547	266	-	30589	
Dawa za pareto	Tani	36	16	23	25	33	33	73	-	49	70	42.9%
Mbolea	Tani	-	-	-	-	-		-	25762	-	-	
Rangi	000 Lita	13564	16842	16621	16222	18402	17451	24857	-	28201	31710	12.4%
Bidhaa za petrol	000 Tani	-	-	-	-	-	-	-	1941	-	-	
Saruji	000 Tani	1026	1186	1281	1366	1422	1630	1756	34793	2313	2409	4.2%
Chuma	Tani	25418	38794	41710	41299	44482	52163	39969	34793	33384	39955	19.7%
Bati	Tani	31742	31018	29573	29737	29898	36492	31743	50664	71276	76912	7.9%
Aluminium	Tani	141	199	171	183	105	110	105	58	59	33	-44.1%
Radio	000 namba	-	-	-	-	-	-	-		-	-	
Betri	Milioni	42	43	74	81	82	75	53	78	93	89	-4.3%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda na Biashara

- Hakuna uzalishaji

VIWANDA- IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 60

ISIC (Rev 3)	Shughuli	Walioajiriwa				Wengine				Jumla			
		2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**
151-4	Vyakula	44564	36668	44365	46584	278	377	305	320	44842	37045	44670	46904
155	Vinywaji	4165	5387	5914	6209	27	63	50	52	4192	5450	5964	6262
160	Tumbaku na Sigara	7061	3815	6883	7227	0	0	0	0	7061	3815	6883	7227
171-2,	Ufumaji na Ushonaji	10325	12631	11988	12588	53	57	236	247	10377	12688	12224	12835
191	Ngozi, bidhaa za ngozi	21	438	648	680	2	2	4	4	23	440	652	684
192	Viatu	1181	216	819	860	6	0	5	5	1187	216	824	865
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	2618	1088	770	809	78	46	24	26	2696	1134	795	834
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji	4420	6265	5577	5856	121	167	92	96	4540	6432	5669	5952
241-2	Utengenezaji wa Kemikali	4960	3725	2944	3091	43	100	30	31	5004	3825	2974	3122
251	Bidhaa za mpira	530	53	1227	1289	1	43	12	13	531	96	1239	1301
252	Bidhaa za Plastiki	2311	4188	4195	4404	18	45	13	14	2328	4233	4208	4418
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	1739	2323	2510	2636	15	52	30	31	1754	2375	2540	2667
271-369	Nyinginezo	7237	18894	20500	21525	242	438	404	424	7480	19332	20904	21949
	Jumla	**91130**	**95691**	**108340**	**113757**	**885**	**1390**	**1205**	**1265**	**92015**	**97081**	**109545**	**115022**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu za awali

** Takwimu za makadirio

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

Maelezo: *1. Shughuli zilizoainishwa hapo juu ni zile zilizochangia angalau asilimia moja (1%) ya ongezeko la dhamani (Value Added) katika utafiti wa mwaka 1999 na 2000*

2. Uchambuzi wa Takwimu umetumia "International Standard Industrial Classification Revision 3 (ISIC Rev3)"

3. Takwimu za 2001 - 2002 zimerekebishwa kutokana na utafiti

4. Takwimu za 2003 - 2004 zimekadiriwa kwa takwimu za mwaka 2001 na 2002

VIWANDA: GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 61 (Sh.milioni)

ISIC (Rev 3)	Shughuli	Mishahara				Malipo Mengine				Jumla			
		2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**
151-4	Vyakula	52689	75131	53748	56435	22890	30482	23350	24517	75579	105613	77098	80953
155	Vinywaji	36275	51012	37004	38854	20637	17551	21052	22104	56912	68563	58056	60958
160	Tumbaku na Sigara	17375	8204	17725	18611	9540	5324	9732	10218	26915	13528	27456	28829
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	10262	10047	10469	10992	3966	2540	4045	4248	14228	12587	14514	15240
191	Ngozi, Bidhaa za ngozi	478	3477	488	512	111	813	113	118	589	4290	601	631
192	Viatu	1032	239	1053	1105	396	197	404	425	1428	436	1457	1530
201- 202	Mbao, Bidhaa za Mbao	760	1995	775	814	218	1119	222	233	978	3114	997	1047
210-221-22	Karatasi, Uchapishaji	17801	15895	18159	19067	5742	9601	5857	6150	23543	25496	24016	25217
241-2	Utengenezaji wa Kemikali	7305	12135	7451	7824	4232	7181	4317	4533	11537	19316	11769	12357
251	Bidhaa za Mpira	5684	304	5798	6088	1418	3668	1446	1518	7102	3972	7244	7607
252	Bidhaa za Plastiki	6272	6020	6398	6718	5242	1536	5347	5614	11513	7556	11745	12332
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	75504	18297	77022	80873	8492	8279	8662	9095	83996	26576	85684	89968
271-369	Nyinginezo	43981	45540	44865	47108	32557	14850	33211	34872	76537	60390	78076	81980
	Jumla	275418	248296	280954	295002	115439	103141	117759	123647	390857	351437	398713	418648

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimerekebishwa

** Makadirio

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

Maelezo: *1. Shughuli zilizoainishwa hapo juu ni zile zilizochangia angalau asilimia moja (1%) ya ongezeko la thamani (Value Added) katika utafiti wa mwaka 1999 na 2000*

2. Uchambuzi wa Takwimu umetumia "International Standard Industrial Classification Revision 3 (ISIC Rev3)"

3. Takwimu za 2001 - 2002 zimerekebishwa kutokana na utafiti

4. Takwimu za 2003 - 2004 zimekadiriwa kwa kutumia takwimu za mwaka 2001 na 2002

VIWANDA MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 62 (Tshs. Millioni)

ISIC (Rev 3)	Shughuli	PATO				GHARAMA				Thamani Iliyoongezeka (Value Added)				Uchakavu wa Mitambo (Depreciation)			
		2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**	2008	2009*	2010**	2011**
151-4	Vyakula	1109701	1509481	1223445	1284618	630456	1015773	695078	729832	479245	493709	528367	554786	30769	78028	33923	35619
155	Vinywaji	842392	862033	928737	975174	536900	362680	591932	621529	305492	499353	336804	353645	40414	36476	44556	46784
160	Tumbaku na Sigara	262120	270390	288987	303436	163175	131493	179901	188896	98945	138897	109086	114541	19731	8577	21753	22841
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	189689	217164	209132	219588	108723	104775	119867	125860	80966	112390	89265	93728	20754	11586	22881	24025
191	Ngozi, bidhaaa za ngozi	8772	18411	9671	10155	5949	14991	6559	6887	2823	3419	3112	3268	277	1780	306	321
192	Viatu	8134	9068	8967	9416	4952	7384	5459	5732	3182	1684	3508	3684	603	877	665	698
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	12077	65272	13315	13981	6175	46069	6808	7148	5902	19203	6507	6833	448	5116	494	519
210-221-22	Karatasi, Uchapishaji	181957	157997	200607	210638	102339	108153	112829	118470	79618	49844	87779	92168	8068	7376	8895	9340
241-2	Utengenezaji wa Kemikali	262743	443673	289674	304158	152480	296794	168109	176515	110263	146879	121565	127643	7191	14158	7928	8325
251	Bidhaa za mpira	149156	16296	164445	172667	77616	7206	85572	89850	71540	9090	78873	82817	2163	730	2385	2504
252	Bidhaa za Plastiki	427974	116192	471841	495433	297107	51383	327561	343939	130866	64809	144280	151494	8944	5203	9860	10353
261-9	Chuma	344234	450190	379518	398494	220977	233025	243628	255809	123257	217165	135891	142685	28597	47743	31528	33105
271-369	Nyinginezo	912429	812180	1005953	1056250	607144	521949	669376	702845	305285	290231	336577	353405	31964	35188	35240	37002
	Jumla	**4711376**	**4948347**	**5194293**	**5454007**	**2913993**	**2901675**	**3212678**	**3373312**	**1797383**	**2046673**	**1981614**	**2080695**	**199924**	**252838**	**220415**	**231436**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimerekebishwa

** Takwimu za makisio

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

Maelezo: *1. Shughuli zilizoainishwa hapo juu ni zile zilizochangia angalau asilimia moja (1%) ya ongezeko la dhamani (Value Added) katika utafiti wa mwaka 1999 na 2000*

2. Uchambuzi wa Takwimu umetumia "International Standard Industrial Classification Revision 3 (ISIC Rev3)"

3. Takwimu za 2001 - 2002 zimerekebiswa kutokana na utafiti

3. Takwimu za 2003 - 2004 zimekadiriwa kwa kutumia takwimu za mwaka 12001 na 2002

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA *

Jedwali Na. 63

Jina la mkoa	Idadi ya Wafanyakazi				Idadi ya Waajiriwa				Mishahara (T. Shs. Millioni)				Thamani iliyoongezeka (Tshs. Milioni)			
	2008	2009*	2010*	2011**	2008	2009*	2010*	2011**	2008	2009*	2010*	2011**	2008	2009*	2010**	2011**
Dodoma	231	168	235	247	-	152	234	246		169	584	613	-	2483	8562	8990
Arusha, Manyara	15296	15312	15603	16384	3295	15230	15495	16270	7076	10446	22329	23445	72285	138690	356830	374671
Kilimanjaro	11548	4467	11780	12369	6964	4454	11699	12284	10408	17150	12308	12924	31858	32629	137290	144154
Tanga	10054	5634	10256	10768	8487	5600	10185	10694	10443	15415	12225	12837	20187	105868	237041	248893
Morogoro	8123	16912	8286	8701	11283	16851	8229	8640	22689	29360	21453	22525	49729	146372	288858	303301
Pwani,	24155	32855	24640	25872	-	32097	24025	25226	-	124439	133234	139895	-	1242636	624421	655641
Dar es Salaam, Pwani***	61	58	62	65	27686	55	61	64	80932	44	79	83	410062	1000	435	457
Lindi	115	262	118	124	26	248	117	123	21	672	1512	1588	34	17212	4139	4346
Mtwara	977	350	997	1047	62	327	990	1040	745	911	534	560	11	45320	7505	7880
Ruvuma	9099	6391	9282	9747	2002	6374	9218	9679	731	16837	16578	17407	1179	56621	32645	34277
Iringa	2884	2426	2942	3089	15363	2381	2922	3068	14749	6994	6322	6638	15028	60718	22191	23300
Mbeya	238	470	243	255	2842	374	241	253	3807	269	533	559	24975	1435	2312	2428
Singida	807	39	823	865	21	35	818	859	3	89	1330	1396	0	175	4447	4669
Tabora	128	296	130	137	224	291	130	136	19148	588	1037	1089	32586	4081	1360	1428
Rukwa	678	157	692	727	82	106	687	722	20	113	1575	1654	123	2928	5324	5590
Kigoma	2195	517	2239	2351	-	512	2223	2334	-	1052	10089	10593	-	3727	19140	20097
Shinyanga	9511	5745	9702	10187	221	5694	9634	10116	2668	14828	9757	10244	30270	68970	32941	34588
Kagera	7181	3421	7326	7692	1794	3354	7275	7639	3628	7434	13729	14415	42160	81636	102088	107192
Mwanza	3445	1224	3515	3690	6979	1197	3490	3665	9302	1310	10053	10555	30805	33759	82384	86503
Mara	659	377	673	706	3800	359	668	701	7535	178	5696	5980	15594	409	11703	12288
Jumla	**107386**	**97081**	**109545**	**115022**	**91130**	**95691**	**108340**	**113757**	**193907**	**248298**	**280954**	**295002**	**776884**	**2044186**	**1981615**	**2080695**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimerekebishwa

** Takwimu za makisio

*** Kuanzia mwaka 2003 takwimu za mkoa wa pwani zimejumuishwa na mkoa wa DSM

Viwanda rasmi vyenye wafanyakazi 10 na zaidi

VIGEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA

Jedwali Na. 65

Mwaka	Mchango katika Pato la Taifa % (Bei za 2001)	Ukuaji wa Sekta (Bei za 2001)	Mchango katika Mauzo nje %	Mchango katika Mauzo nje yasiyo Asilia (%)	Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda (%)
1998	8.37	5.5	6.10	15.40	-
1999	8.47	6.0	5.50	12.40	-15.7%
2000	8.46	4.8	6.50	11.71	44.2%
2001	8.38	5.0	7.23	9.05	29.4%
2002	8.40	7.5	7.40	8.52	17.3%
2003	8.57	9.0	6.79	8.42	27.2%
2004	8.69	9.4	8.28	9.37	31.4%
2005	8.87	9.6	9.31	11.81	41.8%
2006	9.02	8.5	11.24	13.81	25.4%
2007	9.15	8.7	15.28	18.14	57.9%
2008	9.36	9.9	23.84	28.48	139.9%
2009	9.54	8.0	17.74	21.32	-31.7%
2010	9.61	7.9	25.64	30.25	90.3%
2011	9.74	7.8	19.43	22.88	-10.6%

Chanzo: Wizara ya Fedha

SURA YA 15

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

UJENZI

Kiwango cha Ukuaji

304. Mwaka 2011, shughuli za ujenzi zilikua kwa asilimia 9.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 10.2 mwaka 2010. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana hasa na kupungua kwa shughuli za ujenzi wa barabara na madaraja na shughuli za usafiri endelezaji wa ardhi. Aidha, mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.0 kama ilivyokua mwaka 2010.

Mtandao wa Barabara

305. Tanzania ina mtandao wa barabara wenye urefu wa jumla ya kilometa 86,472. Kati ya hizo, kilometa 12,786 ni barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, zikijumuisha kilometa 5,478 sawa na asilimia 43 zilizo katika kiwango cha lami. Kilometa 21,105 ni barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu, kati ya hizo kilometa 840 sawa na asilimia nne ni za kiwango cha lami. Aidha, kilometa 52,581 ni barabara za wilaya zinazounganisha wilaya na vijiji pamoja na barabara viunganishi.

306. Mwaka 2011, jumla ya kilomita 29,369 zilifanyiwa tathmini. Kati ya hizo, kilometa 5,727 sawa na asilimia 59.1 za barabara kuu zilikuwa katika hali nzuri, ikilinganishwa na kilometa 8,364.73 sawa na asilimia 65 mwaka 2010. Hii ina maana kuwa ubora wa barabara umepungua kwa asilimia 5.9 mwaka 2011. Kilometa 3,096 sawa na asilimia 32 za barabara kuu zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 3,578.53 sawa na asilimia 28 mwaka 2010. Aidha, kilometa 862, sawa na asilimia 9 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 842.93 sawa na asilimia 7 mwaka 2010.

307. Katika mwaka 2011, jumla ya kilometa 5,976, sawa na asilimia 30.4 za barabara za mikoa zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 11,012 mwaka 2010 ambazo ni sawa na asilimia 53.3. Kilometa 10,284 sawa na asilimia 52.2 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 7,069.02 mwaka 2010, sawa na asilimia 34.2. Aidha, kilometa 3,424 sawa na asilimia 17.4 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 2,592 mwaka 2010 sawa na asilimia 12.5. Hali ya mtandao wa barabara kwa ujumla hadi kufikia

mwishoni mwa Desemba 2011 ni kama inavyoonekana katika jedwali Na. 15.1 hapa chini.

Jedwali Na.15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Hadi Kufikia Desemba, 2011.

Aina ya Barabara	Uzuri km (%)	Hali ya wastani (%)	Hali Mbaya (%)	Jumla
Barabara Kuu				
Lami	4,611 (83%)	624 (11%)	311 (6%)	5,546 (100%)
Zisizo na Lami	1,116 (27%)	2,472 (60%)	551 (13%)	4,139 (100%)
Jumla ndogo	**5,727**	**3,096**	**862**	**9,685**
Barabara za Mikoa				
Lami	468(58%)	199 (25%)	146 (18%)	813(101%)
Zisizo na Lami	5,508 (29%)	10,085 (53%)	3,278 (17%)	18,871 (99%)
Jumla Ndogo	**5,976**	**10,284**	**3,424**	**19,684**
Jum la Kuu	**11,703**	**13,380**	**4286**	**29,369**

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

Matengenezo ya Barabara na Madaraja

308. Mwaka 2011, Wizara kupitia Wakala wa Barabara ilizifanyia matengenezo Barabara za Mikoa, Barabara Kuu zenye urefu wa kilometa 28,647 na madaraja 2,480. Kiasi cha shilingi bilioni 119.331, sawa na asilimia 67 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matengenezo kilitumika.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

309. Mwaka 2011, Mfuko wa Barabara ulikusanya mapato ya shilingi 401.935 bilioni ikilinganishwa na shilingi 278.231 bilioni zilizokusanywa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 44.5. Ongezeko hilo lilitokana na udhibiti wa mianya ya uchakachuaji wa mafuta ambao husababisha kupungua kwa mapato ya makuasanyo ya ushuru wa mafuta (Fuel Levy). Aidha, Bodi iliongeza ufuatiliaji wa matumizi ya Mfuko kwa kufanya Ukaguzi wa Kiutaalam (Technical Audit) na Ukaguzi wa Kifedha (Financial Audit) kwenye miradi ya barabara ili kubaini thamani halisi ya matumizi ya fedha za mfuko. Katika kuhakikisha kuwa thamani ya fedha katika miradi ya barabara inapatikana Bodi ilianzisha utaratibu wa kuwatumia Wahandisi Washauri (Local Consultants) kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa kiufundi na ubora wa kazi (Value for Money) wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

310. Mwaka 2011, Bodi ya Usajili wa Makandarasi iliendelea kusajili wakandarasi kwa viwango vinavyokidhi mahitaji na kuzingatia usalama wa umma. Aidha, Bodi iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2010 – 2014) ikilenga zaidi katika kuongeza ufanisi katika maeneo manne muhimu ambayo ni: Maadili katika sekta ya ujenzi hususan katika biashara ya ukandarasi; Uwezo na umahiri wa wakandarasi; Usalama kwa watendaji kazi katika sehemu za kazi na umma kwa ujumla; na ufanisi wa Bodi.

311. Mwaka 2011, Bodi ilisajili makandarasi wapya 863 ikilinganishwa na makandarasi 860 mwaka 2010. Aidha, mwaka 2011 Bodi ilifanya ukaguzi katika miradi 2,760 ya ujenzi ikilinganishwa na miradi ya ujenzi 2,112 iliyofanyiwa ukaguzi mwaka 2010. Kati ya miradi iliyokaguliwa mwaka 2011, miradi 1,912 ilikuwa haina kasoro na miradi 848 ilikuwa na kasoro zikiwemo za kutozingatia suala la afya na usalama kazini. Makandarasi katika miradi yenye upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

312. Mwaka 2011, Bodi ya Usajili wa Makandarasi iliendesha mafunzo ya makandarasi katika mikoa ya Shinyanga, Rukwa, Dar es Salaam na Mtwara ambapo washiriki 287 walihudhuria. Aidha, Bodi ilifanya mikutano ya mashauriano na wadau kwa kushirikiana na Bodi ya Wahandisi na Bodi ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ambayo ilifanyika Jijini Dar es salaam. Vile vile, Bodi ilifanya maonesho ya teknolojia, vifaa na huduma za ujenzi yaliyofanyika Jijini Dar es salaam na kuhudhuriwa na washiriki 2,500 ikilinganishwa na washiriki 1,231 waliohudhuria katika maonesho kama hayo mwaka 2010. Kati ya hao, makandarasi walikuwa zaidi ya 900. Aidha, Mwaka 2011 Serikali ilianza maandalizi ya mkakati maalumu wa kuendeleza makandarasi wazalendo ili wawe na uwezo wa kutekeleza kazi kubwa za miundombinu.

Bodi ya Usajili ya Wahandisi

313. Mwaka 2011, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 1,017 wa kada mbalimbali pamoja na kampuni za ushauri 41 ikilinganishwa na wahandisi 582 na makampuni 14 mwaka 2010. Aidha, Bodi inaendeleza uanzishwaji wa kampuni nyingi za ushauri wa kihandisi mikoani. Kwa ujumla Bodi ilifanya vizuri katika suala la usajili.

Jedwali Na: 15.2 Usajili wa Wahandisi katika mwaka 2009 – 2011

Aina za usajili	Usajili 2009	Usajili 2010	Usajili 2011	Badiliko (%)
Wahandisi Wasaidizi Wahitimu	25	23	20	-13.0
Wahandisi Wasaidizi	13	5	4	-20.0
Wahandisi Wahitimu	525	411	594	44.5
Wahandisi Wataalamu	165	67	173	158.2
Wahandisi Wataalamu	91	65	190	192.3
Wahandisi Washauri	17	9	24	166.7
Wahandisi Washauri (Wageni)	9	2	12	500
Makampuni ya Ushauri ya Kizalendo	9	6	14	133.3
Makampuni ya Ushauri ya Kigeni	8	8	27	237.5
JUMLA	**862**	**596**	**1,058**	**77.5**

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

314. Mwaka 2011, Bodi ilisimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu 899. Takwimu za Wahandisi Wahitimu waliojiunga na Mpango wa Mafunzo kwa vitendo kwa mwaka 2002/2003 - 2010/11 zimeoneshwa katika jedwali Na. 15.3.

Jedwali Na. 15.3: Takwimu za Wahandisi wahitimu waliojiunga na Mpango wa Mafunzo kwa vitendo 2002/2003 – 2010/2011

Mwaka wa Fedha	Idadi ya waliojiunga	Wanaoghar imiwa na Serikali	Wanaogharimi wa na waajiri wao	Waliomaliza Mafunzo	Walioajiriw a kabla ya kumaliza	Walioa-hirisha
2002/03	120	110	10	-	60	8
2003/04	169	162	7	20	95	9
2004/05	212	195	17	10	120	15
2005/06	167	137	30	121	81	12
2006/07	218	113	105	78	85	20
2007/08	159	128	31	136	34	12
2008/09	265	156	109	140	79	41
2009/10	263	104	159	176	60	12
2010/11	224	44	180	218	70	15
Jumla	**1797**	**1149**	**648**	**899**	**684**	**144**

Chanzo: Wizara ya Ujenzi

Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

315. Mwaka 2011, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili jumla ya wabunifu majengo 17 na wakadiriaji majenzi 14 ikilinganishwa na wabunifu majengo 20 na wakadiriaji majenzi 13 waliosajiliwa mwaka 2010. Usajili huu ni ongezeko la wataalaam 31 ambao unafanya jumla ya wataalamu waliosajiliwa na Bodi kufikia 520. Aidha, makampuni 13 ya wabunifu majengo na makampuni 7 ya ukadiriaji majenzi yalisajiliwa na Bodi mwaka 2011

ikilinganishwa na makampuni 13 ya wabunifu majengo na makampuni 8 ya ukadiriaji majenzi yaliyosajiliwa mwaka 2010. Hili ni ongezeko la makampuni 20 ambalo linafanya jumla ya makampuni yaliyosajiliwa kufikia 259.

316. Mwaka 2011, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili wataalaamu wa fani hizi wenye sifa za kati 39 ikilinganishwa wataalamu 8 waliosajiliwa mwaka 2010. Ongezeko hili linafanya jumla ya wataalamu wa sifa za kati waliosajiliwa na Bodi hadi kufikia mwaka 2011 kuwa 105. Ongezeko kubwa la usajili ni matokeo ya juhudi za Serikali za kuhamasisha wahitimu wenye sifa zilizoainishwa kuzingatia matakwa ya sheria Na.4 ya mwaka 2010 inayowataka kujitokeza na kusajiliwa na Bodi. Aidha, utekelezaji wa mpango unaogharamiwa na Serikali wa Mafunzo kwa Vitendo ("Enhanced Articled Pupilage Programme"- EAPP) kwa wahitimu wa fani hizi mbili ulipelekea kuongezeka kwa wahitimu wenye sifa ambao walisajiliwa na Bodi.

317. Katika mwaka 2011, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilifuta Usajili wa Mbunifu Majengo mmoja, Mkadiriaji Majenzi mmoja na kampuni moja ya Ubunifu Majengo wote wakiwa wa nje kwa sababu miradi waliyosajiliwa nayo ilikuwa imekamilika. Aidha, Ukaguzi wa majenzi ulifanyika katika mikoa 19 ya Tanzania Bara. Katika zoezi hilo, miradi ya majenzi 1,196 ilikaguliwa ikilinganishwa na miradi 1,296 iliyokaguliwa mwaka 2010.

Baraza la Taifa la Ujenzi

318. Mwaka 2011, Baraza la Ujenzi la Taifa liliendesha mafunzo kwa wadau 250 wa sekta kuhusu shughuli za zabuni; menejimenti ya mikataba na madai ya gharama za ujenzi wa barabara; shughuli za matengenezo na ukarabati wa Majengo; na usuluhidhi wa migogoro. Aidha, ukaguzi wa kiufundi (Technical Audit) wa miradi ya ujenzi ulifanyika katika miradi 100 ya Halmashauri za Wilaya 20 yenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 5.5. Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi huo ni pamoja na kutotumia ipasavyo mikataba ya miradi katika utekelezaji wake, Kukiuka sheria ya manunuzi ya umma Na. 21 ya mwaka 2004 na usimamizi duni wa miradi.

Wakala wa Majengo Tanzania

319. Mwaka 2011, Wakala wa Majengo uliendelea kusimamia miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za viongozi ambazo ni nyumba za Waheshimiwa Majaji katika Mikoa ya Ruvuma, Dar es salaam, Tanga, Arusha,

Tabora, Mwanza, Mbeya na Dodoma. Vilevile, Wakala uliendelea na ujenzi wa nyumba za wakuu wa wilaya katika wilaya za Bariadi, Urambo na Siha, pamoja na ujenzi wa nyumba za viongozi wengine wa Serikali katika wilaya ya Kasulu, na mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Mtwara na Iringa. Aidha, Wakala ulisimamia miradi 94 ya ushauri katika mikoa mbalimbali ambapo kiasi cha shilingi 917,148,903.0 kilipatikana. Hata hivyo, kasi ya ujenzi wa nyumba kwa ajili ya watumishi wa Serikali haikuwa ya kuridhisha kutokana na gharama kubwa za viwanja, kukosekana kwa miundombinu katika viwanja hivyo na kupanda kwa gharama za ujenzi.

Wakala wa Ufundi na Umeme

320. Mwaka 2011, Wakala wa Ufundi na Umeme uliyafanyia matengenezo magari 5,137 sawa na asilimia 58 ya lengo la magari 8,822 kwa mwaka. Kutokufikiwa kwa lengo kulitokana na kupanda kwa bei za vipuli na mitambo. Aidha, katika mwaka 2011, Wakala ulitekeleza miradi 126 ya umeme, miradi minne ya elektroniki, miradi 26 ya mabarafu na viyoyozi, na miradi 37 ya ushauri.

MAENDELEO YA ARDHI

Upimaji wa Mipaka ya Vijiji

321. Mwaka 2011, jumla ya mipaka ya vijiji 261 ilipimwa ikilinganishwa na mipaka 1,207 iliyopimwa mwaka 2010. Upungufu huu katika upimaji ulitokana na kukamilika kwa kazi ya upimaji wa vijiji 11,000 vilivyokuwa vimeandikishwa hadi mwaka 2010. Hivyo, mipaka ya vijiji vilivyopimwa mwaka 2011 ilitokana na vijiji kugawanywa zaidi ya kimoja na kufanya idadi ya vijiji vilivyopimwa kufikia 11,261.

Jedwali Na15.4: Idadi ya Vijiji Vilivyopimwa

Mwaka 2010		Mwaka 2011	
Wilaya	**Idadi ya Vijiji**	**Wilaya**	**Idadi ya Vijiji**
Singida Vijijini	35	Bariadi	99
Bahi/Chamwino	54	Meatu	29
Tarime	39	Maswa	52
Rorya	63	Kishapu	46
Sengerema	23	Korogwe	35
Muleba	98	-	-
Misenyi	73	-	-
Karagwe	45	-	-
Ngara	68	-	-
Kigoma Vijijini	21		-
Kahama	221	-	-
Bariadi	22	-	-
Tabora Vijijini	127	-	-
Babati	5	-	
Kilosa/Mahenge	87	-	-
Shinyanga Vijijini/Kishapu	226	-	-
Jumla	**1,207**	**-**	**261**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Ukaguzi na Uhakiki wa Miliki

322. Mwaka 2011, jumla ya milki 3,535 zilihakikiwa ikilinganishwa na milki 4,317 zilizohakikiwa mwaka 2010. Katika uhakiki huo, migogoro 58 ilijitokeza ambapo migogoro 46 (asilimia 79) ilitatuliwa kiutawala na migogoro 12 haikuweza kutatuliwa, na wahusika walishauriwa kwenda mahakamani. Vile vile, jumla ya milki 950 zilihamishwa kwa kufuata taratibu za kisheria.

Utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji na Hati za Hakimiliki za Kimila

323. Mwaka 2011, kati ya vijiji vilivyopimwa mipaka yake, vyeti vya ardhi ya kijiji 3,283 vilitolewa ikilinganishwa na vyeti 3,265 vilivyotolewa mwaka 2010, na kufanya vyeti vilivyokwishasajiliwa kufikia 7,510. Vile vile, hati za hakimiliki ya kimila 46,063 zilitolewa ikilinganishwa na hati za hakimiliki ya kimila 93,400 mwaka 2010, na kufanya jumla ya hati za hakimiliki ya kimila zilizokwishatolewa nchini kote kufikia 157,968. Idadi ya hati za hakimiliki za kimila ilipungua kutokana na kazi kubwa kufanyika mwaka 2010 kwenye maeneo ya miradi ya majaribio. Aidha, ofisi za masjala za ardhi za vijiji 23 zilianzishwa na kufanya jumla ya masjala hizo nchini ifikie 408 mwaka 2011.

Jedwali Na. 15.5: Jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Hati za Hakimiliki ya Kimila Vilivyotolewa mwaka 2005 - 2011

Mkoa	Vyeti	Hati za Kimila
Pwani	269	4,654
Morogoro	248	803
Dodoma	295	694
Singida	368	6,428
Mtwara	577	307
Lindi	358	1362
Kagera	386	104
Shinyanga	862	62,668
Tabora	225	0
Mwanza	557	134
Mara	268	4072
Kigoma	190	0
Kilimanjaro	237	2714
Arusha	161	156
Tanga	361	2,057
Manyara	247	28,526
Mbeya	727	21,467
Iringa	651	14,265
Rukwa	261	984
Ruvuma	262	6,297
Jumla	7,510	157,692

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Utoaji wa Hati Miliki

324. Mwaka 2011, Serikali ilisajili jumla ya hatimiliki 26,880 ikilinganishwa na hatimiliki 21,170 zilizosajiliwa mwaka 2010. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya nyaraka 28,572 zilisajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi (Sura ya 334); nyaraka 7,449 chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka (Sura ya 117) na nyaraka 600 chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya Mali Zinazohamishika (Sura ya 210).

Jedwali Na. 15.6: Utoaji wa Hati Miliki katika mwaka 2010 na 2011

Ofisi za Kanda	Hati Miliki 2010	Hati Miliki 2011
Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam)	15,561	7,948
Kanda ya Ziwa (Mwanza)	1,961	6,300
Kanda ya Kusini Magharibi (Mbeya)	1,223	4,544
Kanda ya Kaskazini (Moshi)	1,400	5,400
Kanda ya Kati (Dodoma)	600	1,551
Kanda ya Kusini (Mtwara)	425	1,137
Jumla	**21,170**	**26,880**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Upimaji wa Ardhi ya Baharini

325. Mwaka 2011, alama za rejea za vipimo vya baharini kwenye maeneo ya mwambao wa Tanzania zilihakikiwa. Kukamilika kwa uhakiki huo kutasaidia kupima kwa usahihi maeneo ya bahari ya nchi yetu ambayo inahusisha maji ya kina kifupi na kirefu pamoja na eneo la Ukanda wa Kiuchumi Baharini.

Upimaji wa Mashamba na Viwanja

326. Mwaka 2011, upimaji wa viwanja 26,788 na mashamba 706 ulifanyika ikilinganishwa na upimaji wa viwanja 37,820 na mashamba 609 mwaka 2010, kama inavyoonekana katika jedwali Na. 15.7.

Jedwali Na. 15.7: Upimaji wa Viwanja na Mashamba kwa mwaka 2010 – 2011

	Milki zilizoidhinishwa 2010		Milki zilizoidhinishwa 2011	
Mikoa	**Viwanja**	**Mashamba**	**Viwanja**	**Mashamba**
Arusha	1,727	85	1,294	144
Pwani	2,826	226	1,714	134
Dar es salaam	8,228	5	2,425	0
Dodoma	414	1	345	13
Iringa	3,192	10	2,102	31
Kagera	1,220	46	236	108
Kigoma	51	2	448	0
K/njaro	2,808	36	1,043	95
Lindi	568	0	185	19
Manyara	1,115	15	1,075	2
Mara	370	6	818	22
Mbeya	1,098	51	1,361	40
Morogoro	414	53	1,988	20
Mtwara	974	1	1,612	2
Mwanza	6,076	20	5,060	20
Rukwa	262	6	280	6
Ruvuma	655	12	549	1
Shinyanga	1,801	10	1052	6
Singida	562	1	848	0
Tabora	1,678	15	624	23
Tanga	1,781	8	1,729	20
	37,820	**609**	**26,788**	**706**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

327. Mwaka 2011, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaliendelea kushughulikia migogoro 13,203 ya ardhi na nyumba iliyokuwepo mwaka 2010 na migogoro mingine 12,643 iliyopokelewa mwaka 2011. Aidha, mwaka 2011 mashauri 10,092 yaliamuliwa, na mashauri 15,754 yanaendelea kusikilizwa.

Jedwali Na.15.8: Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba

Baraza	Mashauri yaliyokuwepo hadi Juni, 2010	Mashauri yaliyofunguliwa kuanzia Julai, 2010 hadi Juni, 2011	Mashauri yaliyoamuliwa kuanzia Julai, 2010 hadi Juni, 2011	Mashauri yanayoendelea Juni, 2011
Arusha	791	454	351	894
Babati	401	411	347	465
Bukoba	855	880	805	930
Dodoma	343	432	301	474
Ilala	849	489	300	1,038
Iringa	380	217	173	424
Kigoma	285	271	262	294
Kinondoni	1,075	610	451	1,234
Lindi	48	95	70	73
Mbeya	616	484	336	764
Morogoro	634	523	306	851
Moshi	387	371	376	382
Mtwara	27	111	97	41
Musoma	361	534	539	356
Mwanza	1,538	635	375	1,798
Pwani	265	359	289	335
Rukwa	150	203	236	117
Shinyanga	306	265	400	171
Singida	128	263	220	171
Songea	64	172	84	152
Tabora	216	180	154	242
Tanga	370	214	217	367
Temeke	641	1,572	1,039	1,174
Chato	706	128	90	744
Geita	406	216	210	412
Ifakara	204	421	340	285
Karatu	54	48	40	62
Mbinga	22	163	151	34
Njombe	131	101	113	119
Rungwe	191	274	279	186
Same	24	60	42	42
Tarime	458	390	250	598
Simanjiro	72	130	106	96
Kondoa	24	176	175	25
Korogwe	83	350	271	162
Mkuranga	60	91	79	72
Maswa	38	205	110	133
Ukerewe	0	93	91	2
Iramba	0	52	17	35
JUMLA	**13,203**	**12,643**	**10,092**	**15,754**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mipango ya Matumizi ya Ardhi

328. Mwaka 2011, Serikali ilitayarisha mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 158 ikilinganishwa na vijiji 128 mwaka 2010. Mipango hiyo ilitayarishwa katika Halmashauri za Kilosa, Kasulu, Songea, Nanyumbu, Mbarali, Mbozi, Ileje, Kisarawe, Mafia, Muleba, Njombe, Mufindi, Kilolo, Arusha, Kilindi, Handeni, Tanga, Kondoa, Babati, Rufiji, Kilwa, Bariadi na Maswa**.** Mipango hiyo iliandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watumiaji wa ardhi kuwa na mipango endelevu inayozingatia mahitaji ya sasa na baadaye. Hivyo, katika utayarishaji wa mipango hiyo ambayo ilikuwa shirikishi, maeneo kwa ajili ya huduma za jamii pamoja na hifadhi za vyanzo vya maji, misitu, ufugaji, wanyamapori, kilimo cha umwagiliaji na mashamba makubwa yalitengwa.

MAENDELEO YA MAKAZI NA VIJIJI

Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo

329. Mwaka 2011, Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba na Majengo uliendelea kufanya utafiti na kubuni mbinu za kujenga nyumba kwa gharama nafuu kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini. Vile vile, Wakala waliendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vikundi vya ujenzi vilivyoanzishwa katika vijiji, kata na Wilaya.

Hazina ya Ardhi

330. Mwaka 2011, jumla ya maeneo 106 yameainishwa katika Halmashauri 11 kwa ajili ya uwekezaji. Halmashauri hizo pamoja na vijiji vilivyokaguliwa ni: Tanga, vijiji nane; Kisarawe, vijiji 15; Kilwa vijiji 16; Lindi, vijiji 10; Mkinga, vijiji 10; Rufiji, vijiji 13; Muheza, vijiji 3; Morogoro, vijiji 9; Chunya, vijiji 6; Kilombero, vijiji 10; na Iringa, vijiji 6. Zoezi hili ni mwanzo wa uanzishwaji wa Hazina ya Ardhi ambayo itaondoa migogoro ya ardhi nchini kati ya wawekezaji na wananchi.

Maendeleo ya Nyumba

331. Kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya mwaka 2008 ya Mikopo ya Nyumba, mwaka 2011 Serikali ilianzisha kampuni ya kutoa mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi/ununuzi wa nyumba (Tanzania Mortgage Refinancing Company -TMRC). Kampuni hiyo inatoa mikopo kwa benki za biashara ili ziwakopeshe wananchi kwa riba nafuu tofauti na ilivyo sasa. Hadi Aprili 2012, Benki zilizonunua hisa kutoka TMRC ni Benki ya Rasilimali Tanzania, Azania Bancorp, Exim Bank, National Microfinance Bank, CRDB

Bank na Dar es Salaam Community Bank. Tayari benki hizo zimeanza kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

332. Mwaka 2011, Serikali kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilisaini mkataba na benki saba zilizoonesha utayari wa kutoa mikopo kwa ajili ya kununua na kujenga nyumba zinazojengwa na Shirika. Benki zilizosaini mkataba na Shirika ni Benki za: NMB, NBC, Kenya Commercial Bank (Tanzania) Limited, Exim Bank (Tanzania) Limited, Commercial Bank of Africa (Tanzania) Limited, Bank of Africa - BOA Tanzania) Limited na Azania Bank (Tanzania) Limited.

333. Katika mwaka 2011, Shirika la Nyumba la Taifa lilikamilisha miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi 86 kwa ajili ya kuuza. Miradi hii ni pamoja na Mbweni JKT – Dar es Salaam (Nyumba 34|); Kibla – Arusha (Nyumba 48); na Kiwanya 55 Haile Selasie – Arusha (Nyumba 4). Aidha, Shirika lilianza utekelezaji miradi yenye jumla ya nyumba 278 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Miradi hii pamoja na gharama na mapato imeoneshwa kaika jedwali Na. 15.9.

334. Katika mwaka 2010, kulikuwa na miradi 75 ya majengo makubwa ya ghorofa yenye huduma za maduka, nyumba za makazi na ofisi ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya miradi hiyo, miradi 15 ilikamilika mwaka 2011 na miradi 66 inaendelea na utekelezaji.

Jedwali Na.15.9: Miradi ya Ujenzi wa Nyumba za Kuuza katika mwaka 2011

Miradi	Mwaka 2010	Mwaka 2011	Gharama (sh. miln.)		Mapato (Sh. miln.)	
	Idadi ya nyumba	Idadi ya nyumba	Makadirio	Zilizotumika	Matarajio	Makusanyo
Medeli, Dodoma	0	150	14,710.1	3,433.60	20,338.40	233.7
55 Haile Selasie, Arusha	4	0	350.0	0	1,762.0	1,762.0
Ubungo, Dar es Salaam	0	80	5,478.3	670	6,414.2	2,442.9
Kibla, Arusha	48	0	200.0	183.9	9,929.8	3,132.6
Mbweni JKT, Dar es Salaam	34	0	210.0	202.5	15,067.1	596.7
Mchikichini, Dar es Salaam	0	48	4,847.7	3.60	9,529.1	323.1
Jumla	**86**	**278**	**25,796.1**	**4,493.6**	**63,040.6**	**8,491**

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

SURA YA 16

MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Kiwango cha Ukuaji

335. Mwaka 2011, shughuli za kiuchumi za uchukuzi zilikua kwa asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2010. Kwa upande mwingine, shughuli za kiuchumi za mawasiliano zilikua kwa asilimia 19.0 ikilinganishwa na asilimia 22.1 mwaka 2010. Kiwango kidogo cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za uchukuzi kilitokana na kupungua kwa shehena iliyohudumiwa katika bandari za Tanga, Mtwara, Mwanza na Kigoma. Aidha, kupungua kwa kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za mawasiliano kulitokana na kupungua kwa kasi ya uwekezaji katika sekta ya mawasiliano. Shughuli za kiuchumi za uchukuzi zilichangia asilimia 8.0 katika Pato la Taifa mwaka 2011 sawa na ilivyokuwa mwaka 2010 wakati ambapo mchango wa shughuli za kiuchumi za mawasiliano uliongezeka na kuwa asilimia 2.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2010.

UCHUKUZI

Usafiri wa Barabara

336. Mwaka 2011, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi kavu na Majini (SUMATRA) ilitoa leseni 33,020 na ratiba 3,923 za mabasi ya abiria ikilinganishwa na leseni 31,606 na ratiba 3,420 zilizotolewa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 4.5 na 14.7 kwa mtiririko huo. Aidha, jumla ya leseni za magari ya mizigo 49,057 zilitolewa ikilinganishwa na leseni 43,363 zilizotolewa mwaka 2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 13.1. Ongezeko hili lilitokana na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka za kusogeza huduma za leseni karibu na wasafirishaji pamoja na kuongezeka kwa vyombo vya usafiri.

Usafiri wa Abiria mijini

337. Mwaka 2011, idadi ya mabasi mijini iliongezeka kwa asilimia 13.1 hadi mabasi 33,020 ikilinganishwa na mabasi 31,606 mwaka 2010. Miji ya mikoa iliyokuwa na mabasi mengi ni pamoja na Dar es salaam, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na Mbeya. Kwa upande mwingine, hadi Julai 2011, Jiji la Dar es salaam lilikuwa na mabasi madogo 1,568 ikilinganishwa na mabasi madogo 1,747 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 10.3. Kupungua kwa mabasi madogo katika Jiji la Dar es salaam kulitokana na hatua zilizochukuliwa na

SUMATRA za kutotoa leseni mpya kwa mabasi madogo ili kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji. Aidha, katika kipindi hicho mabasi makubwa yaliongezeka hadi mabasi 4,574 kutoka mabasi 4,182 Julai 2010, sawa na ongezeko la asilimia 9.4.

Jedwali Na.16.1: Idadi ya Mabasi ya Abiria katika Miji na Mikoa

Mkoa	2010		2011		Badiliko (%)	
	Mabasi	Mizigo	Mabasi	Mizigo	Mabasi	Mizigo
Arusha	4,672	4,661	4,878	4,742	4.4	1.7
Dar Es Salaam + Pwani	12,644	21,099	11,469	24,166	-9.3	14.5
Dodoma	1,430	1,265	1,582	1,242	10.6	-1.8
Iringa	626	1,027	803	989	28.3	-3.7
Kagera	519	608	787	737	51.6	21.2
Kigoma	641	190	770	222	20.1	16.8
Kilimanjaro	2,707	2,759	3,160	3,065	16.7	11.1
Lindi	142	106	152	106	7.0	0.0
Manyara	181	178	263	213	45.3	19.7
Mara	378	134	552	250	46.0	86.6
Mbeya	1,433	1,748	1,303	1,938	-9.1	10.9
Morogoro	949	893	1288	1311	35.7	46.8
Mtwara	230	454	323	372	40.4	-18.1
Mwanza	2,380	2,946	2,491	3,326	4.7	12.9
Rukwa	78	409	164	464	110.3	13.4
Ruvuma	338	422	417	408	23.4	-3.3
Shinyanga	253	717	336	1,109	32.8	54.7
Singida	583	644	786	871	34.8	35.2
Tabora	252	351	342	493	35.7	40.5
Tanga	1,170	2,752	770	222	-34.2	-91.9
Jumla	**31,606**	**43,363**	**33,020**	**49,057**	**4.5**	**13.1**

Chanzo: SUMATRA

338. Mwaka 2011, kulikuwa na jumla ya ajali za barabarani 23,986 ikilinganishwa na ajali 24,665 zilizotokea mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 2.8. Jedwali Na.16.2 linaonesha mwenendo wa ajali za barabarani kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2011.

Jedwali Na.16.2: Ajali za Barabarani katika Mwaka 2005 - 2011

	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Idadi ya Ajali	16,388	17,039	17,753	20,615	22,739	24,665	23,986
Ongezeko (%)		4	4	16	10	8.5	-2.8

Chanzo: Polisi Usalama Barabarani

Usafiri kwa Njia ya Reli

339. Mwaka 2011, utendaji katika njia ya reli ya kati na TAZARA uliimarika kutokana na kuboreshwa kwa huduma na kuongezeka kwa shehena za mizigo kwenda na kutoka nchi jirani hususan, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Utendaji huu uliongeza uchukuzi kwa njia ya reli ambapo usafirishaji wa shehena ya mizigo uliongezeka kwa asilimia 2.8 na usafirishaji wa abiria uliongezeka kwa asilimia 31.4 mwaka 2011.

Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

340. Mwaka 2011, Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), ilisafirisha tani 267,008 za mizigo ikilinganishwa na tani 256,190 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asillimia 4.2. Aidha, jumla ya abiria 519,036 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 290,046 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 78.9. Kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kulitokana na kuimarika kwa njia ya reli ikilinganishwa na mwaka 2010 ambapo Kampuni ililazimika kusimamisha huduma kwa zaidi ya miezi mitano kutokana na mvua kubwa kunyesha kuanzia Desemba 2009 na kuendelea. Mvua hiyo ilileta mafuriko makubwa yaliyoharibu kwa kiasi kikubwa miundombinu ya reli kati ya Kilosa na Msagali.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

341. Mwaka 2011, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 533,964 za mizigo ikilinganishwa na tani 522,966 za mizigo zilizosafirishwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Idadi ya abiria waliosafiri mwaka 2011 ilikuwa 858,467 ikilinganishwa na abiria 757,987 waliosafirishwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 13.6. Kuongezeka kwa usafirishaji wa mizigo na abiria

kulitokana na kuongezeka kwa abiria na shehena ya mizigo kwenda na kutoka nchi jirani ya Zambia.

Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Usafiri wa Anga

342. Mwaka 2011, Mamlaka ya usafiri wa anga iliendelea kutekeleza jukumu lake la udhibiti wa usalama wa anga kwa kutoa miongozo na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara. Kutokana na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka katika kipindi hicho, idadi ya matukio na ajali zilizotokea zilipungua hadi kufikia 12 ikilinganishwa na matukio 13 mwaka 2010.

343. Mwaka 2011, idadi ya abiria waliowasili na kuondoka katika viwanja vya ndege ilikuwa 3,437,608 ikilinganishwa na abiria 3,027,512 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 13.5. Kati ya hao, abiria 1,833,460 walikuwa wa safari za kimataifa na abiria 1,604,148 walikuwa wa safari za ndani. Aidha, mizigo iliyosafirishwa nchini iliongezeka kutoka tani 28,861 mwaka 2010 hadi tani 39,601 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 37.2. Ongezeko la abiria na mizigo iliyosafirishwa lilitokana na kuongezeka kwa utalii, shughuli za uwekezaji na biashara nchini na huduma mpya za mashirika ya ndege za kigeni nchini kama Turkish Airlines na Egypt Air.

Kielelezo Na. 16.1: Idadi ya abiria waliowasili na kuondoka nchini mwaka 2005-2011



	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Kimataifa	956,448	1,081,148	1,232,848	1,288,281	1,262,216	1,384,855	1,604,148
Ndani ya nchi	1,216,071	1,388,979	1,548,141	1,622,252	1,492,139	1,642,657	1,833,460
Jumla	2,172,519	2,470,127	2,780,989	2,910,533	2,754,355	3,027,512	3,437,608

Kielelezo Na. 16.2: Shehena ya mizigo iliyosafirishwa mwaka 2005-2011



	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Kimataifa	35,686	29,818	27,284	28,843	24,705	25,837	37,084
Ndani ya nchi	4,551	4,706	4,258	4,029	2,532	3,024	2,517
Jumla	40,237	34,524	31,542	32,872	27,237	28,861	39,601

Usafiri wa Majini

344. Mwaka 2011, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ilifanya kaguzi 598 kwa vyombo vidogo vya usafiri majini na kaguzi 50 kwa vyombo vyenye uzito wa tani 50 na zaidi ikilinganishwa na mwaka 2010 ambapo vyombo vidogo 452 na vyombo 34 vyenye uzito wa tani 50 na zaidi vilikaguliwa katika mwambao wa bahari ya Hindi. Aidha, SUMATRA imekuwa ikifanya kaguzi katika Ziwa Tanganyika, Victoria, Rukwa, Nyasa na kwenye mabwawa. Mwaka 2011, SUMATRA ilifanya kaguzi 3,305 za vyombo vidogo na kaguzi 83 kwa vyombo vyenye uzito tani 50 na zaidi ikilinganishwa na mwaka 2010 ambapo kaguzi 2,782 za vyombo vidogo na kaguzi 114 za vyombo vya tani 50 na zaidi zilifanyika.

345. Mwaka 2011, SUMATRA ilitoa jumla ya vyeti 5,812 kwa mabaharia waliohitimu mafunzo kutoka Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam, ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 9.3 ya vyeti 6,409 vilivyotolewa mwaka 2010. Aidha, mwaka 2011, Mamlaka ilitoa leseni 31 kwa makampuni ya uwakala wa meli ikilinganishwa na leseni 33 zilizotolewa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 6.0.

346. Mwaka 2011, idadi ya ajali za majini ziliripotiwa kuongezeka kwa asilimia 38 hadi kufikia matukio 18 ambapo jumla ya watu 260 walipotea ikilinganishwa na matukio 13 ya ajali yaliyoripotiwa mwaka 2010 ambapo watu 54 walipotea.

Uchukuzi Baharini

347. Mwaka 2011, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena zenye uzito wa tani 11,156,769 ikilinganishwa na tani 10,045,462 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa shehena ya magari, vimiminika hasa mafuta na kichele hasa mbolea na ngano kwa ajili ya Tanzania na nchi jirani. Aidha, katika kipindi hicho, bandari ya Dar es salaam ilihudumia asilimia 92.6 ya shehena yote iliyopitia katika bandari zilizo chini ya Mamlaka. Katika mwaka 2011, bandari ya Dar es Salaam ilihudumia shehena yenye uzito wa tani milioni 10.3 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.2 ilikinganishwa na shehena iliyohudumiwa mwaka 2010.

Jedwali Na. 16.3: Shehena iliyohudumiwa kwa kila bandari (Tani)

	2007	2008	2009	2010	2011	Badiliko (%)
Dar es Salaam	7,432,220	7,476,618	7,796,044	8,895,023	10,335,620	16.2%
Tanga	512,372	490,119	495,659	598,538	499,621	-16.5%
Mtwara	143,072	130,763	155,848	85,214	214,039	151.2%
KLM	27,845	36,565	21,245	32,924	10,953	-66.7%
Mwanza	480,568	393,832	327,204	346,294	24,860	-92.8%
Kigoma	107,990	98,448	132,404	79,620	64,079	-19.5%
Kyela	18,098	7,960	8,828	7,849	7,597	-3.2%
Jumla	**8,722,165**	**8,634,305**	**8,937,232**	**10,045,462**	**11,156,769**	**11.1%**

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

348. Shehena iliyohudumiwa katika bandari ya Mtwara iliongezeka kwa asilimia 151.2 kutoka tani 85,214 mwaka 2010 hadi tani 214,039 mwaka 2011. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika ukanda wa kusini hususan katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi. Hata hivyo, shehena iliyohudumiwa katika bandari nyingine za Tanga, Mwanza na Kigoma ilipungua kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kupungua kwa mazao ya kilimo yanayosafirishwa nje; uchache wa meli za kubeba mabehewa katika ziwa Victoria na changamoto zinazolikabili shirika la reli TRL.

349. Mwaka 2011, kitengo cha Kontena (TICTS) kilichopo bandari ya Dar es Salaam kilihudumia jumla ya kontena 354,663 zenye wastani wa urefu wa futi 20 (TEUs) ikilinganishwa na kontena 369,903 zilizohudumiwa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 4.3. Aidha, mwaka 2011, mapato ya Mamlaka yalikuwa shilingi 306,021.38 milioni ikilinganishwa na mapato ya shilingi 253,480.09 milioni yaliyopatikana mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 20.7. Vile vile, muda wa meli za Kontena kusubiri nje ya bandari kabla ya kuhudumiwa ulipungua kufikia wastani wa siku 2.5 mwaka 2011 ikilinganishwa na wastani wa siku 3.6 mwaka 2010, sawa na ongezeko la ufanisi wa asilimia 44. Muda wa kontena kukaa bandarini ulipungua maradufu kufikia siku 10 mwezi Februari 2012 ikilinganishwa na siku 20 mwezi Februari 2009.

Shehena ya Nchi Jirani

350. Jumla ya tani 3,442,402 za mizigo kwenda na kutoka nchi jirani zilihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam mwaka 2010/11 ikilinganishwa na tani 2,441,557.0 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 41. Nchi ya Zambia ilichangia asilimia 43.6 ya shehena yote ya nchi jirani, ikifuatiwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa asilimia 11.6 kama inavyoonyeshwa

katika Jedwali Na. 16.4. Kuongezeka kwa shehena ya nchi hizi kumechangiwa zaidi na kukua kwa shughuli za kiuchumi katika nchi husika.

Jedwali Na. 16.4: Shehena ya Nchi Jirani 2006/07 – 2010/11

Country	2006/07	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11	% kwa nchi 2010/11
Zambia	996,822	1,089,045	1,089,045	1,112,283	1,499,849	43.6
DR Congo	646,549	544,391	544,391	568,275	800,986	11.6
Burundi	178,004	256,089	256,089	327,468	384,648	11.17
Rwanda	134,250	136,560	136,560	261,068	301,778	8.8
Malawi	137,034	111,372	111,372	131,532	136,375	4.0
Uganda	72,902	28,133	28,133	32,612	45,453	1.3
Others	191,034	166,093	166,093	8,319	273,313	7.9
Jumla	2,356,595	2,331,683	2,331,683	2,441,557	3,442,402	100.0

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Uchukuzi kwenye Maziwa

Kampuni ya Huduma za Meli

351. Mwaka 2011, kampuni ya huduma za meli (MSCL) ilisafirisha jumla ya tani 63,682 za mizigo na abiria 297,763, ikilinganishwa na tani 78,639 za mizigo na abiria 328,234 waliosafirishwa mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 19 kwa mizigo na asilimia 9 kwa abiria. Kupungua kwa mizigo na abiria waliosafirishwa na kampuni kulitokana na kupungua kwa shughuli za kibiashara, matatizo ya kiufundi na ushindani uliotokana na magari na meli katika njia ambazo huhudumiwa na meli za shirika.

Kampuni ya Meli ya China na Tanzania

352. Mwaka 2011, kampuni ya SINOTASHIP ilisafirisha shehena ya mizigo yenye jumla ya tani 456,000 kama ilivyokuwa mwaka 2010. Aidha, kampuni ilipata mapato ya dola za Kimarekani 7,294,008.57 mwaka 2011, ikilinganishwa na mapato ya dola za Kimarekani 6,026,689.49 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 21. Mwaka 2011, wastani wa gharama za uendeshaji zilikuwa dola za Kimarekani 5,610,653.93 ikilinganishwa na dola za Kimarekani 5,852,539.93 mwaka 2010. Hivyo, faida iliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2011 iliongezeka kwa asilimia 8 kufikia dola za Kimarekani 1,698,325.15 ikilinganishwa na faida ya dola za Kimarekani 1, 561,667.09 mwaka 2010.

Huduma za Mawasiliano

Shirika la Posta Tanzania

353. Mwaka 2011, Shirika la Posta Tanzania lilisafirisha barua 17,187,242 ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 14,868,866 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 16. Aidha, barua zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2011 ziliongezeka kwa asilimia 19 hadi barua 9, 742,715 ikilinganishwa na barua 8,206,677 zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2010. Ongezeko kwa maeneo yote mawili lilitokana na ukuaji wa utumaji wa barua za kibiashara.

354. Mwaka 2011, vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi vilikuwa 22,066 ikilinganishwa na vifurushi 18,381 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 20. Ongezeko hilo lilitokana na kupatikana kwa nyenzo za usafirishaji katika kipindi hicho. Aidha, vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2011 vilikuwa 9,726 ikilinganishwa na vifurushi 7,716 vilivyotumwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 26. Ongezeko hili lilitokana na kukua kwa biashara na hivyo kuwepo na kupelekeana sampuli za bidhaa mbalimbali.

355. Rejesta zilizotumwa nchini mwaka 2011 zilikuwa 437,038 ikilinganishwa na rejesta 445,748 zilizotumwa mwaka 2010, ikiwa ni upungufu wa asilimia 2. Aidha, rejesta zilizotumwa nje ya nchi mwaka 2011 zilikuwa 41,143 ikilinganishwa na rejesta 33,545 zilizotumwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 22. Ongezeko hilo lilitokana na kuimarika kwa huduma baada ya kuunganishwa na huduma ya “track and Trace”.

356. Mwaka 2011, idadi ya nyaraka na vipeto zilizotumwa kwa njia ya haraka (EMS) nchini ilifikia 536,219 ikilinganishwa na nyaraka 449,970 zilizotumwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 19. Hii ilitokana na Shirika kuwekeza katika matangazo na vitendea kazi kama vile magari na pikipiki. Aidha, idadi ya nyaraka na vipeto vya haraka vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2011 ilikuwa 20,376 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 18,948 vilivyotumwa mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 8. Vile vile, huduma ya usambazaji barua za haraka ndani ya miji (City Urgent Mail -CUM) nayo iliendelea kupanuka ambapo mwaka 2011 barua/nyaraka 55,314 zilisambazwa ikiwa ni zaidi ya mara tano ya barua/nyaraka 10,934 zilizotumwa mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa vyombo vya usafirishaji kama vile piki piki na magari madogo yenye kutoa huduma hii katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza pamoja na kuongezeka wateja wanaotumia huduma hiyo.

357. Mwaka 2011, huduma ya utumaji wa ujumbe wa haraka ndani ya nchi kwa njia ya nukushi ilikuwa nukushi 14,414 ikilinganishwa na nukushi 25,127 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 43. Kupungua huko kulitokana na kukua kwa teknolojia ya utumaji ujumbe kupitia simu za viganjani na mdahalishi. Aidha, huduma ya utumaji ujumbe wa haraka kwenda nje ya nchi kwa nukushi iliongezeka kutoka watumiaji 153 mwaka 2010 hadi watumiaji 918 mwaka 2011. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa wanafunzi pamoja na wadau wengine wenye kutumia huduma hiyo.

358. Utumaji wa fedha kwa njia ya nukushi uliongezeka kutoka nukushi 114,432 mwaka 2010 hadi nukushi 138,752 mwaka 2011, ikiwa ni ongezeko la asilimia 21. Aidha, mwaka 2011, idadi ya wateja waliotuma fedha kupitia mtandao wa kompyuta walikuwa 9,030 ikilinganishwa na wateja 1,487 mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na mabadiliko ya biashara yanayolenga kuboresha mfumo wa utumaji fedha kwa kutumia mtandao wa kompyuta badala ya matumizi ya nukushi. Hadi kufikia Desemba 2011, ofisi 70 zilikuwa zimeunganishwa kwenye mtandao wa kompyuta ikilinganishwa na ofisi 14 za mikoa zilizokuwa zimeunganishwa mwaka 2010. Aidha, utumaji wa fedha kupitia mfumo wa "UPU wa IFS" nao pia uliendelea kutumika ambapo mwaka 2011 'Interstate money order' 920 zilitumwa ikilinganishwa na 1236 za mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 25. Mfumo huu hutumika kutuma fedha katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, na Comoro

359. Mwaka 2011, utumaji wa fedha kwa hawala za Posta (Postal Orders) uliongezeka kwa asilimia 4.0 hadi hawala 833 ikilinganishwa na hawala 804 za mwaka 2010. Licha ya kuonesha kuongezeka, matumizi ya huduma hii yanakabiliwa na changamoto ya teknolojia hususan ya utumaji wa fedha kupitia mifumo ya kompyuta.

360. Mwaka 2011, huduma ya kufanya malipo kwa uwakala ya "Post Giro" ndani ya nchi iliongezeka kwa asilimia 4.0 hadi kufikia wateja 179,269 kutoka wateja 178,533 waliohudumiwa mwaka 2010. Huduma hii hutumika kulipa pensheni za wastaafu na gawio la hisa za Makampuni zilizoorodheshwa katika soko la Hisa Tanzania.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

361. Mwaka 2011, kulikuwa na makampuni 7 yanayotoa huduma ya mawasiliano kwa njia ya sauti kama ilivyokuwa mwaka 2010. Makampuni hayo ni TTCL, Vodacom, Airtel, Tigo, Zantel, Benson Online na Dovetel (Sasatel).

362. Mwaka 2011, watumiaji wa simu za viganjani waliongezeka kutoka watumiaji 20,983,853 mwaka 2010 hadi watumiaji 23,979,870, sawa na ongezeko la asilimia 14.2. Katika kipindi hicho, Kampuni ya Vodacom ndiyo iliyokuwa na wateja wengi ambao ni asilimia 42.9 ya wateja wote wa simu za viganjani. Aidha, watumiaji wa simu za mezani walikuwa 174,678 mwaka 2011 ikilinganishwa na watumiaji 174,511 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 0.09. Aidha, idadi ya makampuni yanayotoa huduma za mawasiliano kwa njia ya takwimu (data) ilipungua kutoka makampuni 80 mwaka 2010 hadi makampuni 79 mwaka 2011, sawa na upungufu wa asilimia 1.3.

Jedwali na.16.5: Idadi ya Wanaotumia Simu za Mikononi na Mezani

Kampuni za Simu	Idadi ya Wateja		Badiliko %
	2010	2011	
VODACOM	8,670,536	10,278,081	19
TIGO	4,477,510	5,263,330	18
AIRTEL	6,021,091	6,834,301	14
ZANTEL MOBILE	1,700,528	1,374,057	-19
SASATEL	24,827	7,461	-70
TTCL MOBILE	86,965	220,932	154
BENSON	2,396	1,708	-28
Jumla simu za mikononi	**20,983,853**	**23,979,870**	**14.3**
TTCL FIXED	159,054	158,669	-0.2
ZANTEL FIXED	15457	16009	3.6
Jumla simu za mezani	174,511	174,678	0.1
Jumla Kuu	**21,158,364**	**24,154,548**	**14.2**

Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

363. Awamu ya II ya utekelezaji wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu wa kilomita 3,000 iliyoanza kutekelezwa mwezi Agosti, 2010 ilikamilika mwezi Machi, 2012. Kukamilika kwa awamu hii pamoja na awamu ya kwanza iliyokuwa na urefu wa kilomita 4,330

kuliwezesha kuunganishwa kwa mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika awamu ya kwanza na ya pili ya mradi wa Mkongo vilijengwa vituo 22 vya kutolea huduma katika maeneo yafuatayo: Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Iringa, Dodoma, Mbeya, Singida, Babati, Arusha, Moshi, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Lindi, Mtwara, Songea, Sumbawanga, Makambako na Biharamulo. Aidha, vituo 9 vilijengwa katika mipaka ya Rusumo (Rwanda), Kabanga na Manyovu (Burundi), Namanga, Horohoro na Sirari (Kenya), Mutukula (Uganda), Kasumulo (Malawi) na Tunduma (Zambia).

364. Huduma za mkongo wa Taifa hutumiwa na watoa huduma 11 wa ndani na nje ya nchi ambao ni TTCL, Zantel, Simba Net, Airtel, MTL (Malawi), MTN (Zambia), MTN, Rwandatel, RDB, Airtel (Rwanda) na UCOM (Burundi). Hadi kufikia Desemba 2011, thamani ya mauzo ya huduma kama zilivyo kwenye mikataba iliyosainiwa na kampuni za watoa huduma za mawasiliano ilikuwa Dola za Kimarekani 12, 969,980. Mwaka 2010 hakukuwa na mapato yeyote kwa kuwa huduma za mkongo zilikuwa hazijaanza kutolewa.

Maendeleo ya Teknolojia ya Habari

365. Mwaka 2011, jumla ya magazeti 40 yalisajiliwa ikilinganishwa na magazeti 7 yaliyosajiliwa mwaka 2010 na hivyo kufanya jumla ya magazeti yote yanayochapishwa nchini kufikia 752. Aidha, idadi ya vituo vya Redio Tanzania Bara iliongezeka na kufikia vituo 70 mwaka 2011. Vile vile, hadi kufikia Desemba 2011, Tanzania bara ilikuwa na vituo vya Televisheni 33.

Jedwali Na. 16.6: Idadi ya Vyombo vya Habari Vilivyosajiliwa

Aina ya vyombo vya habari	2010	2011	Jumla ya vyombo vya habari 2011
Magazeti	7	40	752
Redio	6	11	70
Televisheni	3	4	33

Chanzo: Idara Habari - Maelezo, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Masijala ya Utafiti Tanzania

366. Mwaka 2011, Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia ilitoa jumla ya vibali vya tafiti mpya 260 zikiwa ni pamoja na tafiti zinazofanywa kwa ushirikiano wa taasisi za Serikali, watafiti wa nje pamoja na vyuo vikuu vya Serikali. Tafiti hizo zilifanywa katika nyanja za wanyama pori, sayansi ya utabibu, kilimo, jiografia, historia, siasa, uchumi, sayansi ya jamii, sheria, na

sayansi ya mawasiliano. Aidha, tafiti 145 ziliongezewa muda na kufanya mwaka 2011 kuwa na jumla ya tafiti 405. Vile vile, jumla ya ripoti 183 za muendelezo wa tafiti, ripoti za shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu, zilikusanywa toka tafiti mbalimbali na zilihifadhiwa katika maktaba ya tume kwa ajili ya matumizi kwa wanataaluma na jamii nzima ya watanzania. Kati ya ripoti hizo, baadhi zipo kwenye teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi taarifa na zinaweza kusomwa kupitia inteneti.

Uendelezaji wa Rasilimali Watu

367. Mwaka 2011, Taasisi ya Nelson Mandela ya Arusha ilidahili wanachuo 83, kati ya hao, wanachuo 53 walikuwa wa shahada ya uzamili na wanachuo 30 walikuwa wa shahada ya uzamivu. Katika mwaka huo, taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya ilidahili jumla ya wanachuo 2,591, ikiwa ni ongezeko la asilimia 45.5 ikilinganishwa na wanachuo 1,757 waliodahiliwa mwaka 2010. Kati ya hao, wanachuo 1,926 walidahiliwa katika ngazi ya stashahada na wanachuo 665 walidahiliwa katika ngazi ya shahada ya kwanza mwaka 2011. Aidha, jumla ya wanachuo 361 walihitimu na hivyo kuongeza nguvu kazi ya Taifa katika nyanja ya usanifu majengo, uhandisi na uongozi wa biashara. Vile vile, mwaka 2011 Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam ilidahili wanachuo wapya 1,505 ikijumuisha wanachuo 182 wa astashahada ya teknolojia ya mawsiliano, 825 wa stashahada ya uhandisi na 498 wa shahada ya uhandisi.

Udhibiti wa Mionzi

368. Mwaka 2011, Tume ya Mionzi ilipokea na kutathmini maombi 224 ya leseni za matumizi ya mionzi. Kati ya maombi yaliyopokelewa, 196 yalikubaliwa baada ya kukidhi matakwa na vigezo vya kinga na matumizi salama ya mionzi. Maombi yaliyobaki yalirudishwa kwa waombaji kwa marekebisho kadhaa kabla ya kuyawasilisha tena. Aidha, Tume ya Mionzi ilikagua jumla ya vituo 60 vyenye matumizi ya mionzi ayonisha. Vituo 50 vilikidhi viwango vya usalama katika hali ya kuridhisha. Vituo 10 vilikutwa na kasoro ndogo ndogo kulingana na matakwa ya kinga ya mionzi na hivyo kuamriwa kuzirekebisha. Vile vile, vituo vitatu vya Hospitali za wilaya ya Igunga, Kahama na Kasulu vilifungiwa kutumia mionzi ya x-ray kutokana na kufanya kazi bila leseni kinyume na matakwa ya Sheria ya Nguvu za Atomu namba 7 ya mwaka 2003.

Jedwali Na. 67 **SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Urefu wa Reli	kms.	2721.5	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707
Magari ya Moshi:	Namba	77	103	103	99	99	84	45	43	25	22
Mvuke	Namba	1	1	1	1	1	1	1	1	0	0
Dizeli	Namba	76	102	102	98	98	83	45	0	0	0
Mainlain		-	77	77	73	73	62	5	5	21	19
Shunting		-	25	25	25	25	21	40	38	4	3
Jumla ya mabehewa:	Namba	1479	1779	1592	1951	1828	1912	1648	1357	1071	1326
Abiria	Namba	98	82	83	82	54	102	45	68	50	53
Mizigo ya kawaida	Namba	1104	1104	1104	1464	1369	1369	1190	1093	648	658
Mafuta	Namba	164	164	164	164	164	208	244	178	179	335
Mifugo	Namba	51	69	69	69	69	76	18	39	88	88
Mengineyo	Namba	62	360	172	172	172	157	151	105	106	192
Uchukuzi	Namba										
Abiria	000	685	666	464	514	594	524	392	285	284	227
Mizigo	Tani'000	1446	1443	1002	1169	775	714	429	237	265	138

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 68

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Urefu wa Reli Kuu	Km	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860
Magari ya Moshi	Namba	21	22	58	58	21	19	10	16	15	13
Reli Kuu	Namba	14	15	42	42	15	14	8	11	10	9
Ya kujongeza	Namba	7	7	16	16	6	5	2	5	5	4
Mabehewa ya abiria	Namba	67	60	75	75	66	71	62	53	36	36
Abiria	Namba	106	102	61	61	52	59	53	44	31	30
Chakula	Namba	6	5	5	5	6	8	4	3	2	3
Vifurushi	Namba	9	8	9	9	8	4	5	6	3	3
Mabehewa ya mizigo	Namba	2110	1401	1556	1518	1455	1458	1371	1412	1620	930
Mizigo ya kawaida	Namba	2019	1088	1354	1364	1297	1295	1217	1174	1381	795
Mifugo	Namba	5	2	2	16	20	6	0	0	0	0
Mafuta	Namba	82	103	83	81	72	81	114	196	197	93
Barafu	Namba	4	4	3	8	3	10	4	7	7	7
Mengineyo	Namba	-	148	22	2	2	2	2	2	2	2
Breki	Namba	64	15	64	26	44	46	17	16	16	16
Ballast	Namba	28	45	28	21	17	18	17	17	17	17
Uchukuzi mizigo (Tani)	000	677	147	298	470	555	569	525	333	540	248
Abiria	000	1212	261	390	611	1063	1000	1177	923	758	414

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 69

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Jumla ya meli	Namba	3120	2350	2898	3895	4154	3038	697	1842	1274	1232
Uwezo wa kubeba mizigo	000	4011	4285	5848	11506	18257	16588	7260	17472	18721	24240
Jumla ya abiria	000	516	648	525	1072	664	714	310	141	228	311595
Jumla ya bidhaa zote	000wt	4514	5346	4179	4307	6320	5703	2316	4946	4954	5432
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	3627	4416	3390	3599	5292	4932	2136	4382	4559	4816
Za kawaida	000wt	2022	2650	1928	2107	3164	2762	1053	2430	2159	2474
Saruji	000wt	-	-	-	0	0	0	0	0	0	0
Mafuta	000wt	1402	1696	1382	1311	1909	2054	1013	1852	2400	2342
Mengineyo1	000wt	203	70	80	181	219	116	70	100	0	0
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	717	930	623	708	1027	761	181	466	466	466
Za kawaida	000wt	664	848	581	654	971	713	153	466	419	557
Mafuta	000wt	53	82	32	35	34	48	28	24	47	59
Mengineyo1	000wt	-	-	10	19	22	0	0	7	0	0
Mabadilishano	000wt	168	253	251	308	371	126	-	68	0.1	32

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Jumla ya meli	Namba	186	234	185	215	281	242	95	144	215	201
Uwezo wa kubeba mizigo	000	264	258	440	628	964	551	133	671	1059	1005
Jumla ya abiria	000	0.5	2.7	4	6.4	6.6	7.1	8.3	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000wt	201	259	162	289	519	542	178	359	529	508
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	104	118	127	165	307	330	836	213	357	373
Za kawaida	000wt	81	93	113	111	195	242	817	147	313	365
Mafuta	000wt	22	25	14	54	112	88	19	66	44	8
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	97	141	104	134	212	212	66	145	171	134
Za kawaida	000wt	97	141	104	134	212	212	66	145	171	507
Mafuta	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Jumla ya meli	Namba	194	138	85	215	281	99	36	32	58	129
Uwezo wa kubeba mizigo	000	392	263	106	628	964	251	131	31	455	307
Jumla ya abiria	000	62	33	10	6.4	6.6	10	0	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000	177	141	169	289	519	112	82	95	107	112
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	78	70	44	165	307	53	26	23	39	44
Za kawaida	000wt	57	59	30	111	195	47	22	23	36	35
Mafuta	000wt	20	11	14	54	112	6	4	0	3	9
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	99	71	75	134	212	59	56	72	68	71
Za kawaida	000wt	99	71	75	134	212	59	56	72	68	71
Mafuta	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 70

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Ofisi ndogo Posta	Namba	190	149	139	136	162	162	167	202	171	105
Franchised Post Offices	Namba	83	83	91	92	91	86	113	81	81	151
Ofisi kamili	Namba	151	154	157	157	129	113	172	170	170	163
Jumla	**Namba**	424	386	387	385	382	361	452	453	422	419
Masanduku binafsi	000	305.076	168881	171.7	171.8	172	173	173.5	117		146
Masanduku yaliyokodishwa	000	137.467	143691	148.0	147.5	146	150	130.2	87	120	130
Maombi yasiyotimizwa	000	0.129	0	0	0	0	0	5	4	0	21
Mifuko pekee iliyokodishwa	Namba	222	215	222	214	203	217	182	62	183	361
Barua zilizotumwa bila vifurushi	Mill.	25.04	21.3	25.2	0	28.1	23.7	15	14	29.2	27
Nchini	Mill.			20.1		19.9	16.9	9.8	14	18.7	19
Nje ya nchi	Mill.			5.1		8.2	6.8	5.2		10.5	8
Regista na barua za amana	000	356.561	450066	**562.8**	**488.7**	**1003**	**530**	**306.9**	**377**	**480.4**	**347**
Nchini	000					915	452	146.5	0	305	293
Nje ya nchi	000					40	37	136.2	0	154	34
Vifurushi nchini	000	31.976	29442	43.3	48.4	36	29	18	8.6	14.6	10
Vifurushi vya nje	000	5.76	6699	7.9	6.6	12	12	6.2	2	6.8	11
Leseni za kuuza stamp	Namba	10767	11100	10113	10099	12824	6324	6242	6256	25145	28257
Huduma za haraka, barua na vifurushi	"										
Ndani ya nchi	"	260486	309736	247268	297061	312110	262381	216762	493709	283711	501635
Nje ya nchi	"	19675	29409	30693	37331	36930	12289	14650	4012	18766	16965
EMS Money Fax	"	188790	216710	259449	300357	533821	379084	366382	23165	82002	36357
EMS Fax (Fax message received)	"	4440	16112	22394	22968	23328	14659	121901	103558	31594	1595
Overnight Mail Services	"										
Mifuko ya barua iliyosafirishwa	"	53572	70170	71199	70086	101486	75900	85595	68912	76983	115403
vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa	"	81477.91	21992	20204	21692	28753	20314	12754	13934	2752	12040
Huduma za gari ndogo											
Jumla ya barua zilizosafirishwa	"	8555	6587	5337	5993	3690	6542	4328	268	0	193
Amana za haraka zilizotolewa	"	284495	251685	218937	207997	210440	214558	0	20057	8169	4717
Amana za haraka zilizolipwa		216961	271924	224630	147020	233325	132030	93508	23069	11881	17397
Amana za haraka za nje ya nchi:											
Zilizotumwa	"	2210	1393	1602	1586	1788	1519	1354	1030	1027	998
Zilizopokelewa	"	1605	1061	1202	1001	1105	686	671	150	150	217
Amana za posta zilizouzwa	"	28683	16445	12714	8277	8029	9152	8062	8831	1924	633
Amana za posta zilizolipwa	"	25843	15113	12653	7565	7639	4615	5709	5490	3262	1662
Savings Bank Transactions											
Uwekaji amana (Deposit)	"	173304	144155	102288	66885	42255	25382	24574	9535	18863	13438
Uchukuaji amana (Withdrawal)	"	157532	132538	89517	55392	32294	19534	21122	11663	23025	72358

Chanzo :Shirika la Posta

SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)+

Jedwali Na.73

Maelezo	Kipimo	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Tani-Kilometa:											
Zilizokuwepo	000	40524	28023	91769	33198	42627	32533	-	5313	9482	1662
Zilizotumika	000	17258	11351	58579	18121	22085	18480	-	1508	2888	268
Matumizi	%	42.6	41.0	47.25	54.6	51.8	56.7	-	28.4	30.5	16
Viti-kilometa:											
Vilivyokuwepo	000	317522	238618	343250	334427	365265	306461	469426	41396	59724	7140
Vilivyotumika	000	163597	123433	164553	185085	221307	190006	129000	16469	30527	2946
Matumizi	%	51.5	51.7	47.9	55.3	60.6	62.0	27.5	39.8	51.1	41
Abiria ++	000	137	157	271	197	224	190	188	27	41	9
Mizigo ya ziada	Tani	NA	NA	NA	NA	NA	103	30	9	8	2
Mizigo mingine	Tani	2233	1379	1506	1200	1502	1123	1044	54	145	4
Shehena za Posta	Tani	162	82	235	214	299	241	162	11	30	0

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

+ Zinahusu "scheduled traffic" tu

++ Abiria waliolipa nauli kamili

NA Takwimu hazikupatikana

SURA YA 17

NISHATI

Kiwango cha Ukuaji

369. Katika mwaka 2011, shughuli za kiuchumi za umeme na gesi zilikua kwa asilimia 1.5 ikinganishwa na ukuaji wa asilimia 10.2 mwaka 2010. Kushuka kwa ukuaji wa shughuli za umeme na gesi kulitokana na kushuka kwa uzalishaji wa umeme kutokana na ukame ulioikumba nchi kwa kipindi hicho, kushuka kwa uzalishaji wa umeme katika mitambo inayotumia mafuta ya IPTL na kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia. Mchango wa shughuli za kiuchumi za umeme na gesi katika Pato la Taifa umeendelea kuwa asilimia 1.8 kama ilivyokuwa mwaka 2010.

Umeme

370. Mwaka 2011, jumla ya umeme uliozalishwa katika gridi ya Taifa na vyanzo vingine ulikuwa saa za Gigawati 5,153.4 ikilinganishwa na saa za Gigawati 5,138 zilizozalishwa mwaka 2010. Kati ya hizo, saa za Gigawati 5,024.45 zilizalishwa kwenye gridi ya Taifa na saa za Gigawati 128.96 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya Taifa. Aidha, katika mwaka 2011 umeme uliouzwa ulikuwa saa za Gigawati 3,994.74 ikilinganishwa na saa za Gigawati 4,092 zilizouzwa mwaka 2010. Kutokana na uchakavu wa mitambo ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini, umeme uliopotea ulikuwa saa za Gigawati 1,158.66, sawa na asilimia 22.5 ya umeme uliozalishwa ikilinganishwa na asilimia 32.8 uliopotea mwaka 2010. Mchanganuo wa umeme uliozalishwa katika mwaka 2011 ni kama ifuatavyo: Umeme wa maji ni saa za gigawati 1,992.58; gesi – saa za gigawati 2,668.63; diesel – saa za gigwati 492.19.

UWEZO WA MITAMBO YA UMEME NA KIASI CHA UMEME ULIOTENGENEZWA KWA VITUO

Jedwali Na. 74

Kituo	2008		2009		2010*		2011*	
	Uwezo **MW**	Uliotengenezwa **GWH**	Uwezo **MW**	Uliotengenezwa **GWH**	Uwezo **MW**	Uliotengenezwa **GWH**	Uwezo **MW**	Uliotengenezwa **GWH**
GRIDI YA TAIFA								
Kidatu (Morogoro)	204.0	1061.60	204.0	1097.83	204.0	1110.58	204.0	759.34
Mtera	80.0	344.02	80.0	450.85	80.0	433.31	80.0	229.25
Hale (Tanga)	21.0	60.18	21.0	43.05	21.0	48.96	21.0	2.55
New pangani	68.0	261.99	68.0	166.67	68.0	207.94	68.0	197.32
Nyumba ya Mungu (Moshi)	8.0	25.06	8.0	32.88	8.0	30.17	8.0	29.35
Kihansi	180.0	893.15	180.0	845.62	180.0	867.32	180.0	772.85
Uwemba Min Hydro		2.87	0.8	3.00	0.8	3.00	0.8	1.92
Jumla Hydro	**561.0**	**2648.87**	**561.8**	**2639.90**	**561.8**	**2701.28**	**561.8**	**1992.58**
Ubungo Diesel	34.37	0.00	34.37	0.00	0.00	0.00	34.37	-
Ubungo GTS								
Ubungo-Watsila		266.07	104.76	630.41	100.00	669.83	102.00	631.35
Tegeta-Watsila			43.65	17.51	43.65	243.73	45.00	320.23
Dodoma (Zuzu)	7.44	2.08	7.44	2.43	7.44	1.07	7.44	5.41
Mbeya Iyunga	13.90	0.00	13.90	0.00	13.90	0.00	13.90	-
Musoma	2.56	-	2.56	0.00	2.56	0.00	2.56	-
Mwanza Nyakato	12.50	-	12.50	0.00	12.50	0.00	12.50	-
Tabora	10.20	0.01	10.20	0.00	10.20	0.00	10.20	-
Jumla Thermal	**80.97**	**268.16**	**229.38**	**650.35**	**190.25**	**914.63**	**227.97**	**956.99**
JUMLA GRIDI	**641.97**	**2917.03**	**791.18**	**3290.25**	**752.05**	**3615.91**	**789.81**	**2949.57**
MATAWI MENGINE - ISOLATED STATIONS								
Bukoba	2.56	0.09	2.56	0.12	2.56	0.15	2.56	2.78
Kigoma	6.11	17.82	6.25	15.19	6.25	21.22	12.00	21.14
Kilwa /Masoko	1.24	2.34	1.50	2.44	1.50	1.36	1.50	-
Lindi	2.28	0.04	0.00	0.00	0.00	0.00	0.00	0.00
Mafia	0.85	2.15	0.85	2.63	0.85	2.70	0.85	3.15
Mtwara	4.86	0.00	1.14	0.00	1.14	0.00	18.00	59.21
Njombe	1.28		1.28	0.00	1.28	0.00	-	-
Songea	5.67	17.15	6.43	16.38	6.43	18.76	6.43	17.62
Sumbawanga	2.14	-	1.50	0.00	1.50	0.00	5.00	2.42
Mpanda	1.92	3.95	1.66	4.57	1.66	6.96	2.30	6.90
Ikwiriri	0.85	1.77	0.85	2.30	0.85	2.82	8.45	0.27
Tunduru	0.70	1.83	2.07	2.85	2.07	3.75	2.07	3.64
Masasi	4.50	13.74	4.50	13.23	4.50	10.12	4.50	-
Liwale	0.75	1.31	0.60	1.32	0.60	0.97	1.00	1.20
Ngara	0.95	2.17	0.95	2.57	0.95	2.78	0.95	2.78
Biharamulo	0.95	2.62	0.95	2.42	0.95	3.30	0.95	3.38
Mbinga		1.14	2.26	2.13	2.26	3.10	2.26	3.07
Ludewa		0.10	1.28	0.65	1.28	0.82	1.28	0.80
JUMLA - MATAWI MENGINE	**38.45**	**68.22**	**36.63**	**68.80**	**36.63**	**78.81**	**70.10**	**128.36**
JUMLA KUU - TANESCO	**680.42**	**2985.25**	**827.81**	**3359.05**	**788.68**	**3694.72**	**859.91**	**3077.93**
KUTOKA VYANZO VINGINE (Uganda, TANWAT, Zambia, GTS Songas, IPTL, Kiwira Coal Mine, Kilombero-Ilovo)		**1440.12**		**1443.04**		**1443.04**		**2074.89**
JUMLA YA UMEME ULIOTENGENEZWA		**4425.37**		**4802.09**		**5137.76**		**5152.82**

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

* Za Awali

MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI

Jedwali Na. 75 (Mill. KWH)

Mwaka	Tanzania Bara			Zanzibar	Jumla	Umeme Uliopotea	Jumla ya Umeme Uliotengenezwa
	Taa za Mitaani	Matumizi ya Nyumbani	Biashara na Viwanda				
2001	0.55	980	965	127	2073	675	2748
2002	0.10	1108	1085	133	2326	464	2790
2003	0.04	1029	1257	145	2431	232	2663
2004	0.05	1131	1419	161	2711	40	2751
2005	0.03	900	1519	185	2604	544	3148
2006	0.09	871	1593	204	2668	924	3592
2007	0.01	1420	1459	231	3288	917	4205
2008	0.01	1647	1722	229	3598	827	4425
2009	0.01	1432	1498	186	3116	1686	4802
2010	0.01	1671	2247	174	4092	1046	5138
2011	0.01	1600	2118	277	3995	1159	5154

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

* Za Awali (Provisional)

MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 76

Mkoa	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Dodoma	46	48	49	59	68	79	83	86
Arusha	194	202	193	223	296	236	269	240
Manyara					14	17	19	20
Kilimanjaro	101	102	96	110	109	88	124	118
Tanga	143	156	154	165	169	166	209	219
Morogoro	86	113	107	119	136	121	179	163
Coast &					104	94	106	116
Dar-es-Salaam	1263	1110	1136	1574	1641	1200	1789	1664
Lindi	10	10	12	12	11	11	13	14
Mtwara	19	20	20	29	23	29	27	30
Ruvuma	13	13	13	14	15	15	21	21
Iringa	59	60	61	79	79	85	101	92
Mbeya	105	95	99	109	115	125	139	132
Singida	15	18	46	28	18	26	26	23
Tabora	111	67	71	37	98	84	97	95
Rukwa	9	9	11	12	11	12	17	19
Kigoma	13	9	12	10	12	12	16	18
Shinyanga	174	176	177	195	196	253	313	310
Kagera	20	28	35	36	37	33	44	29
Mwanza	127	136	132	151	173	192	215	201
Mara	42	47	40	95	44	52	110	109
Jumla Tanzania Bara	**2550**	**2419**	**2464**	**3057**	**3369**	**2930**	**3917**	**3719**
Zanzibar	**161**	**185**	**204**	**231**	**229**	**186**	**174**	**277**
JUMLA	**2711**	**2604**	**2668**	**3288**	**3598**	**3116**	**4091**	**3996**

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

* Za Awali

Utafutaji Mafuta na Gesi

371. Katika mwaka 2011, jumla ya futi za ujazo (c3sqf) 31,635,480,487 za gesi asili zenye thamani ya dola za kimarekani 69.40 milioni zilizalishwa ikilinganishwa na futi za ujazo (c3sqf) 28,087,123,320 zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 58.44 zilizozalishwa mwaka 2010. Aidha, jumla ya mikataba 24 ya utafutaji na uzalishaji mafuta ilisainiwa. Shughuli za ukusanyaji wa takwimu za mitetemo ya miamba na uchorongaji wa visima katika maeneo ya nchi kavu na baharini ziliendelea. Visima vinne vya utafutaji wa mafuta vilichorongwa katika maji ya kina kirefu baharini, ambapo gesi asili iligundulika katika visima vitatu kwenye Kitalu namba 1 na 3.

Uagizaji na Mwenendo wa Bei za Mafuta

372. Katika mwaka 2011, mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam yalikuwa lita za ujazo 3,134,063,714 ikilinganishwa na lita za ujazo 2,076,497,009 zilizoaagizwa mwaka 2010. Kati ya hizo, mafuta yaliyoenda nchi za jirani yalikuwa lita za ujazo 1,150,749,146, sawa na asilimia 36.71 ya mafuta yote yaliyoagizwa.

373. Mwaka 2011, bei za mafuta katika soko la dunia zilikuwa zikipanda na kushuka kulingana na nguvu ya soko. Kiwango cha juu cha bei kilikuwa katika mwezi Aprili 2011 ambapo, wastani wa bei kwa mwezi ulikuwa: dola za kimarekani 1,079 kwa tani moja ya petroli, dola za kimarekani 1,1014 kwa tani moja ya dizeli na dola za kimarekani 1,074 kwa tani moja ya mafuta ya taa na ndege. Bei zilishuka kidogo ilipofikia mwishoni mwa mwezi Desemba. Ongezeko hilo la bei lilijidhihirisha pia katika soko la ndani. Hata hivyo, makali ya kupanda kwa bei katika soko la ndani hayakuwa makubwa kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali kurekebisha kodi na kanuni za ukokotoaji wa bei za mafuta. Mwaka 2011, wastani wa bei za mafuta katika soko la ndani ulikuwa shilingi 2,050 kwa lita moja ya mafuta ya diesel, shilingi 2,055 mafuta ya petroli na shilingi 1,625 mafuta ya taa ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1765 kwa dizeli, shilingi 1,736 na shilingi 1,241 mwaka 2010.

Nishati Mbadala

Maporomoko Madogo ya Maji

374. Mwaka 2011, mradi wa kuzalisha umeme kutokana na maporomoko madogo ya maji wa Mawengi, wenye uwezo wa kufua kW 300 ulizinduliwa na jumla ya wateja wapya 300 waliunganishiwa umeme. Utafiti uliofanywa kwenye mikoa mitano ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Kagera na Iringa hadi sasa umebainisha uwezo wa kuzalisha Megawati 475. Wizara kwa kushirikiana na TANESCO wanaendelea kufanya utafiti katika mikoa mingine.

Umeme wa Jua

375. Mwaka 2011, mradi wa uendelezaji wa soko la vifaa vya umeme nuru vijijini ulitekelezwa katika mikoa 14 ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa, Tabora, Kigoma, Pwani, Rukwa, Mbeya, Singida na Manyara. Mfano, mkoa wa Rukwa ulipata umeme jua katika vituo vya afya na zahanati 41, vituo vya polisi 9 na shule 16. Aidha, kaya 70 ziliwekewa umeme jua kwa matumizi ya majumbani na taa za barabarani 240 zilifungwa. Katika mikoa mingine ya Ruvuma na Mbeya, jumla ya mifumo 30 ilifungwa katika kaya mbalimbali.

Jotoardhi na Biofueli

376. Kikosi Kazi kiliundwa na kupewa kazi ya kuandaa mikakati na kuishauri Serikali kuhusu uendelezaji wa jotoardhi nchini. Utafiti uliokwishafanyika katika eneo la Mto Songwe na Ziwa Ngozi unaonesha kuwepo kwa nishati ya joto ardhi. Wataalamu wa Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Jiolojia, Tanzania na TANESCO walibainisha sehemu tatu za kuchimba visima vya *temperature gradient* kwenye eneo la Ziwa Ngozi

Matumizi Bora ya Nishati

377. Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) ilitekeleza mradi wa matumizi bora ya nishati chini ya programu ya Muungano wa Umoja wa Mataifa katika kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi, ambapo taarifa za awali za vifaa vya umeme (electrical equipments and appliances) katika taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali na majengo ya biashara kwa mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha ulifanyika.

SURA YA 18

MAJI

Utangulizi

378. Mwaka 2011, sekta ya maji ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2010. Mchango wa shughuli za usambazaji maji katika Pato la Taifa ulipungua kidogo kufikia asilimia 0.3 mwaka 2011 kutoka asilimia 0.4 mwaka 2010.

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

379. Mwaka 2011, usimamizi wa rasilimali za maji, utafiti na ufuatiliaji wa vyanzo vya maji uliendelea nchini kote. Utafiti wa vyanzo vipya vya maji katika mabonde ya maji ikijumuisha mito, vijito, chemichemi na visima uliendelea mwaka 2011 kwa lengo la kuratibu matumizi sahihi ya maji. Katika utafiti huo, vyanzo vipya 24 vilitambuliwa katika mabonde nane. Idadi ya vyanzo vipya vya maji katika mabonde hayo ni kama ifuatavyo: Pangani (5), Bonde la Kati (4), Rufiji (3), Ziwa Rukwa (3), Ziwa Tanganyika (3), Wami/Ruvu (2), Ruvuma (2) na Ziwa Nyasa (2). Maeneo 254 yenye maji chini ya ardhi katika mabonde yote nane yalibainika kuwa yanafaa kuchimba visima virefu vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na umwagiliaji. Aidha, jumla ya vibali 205 vya haki ya kutumia maji vilitolewa kwa wakulima na vikundi vya watumia maji.

380. Mwaka 2011, hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa lengo la kukabiliana na uchafuzi wa maji na vyanzo vyake, ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro katika matumizi ya maji kwa kutumia Sheria ya Usimamizi wa Maji na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009. Kulikuwa na jumla ya migogoro 27 inayohusu matumizi ya maji ambapo migogoro 25 ilitatuliwa kwenye mabonde ya Mto Pangani (11), Wami/Ruvu (10) na Mto Rufiji (3).

381. Mwaka 2011, sampuli 2,836 kutoka vyanzo mbalimbali vya maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani zilikusanywa na kufanyiwa utafiti wa kimaabara, ikilinganishwa na sampuli 1,648 mwaka 2010. Kati ya hizo, sampuli 2,110, ikiwa ni asilimia 74.4 zilikuwa na viwango vinavyokubalika kwa matumizi ya binadamu. Aidha, sampuli 538 za majitaka toka viwandani na mitambo ya kusafishia maji zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara katika miji

ya Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Morogoro, na Tanga. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa, sampuli 446, sawa na asilimia 82.9 yalikidhi viwango vya kumwagwa kwenye mazingira bila kuleta athari yoyote.

Huduma ya Maji Vijijini

382. Mwaka 2011, miradi 340 ya kusambaza maji vijijini ilikamilika. Kati ya hiyo, miradi 209 ya usambazaji maji vijijini ilijengwa na miradi 131 ilikarabatiwa. Miradi hiyo ilifanikisha kujengwa kwa vituo 2,804 vya kuchotea maji ambavyo viliwanufaisha wanavijiji 700,750 kupata huduma ya maji safi na salama karibu na makazi yao. Katika utekelezaji wa programu ya maji vijijini na usafi wa mazingira, wanavijiji wapatao 422,378 walielimishwa na kuhamasishwa kuhusu usafi wa mazingira. Sambamba na hilo, vyoo bora vya shimo vya mfano 2,551 vilijengwa na kukamilika mwaka 2011 ikilinganishwa na vyoo 763 vya mfano vilivyojengwa mwaka 2010.

383. Idadi ya wananchi wa vijijini waliopata huduma ya maji iliongezeka kutoka wakazi 20,545,945 mwaka 2010, hadi wakazi 20,634,227 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 0.4. Mwaka 2011, uwiano wa wananchi waliopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ilikuwa asilimia 56.6, ikilinganishwa na asilimia 57.8 mwaka 2010. Upungufu wa uwiano huu ulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini na ongezeko kubwa la idadi ya watu lililozidi kasi ya ujenzi wa miradi ya maji vijijini.

Huduma za Maji Mijini

384. Mwaka 2011, uzalishaji wa maji mijini ulipungua hadi kufikia mita za ujazo milioni 116.45, kutoka mita za ujazo milioni 116.55 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 0.08. Katika kipindi cha mwaka 2011, Mamlaka za Maji 19 za miji mikuu ya mikoa ziliweza kutoa huduma ya maji kwa kiwango cha asilimia 86 ya wakazi wa mijini, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 88.9 ya wakazi wa mijini mwaka 2010.

385. Mwaka 2011, idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika Jiji la Dar es Salaam iliendelea kuwa katika kiwango cha asilimia 55.0. Kiwango kidogo cha utoaji huduma ya maji katika jiji la Dar es Salaam

kilitokana na ongezeko kubwa la wakazi lililopelekea mahitaji zaidi ya maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii pamoja na uchakavu wa miundombinu.

386. Mamlaka za maji katika miji mikuu ya mikoa zilikusanya jumla ya shilingi bilioni 48.7 mwaka 2011, ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi bilioni 40.3 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 21. Ongezeko hilo lilitokana na wateja wapya 282,244 waliounganishwa katika mfumo wa maji, ikilinganishwa na wateja wapya 251,610 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Pamoja na ongezeko la mapato, huduma ya maji mijini inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya maji na kasi ya ongezeko la wakazi mijini lisiloendana na uwekezaji katika miundombinu ya maji.

UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI KWA MWAKA 2011

Jedwali 77

Mamlaka	Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo)	Mapato (TShs)
	2010		2011	
Arusha	14,721,190	4,228,767,804	13,130,365	4,439,919,207
Babati	1,150,694	412,582,337	1,102,056	545,791,770
Bukoba	2,290,311	781,849,481	2,379,843	856,364,230
Dodoma	9,667,795	4,080,208,091	9,891,546	5,319,580,534
Iringa	4,229,160	2,129,065,911	4,901,651	2,543,391,568
Kigoma	3,117,511	502,410,725	4,684,263	815,222,870
Lindi	328,902	203,796,544	268,133	175,506,149
Mbeya	11,236,254	3,339,539,484	10,793,446	3,772,790,461
Morogoro	8,900,610	3,801,407,363	8,800,245	4,730,546,495
Moshi	9,102,782	3,102,872,040	9,189,308	3,710,388,357
Mtwara	1,659,664	972,731,617	2,285,218	1,253,598,238
Musoma	3,848,175	1,247,335,118	3,717,139	1,354,049,964
Mwanza	23,492,486	7,304,948,210	22,966,066	9,461,022,328
Shinyanga	3,491,099	1,506,671,775	2,983,817	1,963,006,961
Singida	1,527,053	500,960,728	1,326,238	580,684,186
Songea	2,361,703	734,974,362	2,669,799	986,463,073
Sumbawanga	1,763,680	402,940,915	1,669,100	456,552,113
Tabora	4,149,561	1,340,824,081	3,767,712	1,393,944,777
Tanga	9,513,697	3,696,449,819	9,929,713	4,403,689,730
Jumla	**116,552,327**	**40,290,336,405**	**116,455,658**	**48,762,513,011**

Chanzo: Wizara ya Maji

SURA YA 19

ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Elimu ya Awali

387. Mwaka 2011, idadi ya wanafunzi katika elimu ya awali iliongezeka hadi wanafunzi 1,069,208 kutoka 925,465 mwaka 2010, sawa na ongezeka la asilimia 15.5. Kati ya hao, wasichana walikuwa 530,730, sawa na asilimia 49.6 ya wanafunzi wote na wavulana walikuwa 538,478. Idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 997,081 sawa na ongezeko la asilimia 12.8 ambapo wavulana walikuwa 502,187 na wasichana walikuwa 494,894. Idadi ya wanafunzi kwa shule zisizo za Serikali ilikuwa 72,127 ambapo wavulana walikuwa 36,291 na wasichana walikuwa 35,836.

388. Mwaka 2011, uwiano wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi katika shule za awali za Serikali ulikuwa 1:114 ikilinganishwa na 1:71 mwaka 2010 wakati ambapo kiuhalisia, uwiano unaokubalika ni 1:25. Hii ilitokana na sababu kwamba ukokotoaji uliofanyika haukuwajumuisha waalimu wa elimu ya msingi ambao hufundisha pia shule za awali ili kukwepa kuwahesabu mara mbili. Aidha, kiwango cha jumla cha uandikishaji wa wanafunzi kilikuwa asilimia 44.5 mwaka 2011 wakati ambapo kiwango halisi cha uandikishaji kilikuwa asilimia 42.4.

Elimu ya Msingi

389. Mwaka 2011, idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi ilipungua kwa asilimia 0.6 kutoka wanafunzi 8,419,305 mwaka 2010 hadi wanafunzi 8,363,386. Kati ya hao, wanafunzi 4,159,740 walikuwa wavulana au asilimia 49.7 wakati wasichana walikuwa 4,203,646 au asilimia 50.3. Idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza iliongezeka kutoka wanafunzi 1,356,574 mwaka 2010 hadi wanafunzi 1,388,216 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 2.3.

390. Mwaka 2011, idadi ya shule za msingi za Serikali na zisizo za Serikali iliongezeka kutoka shule 15,816 mwaka 2010 hadi 16,001 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 1.2. Idadi ya shule za Serikali iliongezeka kutoka shule

15,265 mwaka 2010 hadi 15,412 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 1. Vile vile, idadi ya shule zisizo za Serikali iliongezeka kutoka shule 551 mwaka 2010 hadi 589 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 6.9.

391. Kiwango cha jumla cha uandikishaji wa wanafunzi kilipungua kutoka asilimia 106.4 mwaka 2010 hadi asilimia 102.7 mwaka 2011. Vile vile kiwango halisi cha uandikishaji kilipungua kutoka asilimia 95.4 mwaka 2010 hadi asilimia 94.0 mwaka 2011.

392. Idadi ya walimu wenye ujuzi stahili katika shule za Serikali iliongezeka kutoka walimu 156,733 mwaka 2010 hadi walimu 169,233 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 8.0. Hivyo, uwiano wa mwalimu aliyefuzu kwa wanafunzi uliimarika kutoka 1:54 mwaka 2010 hadi 1:49 mwaka 2011. Aidha, kiwango cha kukatisha masomo kiliongezeka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2010 hadi asilimia 3.4 mwaka 2011 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo utoro, kushindwa kumudu mahitaji ya msingi na mimba za utotoni

393. Idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2010 walikuwa 894,889. Kati yao, wavulana walikuwa 435,124 na wasichana walikuwa 459,889. Wanafunzi waliofaulu walikuwa 478,912. Ufaulu huu ni sawa na asilimia 53.5 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani ikilinganishwa na mwaka 2009 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 49.4. Kati yao, wavulana waliofaulu walikuwa 256,817 na wasichana walikuwa 222,095.

Elimu ya Sekondari

394. Idadi ya shule za sekondari katika mwaka 2011 iliongezeka hadi shule 4,367 kutoka shule 4,266 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 2.4. Kati ya hizo, shule 3,425 zilikuwa za Serikali na 942 zisizo za Serikali. Idadi ya shule za sekondari za Serikali iliongezeka kutoka shule 3,397 mwaka 2010 hadi shule 3,425 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 1.0

395. Idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari wa kidato cha kwanza hadi cha sita iliongezeka kutoka wanafunzi 1,638,699 mwaka 2010 hadi 1,789,547 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 9. Kati ya hao, wasichana walikuwa

802,554 sawa na asilimia 44.8 na wavulana walikuwa 986,993 sawa na asilimia 55.2 ikilinganishwa na wasichana 728,528 (asilimia 44.5) na wavulana 910,171 (asilimia55.5) mwaka 2010.

396. Kiwango cha jumla cha uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita kiliongezeka kutoka asilimia 34.0 mwaka 2010 hadi asilimia 36.1 mwaka 2011. Vile vile, kiwango halisi cha uandikishaji kiliongezeka kutoka asilimia 29.9 mwaka 2010 hadi asilimia 32.1 mwaka 2011.

Elimu ya Ualimu

397. Mwaka 2011, idadi ya vyuo vya ualimu ilikuwa 103 ikilinganishwa na vyuo 92 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 11.9. Kati ya hivyo, vyuo vya Serikali vilikuwa 34 na vyuo visivyo vya Serikali 69. Aidha, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali ilikuwa wanachuo 37,698 mwaka 2011 ikilinganishwa na wanachuo 36,648 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Kati ya wanachuo hao, wavulana walikuwa 20,385 (asilimia 54.1) na wasichana walikuwa 17,313 (asilimia 45.9). Mafunzo yaliyotolewa yalikuwa katika ngazi zifuatazo: Elimu Maalum wanachuo 452, Cheti 24,042, Stashahada (tarajali) 11,582 na Stashahada (mafunzo kazini) 1,622.

398. Mwaka 2011, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu vya Serikali ilikuwa 24,243 ikilinganishwa na wanachuo 25,814 mwaka 2010, sawa na upungufu wa asilimia 6.1. Kati ya wanachuo hao, wasichana walikuwa 10,652 (asilimia 43.9) na wavulana walikuwa 13,591 (asilimia 56.1). Aidha, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu visivyo vya Serikali ilikuwa 13,455 mwaka 2011 ikilinganishwa na wanachuo 10,834 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 24.2. Kati ya wanachuo hao, wasichana walikuwa 6,661 (asilimia 49.5) na wavulana walikuwa 6,794 (asilimia 50.5).

Elimu ya Watu Wazima

399. Mwaka 2011, idadi ya wananchi walioshiriki katika Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) iliongezeka kutoka washiriki 924,893 mwaka 2010 hadi 1,050,517, sawa na ongezeko la asilimia 14. Kati ya hao, wanaume walikuwa 499,898, sawa na asilimia 47.6 na wanawake walikuwa 550,619, sawa na asilimia 52.4 ikilinganishwa na washiriki wanaume 451,108 (asilimia 48.8) na wanawake 473,785 (asilimia 51.2) mwaka 2010.

400. Idadi ya washiriki wa Mpango wa Elimu ya Masafa na Ana kwa Ana iliongezeka kutoka washiriki 51,993 mwaka 2010 hadi washiriki 64,338 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Kati ya washiriki hao, wanaume walikuwa 23,657, sawa na asilimia 36.8 na wanawake walikuwa 28,336, sawa na asilimia 63.2 ikilinganishwa na wanaume 29,014 (asilimia 45.1) na wanawake 35,324 (asilimia 54.9) mwaka 2010.

401. Mwaka 2011, idadi ya washiriki wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto waliokosa (MEMKWA) wenye umri wa miaka 11 hadi 18 iliongezeka kwa asilimia 13.3 hadi wanafunzi 82,459 kutoka wanafunzi 72,799 mwaka 2010. Hii ilitokana na wazazi kutokuwa na mwamko wa kuwaandikisha darasa la kwanza watoto wao wa rika lengwa (miaka 7) katika shule za msingi na ufaulu mdogo wa vijana walio katika elimu nje ya mfumo rasmi waliokuwa katika madarasa ya MEMKWA kundirika la I na la II.

Ukaguzi wa shule na vyuo

402. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za elimu ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora. Mwaka 2010/11, jumla ya shule/vyuo/taasisi/asasi 6,215 za elimu zilikaguliwa ikilinganishwa na shule/vyuo/taasisi/asasi 9,960 zilizokaguliwa mwaka 2009/10. Hata hivyo, idadi ya shule/vyuo/taasisi/asasi zilizokaguliwa mwaka 2010/11 zilikuwa asilimia 41.5 ya lengo lililokusudiwa kukaguliwa la shule/vyuo/taasisi/asasi 14,986.

Jedwali Na: 19.1 Taasisi/Asasi Zilizokaguliwa kwa Mwaka 2010/11

Aina ya Taasisi/Asasi	Idadi Taasisi/Asasi-June, 2011	Idadi iliyolengwa kukaguliwa	Idadi halisi iliyokaguliwa	Kiwango cha utekelezaji (% ya idadi iliyokaguliwa)
Shule/Madarasa ya Elimu ya Awali	40730	5,450	2,473	45.4
Shule za Msingi	16001	3,375	1,276	37.8
Vituo vya Elimu ya Ufundi	358	170	55	32.4
Shule/madarasa ya Elimu Maalum	354	140	40	28.6
Vituo vya Elimu ya Watu Wazima	18557	4,328	1,296	29.9
Shule za Sekondari	4367	1,430	1,035	72.4
Vyuo vya Ualimu	103	93	40	43.0
Jumla	**80470**	**14,986**	**6,215**	**41.5**

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Elimu ya Ufundi na Mafunzo

403. Mwaka 2010/2011, idadi ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 240 ikilinganishwa na vyuo 224 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Kati ya hivyo, vyuo 140 vilikuwa ni vya Serikali na vyuo 100 visivyo vya Serikali ikilinganishwa na vyuo 133 vya Serikali na 91 visivyo vya Serikali mwaka 2009/2010.

404. Mwaka 2010/11, idadi ya wanachuo waliojiunga katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ilikuwa 85,040 ikilinganishwa na wanachuo 58,494 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 45.4. Kati ya hao, wanachuo 69,506 walikuwa katika vyuo vya Serikali na 15,534 walikuwa katika vyuo visivyo vya Serikali ikilinganishwa na wanachuo 50,554 waliokuwa katika vyuo vya Serikali na 7,940 waliokuwa katika vyuo visivyo vya Serikali mwaka 2009/2010.

Elimu ya Ufundi Stadi

405. Mwaka 2010/11, idadi ya vyuo vya ufundi stadi ilipungua hadi vyuo 672 kutoka 681 mwaka 2009/10, sawa na upungufu wa asilimia 1.3. Upungufu huu kwa kiasi kikubwa ulichangiwa na vyuo kutokukidhi vigezo vya usajili.

406. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi stadi iliongezeka hadi wanafunzi 104,840 mwaka 2010/11 kutoka 82,962 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 26. Kati ya hao, wanafunzi 92,752 (asilimia 88.5) walikuwa wa kozi ndefu na wanafunzi 12,088 (asilimia 11.5) wa kozi fupi. Uandikishaji katika vyuo vya umma ambavyo vinasimamiwa na VETA ulipungua kutoka vyuo 40,643 mwaka 2009/10 hadi 23,123 mwaka 2010/11. Hii ni kutokana na kuanzishwa kwa utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia umahiri (Competence Based Education and Training – CBET) ambapo ililazimika kuongeza muda wa mafunzo ya awamu ya kwanza kutoka mwaka mmoja hadi miaka miwili.

Elimu ya Juu

407. Mwaka 2010/11, idadi ya ya taasisi za elimu ya juu ilikuwa 32 na kati ya hivyo, vyuo vikuu vilikuwa 27. Idadi ya vyuo vikuu vya Serikali ilikuwa 11 na vya binafsi ilikuwa 16 sawa na ilivyokuwa mwaka 2009/10. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya Serikali iliongezeka kutoka 83,828 (wanaume 55,831 na wanawake 27,997) mwaka 2009/10 hadi 104,130 (wanaume 69,215 na wanawake 34,915) mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 24.2.

408. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu visivyo vya Serikali iliongezeka kutoka 35,123 mwaka 2009/10 hadi wanafunzi 35,509 mwaka 2010/11, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Kati ya hao, wanawake walikuwa 15,045, sawa na asilimia 42 na wanaume 20,464, sawa na asilimia 58 ikilinganishwa na wanawake 14,242, sawa na asilimia 41 na wanaume 20,881 sawa na asilimia 59 mwaka 2010.

409. Mwaka 2010/11, idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu vya Serikali na visivyo vya Serikali ilikuwa 139,639 ikilinganishwa na wanafunzi 118,951 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 17.4. Kati ya hao, idadi ya wanafunzi wa kike ilikuwa 49,960, sawa na asilimia 36 ya wanafunzi wote wakati idadi ya wanafunzi wa kiume ilikuwa 89,679, sawa na asilimia 64.

410. Mwaka 2010/11, Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu ilitoa mikopo kwa wanafunzi 92,791 yenye thamani ya shilingi 231,835,927,151.85 ikilinganishwa na wanafunzi 72,035 waliopata mikopo yenye thamani ya shilingi 197,348,958,875.00 mwaka 2009/10, sawa na ongezeko la asilimia 17.5 ya mikopo iliyotolewa. Aidha, kasi ya urejeshwaji mikopo imekuwa ikiongezeka kwa kiasi kikubwa tangu utaratibu wa kurejesha mikopo ulipoanza. Hadi Desemba 2011, Bodi ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 5,886,658,982.24 ikilinganishwa na shilingi 3,055,600,922.44 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 92.7.

SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 80 (Namba)

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
1986	10789	9855	8401	8679	2363	2276	42363
1987	11626	10870	9528	9162	2313	2322	45821
1988	14258	11195	10373	9180	2313	2240	49559
1989	16034	14815	11275	10018	2980	2360	57482
1990	18654	16340	14199	11157	3777	2859	66986
1991	18892	18679	15459	13915	3646	3355	73946
1992	19299	19443	17044	14864	4136	3874	78660
1993	20267	20110	17597	16713	4261	4016	82964
1994	21589	19823	17513	16474	4179	3863	83441
1995	25200	22237	19118	17067	4541	3903	92066
1996	28289	23874	20197	16468	4528	4035	97391
1997	32043	29748	23810	19697	6412	4846	116556
1998	37094	31218	24925	21182	5163	4748	124330
1999	39144	36682	28589	23996	6305	5248	139964
2000	43643	36734	31132	25456	6654	6143	149762
2001	47204	45078	30531	29188	7198	6601	165800
2002	56101	50371	36989	29045	7711	7126	187343
2003	52863	60643	36906	35653	7780	6885	200730
2004	98738	67294	46546	36385	8353	7572	264888
2005	134963	109398	46188	46489	9710	8444	355192
2006	196391	151448	72167	42584	18211	9691	490492
2007	401011	218060	105770	70796	21789	11668	829094
2008	395930	332393	175353	95214	25240	11743	1035873
2009	480529	308131	159789	167355	31201	12695	1159700
2010	382207	398870	293519	279995	26065	20674	1401330
2011	403873	396724	380528	279117	30265	25164	1515671
Badiliko (%)							
2010 - 2011	5.7	-0.5	29.6	-0.3	16.1	21.7	8.2

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali 80 A

Aina ya Taasisi	2008			2009			2010			2011		
	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla
Shule za Msingi	15257	416	15673	426	15301	15727	15265	551	15816	15412	589	16001
Shule za Sekondari	3039	759	3798	3283	819	4102	3397	869	4266	3425	942	4367
Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari)	33	34	67	34	43	77	34	58	92	34	69	103
Jumla	**18329**	**1209**	**19538**	**3743**	**16163**	**19906**	**18696**	**1478**	**20174**	**18871**	**1600**	**20471**

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali 80B

	2008			2009			2010			2011		
	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla
I. Elimu ya msingi:												
Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII	4261831	4148263	8410094	4248764	4192789	8441553	4203269	4216036	8419305	4159740	4203646	8363386
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za serikali Darasa la I-VII	4203180	4093428	8296608	4182915	4130165	8313080	4127500	4139526	8267026	4076899	4123752	8200651
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII	58651	54835	113486	65849	62624	128473	75769	76510	152279	82841	79894	162735
Jumla ya walimu katika shule za msingi	76638	78257	154895	80066	77119	157185	82170	83686	165856	86098	89351	175449
Jumla ya walimu katika shule za msingi za serikali	74479	74954	149433	76765	74711	151476	78331	80750	159081	81262	85849	167111
Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi	2159	3303	5462	3301	2408	5709	3839	2936	6775	4836	3502	8338
II. Elimu ya sekondari:												
Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI	679124	543279	1222403	812945	653457	1466402	910171	728528	1638699	936003	775106	1711109
Wanafunzi wanaosoma katika shule za serikali, kidato I-VI	58118	451755	509873	728322	565369	1293691	792974	608356	1401330	816909	643333	1460242
Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI	95006	91524	186530	84623	88088	172711	117197	120172	237369	119094	131773	250867
Idadi ya walimu katika shule za serikali	23122	9713	32835	17240	9192	26432	19666	10586	30252	26635	13299	39934
Idadi ya walimu katika shule za binafsi	16790	8181	24971	5732	1790	7522	8155	2110	10265	9722	2490	12212
Jumla ya Walimu wote	39912	17894	57806	22972	10982	33954	27821	12696	40517	36357	15789	52146

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU

Jedwali 80C

	2007			2008			2009			2010			2011		
	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla	Waume	Wake	Jumla
Shahada	-	-	-	4209	1749	5958	5352	2636	7988	-	-	-	-	-	-
Stashahada	4215	1744	5959	16154	8411	24565	17593	10909	28502	8229	5450	13679	2671	-108	2563
Daraja A	4074	5483	9557	66214	69665	135879	70567	72357	142924	4288	4734	9022	5180	5626	10806
Daraja B	-	-	-	22223	16762	38985	17678	13388	31066	-	-	-	-	-	-
Mafunzo Kazini	1747	1491	3238	108800	96587	205387	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Jumla	**10036**	**8718**	**18754**	**217600**	**193174**	**410774**	**111190**	**99290**	**210480**	**12517**	**10184**	**22701**	**7851**	**5518**	**13369**

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WANAFUNZI WALIOJIUNGA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA JINSIA

Jedwali Na. 80D

Taasisi/Kozi	2010/11		
1. CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDM)	**ME**	**KE**	**Jumla**
MSc of Renewable Energy	9	3	12
Master of Arts in Aplied Social Psychology	7	4	11
Master of Development Studies	18	14	32
Master of Education	36	61	97
Mster of Kiswahili	18	31	49
Master of Business Adminstration	99	55	154
Master of Ed in Sc Education	12	4	16
Master of Education Management and Adm.	15	9	24
Master ofd Intergrated Environment Management	3	0	3
Master of Laws	15	12	27
Master ofd Science	39	9	48
Masters of Sc. In Comp Sc.	4	0	4
Master of Sc in Constr. Managmt	1	1	2
Master of Sc in Elect Eng and Info Techn	4	3	7
Master of Health Informatics	1	0	1
Masters of Sc. In Highway Eng.	3	0	3
Masters of Sc. In Marine Sciences	30	13	43
Masters of Sc. In Water Resources Eng.	3	1	4
PHD	24	7	31
PGD in Civil Eng.	1	1	2
PGD in Education	24	21	45
PGD in Elect. Power Eng.	2	0	2
PGD Elect. Eng and Inf. Technology	7	2	9
PGD in Eng. Mgt	1	0	1
PGD in Enterprenuership and enterprise Development	5	3	8
PGD in Law	3	2	5
PGD in Mass Communication	4	1	5
PGD in Mech Eng	1	0	1
PGD in Microfinance	6	4	10
PGD in Scientific Computing	33	8	41
PGD in ICT Policy and Regulations	2	0	2
Masters of Arts	70	34	104
Masters of Enterprenuership and Enterprise Dpt	23	7	30
Masters of International Trade	14	11	25
Masters of Science in International transport and logistics	5	2	7
Masters of Eng. Mgt	22	4	26
Masters of Intergrated water Resources Mgt	7	8	15
Masters of Science in Natural resources Assesment and Mgt	6	8	14
B.A Education	511	364	875
B.A with Education	222	265	487
B.A (Archaelogy)	5	7	12
B.A (Archaelogy & Geography)	3	2	5
B.A (Culture & Haritage)	2	21	23
B.A (Language Studies)	6	6	12
B.A (Economics)	34	48	82
B.A (Economics & Geography)	10	0	10
B.A (Economics & Sociology)	0	1	1
B.A (Economics & Statistics)	21	10	31
B.A (Fine and Performing Arts)	10	18	28
B.A (Geography & Env. studies)	52	28	80
B.A (History & Archeology)	7	6	13
B.A (History & Polit. Science)	9	9	18
B.A (Polit. Science & public Admin)	48	39	87
B.A (Polit. Science & Economics)	3	1	4
B.A (Polit. Science & Language)	11	6	17
B.A (Polit. Science & Sociology)	1	31	32
B.A (Polit. Science & Philosophy)	6	11	17
B.A (Sociology and Philosophy)	9	12	21
B.A (Sociology)	70	83	153
B.A (Statistics)	16	12	28
B.A (History)	10	1	11
B.A Journalism	8	8	16
B.A Mass communication	12	22	34
B.A Public Relations and advertersing	10	17	27
B.Commerce	267	190	457
BSc. in computer science	58	22	80
BSc. With computer Science	32	1	33
BSc. (Education)	121	40	161
BSc. With Education	126	34	160
BSc. General	7	0	7
BSc.with Geology	8	0	8
BSc.Geology	12	1	13
B.B.A	31	21	52
B. Ed. Commerce	7	0	7
B. Ed. In Psychology	26	21	47
B. Ed. In Education Psychology	21	26	47
B. Ed. In Education in Physical Educ,Sports and Culture	12	6	18
B. Ed. Science	37	45	82
B. Ed. Adult Education	23	30	53

Jedwali Na. 80D Linaendelea

B. Ed. Arts	16	34	50
Bachelor of law	65	25	90
BSc. Comp. Eng. & Info. Tech.	38	16	54
BSc. Electr. Engineering	17	0	17
BSc. Electro power Eng.	5	2	7
BSc. Chem. & processing Eng.	15	16	31
BSc. Chemistry	8	3	11
BSc. Electro. Mech. Eng.	3	1	4
BSc. Food and Biochemical	2	3	5
BSc. Mech. Eng.	8	1	9
BSc. Mining Eng.	29	3	32
BSc. Mineral Proc. Eng.	13	8	21
BSc. Civil & Struct. Eng.	32	5	37
BSc. Telecom Eng.	35	8	43
BSc. Civil & Transportation Eng.	18	5	23
BSc. Civil & water Res. Eng.	23	9	32
BSc. Electronics Sc. & Comm.	27	2	29
BSc. Mol. Bio & Biotech	11	5	16
BSc. Aquatic Sc. And Env. Sc & Con	21	2	23
BSc. Wildlife csience and conservation	28	5	33
BSc. Fish & Aquaculture	6	1	7
BSc. Industrial Engineering and Management	11	12	23
Diploma in Computer Sciences	22	3	25
Diploma in Fisheries	0	2	2
Certificate in law	106	49	155
Certificate in Computer Science	19	5	24
Honoria Caus	2	0	2
Jumla :	**3041**	**2033**	**5074**
Idadi ya Walimu	**128**	**65**	
2. CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA MUHIMBILI (MUHAS)	**2010/2011**		
M.D (Doctor of Medicine)	168	59	227
B.Sc. Pharmacy	21	14	35
D.D.S (Doctor of Dental Surgery)	31	9	40
BSc. Env. Health	14	4	18
B. Sc. Nursing Mg.	2	1	3
B.Medical Labaratory Science	16	2	18
B. Sc. In Radiotherapy Treatment	7	0	7
Adv. Dip. Dermatove neurology	10	3	13
Adv. Dip. Nursing	3	5	8
Adv. Dip. Medical Laboratory Techn.	6	5	11
Dip. Diaghostic Radiography	21	6	27
Dip. Enviromental Health Science	38	22	60
Dip. Medical Laboratory Techn	45	17	62
Dip. Orthopaedic Techn	7	4	11
Dipl. In Nursing	3	23	26
Dip. Pharmaceutical Sciences	15	7	22
Msc. Anatomy	2	0	2
MSc. Traditional Medicine Development	2	1	3
MSc. Critical Care and Trauma	2	1	3
Msc. Tropical Desease Control	5	2	7
MSc. Applied Epidemiology	4	1	5
MSc. Epidemiology and Labouratory Mgt	2	0	2
MSc. Parasitology and Entomology	3	1	4
Master of Public Health	8	14	22
Master of Arts (M.A HPM)	5	5	10
MSc. Phamacetical Management	4	3	7
MSc. Hospital and Clinical Phamacy	0	1	1
Masters of Phamacy (M. PHARM)	0	1	1
Masters of Dentistry (M. Dent)	5	1	6
Masters of Medicine (MMED)	18	17	35
Masters of Science Super Specialities	3	0	3
Doctor of Phylosophy (PHD)	1	0	1
Jumla :	**471**	**229**	**700**
Idadi ya Walimu	**176**	**64**	**240**

Jedwali Na. 80D Linaendelea

3. CHUO KIKUU CHA ARDHI (UCLAS)	**2010/2011**		
B.Architecture (ARCH)	256	68	324
BSc.Architecture in Interior Design (A.ID)	30	12	42
BSc. Architecture in Land Scape (A.LA)	16	3	19
B.Sc Build Economics)	183	99	282
B.Sc. (Urb. And regional Planning)	178	39	217
B.Sc. (Building Surveying (BS))	19	20	39
B.Sc. (Land Mgt. and Valuation)	229	64	293
B.Sc. (Env. Engineering)	150	61	211
B.Sc.Geomatics	88	27	115
BSc.Real Estate Finance and Management (REFI)	63	20	83
BSc. Property and Facilities Management (PFM)	57	14	71
BSc. Finance and Accounts (BAF)	45	20	65
BSC. Enviromental Science and Management	110	91	201
BSc. Municipal and Industrial Service(MISE)	50	8	58
BSc.Enviromental Laboratory Technology (ELST)	30	35	65
BSc. Housing and Infrastructure Planning (HIP)	63	15	78
Bachelor of Arts in Economics	43	18	61
BSc. Rural Development Planning (RDP)	40	13	53
BSc. Geoinformatics (GI)	40	23	63
BSc. Geodetic Science (GS)	7	0	7
BSc. Information System Management (ISM)	53	47	100
BSc. Construction Management (CM)	54	19	73
BSc. Civil Engineering	46	4	50
Masters in Ardchitecture	5	1	6
PGD in Construction Economics and Management	16	0	16
M.Sc. In Construction Economics and Management	33	3	36
M.Sc. In Environment Technology and Management	1	1	2
M.Sc. In Disaster and Risk Management	0	1	1
PHD in environmental Technology	1	1	2
PGD Geomatics	2	0	2
M.Sc. In Geomatics	10	0	10
PHD in Geomatics	4	0	4
PGD in Real Estate	3	1	4
M.Sc in Real Estate	13	5	18
Msc in Urban Planning and Mgt	6	3	9
Msc in Urban and Regional Planning and Mgt	3	1	4
Jumla :	**1947**	**737**	**2684**
Idadi ya Walimu	**186**	**51**	**237**

4. CHUO KIKUU CHA DODOMA (UDOM)	**2010/11**		
B.A KISWAHILI	42	4	46
B.A KISWAHILI LINGUISTIC	13	36	49
B.A KISWAHILI LITERATURE	10	20	30
B.A FINE ART DESIGN	5	6	11
B.A FRENCH	10	4	14
B.A ENGLISH	23	11	34
B.A KOREA	2	0	2
B.A. ORIENTAL LANGUAGE (JAPANESE)	2	1	3
B.A FILM AND THEATRE	12	5	17
B.A LITERATURE	21	11	32
B.A TOURISM & CULTURAL HERITAGE	66	71	137
B.A HISTORY	54	23	77
B.A ENVIROMENTAL DISASTER MANAGEMENT	32	234	266
B.COM (ACCOUNTING)	74	66	140
B.COM (HRM)	39	19	58
B.COM (FINANCE)	45	32	77
B.COM (MARKETING)	24	8	32
B.COM (INTERNATIONAL BUSINESS)	19	10	29
B.COM (SMALL BUSINESS INTERPRENEURSHIP)	7	4	11
B.COM (TOURISM HOSPITALITY MANAGEMENT)	15	2	17
B.A DEVELOPMENT STUDIES	35	66	101
B.A ECONOMICS & STATISTICS	35	4	39
B.A GEOGRAPHY & ENVIROMENTAL STUDIES	90	47	137
B.A POLITICAL SCIENCE & PUBLIC ADMINSTRATION	122	80	202
B.A SOCIALOGY	35	109	144
B.A PUBLIC ADMINISTRATION	96	105	201
BACHELOR OF LAW	76	46	122
B.A ECONOMICS AND SOCIALOGY	33	15	48
B.A ENVIROMENTAL ECONOMICS & POLICY	1	1	2
B.A INTERNATIONAL RELATION	100	74	174
B.A ECONOMICS	38	36	74
BBA-FULL TIME	50	31	81

Jedwali Na. 80D Linaendelea

B.A PROJECT PLANNING MANAGEMENT & COMMUNITY DEVELOPMENT	88	53	141
B.A WITH EDUCATION	326	307	633
BED ART	200	101	301
BED MANAGEMENT AND ADMINISTRATION	62	21	83
BED COMMERCE	41	10	51
BED POLICY PLANNING & MANAGEMENT	26	5	31
BED SPECIAL NEEDS	25	56	81
BED SCIENCE	55	27	82
BED EARLY CHILD HOOD EDUCATION	32	34	66
BED PSYCOLOGY	21	53	74
BED ADULT EDUCATION & COMMUNITY DEVELOPMENT	42	34	76
BED SC (ICT)	34	5	39
BSC ED (ICT)	36	5	41
BSC WITH EDUC.	46	32	78
BED GUIDENCE & COUNSELING	41	41	82
BSC STATISTICS	74	11	85
BSC CHEMISTRY	32	7	39
BSC BIOLOGY	23	7	30
BSC PHYSICS	23	3	26
BSC MATHEMATICS	69	7	76
DOCTOR OF MEDICINE	86	33	119
BSC. NURSING	30	15	45
BSC BUSINESS INFORMATION SYSTEM	21	1	22
BSC COMPUTER ENGINEER	75	3	78
BSC. INFORMATION SYSTEM	34	10	44
BSC.COMPUTER SCIENCE	27	12	39
BSC SOFT WARE ENGINEERING	17	4	21
BSC TELECOMMUNICATION ENGINEERING	83	9	92
BSC APPLIED GEOLOGY	20	5	25
BSC MINERAL PROCESSING ENGINEERING	7	0	7
BSC MINING ENGINEERING	28	2	30
BSC NURSING -MIDWIFERY	8	4	12
BSC VITUAL EDUCATION	2	1	3
BSC IN HEALTH INFORMATION SYSTEM	34	9	43
BA IN ARABIC	4	0	4
B.COM IN MANAGEMENT SCIENCE	19	8	27
B.COM PROCUREMENT MANAGEMENT	27	33	60
B.COM IN INFORMATION MANAGEMENT	0	0	0
BA IN PHILOSOPHY	16	1	17
BSC. IN COMPUTER AND INFORMATION SERCURITY	44	4	48
BSC IN VITUAL EDUCATION	1	2	3
BSC IN PETROLEUM ENGINEERING	16	1	17
DIPLOMA IN COMPUTER SCIENCE	13	3	16
POSTIGRADUATE DIPLOMA IN EDUCATION	10	10	20
MASTER OF ART IN EDUCATION	44	17	61
MASTER OF BUSINESS ADMINSTRATION	37	9	46
MASTER OF BUSINESS ADMINSTRATION(EVERNING)	18	8	26
EXECUTIVE MASTER OF BUSINESS ADMINSTRATION	8	1	9
MASTER OF PUBLIC ADMINSTRATION	17	18	35
EVENING MASTER OF PUBLIC ADMINSTRATION	7	5	12
MASTER OF INTERNATIONAL RELATION	16	9	25
MASTER OF DEVELOPMENT STUDIES	22	18	40
EVERNING MADS	7	5	12
MASTER OF ART IN SOCIALOGY	11	6	17
MASTER OF ART IN NATURAL SCIENCE	18	4	22
MASTER OF ART IN DEMOGRAPHY	6	4	10
MASTER OF ART IN KISWAHILI BY DESERTATION	0	1	1
FULL TIME MASTER OF ART IN LINGUISTIC	18	5	23
FULL TIME MASTER OF ART IN KISWAHILI LITERATURE	12	13	25
FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN COMPUTER SCIENCE	18	2	20
FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN DRY LAND BIODIVERSITY CONSERVATION	9	2	11
FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN TELECOMMUNICATION ENGINEERING	3	0	3
MASTERS OF SCIENCE IN MATHEMATICS (MSc. Mathematics)	3	1	4
EVERNING MASTER OF SCIENCE IN TELECOMMUNICATION ENGINERING	9	2	11
FULL TIME MASTER OF SCIENCE IN NURSING - MENTAL HEALTH	0	3	3
Jumla:	**3427**	**2303**	**5730**
Idadi ya Walimu	**487**	**157**	**644**

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo

SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 81 (Namba)

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
1986	12625	12389	11895	10073	730	567	48279
1987	15709	15526	13188	12245	801	756	58225
1988	18007	18897	15326	14358	966	702	68256
1989	20789	19279	18415	14759	1045	716	75003
1990	23585	21870	17599	17685	1481	1094	83314
1991	27554	25143	19237	17371	1922	1639	92866
1992	29027	27044	19378	17891	2018	1758	97116
1993	25703	27651	21894	18367	2223	2097	97935
1994	28657	26971	22784	19809	2573	2011	102805
1995	28498	26242	24098	21199	2334	1938	104309
1996	28002	25807	22494	20318	3168	2243	102032
1997	29768	27461	22406	20627	3408	3381	107051
1998	27125	24756	22029	20409	4826	3428	102573
1999	28333	25747	23120	20255	5667	4493	107615
2000	30789	26601	23469	20430	5894	5011	112194
2001	36305	30820	25004	20762	5892	5116	123899
2002	41593	34209	27540	20681	6418	5534	135975
2003	46891	38506	26385	21650	6430	4859	144721
2004	48752	46167	33240	24476	8847	6229	167711
2005	45276	46321	32063	29248	9183	7046	169137
2006	46968	48013	42878	29796	9569	7956	185180
2007	47437	46927	41340	35746	11299	8667	191416
2008	42971	43232	43177	35980	12576	8594	186530
2009	44255	36384	37064	34061	11851	9096	172711
2010	56620	57876	50778	46820	12269	13006	237369
2011	63282	67205	65859	54521	11083	11926	273876
Badiliko (%)							
2010 - 2011	11.8	16.1	29.7	16.4	-9.7	-8.3	15.4

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

SURA YA 20

AFYA

Utangulizi

411. Katika mwaka 2011, Serikali iliendelea kutoa kipaumbele katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za Afya zenye ubora na viwango stahiki na zinazowafikia wananchi wote kwa wakati. Hii inatokana na ukweli kwamba, maendeleo ya Tanzania yataletwa na wananchi wenye afya na wenye uwezo wa kuzalisha mali, kwani wananchi wenye afya bora ni raslimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

412. Mwaka 2011, Mpango Maalum wa Afya ya Msingi (MMAM) uliendelea kutekelezwa kulingana na mpango kazi kwa lengo la kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi. Utekelezaji wa MMAM unalenga kuwa na zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata, na kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii ikiwa ni pamoja na upatikaji wa dawa na vifaa vya tiba na kuongeza upatikanaji wa rasilimali watu.

413. Katika mwaka 2011, mitaala ya kufundishia watalaam wa kada za afya iliendelea kupitiwa na kuboreshwa ili iendane na wakati na mahitaji ya sasa. Vilevile, Serikali iliendelea kuimarisha ushirikiano wa karibu na wadau mbalimbali wa sekta ya afya ili kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa ubora na viwango vilivyowekwa. Huduma za afya ya uzazi na mtoto ziliendelea kupewa kipaumbele ili kuhakikisha vifo vya akina mama na watoto vinapungua kwa kiasi kikubwa. Huduma za ushauri nasaha kuhusu Virusi vya Ukimwi na Ugonjwa wa UKIMWI ziliendelea kutolewa na wananchi waliendelea kuhamasishwa kupima afya zao pamoja na kuhakikisha dawa za kurefusha maisha kwa waathirika zinakuwepo na kutolewa kwa walengwa kwa wakati na inavyostahili.

Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya

414. Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali kama mashirika ya dini, umma, watu binafsi iliendelea kuboresha huduma za afya kwa kufanya ukarabati

na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, idadi ya vitanda katika vituo vyote vya afya nchini ilikuwa 48,480 ikilinganishwa na vitanda 45,241 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 7.2. Kati ya hivyo, vitanda 25,942 vilikuwa katika vituo vya Serikali na mashirika ya umma, na vitanda 22,538 vilikuwa katika vituo vya watu binafsi na mashirika ya kidini.

Jedwali Na.20.1: Idadi ya Vitanda kwa Aina ya Vituo vya Kutolea Tiba na Umiliki

Umiliki/Mwaka	Aina ya Kituo				Jumla		Badiliko
	Hospitali		Kituo cha Afya				
	2010	2011	2010	2011	2010	2011	
Serikali	15,828	15,937	7,695	8,155	23,523	24,092	2.4%
Mashirika ya kidini	14,638	15,251	3,151	3,978	17,789	19,229	8.1%
Mashirika ya Umma	1,647	1,697	121	153	1,768	1,850	4.6%
Binafsi	1,167	2,196	994	1,113	2,161	3,309	53.1%
Jumla	**33,280**	**35,081**	**11,961**	**13,399**	**45,241**	**48,480**	7.2%

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

415. Mwaka 2011, jumla ya mahudhurio katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma nchini kwa wagonjwa wa nje (out-patient) yalikuwa 41,014,853 ikilinganishwa na 35,776,667 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 14.6. Kati ya hao, asilimia 37.4 walikuwa watoto chini ya umri wa miaka mitano, na asilimia 62.6 walikuwa umri wa miaka mitano na zaidi. Ongezeko hili la mahudhurio lilitokana na mwamko wa jamii katika huduma za afya zitolewazo katika vituo vya afya na utekelezaji wa mpango wa MMAM ambao ulisogeza huduma za afya karibu zaidi na jamii kupunguza umbali. Idadi ya wagonjwa waliolazwa kwa mwaka 2011 ilifikia 1,539,145 ambapo asilimia 47.2 walikuwa ni watoto chini ya umri wa miaka mitano. Idadi kubwa ya watoto waliolazwa ni kwa vile kisayansi wana uwezo mkubwa wa kupata maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa haraka zaidi kuliko watu wazima.

Ukaguzi wa vituo vya Afya

416. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kuvifanyia ukaguzi vituo vya kutolea huduma za afya. Ukaguzi ulifanyika katika mikoa ya Mbeya na Morogoro. Jumla ya vituo 19 katika mkoa wa Mbeya na vituo 11 kutoka mkoa wa Morogoro vilikaguliwa na kati ya hivyo, vituo 6 kutoka katika kila mkoa vilifungwa kutokana na kutokidhi viwango vya utoaji wa huduma za afya.

Matibabu nje ya nchi

417. Katika kipindi cha mwezi Julai - Desemba 2011, jumla ya wagonjwa 262 walipelekwa nje ya nchi kwa matibabu. Kati ya hao, wagonjwa 12, sawa na asilimia 3.4 walikwenda katika hospitali mbalimbali nchini Kenya, Uingereza, Marekani, Uswisi, Ujerumani na Afrika Kusini. Wagonjwa 250, sawa na asilimia 96.6 walikwenda nchini India kwa matibabu.

Elimu ya Afya kwa Wananchi

418. Katika mwaka 2011, huduma za elimu ya afya kwa umma ziliendelea kutolewa kupitia vipindi vya redio, magazeti, kusambaza vipeperushi na kwa njia ya kuweka mabango yanayotoa elimu ya afya ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Huduma hizi zililenga kuipa jamii uwezo kutambua na kudumisha mitindo ya maisha na tabia zinazoboresha afya, na kuepuka tabia hatarishi kwa afya.

419. Katika mwaka 2011, Serikali iliendelea kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati za afya za uendeshaji za Halmashauri (Council Health Management Team - CHMT) kwa kuwajengea uwezo kuhusu mawasiliano nyakati za dharura, majanga na milipuko ya magonjwa katika wilaya za Manyoni, Iramba, Serengeti, Rolya, Simanjiro, Kigoma Vijijini, Kilwa, Chunya, Mbozi, Nkasi, Misungwi, Bariadi, Maswa, Tunduru, Mtwara Vijijini na Kiteto.

Afya ya Uzazi na Mtoto

420. Katika mwaka 2011, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu saratani ya shingo ya kizazi ili waweze kutambua dalili za awali na matibabu yake. Aidha, Wizara imeanzisha vituo 82 vya uchunguzi wa mabadiliko ya awali ya Saratani ya shingo wa kizazi katika mikoa ya Morogoro (15), Kigoma (21),

Iringa (10), Pwani (12), Ruvuma (6), Kilimanjaro (6), Dar es Salaam (10) na Mbeya (2).

421. Katika mwaka 2011, Serikali iligawa pikipiki 370 za kubebea wagonjwa katika mikoa mbalimbali ili kuboresha utoaji wa huduma ya uzazi salama. Aidha, watoa huduma katika mikoa ya Pwani, Tabora, Manyara, Mtwara, Ruvuma, Tanga, Singida, Iringa, Dar es salaam, Arusha, Kilimanjaro, Kagera, Mbeya, Shinyanga na Rukwa, walipata mfunzo ya stadi za kuokoa maisha ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora kwa wanawake wajawazito na watoto wachanga.

Muda wa kuishi

422. Muda wa kuishi kwa mujibu wa maoteo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 inaonesha kuwa wastani wa muda wa kuishi kwa mwaka 2011 uliendelea kubaki kuwa miaka 55. Kwa upande wa wanaume, wastani wa muda wa kuishi ulikuwa miaka 54 na wanawake miaka 57 mwaka 2011 ikilinganishwa na miaka 53 kwa wanaume na miaka 56 kwa wanawake mwaka 2010.

Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria

423. Mwaka 2011, unyunyuziaji wa viuatilifu vya kuua mbu (ukoko) wa malaria ulifanyika katika mikoa ya kanda ya ziwa ya Kagera, Mwanza na Mara. Aidha, Serikali ilitoa mafunzo ya matumizi ya kipimo cha haraka cha kubaini vimelea vya malaria (Rapid Diagnostic Test) kwa wataalam wa maabara na waganga kwa mikoa 11 ya Iringa, Kagera Pwani, Arusha, Manyara, Mwanza, Mara, Singida, Dodoma, Rukwa na Mbeya. Sambamba na hilo, Serikali ilisambaza vyandarua bila malipo katika kaya katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara. Jumla ya vyandarua 17.6 milioni viligawiwa katika kampeni hii. Aidha, jumla ya vyandarua 319,610 viligawanywa kwa wajawazito na watoto kupitia hati punguzo katika kipindi hicho.Vile vile, upuliziaji wa dawa ya kuangamiza mazalia ya mbu (Biolarvicide) katika kata 17 za Jiji la Dar es Salaam ulifanyika. Kata hizo ni: Keko, Miburani, Mtoni, Kurasini, Azimio, Kipunguni, Vingunguti, Mchikichini, Buguruni, Kipawa, Ilala, Mikocheni A, Mikocheni B, Ndugumbi, Mzimuni, Magomeni na Mwananyamala.

Chakula na Lishe

424. Mwaka 2011, Serikali chini ya uratibu wa Taasisi ya Chakula na Lishe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilikamilisha Mkakati wa Taifa wa Lishe wa miaka mitano (2011/12 –2015/16). Mkakati huu uliainisha maeneo manane ya vipaumbele ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini kama ifuatavyo: Kuboresha ulishaji wa watoto wachanga na wadogo; Udhibiti wa upungufu wa vitamini na madini mwilini kwa watu wa rika zote; Udhibiti wa utapiamlo kwa watoto na wanawake wajawazito; Matunzo na huduma za lishe kwa watu wanaoishi na VVU; Matunzo na huduma za lishe kwa watoto, wanawake na kaya zilizo katika mazingira hatarishi; Udhibiti wa magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza yanayosababishwa na ulaji usiofaa; Kuboresha uhakika wa chakula katika kaya; na Kuboresha utafiti upeo, tafiti na mfumo wa taarifa za lishe.

425. Mwaka 2011, matone ya vitamini A na dawa za minyoo ziliendelea kutolewa mara mbili kila mwaka kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika wilaya zote za Tanzania Bara. Zaidi ya asilimia 90 ya watoto waliolengwa walifikiwa na huduma hizi kwa nchi nzima. Vile vile, nakala 17,000 za mwongozo wa kitaifa kuhusu lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI zilichapishwa na kusambazwa kwenye hospitali, vyuo vya afya na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya UKIMWI. Aidha, utafiti wa chakula kinachofaa kuongeza virutubishi vya vitamini na madini kwa ajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI uliendelea kufanyika ili kuboresha chakula hicho. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa chakula hiki ambacho kinatokana na mazao yanayopatikana hapa nchini kina uwezo wa kuboresha afya ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

426. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutoa chakula chenye mjumuisho wa virutubisho (chakula dawa) kwa watu 6,000 wanaoishi na virusi vya UKIMWI wenye hali mbaya ya lishe na watoto yatima wanaoishi kwenye mazingira hatarishi katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Mwanza na Shinyanga.

Huduma za Ustawi wa Jamii

427. Mwaka 2011, mpango wa uwezeshaji haki jamii ulitelekezwa katika halmashauri 9 ambazo ni Arusha, Kilosa, Geita, Kilombero, Songea, Singida Mjini na Korogwe ambapo jumla ya wawezeshaji haki jamii 198 ngazi ya kata na halmashauri walipatiwa mafunzo. Ili kuwezesha utekelezaji wa sheria ya mtoto ya mwaka 2009, katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, Serikali iliandaa kanuni zifuatazo; kanuni zinazohusu: shule za watoto zilizoidhinishwa; taratibu za kumuasili mtoto; makazi ya watoto; ajira kwa watoto; mafunzo maalum kwa watoto; na kanuni zinazohusu watoto wanaokuwa chini ya uangalizi hususan wenye kesi mahakamani.

428. Mwaka 2011, Serikali kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutoa huduma za utengamano kwa wazee, watu wenye ulemavu na watoto kupitia programu ya matunzo katika jamii. Katika kipindi hiki, jumla ya nyumba 36 zilijengwa katika makazi ya: Mkaseka nyumba 20, Hombolo 5, Nyambage 5, Nandanga 2, Busanda 2 na Kalandoto 2. Vilevile, kupitia programu ya marekebisho ya kijamii na kiuchumi kwa watu wanaoishi katika makazi, jumla ya vikundi 44 vilianzishwa kwa lengo la kuwawezesha wahudumiwa kufanya shughuli za uzalishaji mali.Vikundi hivyo hupatiwa mtaji wa shilingi 350,000 kwa kila mmoja. Aidha, watoto na vijana wa wahudumiwa wanaosoma hulipiwa gharama za mahitaji yao ambapo vijana 62 wa shule za msingi, 45 wa shule za sekondari na 5 vyuo vya ufundi walisaidiwa.

429. Mwaka 2011, jumla ya makao 97 kwa ajili ya kulelea watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi yamesajiliwa yakiwa na jumla ya watoto 3,958. Kati yao, wavulana walikuwa 2,296 na wasichana 1,662. Katika kuhakikisha kwamba watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wanatambuliwa na kupatiwa huduma za msingi, jumla ya halmashauri 95 kati ya Halmashauri 133 zilifanya utambuzi ambapo jumla ya watoto 849,051 walitambuliwa, wavulana wakiwa 399,054 na wasichana 499,997.

VYOMBO VYA AFYA NCHINI

Jedwali Na. 84

Aina ya Vyombo	Serikali			Mashirika ya Umma			Mashirika ya Dini na ya Kujitolea			Sekta Binafsi			Jumla		
	2009	**2010**	**2011**	**2009**	**2010**	**2011**	**2009**	**2010**	**2011**	**2009**	**2010**	**2011**	**2009**	**2010**	**2011**
Hospitali Maalum	6	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	6	0	0
Hospitali za Mkoa	18	0	97	0	0	11	0	0	97	0	0	31	18	0	236
Hospitali za Wilaya	90	97	0	0	11	0	0	97	0	0	31	0	90	236	0
Hospitali nyingine	0	0	0	15	0	0	116	0	0	47	0	0	178	0	0
Vituo vya Afya	431	449	449	151	5	5	41	155	155	114	75	75	737	684	684
Zahanati	3526	3773	3773	189	70	70	635	717	717	842	572	572	5192	5132	5132
Nyinginezo*	0	269	0	0	0		0			0	0	4	0	269	4
JUMLA	4071	4588	4319	355	86	86	792	969	969	1003	678	682	6221	6321	6056

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

* Ni pamoja na kliniki maalum, nursing homes, huduma za maabara na x-ray binafsi

HUDUMA ZA AFYA: WALIOFAULU MAFUNZO

Jedwali 85

Kada	Sehemu	2006/07	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11
Waliofaulu Mafunzo ya Afya ya miaka miwili katika Ngazi ya Cheti						
Health Records	Kilimanjaro	20	20	22	24	33
Laboratory	Singida	47	50	63	107	93
Laboratory	Mvumi	40	41	44	49	64
Laboratory	Nkinga	29	30	34	33	41
Laboratory Assistant	Kolandoto	-	-	-	42	54
Laboratory	Litembo	-	-	-	41	44
Pharmaceutical Assistant - KSP	Kilimanjaro	19	24	34	29	33
Clinical Assistants	Songea	40	45	47	63	69
Clinical Assistants	Sumbawanga	41	43	50	55	48
Clinical Assistants	Masasi	31	39	54	57	59
Clinical Assistants	Kigoma	29	27	37	40	41
Clinical Assistants	Maswa	39	41	83	66	81
Clinical Assistants	Musoma	35	35	47	58	50
Waliofaulu Mafunzo ya Afya ya miaka mitatu katika Stashahada						
Dental Therapy	Mbeya	13	15	12	17	21
Dental Therapy	Tanga	20	15	15	21	23
Dental Laboratory Technologists	Dar es salaam	5	5	5	4	5
Medical Laboratory Technicians	Dar es salaam	35	37	54	55	57
Medical Laboratory Technicians	Iringa	15	14	46	54	55
Medical Laboratory Technicians	Mwanza	25	27	32	29	33
Pharmaceutical Technician	Dar es salaam	20	19	24	27	29
Pharmaceutical Technician	Mwanza	23	31	26	34	42
Physiotherapy	Kilimanjaro	17	18	17	28	26
Optometry-KCMC	Kilimanjaro	15	16	13	11	16
Health Officers	Kagera	33	35	50	36	65
Health Officers	Kwimba	31	33	49	41	43
Health Officers	Mpwapwa	15	16	21	29	31
Health Officers	Tanga	17	16	20	28	35
Health Officers	Dar es salaam	21	22	24	34	40

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

IDADI YA WAHITIMU WAUGUZI 2001 - 2011

Jedwali 87

KADA	2001	2002	2003	2004	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011
Adv. Dip. Midwifery	-	-	30	-	38	-	38	-	31	-	23
Adv. Dip. Phn	14	-	21	-	21	-	28	30	22	16	19
Adv. Mental	16	-	4	-	14	-	13	-	19	-	4
Adv. Di. Opthalamic	-	12	-	14	-	15	-	14	-	22	-
Adv. Dip. Paediatric	-	14	-	14	-	16	-	16	-	21	-
Adv. Dip. Theatre	-	12	-	12	-	14	-	20	-	17	-
Adv. Dip. Education	-	12	-	23	-	23	-	18	-	-	29
Diploma in nursing	360	366	372	388	542	511	677	702	814	978	1891
Certificate in nursing	903	970	1240	120	1903	1945	1794	1515	570	1802	1491
Certificate in phn	125	198	206	-	-	-	-	-	-	-	-
Jumla	**1418**	**1584**	**1873**	**571**	**2518**	**2524**	**2550**	**2315**	**1456**	**2856**	**3457**

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI KWA MWAKA 2010 -2011

Jedwali Na. 87A

Aina ya Huduma	2010					2011				
	Serikali	Mashirika ya Umma	Mashirika ya Dini	Binafsi	Jumla	Serikali	Mashirika ya Umma	Mashirika ya Dini	Binafsi	Jumla
Hospitali za Rufaa/ Maalum	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Hospitali za Mkoa	-	-	-	-	-	15937	1697	15251	2196	35081
Hospitali za Wilaya	15828	1647	14638	1167	33280	-	-	-	-	-
Hospitali nyingine	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Vituo vya Afya	7695	121	3151	994	11961	8,155	153	3,978	1,113	13,399
Zahanati	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Jumla	23523	1768	17789	2161	45241	24092	1850	19229	3309	48480

Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 21

MAENDELEO YA JAMII

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

430. Mwaka 2011, vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi viliendesha mafunzo na stadi mbalimbali kwa wananchi 31,877 ikilinganishwa na idadi ya wananchi 31,493 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 1.2. Ongezeko hilo lilitokana na ukarabati wa baadhi ya vyuo na hivyo kuvifanya viwavutie wananchi kujiunga navyo kwa masomo mbalimbali. Mafunzo hayo yalihusu stadi za uashi, useremala, ushonaji, mapishi, ufundi magari, kilimo cha mboga, ufugaji na kujikinga na janga la UKIMWI. Mafunzo ya muda mrefu yalitolewa kwa wananchi 5,329 ikilinganishwa na wananchi 4,913 mwaka 2010, ambapo kati ya hao 2,982 walikuwa wanaume na 2,347 walikuwa wanawake. Mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wananchi 21,630 ambapo 10,545 walikuwa wanawake na 11,085 walikuwa wanaume. Mafunzo ya nje ya vyuo (outreach training) yalitolewa kwa wananchi 4,918 ambapo kati ya hao, wanawake walikuwa 2,517 na wanaume walikuwa 2,401.

431. Mwaka 2011, wanachuo 91 walihitimu mafunzo katika ngazi ya shahada katika vyuo tisa vya maendeleo ya jamii nchini ikilinganishwa na wanachuo 177 mwaka 2010, sawa na upungufu kwa asilimia 48.6. Upungufu huu ulitokana na vyuo kuwa katika kipindi cha mpito kuelekea utoaji mafunzo ya shahada kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Aidha, mwaka 2011, jumla ya wanachuo 515 walihitimu katika ngazi ya stashahada ikilinganishwa na wahitimu 431 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 19.5. Kati ya hao, wanawake walikuwa 369 na wanaume walikuwa 146. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa vyuo vya utoaji mafunzo kutoka vinne hadi kufikia tisa. Katika ngazi ya astashahada, wanachuo 757 walihitimu mwaka 2011 ikilinganishwa na wahitimu 597 mwaka 2010, sawa na ongezeko la asilimia 26.8. Kati ya hao, wanawake walikuwa 567 na wanaume 190.

Jinsia na Maendeleo ya Wanawake

432. Mwaka 2011, Serikali iliendelea kutoa mikopo kwa wanawake wajasiriamali kupitia Halmashauri zao ambapo jumla ya shilingi 88 milioni zilitolewa kwa ajili ya kuendeshea biashara zao. Aidha, Benki ya Wanawake

Tanzania iliendelea kutoa huduma kwa watu binafsi, makampuni na vikundi mbalimbali katika jamii. Mwaka 2011, wananchi hususan wanawake waliendelea kuwezeshwa kiuchumi kupitia Benki ya Wanawake Tanzania (TWB). Jumla ya akaunti 9,108 zilifunguliwa katika Benki ya Wanawake ambapo akaunti 6,889 sawa na asilimia 75.6 zilikuwa za wanawake; akaunti 2009, sawa na asilimia 22.1 ni za wanaume; na akaunti 210 sawa na asilimia 2.3 zilikuwa za makampuni. Aidha, Benki ilivipatia vikundi 195 vya wajasiriamali mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.1.

433. Mwaka 2011, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitoa mafunzo ya biashara kwa wanawake wajasiriamali 350 na iliwawezesha kushiriki katika maonesho ya biashara ya kimataifa yaliyofanyika Julai 2011. Aidha, mwaka 2011, kamati ya kitaifa ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake, watoto na albino ilizinduliwa ikiwa na lengo la kufuatilia masuala yote ya ukatili wa kijinsia na kutoa ushauri wa jinsi ya kutokomeza ukatili nchini. Vile vile, Serikali iliendesha mkutano wa wataalamu na mawaziri kutoka Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu kuhusiana na ukatili wa kijinsia. Mkutano huo ulishirikisha wadau kutoka nchi 11 na lengo la mkutano huo lilikuwa kutafuta namna ya kuweza kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Maendeleo ya Watoto

434. Mwaka 2011, Serikali iliunda mabaraza ya watoto 87 katika ngazi ya Halmashauri. Aidha, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ilisambazwa kwa wasimamizi na watekelezaji wa sheria na pia kanuni na taratibu za utekelezaji wa sheria hiyo ziliandaliwa. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2010/11, Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa huduma, matunzo na ulinzi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kufanya utambuzi wa watoto hao na kuwapa huduma muhimu. Idadi ya watoto wenye mahitaji maalum iliongezeka kutoka 746,823 mwaka 2009/10 na kufikia 813,372 mwaka 2010/11, wanaume wakiwa 431,087 na wanawake ni 382,285. Jumla ya watoto 590,000 ambao ni sawa na asilimia 72 walipewa huduma muhimu za kijamii.

435. Mwaka 2010/11, jumla ya watoto wenye ulemavu katika shule za msingi za Serikali na binafsi walikuwa 36,585, wakiwemo wa kiume 21,273 na wa kike 15,312. Kwa mujibu wa takwimu za BEST za mwaka 2011, kulikuwa na ongezeko la asilimia 2.7 katika uandikishwaji wa darasa la kwanza na ongezeko la asilimia 6.3 ya uandikishwaji wa watoto wenye mahitaji maalum katika darasa hilo. Aidha, jumla ya watoto yatima wanaopata elimu ya msingi ni 225,264,

miongoni mwao wanaume walikuwa 111,809 na wanawake ni 11,3455. Vile vile kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa nguvu kazi na ajira wa mwaka 2006, asilimia 27.5 ya watoto walio katika umri kuanzia miaka 5 – 17 walikuwa katika ajira ya watoto. Katika juhudi za kuhakikisha tatizo la ajira kwa watoto linapungua, Serikali kupitia matukio mbalimbali kama vile, Siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Familia, Siku ya Kupambana na Ajira kwa Watoto, iliendelea kuhamasisha na kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kuzuia tatizo la ajira kwa watoto.

Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

436. Mwaka 2011, kumekuwepo na ongezeko la asilimia 13.8 ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yaliyosajiliwa na kufanya idadi ya mashirika hayo hapa nchini kufikia 5,994 ikilinganishwa na mashirika 5,269 mwaka 2010. Mashirika 725 yalisajiliwa chini ya Sheria ambapo kati ya hayo, mashirika 685 yalipatiwa cheti cha usajili na mengine 40 yalipatiwa cheti cha ukubalifu ikilinganishwa na mashirika 554 yaliyosajiliwa na 28 yaliyopatiwa cheti cha ukubalifu mwaka 2010. Mashirika hayo yamejikita katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo kilimo, jinsia, elimu, afya, UKIMWI na Virusi vya UKIMWI, mazingira, haki za binadamu, maendeleo shirikishi, haki na ustawi wa watoto. Ongezeko hili la mashirika yasiyo ya kiserikali lilitokana na Serikali kuboresha mazingira ya usajili wa mashirika hayo ikiwa ni pamoja na kuwateua Maafisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya na mikoa kuwa wasajili na waratibu wasaidizi wa ngazi husika.

437. Mwaka 2011, mifumo ya kuongeza uwazi na uwajibikaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali iliendelea kuimarishwa kwa kuingiza taarifa mbalimbali zinazohusu sekta hiyo katika tovuti ya Taifa ya uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali http//www.tnnc.go.tz na kuwawezesha wadau zaidi ya 26,000 kupata taarifa mbalimbali.

MWENENDO WA WATALII WALIOINGIA NCHINI NA MAPATO YALIYOPATIKANA



MCHANGO WA MAUZO YA BIDHAA NJE (2011)



MWENENDO WA UZALISHAJI WA UMEME



MWENENDO WA UKUAJI HALISI WA UCHUMI